**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

# RIPOTI KUU YA MWAKA YA UKAGUZI WA UFANISI




**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**MACHI 2026**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

# RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA UFANISI

**MDHIBITI NA MKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI**

**MACHI, 2026**

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT
ISO 9001:2015 Certified

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**NATIONAL AUDIT OFFICE**

ISO 9001:2015 Certified

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,Jengo la Ukaguzi, Barabara ya Mahakama, S.L.P 950,411404 Tambukareli, Dodoma. Simu: 255(026)2161200, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz


**Na. CGA.23/421/2** **30 Machi, 2026**

Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
Chamwino,
**40400 DODOMA.**

**YAH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA UFANISI**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 143 (4) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418, ninawasilisha kwako Ripoti ya Jumla ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi 2026.

Ninawasilisha.

Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

## Kuhusu Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

### Mamlaka

Wajibu wa kikatiba na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na katika Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

**Dira**

Kuwa Taasisi yenye Kuaminika na ya Kisasa katika Ukaguzi wa Umma inayotoa Huduma za Ukaguzi za Viwango vya Juu zinazoimarisha Imani kwa Umma.

**Dhima**

Kutoa huduma za Ukaguzi zenye Kiwango cha Juu kwa njia za Kisasa zenye Kuimarisha Uwajibikaji na Uwazi katika Usimamizi wa Rasilimali za Umma.

**Kauli Mbiu**

Kuwa Taasisi yenye kuaminika na ya Kisasa katika ukaguzi wa umma

### Misingi ya Maadili

**Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo:** Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo

**Kufanya kazi kwa uadilifu:** Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadilina sheria katika utoajiwa huduma za ukaguzi

**Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo:** Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi staiki

**Kufanya kazi kwa utaalam:** Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora

**Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi** Tunahimiza, kuvumbua na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwaajili ya kuboresha huduma za ukaguzi

**Kufanya kazi kwa ushirikiano:** Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje

## YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI ........ viii
ORODHA YA VIELELEZO ........ xii
SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI xv
MUHTASARI ........ xvii
SURA YA KWANZA ........ 1
UTANGULIZI WA JUMLA ........ 1
1.1 Usuli wa Ukaguzi wa Ufanisi ........ 1
1.2 Mamlaka ya Kufanya Ukaguzi wa Ufanisi ........ 2
1.3 Madhumuni ya Ripoti Kuu ........ 2
1.4 Mtazamo wa Ripoti ya Jumla ........ 4
1.5 Uhalali wa Ukaguzi ........ 5
1.6 Mchakato wa Uthibitisho wa Takwimu na Taarifa Zilizotolewa ........ 6
1.7 Muundo wa Ripoti ........ 7
SURA YA PILI ........ 8
MAELEZO YA MPANGO WA PILI NA WA TATU WA MAENDELEO YA TAIFA WA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU ........ 8
2.1 Utangulizi ........ 8
2.2 Usuli kuhusiana na Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu ........ 8
2.3 Miongozo Muhimu na Mfumo wa Kisheria Unaosimamia Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26) ........ 12
2.4 Watendaji Muhimu katika Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26) ........ 13
2.5 Mikakati ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26) ........ 14
2.6 Mahitaji ya Ukaguzi katika Kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26) na Malengo ya Maendeleo Endelevu ........ 16
2.7 Ukaguzi wa Ufanisi Uliofanyika na Uhusiano wake na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22– 2025/26) na Malengo ya Maendeleo Endelevu ........ 17
2.8 Ugharimiaji wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano ........ 20
SURA YA TATU ........ 21



ISO 9001:2015 Certified

UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA ........ 21
3.1 Utangulizi ........ 21
3.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi ........ 26
3.3 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Utoaji wa Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu kwa Watoto ........ 27
3.4 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya vya Umma ........ 36
3.5 Matokeo ya Ukaguzi juu ya Utoaji wa Huduma za Afya za Uzazi ........ 49
3.6 Athari za Changamoto Zilizobainika katika Kuyafikia Malengo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu ........ 58
SURA YA NNE ........ 60
UTOAJI WA HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII NA HUDUMA ZA KISHERIA KWA WANANCHI ........ 60
4.1 Utangulizi ........ 60
4.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi ........ 64
4.3 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Upatikanaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria kwa Watu Wasio na Uwezo ........ 66
4.4 Matokeo ya Jumla ya Ukaguzi kuhusu Utoaji wa Huduma za Chakula, Makazi na Malezi kwa Wazee ........ 75
SURA YA TANO ........ 88
USIMAMIZI WA UHIFADHI WA NAFAKA ZA KIMKAKATI ........ 88
5.1 Utangulizi ........ 88
5.2 Malengo ya Ukaguzi na Mawanda ........ 90
5.3 Matokeo ya Ukaguzi ........ 91
5.4 Athari za Changamoto Zilizobainika katika Kuyafikia Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu ........ 102
SURA YA SITA ........ 103
USIMAMIZI WA USALAMA MAHALI PA KAZI NA UTOAJI WA HUDUMA ZA FIDIA KWA WAFANYAKAZI ........ 103
6.1 Utangulizi ........ 103
6.2 Malengo ya Ukaguzi na Mawanda ya Ukaguzi ........ 107
6.3 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi ........ 108
6.4 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi ........ 115
6.5 Athari za Changamoto Zilizobainika katika kuyafikia Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu ........ 123
SURA YA SABA ........ 125

ISO 9001:2015 Certified

UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI .......... 125
7.1 Utangulizi .......... 125
7.2 Malengo ya Ukaguzi na Mawanda .......... 127
7.3 Matokeo ya Ukaguzi .......... 128
7.4 Athari za Changamoto Zilizobainika katika Kuyafikia Malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu .......... 141
SURA YA NANE .......... 142
USIMAMIZI WA MFUMO WA USAFIRISHAJI .......... 142
8.1 Utangulizi .......... 142
8.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi .......... 146
8.3 Matokeo ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Usimamizi wa Mchakato wa Upangaji wa Maboresho ya Miundombinu ya Barabara .......... 147
8.4 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Usimamizi wa Uendeshaji wa Mizani .......... 155
8.5 Matokeo ya Ukaguzi Katika Usimamizi wa Huduma za Usafiri Mijini katika Majiji Makubwa .......... 164
8.6 Athari za Changamoto Zilizobainshwa katika Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano .......... 175
SURA YA TISA .......... 177
UTUNZAJI WA MAZINGIRA .......... 177
9.1 Utangulizi .......... 177
9.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi .......... 182
9.3 Matokeo ya Ukaguzi katika Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi .......... 183
9.4 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Usimamizi wa Shughuli za Urejeshaji Misitu .......... 193
9.5 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Nishati Jadidifu 203
9.6 Athari za Changamoto Zilizobainika katika kufikia Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu .......... 208
SURA YA KUMI .......... 211
USIMAMIZI WA TARATIBU ZA USHIRIKISHWAJI WA WAZAWA KATIKA SEKTA YA MADINI .......... 211
10.1 Utangulizi .......... 211
10.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi .......... 214
10.3 Matokeo ya Ukaguzi .......... 214
10.4 Athari za Changamoto Zilizobainishwa katika Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano .......... 226
SURA YA KUMI NA MOJA .......... 228

UTAFUTAJI NA USIMAMIZI WA RASILIMALIFEDHA.................................228
11.1 Utangulizi...........................................................228
11.2 Lengo la Ukaguzi na Mawanda............................................232
11.3 Matokeo ya Jumla ya Ukaguzi kuhusu Ukusanyaji wa Mapato Yasiyo ya Kodi ....................................................................234
11.4 Matokeo Jumla ya Ukaguzi wa Usimamizi wa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji wa Shule za Umma ...........................................252
11.5 Athari ya Changamoto Zilizobainishwa katika Kufikia Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu ...............................................................261
SURA YA KUMI NA MBILI ..................................................262
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .................................................262
12.1 Utangulizi...........................................................262
12.2 Hitimisho la Jumla...................................................262
12.3 Mapendekezo..........................................................266

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT
ISO 9001:2015 Certified

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Na. 1: Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi na Taasisi Zilizokaguliwa ........3
Jedwali Na. 2: Mifumo Inayotumika Kukusanya Taarifa za Magonjwa ....... 28
Jedwali Na. 3: Uchambuzi wa Vifaa Tiba kwa ajili ya Uchunguzi wa Matatizo ya Mfumo wa Fahamu............................................ 31
Jedwali Na. 4: Uwiano wa Madaktari Bingwa wa Mfumo wa Fahamu wa Watoto Wenye Matatizo ya Mfumo wa Fahamu katika Mikoa Iliyotembelewa .................................................. 33
Jedwali Na. 5: Ulinganisho wa Madaktari Bingwa/Wenye Ujuzi katika Ngazi za Vituo vya Afya Vilivyotembelewa ............................... 34
Jedwali Na. 6: Hali ya Upatikanaji wa Huduma za Urekebu .................. 35
Jedwali Na. 7: Hali ya Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Maghala ya Bohari ya Dawa......................................................... 38
Jedwali Na. 8: Usahihi wa Makadirio ya Dawa Muhimu ........................ 39
Jedwali Na. 9: Thamani ya Jumla ya Makadirio ya Mahitaji ya Dawa Muhimu Ikilinganishwa na Matumizi Halisi ............................... 42
Jedwali Na. 10: Hali ya Rasilimaliwatu katika Ofisi ya Msajili wa Msaada wa Huduma za Kisheria ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria (2021/22 – 2023/24) ............................................ 73
Jedwali Na. 11: Fedha Zilizotengwa kwa ajili ya Huduma za Msaada wa Kisheria katika Wizara ya Katiba na Sheria kwa Kipindi cha 2021/22 – 2024/25...................................................... 74
Jedwali Na. 12: Upatikanaji wa Huduma za Malezi ya Wazee Kila Mkoa ..... 75
Jedwali Na. 13: Tathmini ya Vibali Vilivyotolewa kwa ajili ya Makazi ya Wazee Katika Nyumba Zilizotembelewa ............................... 78
Jedwali Na. 14: Mikakati Inayohusiana na Usimamizi wa Hifadhi ya Nafaka . 90
Jedwali Na.15: Uchambuzi wa Bajeti na Kiasi Kilichotumika katika Shughuli za Ununuzi wa Nafaka Mwaka 2022/23-2024/25 ................. 94
Jedwali Na. 16: Uhusiano kati ya Viwango vya Akiba na Mfumuko wa Bei ya Chakula ......................................................... 97
Jedwali Na. 17: Nafaka Zilizokaa Zaidi ya Muda Unaotakiwa................... 99
Jedwali Na. 18: Uchakavu wa Maghala na Uwezo Halisi Unaoweza Kutumika hadi Mwaka 2024/25 ...........................................100
Jedwali Na. 19: Uhusiano wa Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi Pamoja na Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano . 105
Jedwali Na. 20: Ongezeko la Maeneo ya Kazi ambayo Hayakusajiliwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi ...........................110
Jedwali Na. 21: Faini ambazo Hazikukusanywa kutoka kwenye Maeneo ya Kazi Yasiyo na Vyeti vya Usajili .......................................111

Jedwali Na. 22: Tozo za Riba Ambazo Hazijawasilishwa kutoka kwa Waajiri Wasiozingatia Sheria .......... 121
Jedwali Na. 23: Upatikanaji wa Miundombinu ya Matibabu ya Majitaka katika Mamlaka za Huduma za Maji .......... 131
Jedwali Na. 24: Ufikiaji wa Viwango vya Ubora wa Majitaka .......... 134
Jedwali Na. 25: Namba ya Mamlaka za Maji Zilizokuwa Zinatumia Tozo Zilizoisha Muda wake katika Kanda nne Zilizotembelewa .. 137
Jedwali Na. 26: Vigezo vya Ubora wa Maji ambavyo Havikupimwa wakati wa Ukaguzi wa Ubora wa Maji na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji .......... 140
Jedwali Na. 27: Uhusiano kati ya Usimamizi wa Mfumo wa Usafirishaji na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu .......... 143
Jedwali Na. 28: Uchambuzi wa Uwepo wa Michepuko na Njia za Kukwepa Mizani .......... 160
Jedwali Na. 29: Idadi ya Matengenezo ya Dharura katika Mizani Zilizochaguliwa .......... 162
Jedwali Na. 30: Uchambuzi wa Kina wa Mipango Kabambe ya Usafirishaji Katika Miji Mikubwa .......... 165
Jedwali Na. 31: Idadi ya Kesi za Watoa Huduma Waliokamatwa Wakiwa Wamebadili Njia Walizosajiliwa Kutoa Huduma .......... 168
Jedwali Na. 32: Ulinganisho Kati ya Ukuaji wa Jiji na Utanuzi wa Miundombinu ya Usafirishaji .......... 170
Jedwali Na. 33: Uhusiano wa Utunzaji wa Mazingira na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano .......... 179
Jedwali Na. 34: Mikakati na Jitihada za Serikali katika Utunzaji wa Mazingira .......... 180
Jedwali Na. 35: Utoaji wa Fedha kwa ajili ya Kuwezesha Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira .......... 184
Jedwali Na. 36: Ujumuishaji wa Viashiria vya Mpango Mkakati wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira katika Mipango ya Utekelezaji ya Mwaka .......... 191
Jedwali Na. 37: Uzalishaji wa Miche Unoafanywa na Wakala wa Huduma za Misitu dhidi ya Mahitaji ya Serikali za Mitaa (2021/22-2024/25) .......... 196
Jedwali Na. 38: Mikakati na Jitihada za Serikali katika Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini .......... 213
Jedwali Na. 39: Hali ya Upitiaji wa Ripoti za Ushirikishwaji wa Wazawa ... 216

Jedwali Na. 40: Utendaji katika Eeo la Uongezaji Thamani ya Madini Nchini Kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/21- 2024/25 ................. 219
Jedwali Na. 41: Idadi ya Wajuzi wa Kigeni katika Migodi Iliyotembelewa Wakati wa Ukaguzi ..................................................... 220
Jedwali Na. 42: Hali ya Utoaji wa Ripoti Juu ya Ushirikishwaji wa Wazawa kutoka katika Sekta Nyeti za Uchumi Kwenda Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi ........................ 223
Jedwali Na. 43: Hali ya Ufanyikaji wa Vikao vya Kamati ya Kisekta ya Ushirikishwaji wa Wazawa katika Baraza la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi ............................................. 225
Jedwali Na. 44: Uhusiano Mahususi ya Utafutaji na Usimamizi wa Rasilimali Fedha na Mpango wa Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano .................... 229
Jedwali Na. 45: Uchambuzi wa Taarifa kwa Asilimia Upungufu wa Mchango wa Mapato Yasiyo ya Kodi kwenye Bajeti ......................... 237
Jedwali Na. 46: Uchambuzi wa Njia za Uratibu kwenye Usimamizi wa Mapato Yasiyo ya Kodi .................................................. 240
Jedwali Na. 47: Vipengele Vinavyopaswa Kuelezwa katika Utafiti kwa ajili ya Vyanzo Vinavyowezekana vya Mapato Yasiyo ya Kodi ....... 243
Jedwali Na. 48: Baadhi ya Vyanzo vya Mapato ambavyo Havikuibuliwa ..... 244
Jedwali Na. 49: Mwelekeo wa Vyanzo, makadirio na Mapato Yaliyokusanywa na Wizara, Idara na Wakala (Sh. bilioni) ......................... 246
Jedwali Na. 50: Makadirio kwa Mashirika ya Umma Yaliyochaguliwa (Kiwango Sh. bilioni) ............................................................ 247
Jedwali Na. 51: Hali ya Mapitio ya Gharama kwa Mashirika ya Umma ....... 248
Jedwali Na. 52: Hali ya Mashine za Kukusanya Mapato kwenye Halmashauri Zilizotembelewa ................................................ 249
Jedwali Na.53: Kiwango cha Fedha za Rukuzu za Ununuzi wa Vitabu Kilichotakiwa na Kilichotengwa ............................... 252
Jedwali Na. 54: Fedha za Ruzuku ajili ya gharama za Shuleni zilizopaswa Kutengwa na zilizotengwa ..................................... 253
Jedwali Na. 55: Mwenendo wa Fedha za Ruzuku za Uendshaji Zinazopelekwa Shule za Msingi .................................................. 254
Jedwali Na. 56: Mwenendo wa Fedha za Ruzuku za Uendshaji Zinazopelekwa kwa Shule za Sekondari ....................................... 255
Jedwali Na. 57: Fedha zilizotenga na zilizotolewa kwa ajili ya Ununuzi wa Vitabu ......................................................... 256
Jedwali Na. 58: Utofauti kati ya Fedha Zilizopaswa Kutolewa na Zilizotolewa ............................................................ 257
Jedwali Na.59: Kiwango kilichotumika na kilichopaswa kutumika kwa Shule za Msingi ............................................................ 258

ISO 9001:2015 Certified

Jedwali Na. 60: Kiwango kilichotumia na kilichopaswa kutumika kwa Shule za Sekondari ........................................................ 258
Jedwali Na. 61: Mtiririko wa Ununuzi wa Vitabu kwa Shule za Mtaala wa Kingereza ........................................................ 259
Jedwali Na. 62: Mtiririko wa Vitabu vya Mtaala wa Kingereza Vilivyoagizwa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ................................ 260
Jedwali Na. 63: Utofauti wa Idadi na Thamani Vitabu Vilivyoagizwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Vilivyosambazwa na Taasisi ya Elimu Tanzania ................................................... 260

ISO 9001:2015 Certified

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1: Kanuni za Ukaguzi wa Ufanisi ........................................1
Kielelezo Na. 2: Mpangilio wa Sura Zilizounda Ripoti Hii ...........................7
Kielelezo Na. 3: Uhusiano wa Mikakati na Mipango ya Kitaifa.....................9
Kielelezo Na.4: Maelezo kwa Ufupi ya kila Maudhui Mahususi Kutoka kwenye Mipango ya Maendeleo ya Taifa .................................. 10
Kielelezo Na.5: Miongozo Muhimu na Mfumo wa Kisheria katika Usimamizi wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano ..................................................................... 13
Kielelezo Na.6: Watendaji Muhimu na Majukumu Yao katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano .............. 14
Kielelezo Na. 7: Muhtasari wa Mikakati ya Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano .................................................. 15
Kielelezo Na.8: Kaguzi za Ufanisi Zilizofanyika Zikihusianishwa na Maudhui ya Malengo ya Maendeleo Endelevu Pamoja na Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano............................ 19
Kielelezo Na.9: Uhusiano kati ya Mipango ya Kitaifa ya Maendeleo, Malengo ya Maendeleo Endelevu, na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Utoaji wa Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu ........................................................ 23
Kielelezo Na.10: Mipango na Mikakati inayohusiana na Upatikanaji wa Dawa Muhimu ......ISO 9001:2015 Certified................................. 24
Kielelezo Na.11: Uhusiano kati ya Utoaji wa Huduma za Afya ya Uzazi na Malengo ya Maendeleo Endelevu, na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ................................ 25
Kielelezo Na.12: Upatikanaji wa Wataalamu wa Kuchunguza Matatizo ya Mfumo wa Fahamu ........................................................ 30
Kielelezo Na.13: Hali ya Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya vya Umma ............................................................. 37
Kielelezo Na.14: Juhudi za Serikali katika Utoaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii na Huduma za Kisheria........................................... 64
Kielelezo Na.15: Mtawanyiko wa Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria Kikanda Nchini............................................................. 67
Kielelezo Na. 16: Kiwango cha Taarifa Katika Ripoti za Utafiti wa Kijamii ... 77
Kielelezo Na.17: Ulinganifu wa Gharama Iliyotumika kwa Tani na Kiasi Kilichonunuliwa .................................................... 93
Kielelezo Na.18: Hali ya Ufikiaji wa Kiwango cha Akiba ya Chakula Kilichotakiwa Kuwapo Kila Mwisho wa Mwaka.................................. 96

Kielelezo Na.19: Mikakati katika Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi ........................................................ 106
Kielelezo Na. 20: Mwenendo Usio thabiti wa Kupungua kwa Vifo Mahali pa Kazi ................................................................ 108
Kielelezo Na. 21: Ukaguzi Usioridhisha wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi katika Maeneo ya Kazi Yaliyosajiliwa .................................. 112
Kielelezo Na. 22:Muhtasari wa Kuchelewa Kufanyika kwa Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi baada ya Usajili ............................................ 113
Kielelezo Na. 23:Idadi ya Maeneo ya Kazi Ambayo Hayakukaguliwa .......... 114
Kielelezo Na. 24:Kiwango cha Madai Yaliyolipwa Fidia Ikilinganishwa na Madai Yaliyosajiliwa Kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25 ................................................................ 116
Kielelezo Na.25:Wastani wa Siku Zinazotumiwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi Kushughulikia Madai Kamili na Halali ........... 118
Kielelezo Na.26: Muda Unaotumika kuanzia Usajili hadi Hatua ya Dai Lililo Tayari kwa Mafao ........................................................ 119
Kielelezo Na.27: Maeneo Yanayopendekezwa kwa ajili ya Maboresho ya Huduma za Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ............................ 122
Kielelezo Na.28:Uelewa wa Wafanyakazi kuhusu Taratibu za Madai .......... 123
Kielelezo Na.29:Muhtasari wa Mikakati na Juhudi za Serikali Kuhusiana na Udhibiti wa Huduma za Maji .................................... 127
Kielelezo Na.30: Idadi ya Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Zilizofanikisha Utoaji Huduma za Maji kwa Asilimia 84 katika Maeneo Yao ya Huduma............................................... 130
Kielelezo Na. 31: Kiwango cha Ufuataji wa Viwango vya Ubora wa Maji ..... 133
Kielelezo Na.32:Mamlaka za Maji safi na Usafi wa Mazingira Zilizofikia Uwiano Unaotakiwa kuazia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2023/24138
Kielelezo Na.33:Mikakati ya Serikali Iliyowekwa Kusimamia Mfumo wa Usafirishaji.......................................................... 145
Kielelezo Na.34: Jitihada za Serikali Katika Usimamizi wa Mfumo wa Usafirishaji ................................................................ 146
KielelezoNa.35:Kiwango cha Mahitaji ya Matengenezo ya Barabara Kilichoshughulikiwa na Mpango wa Mwaka wa Matengenezo ya Barabara ........................................................ 150
Kielelezo Na.36: Muda Uliotumiwa Kusuburia Usafiri wa Mabasi ya Mwendokasi Katika Kuchukua Abiria na Muda Yanaotumia Kufika Mwisho wa Safari ........................................................... 173
Kielelezo Na. 37: Kiwango cha Matumizi ya Mitambo ya Kuzalisha Umeme .. 206
Kielelezo Na.38: Idadi ya Mipango ya Ushirikishwaji wa Wazawa Iliyoidhinishwa dhidi ya Idadi ya Kaguzi zilizofanywa na Tume ya Madini ... 215

ISO 9001:2015 Certified

Kielelezo Na.39:Hali ya Utoaji Ripoti ya Ushirikishwaji wa Wazawa katika Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi .................... 222
Kielelezo Na.40:Mikakati ya Serikali kuhusu Usimamizi Ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi na Fedha za Ruzuku za Uendeshaji wa Shule za Umma ............................................................ 231
KielelezoNa.41:Uchambuzi wa Malengo na Kiwango Kilichokusanywa cha Mapato Yasiyo ya Kodi .................................................... 234
Kielelezo Na.42:Uchambuzi wa Makadirio na Kiwango Kilichokusanywa cha Mapato Yasiyo ya Kodi ........................................... 235
Kielelezo Na. 43: Uchambuzi wa Bajeti Kulingana na Vyanzo vya Mapato ... 236
Kielelezo Na. 44: Asilimia ya Mchango wa Mapato Yasiyo ya Kodi kwenye Bajeti ya Taifa ........................................................... 236
Kielelezo Na. 45: Uchambuzi wa Upungufu na Athari Zake ..................... 239
Kielelezo Na. 46: Kuongezeka kwa Mtiririko wa Utolewaji wa Fedha kwa ajili ya Ununuzi wa Vitabu................................................ 256

ISO 9001:2015 Certified

## SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Nina furaha kuwasilisha Ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi wa Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2025. Ripoti hii inajumuisha ripoti 18 za ukaguzi wa ufanisi, ambazo zinachambua kwa kina juhudi za Serikali katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu, sambamba na malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Uchambuzi umejikita katika utoaji wa huduma za afya; utoaji wa huduma za ustawi wa jamii na huduma za kisheria kwa wananchi; usimamizi wa uhifadhi wa nafaka za kimkakati; na usimamizi wa usalama mahali pa kazi na utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi. Maeneo mengine ni udhibiti wa huduma za maji; usimamizi wa mfumo wa usafirishaji; utunzaji wa mazingira; usimamizi wa taratibu za ushirikishaji wa wazawa katika sekta ya madini; na utafutaji na usimamizi wa rasilimalifedha. Kwa kubainisha mafanikio yaliyopatikana pamoja na upungufu wa kiutendaji, ripoti hii inatoa mwongozo wa kimkakati wa kuimarisha uwezo wa nchi kushindana kiuchumi na kijamii na nchi zingine na usimamizi madhubuti wa rasilimali za umma.

Ninaipongeza Serikali, chini ya uongozi mahiri wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa dhamira yake thabiti ya kuimarisha uwajibikaji, uwazi, na ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za umma. Taifa letu linategemea taasisi za umma kutoa na kudumisha miundombinu muhimu pamoja na kutekeleza programu zinazochochea fursa za kiuchumi. Hivyo, uhusiano uliojengwa katika kuamianiana kati ya wananchi na Serikali yao ni muhimu katika kudumisha mshikamano wa kijamii na kufanikisha matarajio ya kitaifa.

Kama Ofisi ya Ukaguzi, tunafanya kazi kwa ushirikiano na serikali ili kukuza katika sekta za umma utamaduni unaojengwa kwa kuzingatia utendaji bora, uwajibikaji, uwazi, na uadilifu.

Matokeo ya ukaguzi yaliyowasilishwa katika ripoti hii yanaonesha jinsi rasilimali za umma na mipango inavyosimamiwa katika taasisi zilizokaguliwa. Ingawa kuna maeneo yaliyoonesha utendaji mzuri na matumizi bora ya rasilimali, bado taasisi kadhaa zilikabiliwa na changamoto zilizoathiri ufanisi wa kiutendaji na uwezo wa kutoa huduma. Hivyo, ni muhimu kwa Serikali na wadau kushughulikia maeneo yaliyobainika kuwa na upungufu ili kuimarisha ufanisi, uwazi, na uwajibikaji wa taasisi za umma.

Mashirika au taasisi zenye athari kubwa kwa ustawi wa wananchi zinapaswa kuhakikisha kuwa utoaji wa huduma zao ni wenye ufanisi na tija. Ni lazima

kuweka kipaumbele katika kuchukua hatua zinazoboresha michakato ya uendeshaji ili kuzuia upotevu wa fedha za umma na kuhakikisha kuwa kila rasilimali inatumika kikamilifu kwa manufaa ya Watanzania wote.

Ninawasihi maafisa masuuli wote, bodi za mashirika, na mamlaka za usimamizi kutekeleza mapendekezo niliyoyatoa Katika ripoti hii ili kuimarisha uwajibikaji na kuwa na maboresho endelevu katika utoaji wa huduma. Aidha, nalihimiza Bunge na wadau wote kuchukua hatua kulingana na taarifa zilizomo katika ripoti hii ili kuboresha matumizi ya rasilimali za umma na kuongeza athari chanya za mipango ya maendeleo ya taifa.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inaendelea kutekeleza jukumu lake kwa weledi, uhuru, na uadilifu. Kuwapo kwa taasisi imara na zinazowajibika ni muhimu ili kudumisha imani ya wananchi wetu.

Mwisho, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa bidii na weledi usioyumba, ambao ndio msingi wa taasisi hii. Kujitoa kwao ndiko kunafanikisha jukumu letu la kikatiba.



**Charles E. Kichere**
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## MUHTASARI

1. Taarifa hii ya jumla ya ukaguzi inaelezea upungufu uliobainika, hitimisho, pamoja na mapendekezo katika ripoti 18 za ukaguzi wa ufanisi zilizofanyika kwa mwaka 2025. Ripoti hizo zinahusu Utoaji wa Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu na Neva kwa Watoto; Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya vya Umma; Utoaji wa Huduma za Afya ya Uzazi; Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria kwa Wananchi Wasiojiweza; Utoaji wa Chakula, Makazi na Huduma za Malezi kwa Wazee; Usimamizi wa Hifadhi ya Nafaka za Kimkakati; Usimamizi wa Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi; Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi; Udhibiti wa Huduma za Maji; Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Mchakato wa Upangaji wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Barabara; Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Uendeshaji wa Mizani; Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Huduma za Usafiri Mjini katika Majiji Makubwa; Ukaguzi wa Ufanisi katika Utekelezaji wa Miradi ya Nishati Jadidifu; Ukaguzi wa Ufanisi katika Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi; Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Shughuli za Urejeshaji Misitu; Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini; Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya Kodi; Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji wa Shule za Umma.

2. Ripoti hii ni muhtasari wa matokeo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi na tathmini ya kina iliyofanyika kutoka kwenye ripoti hizi 18 za ukaguzi wa ufanisi. Pia, ripoti hii imehusisha matokeo tarajiwa na mchango wake kwenye malengo yaliyowekwa kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26), na ulingano wake kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu. Kwa kuainisha maeneo muhimu ambayo yameonekana katika sekta tofauti, na kutathmini ufanisi wa taasisi za umma, ripoti hii ya jumla inalenga kuleta mafanikio na kutambua umuhimu wa shabaha za mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo ya rasilimali-watu kwenye mipango ya maendeleo. Vilevile, inatoa mchanganuo wa kina kuhusu namna usimamizi wa shuguli za kisekta unavyochochea ufikiwaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo ya Taifa na Malengo ya Maendeleo Endelevu, hatimaye kutoa mwongozo wa maboresho ya kimkakati na utungaji wa sera.

3. Hata hivyo, ripoti hii haikusudii kuwa mbadala wa ripoti 18 huru zilizoandaliwa. Msomaji anashauriwa kusoma ripoti za ukaguzi husika kama zilivyobainishwa hapo juu ili kupata taarifa zaidi.

**Matokeo ya Ukaguzi**

**(i) Utoaji wa Huduma za Afya**

4. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, huduma za afya ya mfumo wa fahamu hazipatikani katika vituo vya kutolea huduma ya afya vya ngazi ya kati na ya msingi. Ukaguzi umebaini kuwa wagonjwa wasiokuwa na uwezo wa kugharimia usafiri kwenda katika hospitali za rufaa za kanda walipatiwa matibabu bila kufanyiwa uchunguzi wa kina. Upungufu katika utoaji wa huduma za afya ya mfumo wa fahamu kwa watoto umesababishwa na uchunguzi usioridhisha wa watoto wenye matatizo ya mfumo wa fahamu pamoja na kutokuwapo kwa matibabu bora kunakosababishwa na uhaba wa wataalamu waliobobea katika matatizo ya mfumo wa fahamu. Hali hii ilidhihirika kupitia uwiano usio sawa baina ya daktari wa watoto na watoto husika, ambapo katika Mkoa wa Dar es Salaam uwiano ulikuwa 1:10,627, ikilinganishwa na mikoa mingine kama vile Rukwa wenye uwiano wa 1:429,805 hali inayoonesha utofauti wa takribani mara 40. Aidha, kulikuwapo na uhaba wa mara kwa mara wa dawa muhimu za matatizo ya mfumo wa fahamu, changamoto za uwezo wa kumudu gharama za dawa hizo, pamoja na upungufu wa huduma za urekebishaji. Pia, nilibaini kuwapo kwa takwimu zisizojitosheleza za maamuzi sahihi kuhusu utoaji wa huduma za afya ya mfumo wa fahamu.

5. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, kasi ya kupungua kwa kiwango cha vifo vya akina mama iliendelea kuwa ndogo kiasi cha kuathiri ufikiwaji wa shabaha namba 3.1 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu, yanayolenga kupunguza uwiano wa vifo vya mama wanaojifungua hadi kufikia vifo 70 kwa kila vizazi hai 100,000. Aidha, idadi ya vifo vilivyobainishwa imeendelea kubaki ileile tangu mwaka 2023, ambapo jumla ya vifo 346 viliripotiwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2025, vikiathiri zaidi wanawake wenye umri wa kati ya miaka 20 mpaka 34. Kwa kiasi kikubwa, vifo hivyo vinasababishwa na hali zinazoweza kuzuilika kama vile kutokwa na damu nyingi baada ya kujifungua na shinikizo la juu la damu wakati wa ujauzito. Vilevile, ukaguzi wangu ulibaini utekelezaji usioridhisha wa jitihada za kupunguza vifo vya akina mama unaofanywa na Wizara ya Afya na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hali iliyodhihirishwa na matumizi duni ya huduma za kliniki ya wajawazito na huduma za baada ya kujifungua, pamoja na uhaba wa wahudumu wa afya wenye ujuzi wa kusaidia kujifungua katika mikoa iliyochaguliwa kama sampuli.

6. Ukaguzi wangu pia ulibaini kuwa, upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya afya vya umma ulikuwa kati ya asilimia 47 na 62 katika miaka ya fedha ya 2022/23 na 2024/25 mtawalia, kiwango ambacho kilikuwa chini ya lengo la

asilimia 79. Upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya afya vya umma haukuwa wa kuridhisha kutokana na utekelezaji usioridhisha wa mchakato wa uagizaji dawa kutoka katika Bohari ya Dawa. Ilibainika kuwa utekelezaji wa mchakato wa uagizaji dawa muhimu ulikuwa kati ya asilimia 31 kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/22 na asilimia 67 kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/25. Upungufu wa upatikanaji wa dawa muhimu umezuia utoaji wa huduma za afya zilizokusudiwa kwa wakati kwa wananchi.

**(ii) Utoaji wa Huduma kwa Wazee na Huduma za Kisheria kwa Wananchi**

7. Ukaguzi wa ufanisi kuhusu huduma za msaada wa kisheria na huduma za wazee unaonesha kuwa, mifumo ya utoaji wa msaada wa kisheria ya Tanzania inafanya kazi kwa kiwango cha chini na kuwaacha mamilioni ya wananchi wasio na uwezo bila kupata haki au mahitaji ya msingi. Msaada wa kisheria unatolewa kwa namna isiyo sawa na umelenga zaidi mijini ambapo karibu asilimia 30 ya watoa huduma wako katika mkoa wa Dar es Salaam, huku usajili wa wasaidizi wa msaada wa sheria na watoa huduma ukishuka idadi na wengi wakifanya kazi kwa vyeti vilivyoisha muda na bila usimamizi wa kutosha. Vilevile, mfumo wa huduma za kijamii kwa wazee unawafikia asilimia 0.08 tu ya wazee waliotambuliwa kuwa wenye uhitaji. Hii ina maana kuwa, asilimia 99.92 ya wazee wenye uhitaji hawapati msaada wowote rasmi. Makazi ya wazee yanayomilikiwa na serikali yanakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi kwa asilimia 67, kukosekana kwa wataalamu kama vile wauguzi na wataalamu wa lishe pamoja na kuwa na majengo chakavu ambayo hayakubuniwa kwa mahitaji ya wazee. Aidha, wazee wanaoishi katika makazi hayo wanakabiliwa na bajeti ndogo ya chakula, utoaji wa huduma za bima ya afya usiotosheleza, na upungufu mkubwa wa vifaa hususani kwa wenye mahitaji maalumu kama vile vifaa vya kusaidia kusikia na fimbo za kutembelea. Upungufu huu umesababishwa na utekelezaji usioridhisha wa shughuli za ufuatiliaji, kukosekana kwa hati miliki kunakochochea uvamizi wa maeneo ya makazi, na kukosekana kwa mfumo jumuishi wa usimamizi. Mambo haya yote yanadhoofisha kufikiwa kwa malengo ya maendeleo ya taifa na kufikia mahitaji ya msingi kwa wananchi wenye uhitaji.

**(iii) Usimamizi wa Uhifadhi wa Nafaka za Kimkakati**

8. Ukaguzi ulibaini upungufu katika ununuzi wa nafaka za kimkakati, ambapo ni asilimia 58 tu ya malengo ya ununuzi wa nafaka yalifikiwa. Hali hii ilisababishwa na utoaji wa fedha usioridhisha kwa kuwa ni asilimia 51.2 tu ya bajeti iliyopangwa ndiyo iliyotolewa kwa miaka minne ya fedha, yaani kutoka Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2023/24. Pia, ukaguzi wangu ulibaini kuwa,

kiwango cha uhifadhi wa nafaka za kimkakati kilichokuwapo mwishoni mwa mwaka kilikuwa chini ya kiwango kinachohitajika cha tani 150,000 na hivyo kushindwa kupambana na mfumuko wa bei. Pia, ukaguzi wangu ulibaini kuwa, uwezo wa kuhifadhi nafaka za kimkakati ulikuwa tani 303,000, ambayo ni sawa na asilimia 43 ya lengo la tani 700,000 chini ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano. Hii ilipunguza ufanisi wa uhifadhi wa nafaka za kimkakati katika kuleta uhimilivu wa bei ya chakula na kuhakikisha usalama wa chakula na hivyo kuhatarisha kufikiwa kwa Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu.

### (iv) Usimamizi wa Usalama Mahali pa Kazi na Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi

9. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi haukusajili asilimia 79 ya maeneo ya kazi 179,196 yaliyotambuliwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Usajili usioridhisha wa maeneo ya kazi umetokana na ushirikiano usiojitosheleza kati ya Wakala wa Usalama Mahali pa Kazi na taasisi zingine za serikali katika kubadilishana taarifa za maeneo ya kazi. Matokeo yake, wafanyakazi walioko katika maeneo ya kazi yasiyosajiliwa waliachwa katika hatari ya vihatarishi visivyotambuliwa, jambo lililoongeza uwezekano wa kutokea kwa ajali na magonjwa yatokanayo na kazi.

Vilevile, ukaguzi wangu ulibaini kuwa, kiwango cha malipo cha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kwa Madai yaliyosajiliwa kilishuka kutoka asilimia 81 kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi asilimia 53 kwa Mwaka wa Fedha 2024/25. Kushuka kwa kiwango cha madai yaliyolipwa ikilinganishwa na madai yaliyosajiliwa kulisababishwa na ongezeko la asilimia 33 la idadi ya madai yaliyosajiliwa, kukataliwa kwa madai kutoka asilimia 17 kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi asilimia 10 Mwaka wa Fedha 2024/25, na ucheleweshaji wa ushughulikiwaji wa madai. Mambo haya yalisababisha ucheleweshaji kwenye uidhinishaji na ulipaji wa madai ya fidia.

### (v) Udhibiti wa Huduma za Maji

10. Katika ukaguzi huu nilibaini kuwa, mamlaka nyingi za Maji hazikufikia malengo ya utoaji huduma ya maji, ambapo asilimia tisa tu kati ya mamlaka za maji 82 zilifikisha kiwango kusudiwa cha asilimia 84 cha utoaji wa huduma za maji. Ukaguzi pia ulibaini kuwa, ni asilimia 30 tu ya mamlaka za maji zina miundombinu ya kutibu majitaka. Pia, nilibaini kuwa, uzingatiaji wa ubora wa maji na viwango vya utoaji wa majitaka kwenda kwenye mazingira havikufikiwa kikamilifu. Hali hii ni pamoja na kutofuata vigezo muhimu vya ubora kama vile

kuwapo kwa mabaki ya klorini katika maji yaliyosambazwa kwa wananchi, ambapo ni asilimia saba tu ya mamlaka za usambazaji maji zilifikia kiwango kinachohitajika. Pia, utoaji wa majitaka haukufikia viwango vinavyotakiwa vya mahitaji ya oksijeni ya kibiolojia na mahitaji ya oksijeni ya kikemikali, hali iliyosababisha athari kwa afya ya jamii na ulinzi wa mazingira. Kadhalika, ukaguzi ulibaini uandaaji, ufuatiliaji, na utekelezaji wa bei za huduma za maji usiojitosheleza, hali iliyochangia asilimia 78 ya mamlaka za maji 59 katika kanda nne zilizotembelewa kutumia bei zilizoisha muda wake. Vilevile, ukaguzi wangu ulibaini kuwa, shughuli za ufuatiliaji hazikufanyika kikamilifu. Mathalani, nimebaini kuwa wakati wa ufuatiliaji wa vigezo muhimu vya ubora wa maji kama vile aseniki, amonia, na bariamu havikupimwa. Hii inaathiri ufikiwaji wa lengo la 6 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo mwaka 2030 na malengo ya upatikanaji wa huduma ya maji kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano ifikapo 2025/26.

### (vi) Usimamizi wa Mfumo wa Usafirishaji

11. Nilibaini kuwa, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi, na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hazikuhakikisha usimamizi madhubuti wa mfumo wa usafiri nchini. Mathalani, nilibaini katika kupanga maboresho ya miundombinu ya barabara, mahitaji hayakutambuliwa ipasavyo au kuwekewa vipaumbele, na hivyo kusababisha matokeo madogo katika kuboresha hali ya barabara kutokana na miradi iliyokuwa ikitekelezwa. Aidha, imegungulika kuwa mifumo ya uendeshaji wa shughuli za mizani barabarani haifanyi kazi kwa kusomana. Pia, matengenezo kinga na udhibiti havikujitosheleza, sababu zinazoweza kutumika kukwepa mizani, hivyo kudhoofisha udhibiti wa uzito wa magari. Kadhalika, katika maeneo ya mijini, nilibaini kutowapo kwa uwiano katika upangaji wa usafiri wa mijini, udhibiti usiojitosheleza, muunganiko wa miundombinu ya usafirishaji usiojitosheleza, na uzingatiaji usiojitosheleza wa makundi yenye mahitahi maalumu, ambayo yote kwa pamoja yalizuia ufikiwaji na ufanisi.

### (vii) Utunzaji wa Mazingira

12. Matokeo ya ukaguzi yanaonesha kwamba, juhudi za nchi ya Tanzania katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, urejeshaji misitu, na miradi ya nishati jadidifu hazikutekelezwa kikamilifu, jambo lililopunguza uwezo wa nchi kushughulikia changamoto za kimazingira. Hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika sekta za maji, kilimo, na nishati zilitekelezwa kwa asilimia 43, 44, na 52 mtawalia. Hii ilisababishwa na upungufu wa rasilimali fedha, uratibu usiojitosheleza, utoaji wa taarifa usioridhisha, na ufuatiliaji

usiojitosheleza. Zaidi ya hayo, shughuli za urejeshaji misitu pia hazikufanyika kwa ufanisi, kwani wastani wa upotevu wa misitu ulifikia hekta 376,970 kwa mwaka. Pia, nimebaini kuwapo kwa kiwango cha chini cha mti kustawi na kukua baada ya kupandwa kutokana na mipango isiyokidhi mahitaji, uratibu usioridhisha, na usimamizi usiojitosheleza.

13. Aidha, ukaguzi wangu kuhusu utekelezaji wa miradi ya nishati jadidifu ulibaini kuwa, miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka katika mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere ilikuwa imefikia asilimia 55.37 pekee licha ya mradi huo kukamilika na kuwa tayari kwa uzalishaji kamili ukiwa na uwezo wa kufua umeme wa megawati 2,115. Kuchelewa kukamilika kwa miundombinu ya usafirishaji wa umeme katika mradi huu kumesababisha megawati 1,175 kutoingizwa kwenye matumizi, kiasi hiki cha umeme ni sawa na mitambo mitano ya kuzalisha umeme, kila mmoja ukiwa na uwezo wa kuzalisha megawati 235.

**(i) Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini**

14. Nilibaini kuwa, usimamizi wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini uliochangia ongezeko la asilimia 171 la ajira za wazawa kati ya mwaka 2020 na mwaka 2024. Hata hivyo, kulikuwa na ongezeko la asilimia 63 ya waajiriwa wa kigeni katika kipindi hicho. Zaidi ya hayo, nilibaini utofauti wa mishahara kwani waajiriwa wa kigeni walilipwa mishahara mikubwa zaidi ya waajiriwa wazawa walio katika nyadhifa za kiutendaji zinazofanana. Vile vile, nilibaini kuwa, kutoka mwaka 2020 hadi 2024, jumla ya thamani ya ununuzi wa huduma na bidhaa za kitanzania ilikuwa asilimia 33, wakati thamani ya ununuzi wa huduma na bidhaa za kigeni ilikuwa asilimia 67. Mambo haya yanabainisha kuwapo kwa changamoto katika usimamizi wa taratibu za uwezeshaji wa wazawa katika sekta ya madini. Hali hii inasababisha kuendelea kuwategemea wataalamu na wazabuni wa kigeni, na kuwanyima fursa wazawa.

**(ii) Utafutaji na Usimamizi wa Rasilimali Fedha**

15. Kulikuwa na upungufu katika kutimiza malengo yaliyowekwa kuhusiana na ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi. Pia, uchangiaji wa mapato yasiyo ya kodi kwenye Bajeti ya Taifa hauridhishi kwa kuwa upo kati ya asilimia 6 hadi asilimia 6.9 kati ya Mwaka wa Fedha 2021 na 2024/25. Hii ilisababishwa na upungufu wa muundo wa taasisi, uwezo mdogo wa kusimamia ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, kutotambua ipasavyo vyanzo vipya vya mapato, mifumo na utaratibu usiyojitosheleza wa makadirio ya mapato yasiyo ya kodi, na

kutofuatilia na kutoa taarifa kuhusu utendaji wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi.

16. Kwa upande mwingine, nilibaini fedha za rukuzu za ununuzi wa vitabu hazikutengwa kwa utoshelevu. Pia, hakukuwa na uwiano katika utengaji wa fedha hizo za ruzuku za uendeshaji shule za msingi na sekondari. Kadhalika, ilibainika kupelekwa kwa kiasi kidogo na kisicho na uwiano sawa cha fedha za uendeshaji shule kila mwezi. Vilevile, utoaji wa fedha za ruzuku za uendeshaji shule haukujitosheleza na haukuwa sahihi. Aidha, ilibainika pia kuwapo kwa ununuzi wa vitabu kwa ajili ya wanafunzi ambao si walengwa.

**Hitimisho**

17. Kaguzi zangu zinatambua juhudi zinazofanywa na wakaguliwa katika kuboresha utendaji wao ili kufanikisha Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Maendeleo Endelevu, ambayo yanalenga kuleta mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Mathalani, juhudi zimeonekana katika maboresho ya utoaji wa huduma za afya, Utoaji wa Huduma za Malezi kwa Wazee na Huduma za Kisheria kwa Wananchi, Usimamizi wa Uhifadhi wa Nafaka za Kimkakati, Usimamizi wa Usalama Mahali pa Kazi na Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi, Udhibiti wa Huduma za Maji, Usimamizi wa Mfumo wa Usafirishaji, Utunzaji wa Mazingira, Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini, na Utafutaji na Usimamizi wa Rasilimali Fedha.

18. Pamoja na juhudi hizi, bado kulikuwa na changamoto kubwa zilizokwamisha ufikiaji wa malengo yaliyokusudiwa. Changamoto zilizobainika katika maeneo niliyokagua yanahitaji hatua za haraka ili kuoanisha juhudi za serikali na Malengo ya Maendeleo Endelevu, pamoja na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, ili kuhakikisha kuwapo kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na ya binadamu.

**Mapendekezo ya Ukaguzi**

19. Yafuatayo ni mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa:

(i) Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Bohari ya Dawa zinahimizwa kuhakikisha utoaji wa huduma unaojitosheleza za afya ya uzazi na huduma za afya ya mfumo wa fahamu, pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa dawa muhimu katika vituo vya afya vya umma;

(ii) Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, zinapaswa kuanzisha mfumo wa kitaifa wa huduma za malezi kwa wazee na msaada wa kisheria. Mfumo huu lazima uhakikishe utoaji wa msaada wa kisheria, utambuzi sahihi wa wazee wasiojiweza, pamoja na upatikanaji wa miundombinu ya kutosha katika nyumba za wazee. Kwa kushirikiana,na taasisi hizi zinaweza kuimarisha uwajibikaji, kuboresha upatikanaji wa haki na huduma za kijamii, pamoja na kulinda utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu;

(iii) Wizara ya Kilimo na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula wanashauriwa kuimarisha uratibu wa kimkakati wa ununuzi, uhifadhi, na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa gharama ili kuwezesha ununuzi wa nafaka na udhibiti wa ubora. Pia, wanashauriwa kufanya tathmini ya hali ya ghala na kuwa na ratiba za matengenezo pamoja na kuwa na ufuatiliaji thabiti wa nafaka zilizohifadhiwa ili kuhakikisha kiwango kinachotakiwa cha kuanzia mwaka kinafikiwa kwa kuzingatia ubora na wingi wa nafaka, na kuimarisha uwazi, ufanisi, na uendelevu katika usimamizi wa uhifadhi wa nafaka;

(iv) Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi zinahimizwa kuimarisha michakato ya usajili wa maeneo ya kazi, kutekeleza ukaguzi wa afya na usalama mahali pa kazi kwa kutumia mfumo wa vipaumbele vya vihatarishi. Pia, wanapaswa kuimarisha ugatuzi wa shughuli za Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi katika Ofisi zake za Kanda kwa kuweka malengo ya utendaji yaliyo wazi pamoja na mfumo wa ufuatiliaji;

(v) Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji inashauriwa kuboresha mfumo wake wa udhibiti kwa kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa masharti ya leseni, ufuatiliaji wa ubora wa maji na uandaaji wa tozo za maji kwa kuanzisha utaratibu mzuri wa kurekebisha hesabu kulingana na utekelezaji wa tozo iliyoisha wakati wa uandaaji wa tozo mpya na hivyo kuboresha ubora wa huduma, uendelezaji wa miundombinu, kutunza mazingira, na ufanisi wa udhibiti kwa jumla;

(vi) Wizara ya Uchukuzi na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI zinahimizwa kuboresha huduma za usafiri wa umma kwa kuhakikisha kuwa upangaji na utekelezaji wa mfumo wa usafiri mjini unazingatia uunganishaji wa miundombinu ya aina tofauti za usafiri, ushirikishaji wa makundi yote



ISO 9001:2015 Certified

yenye mahitaji maalumu na kuunganisha mifumo ya taarifa za usafiri mijini ili kuwezesha ufuatiliaji na udhibiti wa huduma kwa ufanisi;

(vii) Ofisi ya Makamu wa Rais - Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, na Wizara ya Nishati kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji zinahimizwa kuboresha usimamizi wa utunzaji wa mazingira kwa kuimarisha utekelezaji wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuboresha upangaji na utekelezaji wa shughuli za urejeshaji misitu, pamoja na kuhamasisha utekelezaji wa miradi ya nishati jadidifu ili kuhakikisha ulinganifu katika vyanzo vya nishati, unaoimarisha usalama na uendelevu wa nishati nchini;

(viii) Wizara ya Madini, Tume ya Madini, na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi zinahimizwa kuimarisha usimamizi wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa kwa kuendeleza viwanda vya ndani, kuboresha sera za urithishaji wa teknolojia, kuimarisha usimamizi na ukaguzi, pamoja na kuanzisha mfumo wa kisheria wa kitaifa utakaohakikisha kuwa shughuli za ufuatiliaji zinafanyika kikamilifu katika sekta zote; na

(ix) Wizara ya Fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI zianzishe utaratibu wa kutambua vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha udhibiti wa fedha zilizokopwa kwa ajili ya kufadhili miradi ya maendeleo na kutenga fedha za ruzuku kulingana na idadi ya wanafunzi waliosajiliwa ili kuhakikisha ukusanyaji na usimamizi wa rasilimali fedha zinafanyika ipasavyo.


## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI WA JUMLA

### 1.1 Usuli wa Ukaguzi wa Ufanisi

20. Ukaguzi wa ufanisi huchunguza iwapo shughuli, mipango, mifumo au miradi ya Serikali inayohusisha ukusanyaji au matumizi ya fedha za umma katika wizara, idara, mamlaka za serikali za mitaa, na mashirika ya umma inafanya kazi kwa kuzingatia kanuni tatu yaani uwekevu, ufanisi, na tija. Kanuni hizi ni kama zinavyooneshwa kwenye **Kilelezo Na. 1.**

**Kielelezo Na. 1: Kanuni za Ukaguzi wa Ufanisi**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kwa Taarifa Iliyotolewa kutoka katika Mwongozo wa Ukaguzi wa Ufanisi wa Mwaka 2022

21. Ukaguzi wa ufanisi pia unabainisha iwapo malengo yaliyowekwa mwanzoni mwa shughuli yalifikiwa. Taarifa hizi huwezesha kufahamu iwapo, kwa kiasi kikubwa, uwekevu, ufanisi, na tija ilizingatiwa wakati wa utekelezaji wa shughuli. Mapendekezo ya uboreshaji hutolewa kwenye maeneo yanayohisiwa kuwa na upungufu.

22. Ukaguzi wa ufanisi katika sekta ya umma ni muhimu kwa vile unalenga kukuza uwajibikaji, uwazi na utendaji kazi katika shughuli za Serikali ili wananchi wake wapate huduma bora na kwa wakati. Ukaguzi wa ufanisi hutumika pia kama msingi wa kujifunza na kufanya maboresho. Katika ukaguzi wa ufanisi, mambo mbalimbali huzingatiwa katika kuchagua maeneo ya kumakinikia. Mambo haya ni pamoja na malalamiko ya umma na umuhimu wa eneo hilo kuhusiana na maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

## 1.2 Mamlaka ya Kufanya Ukaguzi wa Ufanisi

23. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa mamlaka ya kisheria ya kufanya ukaguzi wa ufanisi na Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 kinaelekeza kuwa:

"Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa madhumuni ya kuzingatia wekevu, ufanisi, na tija ya matumizi yoyote ya rasilimali za taasisi, atahitaji taarifa, kuchunguza, na kutoa taarifa kadiri atakavyoona inafaa kuhusu:

(a) Matumizi ya fedha za umma na matumizi ya rasilimali kwa wizara, idara, wakala, mamlaka za serikali za mitaa, na mashirika na taasisi zingine zote za umma;

(b) Uendeshaji na ufanisi wa utendaji kazi wa maafisa masuuli, wakuu wa idara, na watendaji wakuu wa vyombo vyote hivyo; na

(c) Uzingatiaji wa sheria, kanuni na sera za mazingira na viwango vya ndani ya nchi.

## 1.3 Madhumuni ya Ripoti Kuu

24. Ripoti hii ya jumla inalenga kuwapa taarifa muhimu wabunge, Serikali, vyombo vya habari, umma, pamoja na wadau wengine ili waweze kufanya maamuzi yatakayoongeza uwekevu, tija, na ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za serikali.

25. Ripoti hii inabainisha masuala mbalimbali yaliyoonekana katika kaguzi za ufanisi dhidi ya yale yaliyotarajiwa, pamoja na mchango wake katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26) na kuyafikia Malengo ya Maendeleo Endelevu. Ripoti hii pia inawasilisha matokeo ya tathmini ya utendaji wa taasisi za serikali katika kutimiza majukumu yao katika Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka



ISO 9001:2015 Certified

Mitano (2016/17- 2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22– 2025/26) inayolenga kuleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu.

26. Maeneo yaliyoguswa katika ripoti hii ni pamoja na Utoaji wa Huduma za Afya, Utoaji wa Huduma za Malezi kwa Wazee na Huduma za Kisheria kwa Wananchi, Usimamizi wa Uhifadhi wa Nafaka za Kimkakati, Usimamizi wa Usalama Mahali pa Kazi na Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi, Udhibiti wa Huduma za Maji, Usimamizi wa Mfumo wa Usafirishaji, Utunzaji wa Mazingira na Usimamizi wa Mikakati ya Nishati Safi, Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini, na Utafutaji na Usimamizi wa Rasilimali Fedha.

27. Pia, ripoti inawasilisha matokeo ya tathmini ya kiwango ambacho shughuli za serikali zimechangia kufikia malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26) na Malengo ya Maendeleo Endelevu. **Jedwali Na. 1** linatoa muhtasari wa ripoti za ukaguzi wa ufanisi pamoja na taasisi zilizokaguliwa.

**Jedwali Na. 1: Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi na Taasisi Zilizokaguliwa**

| Ripoti ya Ukaguzi | Taasisi Iliyokaguliwa |
|---|---|
| Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya ya Umma | Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Bohari ya Dawa |
| Utoaji wa Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu na Neva kwa Watoto | Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| Utoaji wa Huduma za Afya ya Uzazi | Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria kwa Wananchi Wasiojiweza | Wizara ya Katiba na Sheria |
| Utoaji wa Chakula, Makazi na Huduma za Malezi kwa Wazee | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| Usimamizi wa hifadhi ya nafaka za kimkakati | Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula na Wizara ya Kilimo |
| Usimamizi wa ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi | Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi na Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano |
| Utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi | Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi. |
| Udhibiti wa Huduma za Maji | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji |
| Usimamizi wa Mchakato wa Upangaji wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Barabara | Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |

| Ripoti ya Ukaguzi | Taasisi Iliyokaguliwa |
|---|---|
| Usimamizi wa Uendeshaji wa Mizani | Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara Nchini |
| Usimamizi wa Huduma za Usafiri Mjini katika Majiji Makubwa | Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Uchukuzi |
| Utekelezaji wa Miradi ya Nishati Jadidifu | Wizara ya Nishati na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji |
| Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi nchini Tanzania | Ofisi ya Makamu wa Rais |
| Usimamizi wa Shughuli za Urejeshaji Misitu | Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini | Wizara ya Madini, Tume ya Madini, na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| Ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya Kodi | Wizara ya Fedha |
| Usimamizi wa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji wa Shule za Umma | Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi katika Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi Mwaka 2025

## 1.4 Mtazamo wa Ripoti ya Jumla

28. Ripoti hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa juhudi na shughuli mbalimbali za Serikali katika mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya rasilimali-watu kama zinavyohusishwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu sambamba na utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26).

29. Kwa kutambua umuhimu wa ajenda hii katika kuleta mabadiliko kwenye maisha ya wananchi, Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Umma za Ukaguzi lilijumuisha Malengo ya Maendeleo Endelevu kama kipaumbele mtambuka katika Mpango-mkakati wake wa Mwaka 2017 hadi 2022. Shirika lilitoa wito kwa wanachama wake kuchangia katika ufuatiliaji na mapitio ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ndani ya muktadha wa juhudi mahususi za maendeleo endelevu za kitaifa na mamlaka ya taasisi husika za ukaguzi.

30. Tanzania, kama nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa, inashiriki utekelezaji wa Ajenda ya Mwaka 2030. Ajenda hii inasisitiza kuwapo kwa mpango jumuishi wa hatua za kupata suluhisho la kiuchumi, kimazingira, na kijamii kwa ajili ya kufikia maendeleo endelevu unaojumuisha malengo 17 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Malengo ya Maendeleo Endelevu, pamoja na masuala mengine muhimu, yanaweka jitihada katika kukabiliana na umaskini na njaa, kupunguza ukosefu wa usawa, kujenga jamii zenye amani na haki, kukuza

usawa wa kijinsia, na kulinda maliasili. Kwa kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu ni kabambe na yanaingiliana, mafanikio na ufikiwaji wake ni mchakato mgumu na unahitaji ushirikiano wa pamoja.

31. Kadhalika, kuzinduliwa kwa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 kama nyenzo ya kuelekeza juhudi za kitaifa katika kufanikisha malengo ya kiuchumi na kijamii, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliandaa Mpango wa Muda Mrefu wa Mwaka 2011/12 hadi 2025/2026. Utekelezaji wa Mpango huu umegawanywa katika awamu kuu tatu za mpango wa maendelo wa miaka mitano inayolenga kuelekeza jitihada za kitaifa kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi ikiwa sambamba na kupunguza umaskini na na kuleta maendeleo ya watu.

32. Mipango ya taifa ya maendeleo ya miaka mitano inaingiliana na inaandaliwa kulingana na maudhui. Maudhui ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) ni "kukuza viwanda kwa mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu" na maudhui ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022–2025/2026) ni "kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu".

Mipango hii miwili inalenga kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 ambayo ina lengo la kuigeuza Tanzania kuwa nchi yenye hadhi ya uchumi wa kipato cha kati na kuendeleza mageuzi ya kuwa nchi ya viwanda kufikia mwaka 2025. Jitihada za kuondoa umaskini na kuboresha hali ya maisha, utawala bora, na uwajibikaji zimejumuishwa kwenye mipango hii miwili.

33. Kwa kuzingatia mamlaka na majukumu yake, taasisi za ukaguzi zina majukumu muhimu. Taasisi hizo ndio msingi wa kuwapo kwa taasisi zenye ufanisi, zinazowajibika, na shirikishi kwa maendeleo endelevu na zinazoweza kusaidia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Hivyo, ripoti hii ya jumla imetokana na uchambuzi uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kutoka kwenye kaguzi 15 za ufanisi zilizotathmini athari za shughuli za Serikali katika kuwezesha kufikiwa kwa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26), Malengo ya Maendeleo Endelevu, na Malengo ya Afrika ya Mwaka 2063.

## 1.5 Uhalali wa Ukaguzi

34. Kama moja ya nchi zilizosaini Ajenda ya Mwaka 2030 kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu, Tanzania imechukua hatua za kujumuisha ajenda hii

katika muktadha wa kitaifa. Wakati wa uanzishaji wa Ajenda ya Mwaka 2030, Tanzania ilikuwa ikiandaa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Hivyo, sehemu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu yaliakisiwa katika mpango huo.

35. Aidha, kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Tanzania imejiwekea matarajio ya kufanikisha lengo la kuwa na ukuaji wa uchumi kwa angalau asilimia 8 kwa mwaka. Viwango hivyo vya ukuaji vinachukuliwa kuwa muhimu katika kupunguza umaskini na kuisukuma Tanzania kutoka nchi isiyoendelea hadi nchi ya uchumi wa kipato cha kati yenye kiwango cha juu cha maendeleo ya binadamu. Dira ya Taifa ya Maendeleo ina maono ya kubadili uchumi ambao awali ulitegemea uzalishaji wa chini wa kilimo hadi kufikia uchumi wa kilimo wenye tija. Ili Malengo ya Maendeleo Endelevu yafikiwe, Serikali, Bunge, sekta binafsi, asasi za kiraia, na mtu mmojammoja, wanapaswa kutimiza wajibu wao.

36. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kama mkaguzi wa nje wa Serikali, ni kiungo muhimu katika kuhakikisha kuwa, Serikali inatekeleza wajibu wake wa kutoa huduma zinazohitajika kwa wananchi na kulijulisha Bunge kuhusu utendaji wa serikali na hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu yanafikiwa.

37. Hivyo, ili kuitikia wito huo wa kuchangia kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeunganisha ukaguzi wake wa ufanisi na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030. Kadhalika, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeunganisha ukaguzi wake wa ufanisi na maeneo ya vipaumbele na shughuli za kimkakati za Mpango wa Maendeleo ya Taifa ili kutathmini utekelezaji wake na kutoa mapendekezo ya maboresho zaidi. Baadhi ya malengo hayo yamegusiwa katika kaguzi 19 zilizofanyika.

## 1.6 Mchakato wa Uthibitisho wa Takwimu na Taarifa Zilizotolewa

38. Ukaguzi wa ufanisi ulifanywa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Ukaguzi kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi. Viwango hivyo vinaitaka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kupanga na kufanya ukaguzi ili kupata ushahidi wa kutosha na unaofaa utakaokuwa msingi mzuri wa matokeo, hitimisho, na mapendekezo kulingana na lengo au malengo ya ukaguzi.


39. Kwa kufuata kanuni za ukaguzi, wakaguliwa wote walipewa fursa ya kujadili na kutoa maoni yao kuhusu matokeo ya ukaguzi na kusahihisha makosa yaliyojitokeza katika rasimu ya ripoti hii. Wakaguliwa hao ni pamoja na Wizara ya Afya, Bohari ya Dawa; Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za

Mitaa; Wizara ya Katiba na Sheria; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu; Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula; Wizara ya Kilimo; Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi; Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano; Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi; Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji; Wizara ya Ujenzi; Wakala wa Barabara Nchini ; Wizara ya Uchukuzi; Wizara ya Nishati; Ofisi ya Makamu wa Rais; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Madini; Tume ya Madini; Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Wizara ya Fedha.

## 1.7 Muundo wa Ripoti

40. Ripoti hii ina sura 12 kama zinavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 2**:

**Kielelezo Na. 2: Mpangilio wa Sura Zilizounda Ripoti Hii**



# SURA YA PILI

# MAELEZO YA MPANGO WA PILI NA WA TATU WA MAENDELEO YA TAIFA WA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU


## 2.1 Utangulizi

41. Sura hii inahusu maelezo ya Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Masuala muhimu yanayojumuishwa katika sura hii ni pamoja na mfumo wa kisheria na miongozo inayosimamia utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano; wahusika wakuu katika utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; na mikakati ya utekelezaji wa Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Masuala mengine yanayojumuishwa ni uhusiano uliopo baina ya kaguzi za ufanisi zilizofanyika na mipango ya maendeleo ya taifa ya miaka mitano na malengo ya maendeleo endelevu; na mifumo ya ufadhili katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya taifa ya miaka mitano.

## 2.2 Usuli kuhusiana na Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

42. Mwaka 1999 Tanzania ilizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 ambayo ni nyenzo ya kuunganisha juhudi za taifa katika kufikia malengo ya maendeleo tarajiwa ya kijamii na kiuchumi. Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 unafanyika kupitia Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa Mwaka 2011/12–2025/26. Aidha, mwaka 2015 Tanzania iliingia makubaliano ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Makubaliano hayo yalijumuishwa kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26), mipango-mkakati na mipango ya mwaka ya taasisi za Serikali. **Kielelezo Na. 3** kinaonesha uhusiano wa mikakati na mipango na mikakati ya kitaifa.

**Kielelezo Na. 3: Uhusiano wa Mikakati na Mipango ya Kitaifa**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi Kutoka Kwenye Mikakati na Mipango ya Kitaifa, 2025

43. Utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Muda Mrefu kwa kipindi cha Miaka 2011/12–2025/26 uligawanywa katika mipango ya maendeleo ya miaka mitanomitano, ambapo, kila mpango ulikuwa na maudhui mahususi kama inavyooneshwa hapa chini.


***Maudhui Mahususi ya Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano***

44. Mipango ya maendeleo ya miaka mitano ina maudhui mahususi tofauti, ambayo inaweka umuhimu kwenye jambo ambalo linatekelezwa na taasisi husika ya serikali. Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2011/12–2015/16 uliokuwa na dhima ya "kufungua fursa zilizojificha za ukuaji wa uchumi", uliainisha maeneo, ambayo kama hatua zingechukuliwa, zingefungua fursa za kiuchumi. Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21 ulikuwa na dhima ya "kujenga uchumi wa viwanda".

45. Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (202122-2025/26) ulikuwa na dhima ya "kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu", kwa lengo la kuakisi malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ili kujenga uchumi wenye ushindani, imara, wa kipato cha kati, unaotegemea viwanda, na wenye uwezo wa kushindana kimataifa bila kupoteza dhamira ya kuleta maendeleo kwa watu. Mipango hii ya maendeleo hulenga kujenga msingi wa kuibadilisha Tanzania ili kuhakikisha makubaliano ya kimataifa na kikanda (k.m. Ajenda ya Afrika ya Mwaka 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu) yameingizwa katika mipango ya maendeleo ya taifa na

mifumo ya utekelezaji wa mipango hiyo. **Kielelezo Na. 4** kinatoa maelezo kwa ufupi ya kila mpango wa maendeleo na maudhui yake mahususi.

**Kielelezo Na. 4: Maelezo kwa Ufupi ya kila Maudhui Mahususi Kutoka kwenye Mipango ya Maendeleo ya Taifa**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Mikakati ya Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, 2025

ISO 9001:2015 Certified

**Umuhimu wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) na Malengo ya Maendeleo Endelevu**

46. Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) inalenga kutumia rasilimali ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Dira hii inakusudia kuifanya nchi kuwa ya uchumi wa kipato cha kati na kuendeleza mageuzi ya kuwa nchi ya viwanda kufikia mwaka 2025. Ufikiaji wa Dira kutaifanya nchi kuwa na maisha bora na endelevu; kuwa na amani, utulivu na umoja; kuwa na uongozi bora na utawala wa sheria; kuwa na jamii iliyoelimika; na kuwa na uchumi imara na wenye ushindani.

47. Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) inalenga pia kutekeleza mipango-mkakati na makubaliano ya kisekta, kikanda, na kimataifa ikiwa pamoja na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu yaliyopitishwa tarehe 25 Septemba 2015 na nchi wanachama 193 za Umoja wa Mataifa ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii.

Mipango hii ya maendeleo inaweka bayana orodha ya maeneo ya vipaumbele na shughuli za kimkakati ambazo ni muhimu ili kuimarisha kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu.

48. Malengo ya Maendeleo Endelevu yamejumuisha malengo 17 na shabaha 169 zinazoelekeza hatua za Serikali, mashirika ya kimataifa, asasi za kiraia, na taasisi zingine katika kipindi cha miaka 15 (2016-2030).

49. Ajenda inaweka mkakati wa siku zijazo, ikiongoza ulimwengu kuelekea njia endelevu zaidi na thabiti. Inaelekeza pia mabadiliko ya viwango vya maisha na mapito kwa njia jumuishi zaidi za maendeleo zenye nguvu na endelevu.

50. Kadhalika, Malengo 17 ya malengo tarajiwa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu yanalenga kuhakikisha kunakuwa na kazi zenye staha na ukuaji kiuchumi; kuwa na viwanda, uvumbuzi, na miundombinu; kupunguza matabaka; kuwa na miji na jamii endelevu; kuwa na matumizi na uzalishaji bora; kuchukua hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; kuhifadhi maisha ya viumbe wa majini na ardhini; kuwa na amani, haki na taasisi imara; na kuwa na ushirika wa malengo. Malengo haya yote yamehusishwa kwenye maeneo makuu matatu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo ni malengo ya uchumi, jamii, na mazingira.

*Uhusiano wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano*

ISO 9001:2015 Certified

51. Tanzania ikiwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa inatakiwa kutekeleza seti 17 za Malengo ya Maendeleo Endelevu ili kufikia maendeleo endelevu ya watu. Malengo ya Maendeleo Endelevu yanashabihiana, yakilenga kutatua changamoto za kimaendeleo zinazowakabili Watanzania na dunia kwa ujumla. Changamoto hizo zinahitaji hatua zichukuliwe za kutokomeza njaa, kulinda mazingira, na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.


52. Wizara ya Fedha imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu yanajumuishwa katika muktadha wa kitaifa na kutekelezwa ipasavyo. Juhudi zimefanywa ili kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu yameingizwa katika mipango na mikakati ya kisekta. Hivyo, utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya kitaifa pia utaathiri mafanikio ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na malengo ya kitaifa ya maendeleo. Katika kuhakikisha kuwa kuna utekelezaji mzuri wa Malengo ya Maendeleo Endelevu nchini, Kundi la Wabunge wa Maendeleo Endelevu limepewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika ngazi ya mitaa

na kutoa maoni na miongozo ya mara kwa mara. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kuwa malengo haya ya mipango ya maendeleo na Malengo ya Maendeleo Endelevu si tu yanafikiwa bali pia kanuni za tija, ufanisi, na uwekevu zinadumishwa kwa kiwango cha juu na taasisi zinazohusika wakati wa kutekeleza programu na shughuli zitakazowezesha kufikiwa kwa malengo hayo.

## 2.3 Miongozo Muhimu na Mfumo wa Kisheria Unaosimamia Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26)

53. Miongozo muhimu na mfumo wa kisheria unaosimamia utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26) unajumuisha sera, mipango-mkakati, na bajeti kwa taasisi zenye dhamana ya utekelezaji. Hivyo, kila sekta ya uchumi imeendelea kuongozwa na sheria zake. Hivyo, utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26) unaongozwa na sheria zilizo chini ya wizara, idara, na wakala husika, tawala za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa, mashirika ya umma, bodi mbalimbali, na wadau wengine. Vyombo, mifumo ya kisheria, na wadau muhimu katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26) wameelezewa katika **Kielelezo Na. 5** hapa chini.

**Kielelezo Na. 5: Miongozo Muhimu na Mfumo wa Kisheria katika Usimamizi wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano**





***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi Kutoka Kwenye Miongozo na Mfumo wa Kisheria katika Usimamizi wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano, 2025

## 2.4 Watendaji Muhimu katika Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26)

ISO 9001:2015 Certified

54. Utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya taifa ya miaka mitanomitano unagusa wizara, idara, wakala mbalimbali wa serikali, tawala za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa, mashirika ya umma, bodi mbalimbali, na wadau wengine katika utekelezaji wa shughuli za kila siku zilizopagwa katika mipango yao ya maendeleo ya kila mwaka. Utekelezaji umegawanyika katika ngazi zote zikiwemo mipango, uratibu, utekelezaji, na ufuatiliaji na tathmini ya mafanikio ya mipango ya maendeleo ya taifa ya miaka mitano kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 6** hapa chini.

**Kielelezo Na. 6: Watendaji Muhimu na Majukumu Yao katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Wadau wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano, 2025

## 2.5 Mikakati ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26)

55. Mikakati inayoongoza mageuzi ya kitaasisi na kisera katika utekelezaji wenye tija wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano inajumuisha Mpango wa Utekelezaji - Sehemu ya Kwanza; Mkakati wa Fedha - Sehemu ya Pili; Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini - Sehemu ya Tatu; na Mkakati wa Mawasiliano - Sehemu ya Nne. Mikakati hii imeainisha maeneo muhimu ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano. Mikakati hii ni kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 7** hapa chini.

**Kielelezo Na. 7: Muhtasari wa Mikakati ya Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Mikakati ya Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano wa Mwaka 2025

### (a) Mpango wa Utekelezaji - Sehemu ya Kwanza

56. Mpango huu unaelezea maeneo ya kuzingatia na vipaumbele vya miradi ya kimkakati. Mpangokazi huu pia unaonesha maendeleo na hali ya maeneo au miradi, changamoto na fursa, malengo ya utekelezaji, shabaha, shughuli, muda wa utekelezaji, chanzo cha fedha, majukumu, na wadau mbalimbali.

### (b) Mkakati wa Fedha - Sehemu ya Pili

57. Mkakati huu unaonesha utekelezaji na makusanyo ya fedha kutoka kwenye vyanzo vya kawaida na vipya kwa ajili ya kugharimia Mpango. Mkakati pia unajumuisha mafunzo na uzoefu kutoka nchi zilizoteuliwa na hatua zilizopendekezwa kuchukuliwa ili kutambua kiasi kilichokadiriwa cha kugharimia Mpango wa Maendeleo ya Miaka Mitano.

### (c) Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini - Sehemu ya Tatu

58. Mkakati huu ni nyenzo ya usimamizi wa matokeo inayosisitiza uratibu, uzingatiaji wa muda, viashiria vya utendaji, utoaji wa maoni, na taratibu za usahihishaji wa kasoro za kiutekelezaji. Mkakati huu unaweka msisitizo kwenye ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano.

**(d) Mkakati wa Mawasiliano - Sehemu ya Nne**

59. Mkakati huu unafafanua mbinu inayopaswa kutumika kuhakikisha kuna mtiririko mzuri wa taarifa na kukuza ushirikiano kwa wadau wote katika kipindi chote cha utekelezaji kisha kujadili matokeo yaliyotarajiwa na athari za utekekelezaji wake badaye.

## 2.6 Mahitaji ya Ukaguzi katika Kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) na Malengo ya Maendeleo Endelevu

60. Mahitaji ya kufanya kaguzi za ufanisi zinazoelezea dhamira za Malengo ya Maendeleo Endelevu yanatokana na umuhimu wa malengo hayo katika ngazi za kitaifa na kimataifa katika kuelezea maendeleo ya kiuchumi kwa njia endelevu. Mahitaji ya ukaguzi yanayoelezea dhamira za Malengo ya Maendeleo Endelevu yanaweza kufafanuliwa zaidi kama inavyooneshwa katika vifungu vifuatavyo.

**(a) Jukumu la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

61. Dhima ya kwanza ya Kongamano la Kimataifa la 22 kwa Taasisi Kuu za Umma za Ukaguzi lilikuwa kutoa wito kwa wanachama wake kuchangia ufuatiliaji na mapitio ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Kongamano hilo liliainisha umuhimu na dhamira ya kufanya kaguzi zinazohusisha kuangalia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa njia mbalimbali. Kongamano hilo lilizaa Azimio la Abu Dhabi ambalo liliweka chachu kwenye kuangalia utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu.

62. Kadhalika, mwaka 2015, Kamati ya Kubadilishana Maarifa pamoja na taasisi kuu za umma za ukaguzi kupitia mikakati yake ya maendeleo, zilizindua jukwaa la jamii la Malengo ya Maendeleo Endelevu na kuhamasisha jukumu la taasisi za ukaguzi kufanya kaguzi za Malengo ya Maendeleo Endelevu. Hayo yote ni miongoni mwa sababu za kukagua utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

**(b) Utekelezaji Usioridhisha wa Malengo ya Maendeleo ya Endelevu Nchini**

63. Kwa mujibu wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Maandalizi ya Utekelezaji wa Malengo ya

Maendeleo Endelevu (Machi 2018), Lengo Na. 17 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linataka kukomesha umaskini wa aina zote; kuwapo kwa afya bora na ustawi, elimu bora, usawa wa kijinsia, maji safi na usafi wa mazingira, nishati nafuu na safi, na kazi yenye heshima; na ukuaji wa uchumi na uvumbuzi wa viwanda na miundombinu.

64. Shabaha nyingine ni kupunguza utofauti wa usawa; kuwapo kwa miji na jamii endelevu; matumizi na uzalishaji kwa uwajibikaji; mpango wa kudhibiti mabadiliko ya tabianchi; uhai wa viumbe wa majini na nchikavu; amani, haki na taasisi imara; na kuwapo kwa ushirikiano katika utekelezaji wa malengo na kusimamia matumizi ya rasilimali asilia kwa uendelevu.

65. Ripoti hiyo ilionesha kuwa, Malengo ya Maendeleo Endelevu yanaunganisha pande tatu za maendeleo endelevu yaani uchumi, jamii, na mazingira, kwani yanaonekana kuwa malengo yanayohusiana kwa karibu. Hali hii ina maana kwamba hakuna lengo moja linalokinzana na lingine. Hivyo, malengo yote yanahitaji mbinu za kina na shirikishi katika utekelezaji wake.

**(c) Tathmini ya Tanzania katika Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu**

Uhitaji wa ukaguzi wa ufanisi katika kufuatilia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu unatoa fursa muhimu ya kupima kiwango cha mafanikio yake. Kwa mfano, kupitia ukaguzi wa eneo hili, nchi inaweza kutathmini ikiwa Wizara ya Fedha, kama msimamizi mkuu wa utekelezaji wa malengo haya, inatekeleza majukumu yake ipasavyo. Pia, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kama mratibu wa mamlaka za serikali za mitaa, ambazo ni watekelezaji wakuu, inatekeleza Ajenda ya Mwaka 2030 kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu katika muktadha wa kitaifa kupitia utambuzi na uhamasishaji wa usimamizi wa rasilimali, ujenzi wa uwezo wa utekelezaji, na ufuatiliaji na utoaji wa taarifa kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa malengo hayo.

## 2.7 Ukaguzi wa Ufanisi Uliofanyika na Uhusiano wake na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) na Malengo ya Maendeleo Endelevu

66. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, zilifanyika kaguzi 19 za ufanisi zilizoelezea utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26) na Malengo ya Maendeleo Endelevu.

67. Maudhui ambayo yamehusishwa kwenye kaguzi hizi ni yale yanayohusiana na maendeleo ya watu na mageuzi ya kiuchumi kama yalivyoainishwa kwenye mipango hiyo. Mipango yote hii imeweka maeneo ya vipaumbele ambayo ni muhimu katika kuhakikisha utekelezaji wake madhubuti. Maeneo ya vipaumbele kwa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) ni kuimarisha ukuaji wa viwanda kwa mageuzi ya kiuchumi; kuchochea maendeleo ya watu; kuboresha mazingira rafiki ya uendelezaji biashara; na kuimarisha ufanisi wa utekelezaji. Kadhalika, maeneo ya vipaumbele kwa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26) ni kuchochea uchumi shirikishi na shindani; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza uwekezaji na biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza ujuzi.

68. Maendeleo ya watu yanalenga kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu na mipango ya maendeleo ya taifa. Dhima ya maendeleo ya watu ni uboreshaji wa maisha ya watu katika nyanja zote za umma, binafsi, jamii, siasa, na uchumi. Mageuzi ya kiuchumi yanazitaka nchi kufanya maboresho ya sera za kiuchumi kwa kuzingatia ushirikishaji, mageuzi mbalimbali ya ajira za kutosha, ambazo ni jumuishi, ulinzi wa dunia, na uimarishaji wa misingi ya ekolojia katika nyanja ya uchumi.

69. Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) ni nyenzo zilizokubalika katika kutathmini maendeleo ya uchumi na watu kimataifa na kitaifa mtawalia. Muhtasari wa kaguzi za ufanisi zilizofanyika na maudhui yake kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu ni kama unavyowasilishwa katika **Kielelezo Na. 8** hapa chini. Maelezo zaidi yanawasilishwa kwenye **Kiambatisho Na. 1**.

**Kielelezo Na. 8: Kaguzi za Ufanisi Zilizofanyika Zikihusianishwa na Maudhui ya Malengo ya Maendeleo Endelevu Pamoja na Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano**

| Jina la Ukaguzi | Maudhui ya Malengo ya Maendeleo Endelevu Pamoja na Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano |
|---|---|
| Utoaji wa Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu na Neva kwa Watoto | Lengo la 3, Shabaha 3.8 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.5 |
| Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya ya Umma | Lengo la 3, Shabaha 3.8 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.5 |
| Utoaji wa Huduma za Afya ya Uzazi | Lengo la 3, Shabaha 3.1 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.5 |
| Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria kwa Wananchi Wasiojiweza | Lengo la 1, 5,10 na 16. Shabaha 1.3, 5.2, 10.3 na 16.3; na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.5 |
| Utoaji wa Chakula, Makazi na Huduma za Malezi kwa Wazee | Lengo la 1, Shabaha 1.3, Lengo la 3, Shabaha 1.3 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.5 |
| Usimamizi wa hifadhi ya nafaka za kimkakati | Lengo la 2, Shabaha 2.1 na 2.2 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.3 |
| Usimamizi wa ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi | Lengo la 8, Shabaha 8.8, Lengo la 3, Shabaha 3.9 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.5 |
| Ufanisi kuhusu utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi | Lengo la 8, Shabaha 8.8, Lengo la1, Shabaha 1.3 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.5 |
| Udhibiti wa Huduma za Maji | Lengo la 6, Shabaha 6.1 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.5 |
| Usimamizi wa Mchakato wa Upangaji wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Barabara | Lengo la 11, Shabaha 11.2, Lengo la 9, Shabaha 9.1 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.2 |
| Usimamizi wa Uendeshaji wa Mizani | Lengo la 9, Shabaha 9.1, na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.2 |
| Usimamizi wa Huduma za Usafiri Mjini katika Majiji Makubwa | Lengo la 11, Shabaha11.2 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.2 |
| Utekelezaji wa Miradi ya Nishati Jadidifu | Lengo la 7, Shabaha 7.2 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.2 |
| Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi nchini Tanzania | Lengo la 2,6 na 13, Shabaha 2.3, 6.1, 13.1 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.3 |
| Usimamizi wa Shughuli za Urejeshaji Misitu | Lengo la 15, Shabaha 15.1 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.3 |
| Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini | Lengo la 8, 9 na12; na Shabaha 8.5, 9.3 na 12.6 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.3 |
| Usimamizi wa Deni la Serikali | Lengo la 17, Shabaha 17.4 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.2 |
| Ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya Kodi | Lengo la 17, Shabaha 17.4 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.2 |
| Usimamizi wa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji wa Shule za Umma | Lengo la 4, Shabaha 4.1 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, Aya 5.5 |

***Chanzo***: Malengo ya Maendeleo Endelevu, Mpango wa Pili na wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano na Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi, 2025

## 2.8 Ugharimiaji wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano

70. Kwa mujibu wa Mkakati wa Fedha wa Mwaka 2018 wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, mafanikio ya mpango ambayo yamejikita katika kuimarisha mabadiliko ya kiuchumi, maendeleo ya watu, maendeleo ya viwanda, na kukuza ufanisi wa utekelezaji yanabebwa na ukusanyaji bora wa rasilimali-fedha na mapato, na utaratibu mzuri wa ugharimiaji. Ugharimiaji wa utekelezaji unajumuisha vyanzo vya kawaida vya kodi na mapato pamoja na vyanzo vipya vya fedha.

71. Chanzo cha kawaida cha fedha kinajumuisha mapato ya kodi, mapato yasiyo ya kodi, ukopaji wa ndani, na fedha za nje. Vyanzo vipya vya fedha pia vimeanzishwa ili kuongezea vyanzo vya kawaida. Vyanzo hivi vinajumuisha vyanzo vya fedha vya ndani na nje kupitia fursa zinazohusiana na bidhaa mpya zinazojumuisha dhamana ya soko la nje; dhamana za serikali za mitaa/dhamana za manispaa; ufadhili wa mabadiliko ya tabianchi; taasisi za fedha za maendeleo; Mfuko wa Usawa wa Pensheni; ubia wa sekta binafsi na umma; na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje.

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT
ISO 9001:2015 Certified

## SURA YA TATU

## UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA

### 3.1 Utangulizi

72. Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na utoaji wa Huduma za Afya. Inaelezea maeneo ya ukaguzi, Wizara na Taasisi za Serikali zilizohusika katika ukaguzi, uhusiano wa kaguzi hizi na athari za matokeo yake katika Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano.

73. Kaguzi za ufanisi zilizohusika katika sura hii ni:
(a) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu kwa Watoto;
(b) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya vyaa Umma; na
(c) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Afya ya Uzazi.

#### 3.1.1 Usuli

74. Matatizo ya mfumo wa neva yamekuwa yakieenea miongoni mwa watoto yakiathiri ubongo, uti wa mgongo na mishipa ya neva, na mara nyingi husababisha ulemavu kwa watoto. Takwimu zilizorekodiwa kupitia Mfumo wa Jeeva katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili zinaonesha kuwa, kuanzia 2021, 2022, 2023, hadi 2024, idadi ya watoto wenye matatizo ya mfumo wa fahamu ilikuwa 4037, 4322, 3906, na 3142, mtawalia. Uchambuzi ulionesha kuwa matatizo yaliyoripotiwa mara kwa mara yalikuwa kifafa, kupooza ubongo na usonji, homa ya uti wa mgongo, ugonjwa wa kuwa na kromosomu za ziada, ugonjwa wa mishipa ya fahamu, kupooza upande mmoja wa mwili, Kichwa kujaa Maji, mgongo wazi, na maambukizi ya ubongo na utando wake.

75. Aidha, wagonjwa wengi hawakupata matibabu kutoka kwa daktari bingwa wa mfumo wa fahamu, na upimaji wa kawaida mara nyingi haupatikani kwa sababu ya gharama kubwa na miundombinu duni. Utafiti wa Ali Mohamed pamoja na wenzake (2024) ulionesha kuwa watoto wengi walio na matatizo ya mfumo wa fahamu bado hawajatambuliwa na hawajatibiwa. Hii ni kwa sababu ya kuwapo kwa madaktari wachache wa mfumo wa fahamu na ufikiaji mdogo wa huduma za upimaji wa matatizo ya mfumo wa fahamu, kama vile uchunguzi wa ubongo au vipimo vya kuangalia utendaji wa mfumo wa fahamu. Matokeo yake, majibu ya vipimo mara nyingi hucheleweshwa, na endapo hospitali

isipoweza kutoa huduma hii, familia hugeukia waganga wa jadi au wa imani, ambayo hucheleweshа zaidi utoaji wa huduma inayofaa.

76. Kwa upande mwingine, Tanzania inaendelea kukabiliwa na upungufu wa mara kwa mara wa dawa muhimu, hususani katika maeneo ya pembezoni na magumu kufikika, kama ilivyothibitishwa na tafiti za hivi karibuni. Utafiti uliofanyika katika Mkoa wa Dodoma ulionesha kuwa, dawa muhimu zilipatikana kwa takribani asilimia 70 kwenye vituo vya afya katika kipindi cha miezi mitatu, huku baadhi ya dawa kama vile dawa za kuongeza damu aina ya madini-chuma zikikosekana kwa zaidi ya siku 14 katika zaidi ya nusu ya vituo vya afya. Vilevile, utafiti wa mwaka 2025 uliofanyika katika Mkoa wa Mwanza uliripoti upatikanaji wa wastani wa juu wa dawa wa asilimia 94.4 lakini ukiambatana na ukosefu wa mara kwa mara na wa muda mrefu wa dawa, ambapo kwa wastani kulikuwa na matukio matatu ya ukosefu wa dawa na siku 94 za ukosefu wa dawa ndani ya kipindi cha miezi mitatu. Upungufu mkubwa zaidi ulibainika katika dawa muhimu za afya ya uzazi, ikiwemo glukoneti ya kalsiamu kwa asilimia 93.4 na misoprostoli (asilimia 32.9).

77. Aidha, licha ya jitihada zilizochukuliwa na Serikali kuboresha huduma za afya ya uzazi, bado kuna changamoto kadhaa zikiwemo upungufu wa utoaji wa huduma bora katika vituo vya Huduma za Afya za Dharura kwa Mama na Mtoto unaosababishwa na idadi ndogo na ujuzi usioridhisha wa watumishi wa afya, miundombinu isiyotosheleza kusaidia utoaji wa huduma za Afya za Dharura kwa Mama na Mtoto, upungufu katika mifumo ya uhusiano kati ya jamii na huduma za afya ya uzazi kwa mama, pamoja na ukosefu wa utekelezaji wa hatua za ufuatiliaji baada ya kufanyika kwa mapitio ya vifo vya mama na watoto wachanga katika ngazi ya mkoa, wilaya, na vituo vya afya.


78. Serikali inaendelea kukabiliwa na changamoto kadhaa zinazokwamisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi kwa mama licha ya juhudi za kupunguza vifo vya akina mama. Vifo hivi husababishwa na matatizo ya moja kwa moja ya uzazi kama vile shinikizo la juu la damu wakati wa ujauzito, kutokwa na damu nyingi wakati wa kujifungua na maambukizi ya uzazi huku visababishi visivyo vya moja kwa moja kama upungufu wa damu na magonjwa ya mfumo wa moyo na mishipa vikichangia kwa kiasi kikubwa.

## 3.1.2 Uhusiano kati ya Usimamizi wa Huduma za Afya, Malengo ya Maendeleo Endelevu, na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

### (a) Utoaji wa Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu kwa Watoto

79. Uhusiano kati ya Utoaji wa Huduma za Afya ya Mfumo wa Neva na Malengo ya Maendeleo Endelevu, na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano unawasilishwa kwenye **Kielelezo Na. 9.**

**Kielelezo Na.9:Uhusiano kati ya Mipango ya Kitaifa ya Maendeleo, Malengo ya Maendeleo Endelevu, na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Utoaji wa Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu**





*Chanzo:* Uchambuzi wa Wakaguzi Kuhusu Uhusiano wa Huduma za Afya za Mfumo wa Fahamu na Mikakati ya Serikali, 2025

## (b) Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya vya Umma

80. Upatikanaji na ufikivu wa dawa muhimu unaendana na Lengo la tatu la Maendeleo Endelevu, linalosisitiza juu ya afya njema na ustawi, shabaha ya 3.8 inayohimiza juu ya kufanikisha huduma za afya kwa wote ikijumuisha ulinzi dhidi ya hatari za kifedha, upatikanaji wa huduma bora za afya, pamoja na upatikanaji wa dawa na chanjo salama zenye ubora na bei nafuu kwa wote. Upatikanaji na ufikivuwa dawa muhimu pia unachangia kupunguza umaskini (Lengo la kwanza la Malengo ya Maendeleo Endelevu) kwa kujenga uwezo wa jamii zinazokabiliana na umaskini na kupunguza athari za mshtuko unaotokana na changamoto za kiafya. Aidha, unachangia kupunguza ukosefu wa usawa katika jamii kwa kuwezesha na kukuza ushiriki wa kijamii, kiuchumi, na kisiasa kwa wote (Lengo la 10 la Malengo ya Maendeleo Endelevu).

Mipango na mikakati mingine ya kitaifa inayohusiana na upatikanaji wa dawa muhimu imewasilishwa katika **Kielelezo Na. 10.**

**Kielelezo Na. 10: Mipango na Mikakati inayohusiana na Upatikanaji wa Dawa Muhimu**





***Chanzo:*** Muhtasari wa Wakaguzi kuhusu Mipango na Mikakati ya Taifa, 2025

### (c) Utoaji wa Huduma za Afya ya Uzazi

Uhusiano kati ya Utoaji wa Huduma za Afya ya Uzazi na Malengo ya Maendeleo Endelevu, na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano unawasilishwa kwenye **Kielelezo Na. 11**.

**Kielelezo Na. 11: Uhusiano kati ya Utoaji wa Huduma za Afya ya Uzazi na Malengo ya Maendeleo Endelevu, na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Mipango Mkakati, 2025

## 3.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

### 3.2.1 Malengo ya ukaguzi

81. Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa kufanya tathmini na kubaini iwapo Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Bohari ya Dawa zilihakikisha utoaji wa huduma za afya.

82. Mathalani, ukaguzi ulitathmini iwapo:

(a) Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilifanikiwa kutoa huduma za kutosha za afya ya mfumo wa fahamu na neva kwa watoto nchini ili kuwawezesha kukua na kufanya kazi ipasavyo;

(b) Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Bohari ya Dawa zilihakikisha upatikanaji endelevu wa dawa muhimu katika vituo vya afya vya umma ili kuwezesha utoaji wa huduma bora za afya; na

(c) Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI zilihakikisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi nchini ili kuchangia kupunguza vifo vya akina mama hadi kufikia vifo 70 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo mwaka 2030, kulingana na Lengo la 3.1 la Malengo ya Maendeleo Endelevu.

### 3.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

ISO 9001:2015 Certified

83. Wizara ya Afya na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI walikuwa wakaguliwa wakuu katika Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu na Neva. Ukaguzi huu ulilenga kutathmini ufanisi wa uchunguzi wa watoto wenye matatizo ya mfumo wa fahamu, upatikanaji wa vifaa vya uchunguzi, uwapo wa wataalamu husika (mafundi wa vifaa tiba, wataalamu wa mionzi, na madaktari bingwa wa mfumo wa fahamu), utoaji wa huduma za kina za urekebu, pamoja na upatikanaji wa takwimu kwa ajili ya maamuzi sahihi katika utoaji wa huduma za afya ya mfumo wa fahamu. Ukaguzi ulifanyika kwa kipindi cha miaka minne ya fedha kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25.

84. Kwa upande wa Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya vya Umma, Taasisi zilizokaguliwa zilikuwa Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, na Bohari ya Dawa. Ukaguzi huu ulilenga kutathmini upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya afya vya umma na ufanisi wa utekelezaji wa uagizaji wa dawa. Ukaguzi huu pia ulifanyika kwa kipindi cha miaka minne ya fedha kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25.

85. Aidha, Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Afya ya Uzazi ulitathmini Wizara ya Afya na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kuhusu upatikanaji wa huduma za Afya za Dharura kwa Mama na Mtoto, uwepo na utekelezaji wa mifumo ya ukusanyaji wa taarifa mbalimbali, ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za afya ya uzazi kwa mama, ufanisi wa mifumo ya rufaa, pamoja na utoaji wa kampeni za uhamasishaji na elimu kwa jamii kuhusu afya ya uzazi, kwa kipindi cha miaka mitano ya fedha kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi Mwaka wa Fedha 2024/25

## 3.3 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Utoaji wa Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu kwa Watoto

86. Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi kuhusu utoaji wa huduma za afya ya mfumo wa fahamu kwa watoto nchini.

### 3.3.1 Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu kwa Watoto Hazikutolewa vya Kutosha

87. Nilibaini kuwa huduma za afya ya mfumo wa fahamu hazikutolewa vya kutosha kwa watoto. Hali hii ilikuwa kinyume na matakwa ya aya ya 4.3 ya Mpango Mkakati wa Taifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza wa mwaka 2021–2026, inayotaka huduma za afya kwa magonjwa yasiyoambukiza, ikiwemo matatizo ya mfumo wa fahamu, zipatikane, ziweze kufikiwa kirahisi na ziwe nafuu katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini.

88. Hali hii ilijidhihirisha kupitia upungufu wa matibabu kwa watoto waliogundulika kuwa na matatizo ya mfumo wa fahamu nchini. Kutokana na kukosekana kwa takwimu mahsusi za matatizo ya mfumo wa fahamu kwa watoto nchini Tanzania, ukaguzi ulipitia utafiti wa Shirika la Afya Duniani wa mwaka 2022 kuhusu kuenea kwa ugonjwa wa kifafa nchini, uliokadiria kuwa takribani watu 450,000 waliishi na ugonjwa huo. Hata hivyo, wengi wao hawakupata matibabu stahiki, wakiwemo watoto. Aidha, nilibaini kuwapo kwa idadi kubwa ya watoto wenye matatizo ya mfumo wa fahamu ambao hawakutambuliwa na Wizara ya Afya, kutokana na kukosekana kwa takwimu zinazoonesha idadi ya watoto waliogundulika kuwa na matatizo ya mfumo wa fahamu toka kuzaliwa. Huduma za afya ya mfumo wa fahamu hazikutolewa vya kutosha kama ilivyofafanuliwa hapa chini:

### (a) Kutopatikana kwa Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu katika Vituo vya Afya Ngazi ya Chini

89. Licha ya kuwapo kwa matatizo endelevu ya mfumo wa fahamu kwa viwango tofauti, vituo vya afya vya ngazi ya chini vilibainika kutotoa matibabu ya kutosha. Hali hii ilitokana na ukweli kwamba huduma za afya ya mfumo wa fahamu zilijikita zaidi katika ngazi za juu, kuanzia Hospitali za Kanda hadi Hospitali ya Taifa. Aidha, nilibaini kuwa huduma hizi, ambazo zilipatikana zaidi katika ngazi ya juu (Hospitali za Rufaa, za Kanda na za Kitaifa), zilisambazwa kwa kiwango kisicho sawa. Huduma hizo zilijikita zaidi katika Mkoa wa Dar es Salaam na kuwa pungufu katika Mikoa ya Mwanza na Dodoma kutokana na uhaba wa wataalamu na upungufu wa vifaa vya uchunguzi na matibabu. Matokeo yake, wagonjwa kutoka Mikoa ya Rukwa, Katavi na Shinyanga walilazimika kusafiri zaidi ya kilomita 500 ili kupata huduma hizo.

### (b) Upungufu wa Utambuzi na Ueneaji wa Uzito wa Matatizo ya Mfumo wa Fahamu

90. Nilibaini kuwa Wizara ya Afya haikufanya utambuzi wala tathmini ya kiwango, usambaaji na ueneaji wa matatizo ya mfumo wa fahamu nchini kutokana na kuwapo kwa mifumo mingi ya ukusanyaji wa taarifa, hali iliyofanya iwe vigumu kuunganisha taarifa kutoka vituo vya ngazi za chini. Hali hii ilikuwa kinyume na aya ya 120 ya Mpango wa Kimataifa wa Shirika la Afya Duniani wa Hatua Shirikishi kuhusu Kifafa na Matatizo Mengine ya Mfumo wa Fahamu wa mwaka 2022–2031, inayosisitiza kuwapo kwa ushahidi kupitia tafiti zenye ubora wa juu ili utumike kama chanzo cha taarifa katika sera, mipango na programu mbalimbali za matatizo ya mfumo wa fahamu.

91. Aidha, nilibaini kuwa kulikuwa na mifumo saba ya taarifa katika ngazi mbalimbali za hospitali kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 2**, bila kuunganishwa kwa taarifa kutoka vituo vya ngazi za chini. Jambo hili lilionesha changamoto katika utambuzi wa kitaifa wa maambukizi ya magonjwa kutokana na ukusanyaji wa taarifa kutoka kwenye mifumo mbalimbali kufanywa kwa njia isiyo ya kielektroniki mfano, mfumo wa karatasi.

**Jedwali Na.2: Mifumo Inayotumika Kukusanya Taarifa za Magonjwa**

| Jina la Mfumo | Jina la Hopsitali | Idadi ya Hospitali |
|---|---|---|
| E-MEDICAL | Hospitali za Kanda ya Mbeya na Mtwara | 5 |
| | Hospitali ya Kanda ya Chato | |
| | Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili | |
| | Hospitali ya Magonjwa ya Kuambukiza ya Kibong'oto | |

| Jina la Mfumo | Jina la Hopsitali | Idadi ya Hospitali |
|---|---|---|
| | Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe | |
| MEDIPRO | Hospitali ya Benjamini Mkapa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete | 1 |
| HEALTH E-HMS | Hospitali ya Kanda ya Bugando | 32 |
| | Kituo cha Matibabu cha Kikristo cha Kilimanjaro | |
| | Hospitali zote za Rufaa | |
| JEEVA | Hospitali ya Taifa ya Muhimbili - Upanga | 2 |
| | Hospitali ya Taifa ya Muhimbili -Mloganzila | |
| (HEALTH AI) OPEN CLINIC | Hospitali ya Huduma za Urekebu katika Jamii (CCBRT) | 1 |
| INAYA | Taasisi ya Saratani ya Ocean Road | 1 |
| DHIS | Hospital zote za Wilaya | 184 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Mifumo ya Afya Iliyopo katika Ngazi Husika za Hospitali Mwaka 2025

92. Nilibaini upungufu wa utambuzi na tathmini ya kiwango, uenevu wa matatizo ya mfumo wa fahamu ulitokana na mifumo ya kurekodi taarifa isiyounganishwa na kukosekana kwa mfumo wa kitaifa wa taarifa za afya unaoaminika, ikiwemo kukosekana kwa kanzidata au usajili wa kitaifa wa afya ya mfumo wa fahamu.

### 3.3.2 Uchunguzi wa Watoto Wenye Matatizo ya Mfumo wa Fahamu Usiojitosheleza


93. Nilibaini kuwa Wizara ya Afya na Ofisi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hazikuhakikisha uchunguzi wa mapema na wenye ufanisi wa matatizo ya mfumo wa fahamu kwa watoto wachanga. Hali hii ilidhihirika kupitia utoaji usio na usawa wa huduma za uchunguzi katika ngazi mbalimbali za vituo vya afya, ambapo vifaa vya uchunguzi wa matatizo ya mfumo wa fahamu vilipatikana zaidi katika hospitali za kitaifa, za kibingwa na za kanda, na hivyo kupunguza uwezo wa kugundua mapema na kudhibiti magonjwa haya katika ngazi za chini.

94. Aidha, nilibaini kuwa vituo vingi vya afya vilikosa vifaa muhimu vya uchunguzi vinavyohitajika kugundua matatizo ya mfumo wa fahamu kwa watoto. Ingawa mashine za CT-Skani na mashine ya upigaji picha kwa mionzi ya sumaku (MRI) zilipatikana katika hospitali za kitaifa na baadhi ya hospitali za rufaa za mikoa, vifaa muhimu vya kupima umeme wa kichwani vilipatikana katika hospitali za kitaifa pekee. Hali hii ilizikosesha Hospitali za Ngazi za Mikoa na Kanda uwezo wa kufanya uchunguzi wa kina wa matatizo ya mfumo wa fahamu. Matokeo yake, wagonjwa wengi walipewa rufaa kwenda hospitali za kitaifa na kusababisha msongamano wa wagonjwa.

### (a) Uhaba wa Wataalamu wa Kuchunguza Matatizo ya Mfumo wa Fahamu

95. Mapitio yangu ya taarifa ya rasilimaliwatu katika sekta ya afya Tanzania Bara mwaka 2025 yalibaini kuwa vituo vya afya vilikuwa na idadi ndogo ya wataalamu wenye sifa na ujuzi wa kiufundi wa kuendesha na kutunza vifaa muhimu vya uchunguzi na kutoa huduma bora za watoto wachanga, kinyume na viwango vya taaluma vilivyoainishwa katika Viwango vya Msingi vya Vituo vya Sekta ya Afya, aya ya 1–4, vinavyotaka kila kituo kuwa na idadi na mchanganyiko unaofaa wa taaluma ili kuhakikisha uchunguzi wa ufanisi wa matatizo ya mfumo wa fahamu kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 12.**

**Kielelezo Na.12: Upatikanaji wa Wataalamu wa Kuchunguza Matatizo ya Mfumo wa Fahamu**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Rasilimaliwatu katika Sekta ya Afya, Tanzania Bara Mwaka 2025

96. **Kielelezo Na. 12** kinaonesha uhaba wa wataalamu wanaohitajika kuchunguza matatizo ya mfumo wa fahamu, ambapo makundi yaliyoathirika zaidi yalikuwa ni madaktari bingwa wa mionzi na mafundi wa teknolojia ya mionzi kwa asilimia 89 kila moja, yakifuatiwa na wanasayansi wa mionzi kwa asilimia 83. Aidha, ilibainika kuwa kulikuwa na madaktari bingwa wa mfumo wa fahamu wa watoto watatu pekee, katika Hospitali ya Taifa pekee, bila ya kuwapo kwa utambuzi wa viwango vya uhitaji wa utaalam huo.

97. Uhaba huo ulitokana zaidi na juhudi zisizotosheleza za Serikali katika kuwezesha mafunzo na kuhakikisha kuwapo kwa wataalamu wanaohitajika nchini. Matokeo yake, wataalamu waliokuwapo walielemewa na wingi wa kazi, hivyo kuathiri uchunguzi, na hatimaye kuzuia uchunguzi kwa watoto wenye matatizo ya mfumo wa fahamu unaojitosheleza.

### (b) Upungufu wa Vifaa Tiba vya Kusaidia Uchunguzi wa Watoto Wenye Matatizo ya Mfumo wa Fahamu

98. Mapitio yangu ya orodha ya vifaa tiba yalibaini uhaba wa vifaa vya uchunguzi vinavyohitajika kugundua matatizo ya mfumo wa fahamu kwa watoto, kinyume na Viwango vya Msingi vya Vituo vya Sekta ya Afya, aya ya 1–4, 2017, vinavyotaka ngazi mbalimbali za vituo vya afya kuwa na vifaa tiba vya kutosha kwa ajili ya uchunguzi. **Jedwali Na. 3** linaonesha hali ya upatikanaji wa vifaa tiba kwa uchunguzi wa matatizo ya mfumo wa fahamu katika ngazi mbalimbali za vituo vya afya.

**Jedwali Na. 3: Uchambuzi wa Vifaa Tiba kwa ajili ya Uchunguzi wa Matatizo ya Mfumo wa Fahamu**

| Jina la Kifaa Tiba | Ngazi ya Hospitali | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Taifa | Maalumu za Kitaifa | Kanda | Mkoa |
| Kifaaa cha Upimaji wa Umeme wa Ubongo | Kipo | Kipo | Kipo | Hakipo |
| Kifaa cha Upimaji wa Umeme wa Misuli | Kipo | Hakipo | Hakipo | Hakipo |
| Mashine ya Upigaji picha kwa mionzi ya sumaku | Kipo | Hakipo | Kipo | Hakipo |
| Kifaa cha CT-Skani | Kipo | Hakipo | Kipo | Kipo |
| Vichambuzi vya Vinasaba | Hakipo | Hakipo | Hakipo | Hakipo |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Vifaa Tiba Vilivyopo kwa Uchunguzi wa Matatizo ya Mfumo wa Fahamu Mwaka 2025

***Ufunguo***

| | | |
|---|---|---|
| (kijani) | : | Kipo |
| (nyekundu) | : | Hakipo |

99. **Jedwali Na. 3** linaonesha upungufu wa vifaa vya uchunguzi wa matatizo ya mfumo wa fahamu katika ngazi mbalimbali za vituo vya afya. Vifaa kama vile vichambuzi vya vinasaba havikupatikana kwa urahisi katika ngazi zote za hospitali; kifaa cha kupima umeme wa misuli kilipatikana katika ngazi ya kitaifa pekee, na kifaa cha kupima umeme wa ubongo kilipatikana katika hospitali za kanda. Hata hivyo, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando haikuwa na daktari

bingwa wa mfumo wa fahamu kwa ajili ya kutafsiri matokeo ya Kipimo cha Umeme wa Kichwani. Aidha, Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe haikuwa na Mashine ya upigaji picha kwa mionzi ya sumaku (MRI) wala CT-Skani kwa ajili ya uchunguzi wa kina zaidi.

100. Uhaba wa vifaa vya kupima changamoto za mfumo wa fahamu ulitokana na kukosekana kwa mwongozo wa viwango vya kitaifa wa usambazaji wa vifaa tiba katika vituo vya afya. Mapitio yangu ya Viwango vya Msingi vya Vituo vya Sekta ya Afya, aya ya 1–4, 2017, yalibaini kuwa miongozo hiyo haikujumuisha ipasavyo vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya uchunguzi wa matatizo ya mfumo wa fahamu. Hali hii ilidhihirishwa na kutokuwapo kwa baadhi ya vifaa vya mfumo wa fahamu, ikiwemo kifaa cha Upimaji wa Umeme wa Misuli na vifaa vya uchunguzi wa vinasaba katika viwango vya msingi.

101. Mahojiano yangu na maafisa kutoka vituo vya afya nilivyotembelea yalionesha kutojumuishwa kwa vifaa vya juu vya uchunguzi katika miongozo kuliathiri uwezo wa hospitali za kanda na za mikoa kutoa tathmini ya kina ya matatizo ya mfumo wa fahamu. Kutokana na hali hiyo, watoto walipatiwa matibabu bila kufanyiwa uchunguzi wa kutosha, kama ilivyobainika katika hospitali za rufaa za mikoa zilizotembelewa, ambapo watoto wenye kifafa walitibiwa kwa dawa za kifafa bila kuthibitishwa zaidi aina ya ugonjwa huo kupitia Kipimo cha Umeme wa Kichwani ili kubaini iwapo mtoto alikuwa na kifafa cha jumla au cha sehemu jambo ambalo ni muhimu ili kuwezesha utoaji wa dawa sahihi kulingana na aina ya kifafa kilichogundulika.

### 3.3.3 Ukosefu wa Matibabu Bora kwa Watoto Wenye Matatizo ya Mfumo wa Fahamu

102. Nilibaini kuwa watoto wenye matatizo ya mfumo wa fahamu walikuwa na ufikivu mdogo wa huduma bora za matibabu. Hususan, ufikivu wao wa huduma za kibingwa, vifaa tiba, pamoja na dawa nafuu na za kutosha kwa ajili ya matibabu haukuwa wa kuridhisha, hali iliyokuwa kinyume na Mpango Mkakati wa Rasilimaliwatu kwa Afya wa mwaka 2021 hadi mwaka2026, unaitaka Serikali kuhakikisha usambazaji wenye usawa wa rasilimaliwatu katika sekta ya afya wenye ujuzi unaofaa. Aidha, Lengo la Kimataifa 2.2 la Mpango wa Kimataifa wa Shirika la Afya Duniani wa Hatua Shirikishi kuhusu Kifafa na Matatizo Mengine ya Mfumo wa Fahamu wa mwaka 2022 hadi mwakav2031 linalenga kuhakikisha upatikanaji wa asilimia 80 ya dawa muhimu na vifaa maalumu vinavyohitajika kudhibiti matatizo ya mfumo wa fahamu katika huduma za afya ya msingi ifikapo mwaka 2031.

Kutokuwapo kwa matibabu bora kulidhihirishwa zaidi na uhaba na usambazaji usio na usawa wa madaktari bingwa, kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4**

**Jedwali Na. 4: Uwiano wa Madaktari Bingwa wa Mfumo wa Fahamu wa Watoto Wenye Matatizo ya Mfumo wa Fahamu katika Mikoa Iliyotembelewa**

| Mkoa | Idadi ya Wagonjwa | | Madaktari Bingwa wa Mfumo wa Fahamu kwa Watoto | Uwiano |
|---|---|---|---|---|
| | Kifafa | Ulemavu wa Ubongo | | |
| Dar es Salaam | 11,609 | 11,825 | 2 | 1:11,717 |
| Dodoma | 3,563 | 2,080 | 0 | 0 |
| Mwanza | 3,358 | 1,837 | 0 | 0 |
| Rukwa | 966 | 834 | 0 | 0 |
| Tabora | 1,865 | 2,229 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **21,361** | **18,805** | **2** | **1:20,083** |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Mfumo wa Utoaji wa Taarifa wa DHIS 2 wa Mwaka 2025

103. **Jedwali Na. 4** linaonesha kuwa Jiji la Dar es Salaam lilikuwa na watoto 11,609 wenye kifafa na watoto 11,825 wenye ulemavu wa ubongo ilhali kulikuwa na madaktari bingwa wa mfumo wa fahamu wawili pekee wa kuhudumia idadi hiyo ya watoto. Wakati huo huo, mikoa ya Tabora, Dodoma, Mwanza na Rukwa kwa pamoja ilikuwa na takribani watoto 20,000 wenye matatizo ya mfumo wa fahamu, lakini hakukuwa na daktari bingwa wa mfumo wa fahamu aliyekuwapo. Hali hii inaashiria kuwa kila daktari bingwa wa mfumo wa fahamu alikuwa akihudumia takribani watoto 20,083 wenye matatizo ya mfumo wa fahamu, jambo linaloonesha uhaba mkubwa wa rasilimaliwatu hususani madaktari bingwa wa mfumo wa fahamu kwa watoto.

ISO 9001:2015 Certified

104. Aidha, kutokuwapo kwa matibabu bora kulidhihirishwa zaidi na mambo yafuatayo:

### (a) Uwiano Usio Sawa na Uhaba wa Wataalamu

105. Nilibaini uhaba wa wataalamu wa mfumo wa fahamu katika ngazi mbalimbali za vituo vya afya. Zaidi ya hayo, mgawanyo wa wataalamu hao ulijikita zaidi katika miji mikubwa, hali iliyokuwa kinyume na aya ya 5.4.1 ya Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa 2021–2026, uliolenga kutumia Kipimo cha Ukubwa wa Kazi katika Mahitaji ya Ajira – Uchanganuzi wa Uwekaji Vipaumbele na Uboreshaji ili kugawa watumishi wa afya kulingana na mahitaji halisi.

106. Uhaba wa wataalamu wenye uwezo wa kutibu matatizo ya mfumo wa fahamu kwa watoto katika ngazi zote za utoaji wa huduma ulionekana zaidi katika vituo vya afya vya ngazi ya msingi vilivyopo vijijini, ambavyo ndiyo ngazi ya kwanza ya huduma kwa wananchi, kama inavyoainishwa katika **Jedwali Na. 5**.

**Jedwali Na. 5: Ulinganisho wa Madaktari Bingwa/Wenye Ujuzi katika Ngazi za Vituo vya Afya Vilivyotembelewa**

| Kada | Huduma za Afya za Ngazi ya Juu | | Huduma za Afya za Ngazi ya Kati | | Vituo vya Afya vya Msingi | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uhitaji | Waliopo | Uhitaji | Waliopo | Uhitaji | Waliopo |
| Daktari Bingwa wa Mfumo wa Fahamu wa Watoto | H | 2 | H | 0 | H | H |
| Daktari Bingwa wa Watoto | 112 | 62 | 10 | 15 | H | 2 |
| Mwanasaikolojia wa Kliniki | H | 2 | H | H | H | H |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Wataalamu wa Kibingwa katika Vituo vya Afya wa Mwaka 2025

**Ufunguo:**
*H= Haujabainishwa*

107. **Jedwali Na. 5** linaonesha kuwa wataalamu mabingwa walijikita zaidi katika hospitali za ngazi ya juu, huku kukiwa hakuna mwanasaikolojia wa kliniki katika ngazi za kati na za msingi. Jedwali hilo pia linaonesha kuwa madaktari wa watoto walipatikana katika hospitali mbili (Igunga na Mbangala Rangi Tatu) tu kati ya hospitali tano za wilaya zilizotembelewa.

108. Kwa ujumla, huduma za kibingwa za mfumo wa fahamu ziliendelea kupatikana katika hospitali za ngazi ya juu, hali iliyosababisha ufikiwaji mdogo wa huduma hizo katika ngazi za mikoa na wilaya, ambako wananchi wengi huanza kupata huduma za rufaa. Hali hii ilikuwa kinyume na lengo la Serikali la kuweka wataalamu mabingwa katika hospitali za wilaya kwa taaluma nne kuu, ambazo ni: tiba ya ndani, afya ya watoto, uzazi na magonjwa ya wanawake, pamoja na upasuaji.

109. Vilevile, nilibaini mgawanyo usio na usawa wa wataalamu ambao ulitokana na matumizi ya vigezo vya ajira vilivyopitwa na wakati, mifumo ya ushauri elekezi isiyojitosheleza na msaada kutoka kwa wataalamu wa ngazi za juu usioridhisha, pamoja na upendeleo wa kuwaweka watumishi katika maeneo ya mijini.

### 3.3.4 Huduma za Urekebu Zisizojitosheleza

110. Nilibaini upungufu wa huduma za urekebu kwa watoto wenye matatizo ya mfumo wa fahamu nchini. Huduma za urekebu zilipatikana zaidi katika ngazi ya juu kwa asilimia 59, ilhali katika ngazi ya msingi zilipatikana kwa asilimia 13 pekee. Aidha, nilibaini kuwa huduma hizi hazikupatikana katika ngazi ya vituo vya afya na zahanati. Hali hii inaonesha kuwa watoto wenye matatizo ya mfumo wa fahamu hawakupata huduma za urekebu za kutosha katika ngazi mbalimbali za vituo vya afya. **Jedwali Na. 6** linaonesha hali ya upatikanaji wa huduma za urekebu.

**Jedwali Na. 6: Hali ya Upatikanaji wa Huduma za Urekebu**

| Ngazi ya Kituo cha Afya | Kiwango cha Upatikanaji (%) |
|---|---|
| Ngazi ya Juu | 59 |
| Ngazi ya Kati | 55 |
| Ngazi ya msingii | 13 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Wigo wa Huduma za Urekebu katika Vituo vya Afya vya Ngazi ya Juu, Kati na Msingi Mwaka 2025

111. Aidha, nilibaini kuwa tiba ya viungo (ndiyo ilikuwa huduma ya urekebishaji iliyopatikana kwa urahisi zaidi, katika kila kituo cha afya kuanzia Hospitali ya Taifa hadi hospitali za wilaya.

112. Pia, kulikuwapo na idadi ndogo ya wataalamu wa huduma za urekebu, hali iliyooneshwa na kutokuwapo kwa huduma za tiba ya usemi na lugha katika ngazi zote za vituo vya afya, isipokuwa katika ngazi ya kitaifa. Hali hii ilitokana na ukweli kwamba kulikuwa na taasisi moja tu ya mafunzo nchini iliyokuwa ikitoa programu ya tiba ya usemi na lugha. Upungufu na mgao usio na usawa wa huduma za urekebu uliwalazimisha watoto wenye matatizo ya mfumo wa fahamu na walezi wao kusafiri umbali mrefu kufuata huduma katika hospitali za ngazi ya juu, hali iliyosababisha ucheleweshaji wa upatikanaji wa huduma hizo na gharama kubwa za usafiri, hususani kwa familia zinazoishi vijijini.

### 3.3.5 Upungufu wa Takwimu kwa ajili ya Uamuzi Sahihi katika Utoaji wa Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu

113. Nilibaini upungufu wa takwimu kuhusu matatizo ya mfumo wa fahamu kwa watoto, kwani mifumo saba iliyokuwapo haikuwezesha kwa urahisi ujumuishaji na uchanganuzi wa takwimu za watoto wenye matatizo ya mfumo wa fahamu. Aidha, mfumo wa kufuatilia matatizo ya mfumo wa fahamu haukuhakikisha upatikanaji na ukamilifu wa takwimu muhimu katika ngazi ya msingii, kwani kulikuwa na takwimu za magonjwa mawili tu, ambayo ni kifafa

na ulemavu wa ubongo. Hali hii ilisababisha kuwapo kwa takwimu zisizokamilika kwa watoto wenye matatizo ya mfumo wa fahamu.

114. Aidha, nilibaini kuwa, utambuzi na ufuatiliaji wa watoto waliozaliwa waliopata changamoto ya kukosa hewa ya kutosha kwenye ubongo wakati wa kuzaliwa haukuwa wa kuridhisha, licha ya Mfumo wa Taarifa za Afya (MTUHA) Namba 21 kuanzishwa mwaka 2025 ukiwa na kipengele cha kuweka taarifa za watoto waliozaliwa na changamoto ya kukosa hewa ya kutosha kwenye ubongo. Hata hivyo, nilibaini kuwa katika ngazi ya msingi, takwimu sahihi za watoto wenye hali hiyo hazikurekodiwa ipasavyo.

115. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa Wizara ya Afya haikufanya utambuzi wala kutathmini kiwango cha uenevu wa matatizo ya mfumo wa fahamu nchini kutokana na kuwapo kwa mifumo mingi ya kufuatilia takwimu za matatizo ya mfumo wa fahamu pamoja na kutokuwapo kwa uthabiti katika ufuatiliaji wa taarifa hizo katika ngazi ya hospitali. Mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa taarifa za hospitali ya Taifa ya Muhimbili uliainisha makundi 99 ya matatizo ya mfumo wa fahamu, tofauti na mfumo wa Kielectroniki wa Usimamizi wa Hospitali ambapo ulianisha makundi nane na mfumo wa kidijitali unaotumika kukusanya, kuchambua, na kusimamia takwimu za afya katika ngazi ya wilaya ukianisha makundi mawili pekee, huku matatizo mengine ya mfumo wa fahamu yakiwekwa kwenye kundi la magonjwa mengine. Aidha, Mfumo wa Habari wa Usimamizi wa Uendeshaji wa Afya wa Serikali, Mfumo wa Habari wa Usimamizi wa Afya, na Mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa taarifa za hospitali ya Taifa ya Muhimbili ilifanya kazi kwa kujitegemea, ikiwa na miundo tofauti ya takwimu zinazokusanywa, viwango vya utoaji wa taarifa, na wigo wa ufuatiliaji wa matatizo ya mfumo wa fahamu, hali iliyosababisha kuwapo kwa taarifa zisizo na uwiano.

116. Changamoto zilizoibuliwa zilitokana na kutobainishwa ipasavyo kwa mahitaji ya takwimu kabla ya uundaji wa mifumo pamoja na kutozishirikisha kada zote husika wakati wa uundaji wa mifumo hiyo. Matokeo yake, takwimu zilizotumika katika kufanya maamuzi na kubaini afua za utekelezaji hazikukamilika.


## 3.4 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya vya Umma

117. Sehemu hii inatoa matokeo ya jumla ya ukaguzi kuhusu Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya vya Umma.

### 3.4.1 Upatikanaji Usiojitosheleza wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya vya Umma

118. Kupitia mapitio ya takwimu zilizotolewa kutoka Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Ugavi wa Dawa kuhusu upatikanaji wa dawa muhimu zilizopatikana Wizara ya Afya, nilibaini kuwa upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya afya vya umma uliendelea kuwa chini ya lengo la asilimia 79 kama ilivyoainishwa katika Mpango Mkakati wakati wa Wizara ya Afya wa Mwaka 2021/22–2025/26 kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 13.**

**Kielelezo Na. 13: Hali ya Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya vya Umma**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Upatikanaji wa Dawa Muhimu kutoka Wizara ya Afya wa Mwaka 2025

119. **Kielelezo Na. 13** kinaonesha upungufu wa dawa muhimu katika vituo vya afya vya umma katika miaka yote minne ya fedha iliyokaguliwa. Pengo kubwa zaidi lilionekana katika Mwaka wa Fedha 2022/23, ambapo upatikanaji wa dawa hizo ulikuwa chini ya lengo kwa asilimia 32. Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, pengo hilo lilipungua kwa asilimia 17 ikilinganishwa na lengo.

120. Kupitia mahojiano na maafisa kutoka Wizara ya Afya na ziara katika vituo vya afya, nilibaini kuwa vituo hivyo kwa ujumla vilipata alama za chini katika upatikanaji wa dawa muhimu. Hii ilitokana na jukumu lao kuu la kutoa huduma maalumu, jambo lililomaanisha kuwa havikuwa na akiba ya dawa zote zinazohitajika katika vituo vya afya vya ngazi za msingi. Hali hii iliendelea licha

ya orodha ya dawa muhimu kuonesha kuwa dawa hizo zinapaswa kupatikana daima katika ngazi hizo.

### 3.4.2 Upatikanaji wa Akiba ya Dawa Muhimu katika Maghala ya Kanda na Ghala Kuu la Bohari ya Dawa

121. Kulingana na taarifa za kifamasia zilizotolewa kutoka mfumo wa EPICOR, nilibaini kuwa akiba ya dawa muhimu katika maghala ya Bohari ya Dawa ilikuwa chini ya kiwango cha lengo la asilimia 90 lililotajwa katika Mpango Mkakati wa Nusu Muhula wa Bohari ya Dawa (2021–2026), kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 7**.

**Jedwali Na. 7: Hali ya Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Maghala ya Bohari ya Dawa**

| Mwaka wa Fedha | Zaidi ya Mwezi 1 (%) | Zaidi ya Miezi 4 (%) | Zaidi ya Miezi 9 (%) | Lengo (%) |
|---|---|---|---|---|
| 2021/22 | 57 | Hakukuwa na Takwimu | Hakukuwa na Takwimu | 90 |
| 2022/23 | 64 | 40 | 21 | 90 |
| 2023/24 | 60 | 37 | 19 | 90 |
| 2024/25 | 66 | 40 | 17 | 90 |

***Chanzo:*** Taarifa kutoka Bohari ya Dawa kuhusu Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Maghala ya Bohari ya Dawa Miaka 2021/22 – 2024/25

NAOT ISO 9001:2015 Certified

122. **Jedwali Na. 7** linaonesha kuwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 na 2024/25, upatikanaji wa dawa muhimu katika maghala ya Bohari ya Dawa ulikuwa kati ya asilimia 34 hadi asilimia 53, kiwango kilichozidi akiba ya mwezi mmoja. Hata hivyo, akiba hiyo haikutosha kuendeleza usambazaji wa dawa kwa kipindi cha mwezi mmoja hadi mitatu katika vituo vyote vya afya nchini.

123. Aidha, nilibaini kuwa upatikanaji wa akiba ya dawa muhimu kwa kiwango cha asilimia 60 hadi 63 ili kufanikisha usambazaji katika vituo vya afya kwa kipindi cha miezi minne hadi minane haukutosha. Upatikanaji wa dawa muhimu kwa kipindi cha zaidi ya miezi tisa ulipungua kutoka asilimia 21 katika Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi asilimia 17 katika Mwaka wa Fedha 2024/25.

124. Kwa ujumla, nilibaini kuwa upatikanaji usiotosha wa dawa muhimu katika Bohari ya Dawa ulisababishwa na mambo kadhaa, ikiwemo ukosefu wa makadirio sahihi, ununuzi na uzalishaji usiotosha wa dawa muhimu nchini, usambazaji usiotosha, pamoja na ufuatiliaji usiojitosheleza wa upatikanaji wake. Sababu hizi zimefafanuliwa kwa kina katika sehemu zifuatazo:

### 3.4.3 Makadirio na Mipango ya Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya vya Umma

125. Nilipitia Mipango ya Mwaka na makadirio yaliyofanywa na Wizara ya Afya pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na kutembelea vituo vya afya ili kutathmini upatikanaji wa dawa muhimu. Nilibaini upungufu uliokuwa kinyume na aya ya 1 ya Mwongozo wa Makadirio ya Vifaatiba, Tanzania Bara wa mwaka 2023, ambao inaelekeza vituo vya afya kufanya makadirio kuanzia ngazi ya chini kwenda ya juu na kuwasilisha makadirio hayo kwenye Bohari ya Dawa ifikapo tarehe 31 Januari kila mwaka ili kusaidia uaandaaji wa bajeti za serikali na maamuzi ya ununuzi, na kuhakikisha utoaji wa huduma za afya unaojitosheleza. Upungufu huo umefafanuliwa katika sehemu zifuatazo:

**(a) Wizara ya Afya, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Haikuandaa kwa Kiwango cha Kutosha Makadirio ya Kitaifa ya Mahitaji ya Dawa Muhimu**

126. Mapitio yangu ya Takwimu za Makadirio ya Kitaifa ya Mahitaji ya dawa muhimu kwa miaka ya fedha 2021/22 hadi 2024/25 yalionesha kuwa usahihi wa makadirio kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2021/22 hadi 2023/24 ulikuwa wastani wa asilimia 77, jambo lililokuwa kinyume na aya ya 1 ya Mwongozo wa Makadirio ya Vifaatiba, Tanzania Bara wa mwaka 2023, unaohitaji vituo vya afya vya umma kutumia mbinu ya makadirio kutoka ngazi ya chini kwenda juu ili kukadiria kwa usahihi mahitaji ya vifaatiba ili kubainisha mahitaji yanayohitajika kwa ajili ya kuhudumia wananchi.

127. **Jedwali Na. 8** linaonesha usahihi wa makadirio kuanzia Miaka ya Fedha 2021/22 hadi 2024/25.

**Jedwali Na.8: Usahihi wa Makadirio ya Dawa Muhimu**

| Mwaka wa Fedha | Usahihi wa Makadirio ya Mahitaji(%) |
|---|---|
| 2021/22 | 82 |
| 2022/23 | 72 |
| 2023/24 | 77 |
| 2024/25 | Makadirio hayajakamilika |
| **Wastani** | **77** |

***Chanzo:*** Ripoti za Mikutano ya Mwaka ya Timu ya Kitaifa ya Makadirio kuanzia Miaka ya Fedha 2020/21 hadi 2024/25

128. **Jedwali Na. 8** linaonesha kuwa makadirio ya mahitaji yaliyokuwa sahihi zaidi yalikuwa asilimia 82 katika Mwaka wa Fedha 2021/22, huku makadirio

yasiyo sahihi zaidi yakiwa asilimia 72 katika Mwaka wa Fedha 2022/23. Hali ya usahihi wa makadirio kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 ilikuwa bado haijakamilika, kwani hesabu za matumizi ya vifaatiba zilikuwa zinaendelea wakati wa ukaguzi. Upungufu uliobainika katika usahihi wa makadirio ya mahitaji ya kitaifa ya dawa muhimu ulitokana na ukosefu wa zana za kuzingatia makadirio pamoja na kutokuwapo kwa maandalizi ya shughuli za makadirio ya chini kwenda juu.

**(b) Kutokuwapo kwa Usahihi katika Takwimu Zilizotumika kwenye Makadirio**

129. Nilibaini kuwapo kwa takwimu zisizo sahihi zilizotumika katika makadirio, kama inavyothibitishwa na dosari zifuatazo:

**(i) Kutokujumuishwa kwa Dawa Muhimu katika Makadirio ya Mahitaji**

130. Kupitia mapitio ya Ripoti za mwaka za Timu ya Kitaifa ya Makadirio, nilibaini kuwa mahitaji ya baadhi ya dawa muhimu, kama vile Dawa ya Kupunguza Maumivu Makali wakati wa Uchungu wa Kujifungua, Adrenalini, sindano ya kupunguza maumivu makali na kiunganishi cha ABOD, hayakukadiriwa wala kujumuishwa katika makadirio ya kitaifa ya mahitaji. Licha ya Wizara ya Afya kuonesha katika Ripoti za mwaka za Timu ya Kitaifa ya Makadirio kwamba baadhi ya dawa muhimu hazikukadiriwa, Wizara haikuwa na kumbukumbu za kuthibitisha kiasi cha dawa muhimu ambazo hazikujumuishwa katika makadirio kwa miaka ya fedha 2021/22 hadi 2024/25. Hivyo basi, sikuweza kuthibitisha kiwango cha dawa muhimu ambazo hazikukadiriwa katika kipindi cha ukaguzi huu.

131. Kuachwa kwa dawa muhimu katika makadirio ya mahitaji kulisababishwa na uelewa mdogo miongoni mwa watumishi waliokuwa wakifanya makadirio, hususani katika vituo vya afya vya ngazi ya msingii kama vile zahanati. Nilibaini kuwa shughuli za makadirio katika zahanati zote nilizotembelea zilikuwa zikifanywa na watumishi wasiokuwa na mafunzo ya fani ya ufamasia.

**(ii) Kujumuishwa kwa Dawa Zisizo Muhimu katika Makadirio ya Mahitaji**

132. Mapitio ya ripoti za mwaka za Timu ya Kitaifa ya Makadirio yalionesha kuwa vituo vya afya vya umma vimekuwa vikikadiria mahitaji ya dawa zisizo muhimu kama vile sindano ya Aminofilini, vidonge vya Aminofilini, dawa za mfumo wa Neva na vidonge vya maambukizi ya bakteria licha ya dawa hizi kuondolewa na Timu ya Kitaifa ya Makadirio wakati wa zoezi la makadirio. Ingawa Wizara ya Afya ilionesha katika Ripoti za mwaka za Timu ya Kitaifa ya

Makadirio kwamba dawa zisizo muhimu zilijumuishwa katika makadirio ya mahitaji, nilibaini kuwa Wizara ya Afya ilishindwa kuwasilisha ushahidi wa kiasi cha dawa hizo katika makadirio kwa Miaka ya Fedha 2021/22 hadi 2024/25. Aidha, nilibaini kuwa Wizara ilishindwa kutoa takwimu hizo kutokana na utunzaji kumbukumbu usiojitosheleza katika makadirio ya dawa muhimu.

### (c) Ukosefu wa Ulinganifu na Ufanyaji Kazi wa Pamoja kwa Mifumo Inayotumika Wakati wa Makadirio na Ufuatiliaji wa Dawa Muhimu

133. Kupitia ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA katika vituo vya afya vya ngazi ya halmashauri nilivyotembelea, nilibaini kuwa mfumo wa GoT-HoMIS, unaotumika na idara za tiba katika vituo vya afya vya ngazi ya halmashauri, na mfumo wa e-LMIS, unaotumika na vituo vyote vya afya kwa ajili ya kuagiza na kuripoti dawa muhimu, havikuwa na uwezo wa kubadilishana taarifa. Hali hii ilikuwa kinyume na Kanuni ya 25 ya Kanuni za Jumla za Serikali za Kielektroniki za mwaka 2020, inayozitaka mamlaka ya serikali, mtandao na taasisi za umma kushirikiana katika uundaji na utekelezaji wa mifumo ya TEHAMA, na kuzingatia ulinganifu wa mifumo wakati wa maboresho yake.

134. Vilevile, maafisa wa idara za tiba katika vituo vya afya vya ngazi ya halmashauri nilivyowahoji walieleza kuwa ukosefu wa ulinganifu wa kutosha kati ya mifumo hiyo miwili ulihitaji uhamishaji wa taarifa za matumizi kutoka GoT-HoMIS kwenda e-LMIS kwa njia ya kawaida isiyo ya kielektroniki. Hali hii imeathiri ushirikiano kati ya mifumo kupitia ubadilishanaji wa taarifa katika utoaji wa huduma za Kielektroniki za Serikali

135. Ubadilishanaji wa taarifa usio wa kielektroniki kutoka GoT-HoMIS kwenda e-LMIS wakati wa makadirio mara nyingi husababisha makosa katika uwasilishaji wa takwimu za matumizi. Makosa haya ni pamoja na uwasilishaji wa kujirudia wa dawa na kuachwa kwa takwimu za matumizi za baadhi ya dawa muhimu.

### (d) Utunzaji wa Kumbukumbu Usiojitosheleza wa Nyaraka katika Mchakato wa Mapitio ya Makadirio ya Mahitaji

136. Mahojiano na Maafisa kutoka Timu za Usimamizi wa mfumo wa usimamizi wa afya – Mkoa, Halmashauri na kwenye Vituo vya Afya vilivyotembelewa, pamoja na ukaguzi wa mfumo wa e-LMIS, yalibaini kuwa makadirio ya mahitaji kutoka vituo vya afya yalipitiwa na kuidhinishwa na msimamizi wa kila kituo kabla ya kuwasilishwa kwenye mfumo. Aidha, Baraza la usimamizi wa Mfumo wa Afya wa Mkoa zilipitia takwimu za makadirio ya

mahitaji zilizowasilishwa kutoka vituo vya afya, na kuziidhinisha kupitia mfumo wa e-LMIS, ili kujua iwapo zilikuwa na dosari au kutoidhinishwa.

137. Katika hatua zote za zoezi la makadirio ya mahitaji, mchakato wa mapitio na uidhinishaji ndani ya mfumo ulikosa nyaraka ambazo zingethibitisha na kutoa uhakika kwa mamlaka ya kuidhinisha hatua inayofuata. Ukosefu huo wa nyaraka uliinyima mamlaka inayofuata ushahidi wa kuonesha kuwa takwimu za makadirio zilizoidhinishwa zilikuwa zimepitiwa. Dosari katika mfumo zilikiuka Aya za 3.2.1, 3.2.2, na 3.2.3 za Mwongozo wa Makadirio ya Vifaatiba Tanzania Bara (2023), zinazotaka mabaraza ya usimamizi wa mifumo ya afya ngazi ya mkoa, halmashauri na kwenye vituo vya afya kuhakiki takwimu za makadirio ya mahitaji zilizotayarishwa na mfumo. Wakati wa uidhinishaji wa makadirio na nyaraka zilizowasilishwa, marekebisho na mabadiliko yote huchukuliwa kuwa tayari yamefanyiwa kazi.

138. Nilibaini pia kuwa mabaraza ya usimamizi wa afya katika vituo vyote vya afya nilivyotembelea hayakutoa ripoti zozote za mchakato wa makadirio kwa ajili ya Msimamizi wa Kituo cha Afya kupitia na kuidhinisha. Aidha, hakukuwa na barua za maelezo, uidhinishaji na uwasilishaji kwa ngazi inayofuata kwa ajili ya mapitio zaidi, kama inavyohitajika kwa mujibu wa aya ya 3.2 ya Mwongozo wa Makadirio ya Vifaatiba, Tanzania Bara (2023).

139. Kutokana na makadirio yasiyo sahihi ya mahitaji ya dawa muhimu, nilibaini pengo kati ya mahitaji yaliyokadiriwa na matumizi halisi katika vituo vya afya vya umma nchini kote. Jedwali **Na.9** linaonesha thamani ya jumla ya makadirio ya mahitaji ikilinganishwa na matumizi halisi kwa Miaka ya Fedha 2021/22 hadi 2024/25.

**Jedwali Na. 9: Thamani ya Jumla ya Makadirio ya Mahitaji ya Dawa Muhimu Ikilinganishwa na Matumizi Halisi**

| Mwaka wa Fedha | Thamani ya Makadirio ya Mahitaji (Sh. bilioni) | Matumizi Halisi (Sh. bilioni) | Tofauti (Sh. bilioni) |
|---|---:|---:|---:|
| 2021/22 | 483.9 | Hakukuwa na Taarifa | Haihusiki |
| 2022/23 | 492.1 | 683.5 | 191.4 |
| 2023/24 | 668.0 | 867.5 | 199.5 |
| 2024/25 | 657.6 | Haikubainishwa | Haihusiki |

***Chanzo:*** Ripoti za Mikutano ya Mwaka ya Timu ya Kitaifa ya Makadirio ya Mahitaji ya Dawa kwa Miaka ya Fedha 2021/22 hadi 2024/25

140. **Jedwali Na. 9** linaonesha kuwa makadirio ya kitaifa ya mahitaji hayakuwa ya kutosha, kwani mara kwa mara yalikuwa chini ya matumizi halisi katika miaka yote ya fedha. Tofauti kati ya makadirio ya mahitaji na matumizi halisi ilikuwa kati ya Shilingi bilioni 191.4 na bilioni 199.5. Aidha, nilikusudia kutathmini kiasi na thamani ya makadirio ya mahitaji ya dawa muhimu ikilinganishwa na matumizi yake halisi katika ngazi mbalimbali za vituo vya afya. Hata hivyo, Wizara ya Afya haikutoa taarifa hizo, ikieleza kuwa kulikuwa na upungufu katika utunzaji wa kumbukumbu kuhusu makadirio na matumizi ya dawa muhimu.

141. Makadirio yasiyo sahihi ya mahitaji husababisha tofauti kati ya dawa zilizopangwa na zinazohitajika, na hivyo kusababisha upungufu wa dawa usio wa lazima au ziada ya dawa. Hali hii husababisha upatikanaji mdogo na usio thabiti wa dawa muhimu katika vituo vya afya vya umma na kuongezeka kwa dawa zilizokwisha muda wake ndani ya mnyororo wa usambazaji wa dawa na vifaatiba.

### 3.4.4 Bohari ya Dawa Haikuzalisha Dawa Muhimu ili Kuhakikisha Kiwango cha Kutosha cha Akiba Yake

142. Kupitia mapitio ya Ripoti ya Utendaji wa Biashara ya Mwaka ya Bohari ya Dawa kwa mwaka 2023, nilibaini juhudi mbalimbali zilizofanywa na Bohari ya Dawa. Juhudi hizo zilijumuisha usajili wa Kampuni ya Uzalishaji ya Bohari ya Dawa MediPharm Limited. MediPharm ni kampuni ndani ya Bohari ya Dawa inayohusika na uzalishaji wa dawa na vifaatiba. Ilianzishwa mwaka 2023 kwa ajili ya kushughulikia uzalishaji wa vifaatiba pamoja na dawa muhimu, ambayo ni miongoni mwa majukumu ya msingi ya Bohari ya Dawa.

143. Juhudi nyingine iliyofanywa ilikuwa uzalishaji wa vifaatiba katika viwanda vya Bohari Keko na Idofi. Ukaguzi ulibaini kuwa katika Miaka ya Fedha 2022/23 hadi 2023/24, Bohari ya dawa ilizalisha barakoa 624,950 na jozi 2,029,033 za glovu katika kiwanda cha Idofi, pamoja na kiwanda cha Maski za Upasuaji na Maski za N95 kilichopo Bohari ya Dawa Keko, lakini hakuna dawa muhimu zilizozalishwa katika kipindi hicho.

144. Ukaguzi wangu ulibaini sababu kadhaa zilizozuia Bohari ya Dawa kuzalisha dawa muhimu. Sababu hizo ni pamoja na ukosefu wa rasilimali za kifedha na rasilimaliwatu kwa ajili ya uzalishaji wa ndani wa dawa muhimu, pamoja na ukosefu wa maendeleo ya viwanda vya kutengeneza dawa muhimu nchini. Maelezo ya kina kuhusu mambo haya yamewasilishwa katika sehemu zinazofuata hapa chini.

## (a) Bohari ya Dawa Haikuweza Kupata Rasilimaliwatu na za Kifedha za Kutosha ili Kuendeleza Uzalishaji wa Ndani wa Dawa Muhimu

145. Kupitia mapitio ya Taarifa za Utendaji za Bohari ya Dawa kwa kipindi cha Miaka ya Fedha 2021/22–2024/25, nilibaini kuwapo kwa upungufu mkubwa katika ujenzi wa viwanda vya kuzalisha dawa muhimu. Kwa Kiwanda cha Idofi kilichopo Mkoa wa Njombe, ni Shilingi bilioni 8.85 pekee (sawa na asilimia 31) kati ya bajeti ya jumla ya Shilingi bilioni 28.16 zilitolewa, huku viwanda binafsi vikipewa kati ya asilimia 27 na 34 ya bajeti iliyoidhinishwa. Matokeo yake, maendeleo ya ujenzi yalibaki kuwa madogo, takribani asilimia 23 kufikia Mwaka wa Fedha 2024/25, ambapo shughuli muhimu kama usimikaji wa mitambo, mifumo ya usimamizi wa taka, mifumo ya upatikanaji wa umeme, na miundombinu ya TEHAMA hazikukamilika. Utekelezaji huu unakwenda kinyume na Kifungu cha 4(2)(a) cha Sheria ya Bohari ya Dawa ya mwaka 1993 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2021), kinachoitaka Bohari ya Dawa kuanzisha mifumo bora ya uzalishaji na usambazaji wa vifaa vya tiba.

146. Aidha, licha ya kuidhinishwa kwa Taarifa ya Mwisho ya Upembuzi yakinifu mwezi Desemba 2022, Bohari ya Dawa haikuanza ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha dawa muhimu kilichopangwa kujengwa katika Eneo la Viwanda la Zegereni, Kibaha mkoani Pwani. Upembuzi huo ulikadiria gharama za jumla za ujenzi kuwa Shilingi bilioni 53.29, ikijumuisha shilingi bilioni 21.22 kwa mitambo na vifaa na Shilingi bilioni 32.06 kwa kazi za ujenzi, pamoja na gharama za uendeshaji zilizofikia Shilingi bilioni 28.38. Hata hivyo, mapitio ya bajeti za Bohari ya Dawa yalithibitisha kuwa hakuna fedha zilizotengwa wala kutolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Ingawa Bohari ya Dawa iliomba Shilingi bilioni 100 kutoka Wizara ya Fedha mwaka 2023 kwa ajili ya kuunga mkono uwekezaji wa mitaji, fedha hizo hazikutolewa, jambo lililokwamisha mpango wa uzalishaji wa ndani wa dawa muhimu.

147. Mbali na changamoto za kifedha, nimebaini pia upungufu mkubwa katika rasilimaliwatu kwa ajili ya uzalishaji wa dawa ndani ya nchi. Upembuzi yakinifu kwa mwaka 2022 ulitaka kuanzishwa kwa miundo ya kiutendaji kwa hatua za awali na za uendeshaji kamili za shughuli za uzalishaji wa Bohari ya Dawa. Hata hivyo, hadi kufikia Novemba 2025, Bohari ya Dawa haikuandaa muundo kamili wa shirika kwa kampuni yake tanzu ya uzalishaji. Ingawa Bohari ya Dawa ilimshirikisha mshauri elekezi mwezi Oktoba 2025 ili kuandaa muundo wa shirika, mipango ya kimkakati na ya biashara, pamoja na bajeti ya uendeshaji kwa Bohari ya Dawa, bado idadi ya watumishi ni ndogo. Mahojiano na maafisa wa Bohari ya Dawa yalionesha kuwa ni mameneja wa muda tu waliopo, na majukumu yao kwa sasa yamejikita katika uzalishaji wa barakoa na

glavu, hali inayozuia maendeleo kuelekea uzalishaji kamili wa dawa muhimu nchini.

### (b) Bohari ya Dawa Haikuendeleza Ipasavyo Viwanda vya Ndani vya Kuzalisha Vifaatiba

148. Kupitia mapitio ya Mipango Mkakati na Mipango ya Uendeshaji ya Bohari ya Dawa kwa kipindi cha Miaka ya Fedha 2020/21–2024/25, nilibaini kuwa Bohari ya Dawa haikuanzisha kiwanda chochote cha kuzalisha dawa muhimu kama ilivyopangwa. Matokeo haya hayalingani na Malengo ya 38 na 39 ya Mpango Mkakati wa Bohari ya Dawa wa mwaka 2021–2026, yaliyokusudia kuanzisha viwanda sita vya serikali na kiwanda kimoja cha ubia kati ya sekta ya umma na binafsi kufikia Juni 2026, ambapo ujenzi ulipangwa kuanza Mwaka wa Fedha 2021/22. Kufikia Mwaka wa Fedha 2024/25, ni viwanda viwili pekee vya serikali, kiwanda cha glovu cha Idofi mkoani Njombe na kiwanda cha barakoa jijini Dar es Salaam ndivyo vilivyojengwa, huku viwanda vinne vya serikali vilivyopangwa na kiwanda cha ubia kimoja havikuanzishwa, na hakukuwa na kiwanda cha dawa muhimu kilichokuwa kinafanya kazi.

149. Nimebaini pia kuwa ucheleweshaji wa kuidhinisha kiwanda cha dawa cha ubia umechangia kwa kiasi kikubwa kutojengwa kwa viwanda vilivyopangwa. Mapitio ya Taarifa ya Utendaji ya Robo ya Nne ya Mwaka wa Fedha 2022/23 yalionesha kuwa Wizara ya Fedha, kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, haikuidhinisha muundo wa biashara wa ubia uliopendekezwa, uliomtaka mwekezaji kujenga, kuendesha na kisha kukikabidhi kiwanda kwa Bohari ya Dawa baada ya kipindi kisichozidi miaka 25. Serikali ilikataa muundo huo kutokana na hofu kwamba kiwanda kingekuwa kimepitwa na wakati wa kukabidhiwa, hivyo Bohari ya Dawa ikalazimika kuandaa muundo mbadala wa biashara. Aidha, mapitio ya utendaji wa Bohari ya Dawa na maombi ya fedha za mitaji yalionesha kuwa kutotolewa kwa fedha kutoka serikali kuu kulikuwa sababu kuu ya kushindwa kujenga viwanda vilivyolengwa katika kipindi cha ukaguzi.

150. Kutokana na kutokuwapo kwa viwanda vya kuzalisha dawa muhimu, Bohari ya Dawa iliendelea kutegemea kwa kiwango kikubwa uagizaji kutoka nje. Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, ni Shilingi bilioni 21.63 pekee (sawa na Asilimia 7.1) kati ya Shilingi bilioni 304.56 zilizopangwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba zilipatikana kutoka kwa wazalishaji wa ndani. Hivyo basi, Bohari ya Dawa haikufanikiwa kupata faida zilizotarajiwa kama zilivyoainishwa kwenye Taarifa ya Mwisho ya upembuzi yakinifu (2022), ambayo ilikadiria faida baada ya kodi kuanzia Shilingi bilioni 4.93 katika mwaka wa kwanza hadi Shilingi bilioni

6.27 kufikia mwaka wa tano. Kutokana na ucheleweshaji wa ujenzi na uendeshaji wa kiwanda cha uzalishaji dawa cha Zegereni Kibaha, Bohari ya Dawa haikufikia faida jumla ya Shilingi bilioni 27.84 iliyokadiriwa kwa kipindi cha miaka mitano ya mwanzo ya uendeshaji.

### 3.4.5 Bohari ya Dawa Haikununua na Kudumisha Kiwango cha Kutosha cha Akiba ya Dawa Muhimu

151. Kupitia mapitio ya Mipango ya Ununuzi ya Bohari ya Dawa na taarifa za utekelezaji kwa kipindi kilichokaguliwa, nimebaini utekelezaji mdogo wa ununuzi uliopangwa, ukiwa na tofauti kati ya asilimia 21.1 hadi 37, kinyume na Kanuni ya 77 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013. Utekelezaji wa ununuzi wa vifaatiba uliopangwa uliendelea kuwa mdogo, ukiwa asilimia 20 kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, asilimia 26 kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, na asilimia 34.5 kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, hali inayoonesha upungufu ya kudumu licha ya utendaji wa kipekee katika Mwaka wa Fedha 2022/23 ambapo utekelezaji ulizidi mpango kwa asilimia 37. Nilibaini pia upungufu wa fedha uliotokana na kuongezeka kwa madeni ya Hospitali za Umma kwa dawa muhimu zilizokwisha kusambazwa awali. Aidha, nilibaini kuwa utekelezaji usiojitosheleza wa mipango ya ununuzi umechangia moja kwa moja upungufu wa dawa muhimu katika hospitali za umma, kama inavyoonekana kupitia kupungua kwa viwango vya uagizaji wa dawa.

152. Aidha, nimebaini kuwa Bohari ya Dawa haikununua dawa muhimu kwa wakati, na ucheleweshaji wa usambazaji ulizidi kikomo cha siku 180 kwa bidhaa zisizo na mikataba, kinyume na Mpango Mkakati wa Watu wa Nusu Muhula wa Bohari ya Dawa (2021–2026). Ucheleweshaji ulikuwa mkubwa zaidi Mwaka wa Fedha 2022/23, ambapo asilimia 93 ya bidhaa zilizonunuliwa ziliwasilishwa kwa kuchelewa, ingawa maboresho yalionekana katika miaka iliyofuata, huku ucheleweshaji ukipungua kwa asilimia 26 Mwaka wa Fedha 2023/24 na kupungua zaidi kwa asilimia 30 Mwaka wa Fedha 2024/25. Ingawa Bohari ya Dawa ilihusisha ucheleweshaji na mahitaji ya nyaraka kutoka kwa wasambazaji wa nje, upatikanaji wa vyombo vya usafirishaji, na kiwango cha chini cha uangizaji, ukaguzi ulibaini upungufu katika utekelezaji wa masharti ya mikataba kama sababu kuu. changamoto hii ya ufuatiliaji wa mikataba ilikuwa kati ya asilimia 31 hadi 67 katika kipindi cha ukaguzi, hali iliyopunguza uwezo wa Bohari ya Dawa kudhibiti utendaji wa wasambazaji na kuchangia akiba ya dawa kubaki chini ya viwango vilivyolengwa. Pamoja na upungufu huu, mapitio ya faili moja ya ununuzi yaliyoteuliwa yalithibitisha kuwa masharti ya ushindani na uwazi chini ya Kifungu cha 64(1) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 yalizingatiwa.

### 3.4.6 Bohari ya Dawa Haikusambaza Dawa Muhimu kwa Ufanisi ili Kuhakikisha Upatikanaji kwa Wakati

153. Nimebaini kuwa Bohari ya Dawa haikuhakikisha uchukuaji wa dawa muhimu kwa wakati katika bandari, kati ya Mwaka wa Fedha 2021/22–2024/25. Sehemu kubwa ya shehena ziliidhinishwa baada ya muda wa msamaha kuruhusiwa, kuanzia asilimia 97 Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi asilimia 32 Mwaka wa Fedha 2024/25, kinyume na Sheria ya Bohari ya Dawa ya mwaka 1993 (kama ilivyorekebishwa) na masharti ya tozo za Mamlaka ya Bandari Tanzania. Ucheleweshaji huu ulisababishwa zaidi na uratibu usiojitosheleza wa Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini, wasambazaji kuwasilisha nyaraka za usafirishaji kwa kuchelewa na wasambazaji, ucheleweshaji wa utoaji wa vibali vya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania, pamoja na changamoto za mpito wakati majukumu ya uchukuaji yaliporejeshwa Bohari ya Dawa. Matokeo yake, Bohari ya Dawa ilipata gharama zilizotokana na uhifadhi wa mizigo bandarini zilizofikia shilingi milioni 562.12 katika kipindi cha ukaguzi, hali iliiweka Bohari ya Dawa kwenye gharama zisizohitajika na hatari ya kupanda kwa bei za dawa.

154. Nimebaini pia kuwa Bohari ya Dawa haikuwa na miundombinu ya kutosha ya kuhifadhi na kusambaza ili kuwezesha usambazaji wa dawa muhimu kwa wakati. Eneo la maghala lililopo lilikuwa mita za mraba 68,859 dhidi ya mahitaji ya mita za mraba 100,000 (upungufu wa asilimia 31), huku uwezo wa hifadhi ya baridi ukiwa mita za ujazo 1,789 ikilinganishwa na mahitaji ya mita za ujazo 2,500 (upungufu wa asilimia 28). upungufu huu ulikiuka matakwa ya kisheria kuhusu mifumo bora ya hifadhi na usambazaji na yaliongeza changamoto za kifedha kutokana na kuongezeka kwa madeni ya hospitali za umma. Madeni yaliyosalia yalipanda kutoka shilingi bilioni 13.21 Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi shilingi bilioni 123.27 Mwaka wa Fedha 2024/25, hali iliyopunguza uwezo wa Bohari ya Dawa kuwekeza katika miundombinu ya hifadhi ya ziada na kuchangia kushindwa kufikia lengo la upatikanaji wa dawa muhimu kwa kiwango cha asilimia 90.

155. Vilevile, nilibaini Bohari ya Dawa haikuhakikisha usafirishaji wa dawa muhimu kwa wakati kwenda kwenye vituo vya afya vya umma, kwani usafirishaji mara nyingi ulizidi kikomo cha siku 20 kilichowekwa kwenye Mkataba wa Huduma kwa Wateja na taratibu za uendeshaji wa ugavi. Ucheleweshaji ulianzia siku 21 hadi kufikia siku 1,535 katika baadhi ya vituo, huku ucheleweshaji wa utoaji wa ankara ukihusisha kati ya asilimia 4 na 31 ya maagizo katika vituo vilivyotembelewa. Ingawa kiwango cha dawa ambazo hazikusafirishwa kilipungua kwa muda katika baadhi ya mikoa, baadhi ya vituo vilikuwa na viwango vya juu vya uagizaji ambao haukusafirishwa, hadi kufikia asilimia 38.

Changamoto hizi zilisababishwa na kuongezeka kwa madeni ya vituo vya afya, utendaji usioridhisha wa wasambazaji ambapo asilimia 47 ya wasambazaji walikuwa na utendaji usioridhisha pamoja na madeni ya Bohari ya Dawa kwa wasambazaji yaliyofikia shilingi bilioni 180.43. Kwa ujumla, changamoto hii ilipunguza uwezo wa Bohari ya Dawa kutimiza maagizo, kuchangia upungufu wa dawa, na kupunguza uwezo wa Bohari ya Dawa kukidhi mahitaji ya dawa muhimu katika vituo vya afya vya umma.

### 3.4.7 Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, na Bohari ya Dawa Hawakufanya Ufuatiliaji wa Upatikanaji wa Dawa Muhimu Unaojitosheleza

156. Licha ya uwekezaji uliofanywa na Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Bohari ya Dawa katika mifumo na miongozo kama Afya SS, ILS, Mfuko wa Mzunguko wa Vifaatiba na Mwongozo wa Kamati ya Tiba na Dawa, pamoja na mafunzo kwa watumishi, ukaguzi ulibaini upungufu wa kudumu katika ufuatiliaji na usimamizi shirikishi katika mnyororo wa usambazaji wa dawa muhimu. Changamoto hii iliathiri uangalizi wa kina katika vituo vya afya, kupunguza ufanisi wa mnyororo wa ugavi, na kupunguza maboresho yaliyokusudiwa katika matumizi ya rasilimali, usalama wa dawa na upatikanaji wake, hali inayoonesha haja ya kuimarisha utekelezaji na mifumo ya uwajibikaji.

157. Kuhusiana na kuharibika na uondoaji wa dawa zilizokwisha muda wake, ukaguzi ulibaini kuwa ingawa bohari ya dawa iliendelea kudumisha viwango vya kuharibika chini ya lengo la Mpango Mkakati wa Muda kati wa Awamu ya Tatu kwa asilimia 1, kiwango hicho kilionesha mwelekeo wa kuongezeka, kikapanda kutoka asilimia 0.41 katika Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi asilimia 0.97 Mwaka wa Fedha 2024/25, huku thamani ya dawa zilizoharibika ikifikia Shilingi bilioni 6.50 Mwaka wa Fedha 2024/25. Sababu zilizochangia ni pamoja na makadirio yasiyo sahihi, kupokea dawa zenye muda mfupi wa matumizi kutokana na kukosekana kwa uzalishaji wa ndani wa bidhaa zenye muda mfupi wa matumizi, akiba kupita kiasi, mabadiliko ya miongozo ya matibabu, mahitaji madogo au yasiyotabirika, ucheleweshaji wa usafirishaji unaoathiri muda wa matumizi ya dawa, na upungufu katika ufuatiliaji wa akiba kwa ajili ya usambazaji upya.

158. Katika ngazi ya vituo vya afya, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ilipanga na kutekeleza ufuatiliaji wa upatikanaji na kuharibika kwa dawa mara moja katika Mwaka wa Fedha 2023/24 na kuacha miaka ya fedha 2021/22, 2022/23 na 2024/25 bila shughuli za ufuatiliaji zilizopangwa au kutekelezwa. Uangalizi huu usiojitosheleza pamoja na ukosefu wa mfumo madhubuti wa usambazaji

upya uliosababisha kuendelea kuharibika kwa dawa katika vituo vya afya vilivyotembelewa, ambapo jumla ya dawa zilizoharibika zilifikia thamani ya shilingi milioni 171.55 (2021/22–2024/25), ikiwemo hasara kubwa katika Hospitali ya Benjamin Mkapa na ongezeko la hali hii katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

159. Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI haikutekeleza ukaguzi na ufuatiliaji wa dawa katika miaka ya fedha 2021/22 na 2022/23, na kiwango cha usimamizi kilipungua Mwaka wa Fedha 2024/25. Wakati huo huo, mabaraza la Usimamizi wa Mfumo wa Afya wa Mkoa, Wilaya na Vituo vya Afya yalionesha upungufu kati ya shughuli zilizopangwa na zilizotekelezwa, changamoto katika uandaaji wa taarifa, na mikutano isiyo thabiti. Ingawa Wizara ya Afya ushauri wa matumizi ya mfumo mpya wa ugavi uliongezeka, hata hivyo haukufikia halmashauri zote na ulikosa mpangilio wa kujenga uwezo. Zaidi ya hayo, utaratibu wa Bohari ya Dawa wa kushughulikia malalamiko ulikumbwa na ucheleweshaji wa mrejesho na utatuzi wa baadhi ya kesi, hali iliyodhoofisha uratibu, uwajibikaji na kuathiri imani kwa wateja.

## 3.5 Matokeo ya Ukaguzi juu ya Utoaji wa Huduma za Afya za Uzazi

160. Sehemu hii ina matokeo ya ukaguzi kuhusu utoaji wa Huduma za Afya ya Uzazi nchini Tanzania.

### 3.5.1 Upatikanaji Mdogo wa Huduma za Dharura za Uzazi na Mtoto Mchanga

161. Nilibaini utoaji usioridhisha wa Huduma za Dharura za Uzazi na Mtoto Mchanga katika Vituo vya afya vya mwanzo ambayo ilikuwa kinyume na Kifungu cha 5.1.5 cha Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya 2021-2026, ambapo dhamira ya Wizara ya Afya katika kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya, kwa ushirikiano na wadau, Serikali ilitakiwa kuhakikisha kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za dharura za uzazi na watoto wachanga, kwa msisitizo maalumu juu ya upatikanaji thabiti na matumizi sahihi ya vifaa na Taratibu muhimu za kuokoa maisha wakati wa kujifungua na huduma za haraka baada ya kujifungua. Upatikanaji mdogo wa huduma ya dharura ya uzazi ulihusishwa na upungufu unaofafanuliwa hapa chini.

#### (a) Utoaji Duni wa Huduma za Dharura za Uzazi na Watoto Wachanga

162. Nilibaini kuwa utoaji wa huduma za dharura za uzazi na kwa watoto wachanga haukuwa wa kuridhisha kwa ngazi zote mbili; ya msingi na ya jumuishi kwa kuzingatia ikiwa kazi muhimu za ishara zilitekelezwa katika miezi mitatu

iliyopita. Katika ngazi ya zahanati Kituo cha kwanza kufikiwa na wanawake wengi wajawazito), ni huduma rahisi pekee ndio zilipatikana mara kwa mara: zahanati zote 5/5 zilitoa antibiotiki za sindano, huku dawa za kusisimua mji wa uzazi na dawa za kuzuia kifafa cha mimba zikipatikana katika vituo 4/5 na 3/5 mtawalia, na huduma ya kumsaidia mtoto mchanga kupumua katika vituo 4/5. Hata hivyo, huduma muhimu za kuokoa maisha ambazo zinahitaji ujuzi wa hali ya juu na vifaa maalumu hazikupatikana kwa kiasi kikubwa: kutolewa kwa kondo la nyuma kwa mkono kulifanyika katika vituo 3/5 pekee, na usafishaji wa masalia ya ujauzito kulifanyika katika vituo 2/5 kutokana na upungufu wa ujuzi wa watumishi. Aidha, uzazi wa kusaidiwa kwa vifaa ulipatikana katika vituo 2/5 pekee, hasa kutokana na ukosefu wa vifaa vya vakyumu na koleo-uzazi.

163. Upungufu huu ulichangiwa na uhaba wa wafanyakazi wenye mafunzo na vifaa tiba maalumu, vilivyochangiwa na ugawaji wa rasilimali uliopendelea vituo vya ngazi za juu, na kuviacha vituo vya ngazi ya msingi vikiwa havina uwezo wa kutoa huduma za dharura za uzazi, hivyo kuchochea ongezeko kubwa la uhitaji wa mifumo ya rufaa.

164. Kwa upande wa huduma jumuishi nilibaini tofauti kubwa kati ya ngazi ya kituo na upungufu wa utayari hata pale ambapo huduma zilikuwapo. Hospitali za Wilaya zilionesha upatikanaji wa juu wa CEmONC (201 kati ya 219, au asilimia 92), lakini ni vituo 491 tu kati ya 924 (asilimia 53) vilitoa CEmONC, ikimaanisha karibu nusu ya vituo vilikosa uwezo kamili wa upasuaji na huduma za kuongezewa damu. Ingawa kiwango cha jumla ya utayari wa CEmONC kilikuwa kwa wastani wa asilimia 71, vikwazo vikuu vilibaki haswa katika vifaa vya ganzi, vinavyopatikana katika asilimia 21 tu ya vifaa vyote, utoshelevu wa usambazaji wa damu, na utoshelevu wa asilimia 56 ( usalama kwa asilimia 60).

165. Kutolingana kati wafanyakazi wa ngazi za juu za vituo vya afya wenye mafunzo ya upasuaji (asilimia 95) na anesthesia (asilimia 92) dhidi ya vifaa vichache vya anesthesia na huduma zisizokamilika za damu zinaonesha kuwa vituo vinaweza kuwa na ujuzi lakini havina zana na mifumo muhimu ya kutoa upasuaji wa dharura kwa usalama. Kwa hivyo, wanawake walio na shida wana hatari ya kucheleweshwa au kukosa huduma ya kuokoa maisha, na kusababisha vifo vya mama na watoto wachanga vinavyoweza kuzuilika kwa matumizi ya utaalam wa kliniki uliopo.

**(b) Kutolingana kati ya Idadi ya Watumishi wa Afya wenye Ujuzi na Mahitaji ya Huduma ya Uzazi katika Vituo vya Afya**

166. Nilibaini uhaba mkubwa na upatikanaji usiotosheleza wa wafanyakazi wa afya katika ngazi zote za huduma, kinyume na Mpango Mkakati wa Tano wa

Sekta ya Afya na Matumizi Yaliyokusudiwa ya Kipimo cha Ukubwa wa Kazi katika Mahitaji ya Ajira – Uchanganuzi wa Uwekaji Vipaumbele na Uboreshaji. Upungufu wa wafanyakazi ulikuwa maubwa, na kufikia asilimia 67 katika hospitali za wilaya, asilimia 58 katika zahanati, na asilimia 43 katika vituo vya afya, wakati hospitali za taifa na za mikoa zilikuwa na upungufu wa asilimia 28 na asilimia 15, mtawalia. Uwiano wa wafanyakazi ulitofautiana na viwango vya kitaifa, na wodi za wafanyakazi zilifanya kazi kwa uwiano wa mkubwa kama 1:10 katika hospitali za wilaya na 1:7 katika vituo vya afya na zahanati, ikizuia ufuatiliaji endelevu, ufanyikaji kwa wakati, na utoaji wa huduma za dharura za uzazi na mtoto mchanga unaojitosheleza.

167. Pia, nilibaini tofauti za mijini na vijijini na mchanganyiko wa ujuzi usio na usawa, na maeneo ya vijijini yalikabiliwa na uhaba mkubwa wa wakunga, madaktari wa uzazi, na madaktari wa ganzi licha ya idadi kubwa ya wanaojifungua. Maeneo ya mijini yalichangia asilimia 54 ya wafanyakazi wa afya ikilinganishwa na asilimia 46 katika maeneo ya vijijini, wakati mikoa kama vile Mwanza na Kigoma ilikuwa na viwango vya chini vya wafanyakazi (wafanyakazi wenye ujuzi 14-16 kwa kila watu 10,000). Kazi nyingi kupita kiasi, zenye wastani wa saa 52 kwa wiki, zilichangia uchovu wa kazi, kuongezeka kwa kuondoka kazini kwa wafanyakazi, na kushuka kwa ubora wa huduma. Changamoto hizi zilisukumwa na upangaji wa rasilimaliwatu usiojitosheleza, matumizi ya sehemu ya Kiashiria cha Mahitaji ya Watumishi kulingana na Wingi wa Kazi motisha ndogo ya kupelekwa vijijini, na mafunzo ya huduma za dharura za uzazi na Watoto wachanga ambayo hayajafadhiliwa, hatimaye kuongeza hatari za uzazi na watoto wachanga, kuongeza ukosefu wa usawa wa kiafya, na kupunguza maendeleo kuelekea lengo la 3.1 la Malengo ya Maendeleo Endelevu.

**(c) Mgao wa Bajeti ya Huduma za Afya ya Uzazi Isiyojitosheleza**

168. Nilibaini upungufu mkubwa wa ufadhili na kuongezeka kwa utegemezi wa wafadhili katika huduma za afya ya uzazi, kinyume na Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya V (2021-2026), ambao unasisitiza kupanua ufadhili wa afya ya ndani. Uchambuzi wa bajeti za afya ya uzazi, mama, mtoto mchanga, mtoto na vijana walio katika umri wa balehe za Miaka ya Fedha 2022/23 - 2024/25 ulionesha kupungua kwa sehemu ya ufadhili wa ndani kutoka asilimia 85 hadi asilimia 68, wakati ufadhili wa nje ya nchi uliongezeka kutoka asilimia 15 hadi asilimia 32. Licha ya uwezo mkubwa wa matumizi ya mfuko wastani wa asilimia 94.7 katika kipindi hicho mgao halisi haukuzidi asilimia 50 ya bajeti iliyoidhinishwa, ikionesha kuwa kikwazo kikuu cha utoaji wa huduma kilitolewa kwa fedha pungufu. Mnamo Mwaka wa Fedha 2024/25, fedha za ndani zilitolewa kwa asilimia 41 tu ya kiasi kilichoidhinishwa, wakati fedha za kigeni zilitolewa

kwa asilimia 59, na kuendelea na utegemezi wa ufadhili wa nje. Pengo hili la ufadhili lilionekana zaidi katika makadirio ya mahitaji ya bidhaa za Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto Mchanga, Mtoto na Vijana, ambapo upungufu wa dola milioni 19.7 mnamo 2025 ulileta hatari kubwa ya upungufu wa bidhaa nchini kote (kuishiwa na akiba ya bidhaa).

169. Ukaguzi huu pia ulibaini ukosefu wa usawa na utegemezi wa wafadhili katika ufadhili wa Mipango Kabambe ya Afya katika Halmashauri. Mgao kwa kila mtu kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 ulitofautiana, kutoka Shilingi 16,310 jijini Dar es Salaam hadi Shilingi 7,394 mkoani Mwanza, huku mikoa ya Dodoma na Kigoma pia ikikabiliwa na ufadhili mdogo kwa kila mtu licha ya mahitaji makubwa ya huduma. Muundo huu wa ugawaji haukuwa ukitegemea idadi ya watu, kinyume na Mkakati wa Ufadhili wa Afya (2016-2026), na hivyo kusababisha upatikanaji usio sawa wa rasilimali za afya katika mikoa yote. Aidha, ufadhili wa nje ulichangia sehemu kubwa zaidi ya bajeti ya afya katika halmashauri (asilimia 41.37), wakati ufadhili wa ndani ulitegemea sana uchangiaji wa gharama na ada za watumiaji (asilima 25.35), huku uhamisho wa fedha kutoka serikalini ukichangia asilimia 18.6 tu. Muundo huu wa ufadhili unaweka mfumo wa afya katika hatari endapo misaada ya wafadhili itayumba na inasisitiza hitaji la kuimarisha uhamasishaji endelevu wa rasilimali za ndani ili kuhakikisha upatikanaji wa fedha ulio na usawa na unaotabirika kwa huduma za afya ya uzazi.

### 3.5.2 Ukusanyaji wa Taarifa za Vifo vya Uzazi, Ufuatiliaji, na Utoaji wa Ripoti Usiojitosheleza

170. Mapitio yangu ya Ripoti ya Ufuatiliaji na Majibu ya Vifo vya Mama na Uzazi kwa Miaka Sita (2018-2023), iliyotolewa Machi 2025, nilibaini ukusanyaji takwimu za vifo vya wajawazito usiojitosheleza, ufuatiliaji na kuripoti. Hii ilikuwa kinyume na Lengo la 3.3.3 la Miongozo ya Ufuatiliaji na Majibu ya Vifo vya Mama na Uzazi, 2019, ambayo inasisitiza juu ya utoaji wa taarifa, mapendekezo, na uchukuaji wa hatua ili kuondoa vifo vya wajawazito vinavyoweza kuzuilika katika vituo vya afya.

171. Ukusanyaji wa taarifa za vifo vya wajawazito, ufuatiliaji, na utoaji wa kuripoti usiojitosheleza ulionekana katika utekelezaji usioridhisha wa mfumo wa Ufuatiliaji na Majibu ya Vifo vya Mama na Uzazi, matumizi machache ya taarifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Vifo vya Uzazi na Watoto Wachanga kwa hatua zinazotegemea ushahidi, na utunzaji wa kumbukumbu usiojitosheleza. Maelezo ya kila kipengele yametolewa hapa chini.

**(a) Utekelezaji Usioridhisha wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Vifo vya Uzazi na Watoto Wachanga**

172. Nilibaini kuwa Wizara ya Afya na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI hazikutekeleza kikamilifu Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Vifo vya Uzazi na Viini-tete katika vituo vya afya, kinyume na Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Vifo vya Uzazi na Watoto Wachanga wa mwaka 2019. Changamoto zilizobainika ni pamoja na kushindwa kufanya ukaguzi wa vifo vya uzazi ndani ya siku saba zinazohitajika, kamati za Ufuatiliaji na Mwitikio wa vifo vya Uzazi zisizofanya kazi au zisizofanya kazi katika vituo kadhaa, mikutano ya ukaguzi isiyo ya kawaida na ambayo haikuwekewa kumbukumbu vizuri, na ufuatiliaji na maoni yasiyolingana ya kiwango cha kitaifa. Hivyo, asilimia 80 ya vifo vya wajawazito vilivyotokea katika vituo havikufanyiwa mapitio, ambapo ni vifo 71 tu kati ya 358 vilivyofanyiwa mapitio kwenye Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Vifo vya Uzazi na Watoto Wachanga Matumizi haya madogo ya Mfumo wa Ufuatiliaji na na Tathmini ya Vifo vya Uzazi na Viini-tete yaliodhoofisha dhumuni lake lake la la kubaini mambo yanayoweza kuzuilika na kuchochea hatua za marekebisho katika ngazi ya vituo na mifumo.

173. Licha ya kupungua kwa kiasi kwa vifo vya uzazi vilivyoripotiwa kutoka 1,640 mnamo 2020 hadi 1,498 mnamo 2024, visibabishi vikuu vya vifo ambavyo ni utokaji wa damu wakati wa uzazi (asilimia 44-46), kifafa cha mimba (asilimia 16-17), na maambukizi baada ya uzazi au matatizo ya utoaji mimba yalikuwa karibu asilimia 9 hadi 10 vilionekana kutobadilika. Hali hii iliashiria udhaifu katika kutafsiri matokeo ya vifo vya uzazi na viini-tete kuwa hatua Madhubuti za kuzuia vifo. Aidha, nilibaini kuwa ni Mipango Kazi 44 tu ndiyo iliyoandaliwa kwa ajili ya vifo 71 vilivyofanyiwa maptitio, jambo liliacha pengo la asilimia 38 katika hatua zilizopendekezwa. Vilevile, kutofautiana kati ya rejista za kituo na taarifa za Mfumo wa Taarifa za Afya wa Wilaya kulidhoofisha ufuatiliaji na ufanyikaji maamuzi. Changamoto hizi zilitokana na uchache wa watumishi, mafunzo yasiyotosheleza, wingi wa kazi, utanzaji duni wa nyaraka, usimamizi usiojitosheleza, na changamoto za usimamizi wa takwimu. Kwa pamoja, mabo haya yalisababisha kujirudia kwa vifo vya uzazi kutokana na visababishi vinavyofanana, kuchelewesha hatua za kurekebisha, na kupunguza ufanisi wa Mfumo wa Ufuatiliaji wa Vifo vya Uzazi na Viini-tete katika kuboresha matokeo ya afya ya uzazi.

ISO 9001:2015 Certified

**(b) Matumizi Yasiyotosheleza ya Takwimu Zilizokusanywa kwa kwa ajili ya Hatua au Mapendekezo ya Kupunguza Vifo vya Uzazi**

174. Nilibaini kuwa Wizara ya Afya na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI hazikutumia kwa ufanisi takwimu zilizokusanywa za vifo vya uzazi kusanifu,

kuweka kumbukumbu, na kutekeleza zinazozingati ushahidi , kinyume na Lengo la 3.3.3 la Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Vifo vya Uzazi na Watoto Wachanga waa mwaka 2019. Ingawa mapitio ya ya Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Vifo vya Uzazi na Watoto Wachanga yalikusudiwa kutambua sababu za kifo na kutoa suluhisho linaloweza kutekelezeka, matokeo hayakutafsiriwa kwa utaratibu katika hatua zilizolengwa. Matokeo yake, vifo vya akina mama vinavyoweza kuzuilika viliendelea kujirudia. Aidha, ukaguzi ulibaini vifo 198 kutoka Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25 vya akina mama vilivyotokana na uzazi katika vituo vilivyotembelewa, ambavyo vyote vilionekana vingeweza kuepukika na haswa vilisababishwa na kuvuja damu wakati wa uzazi na shida ya shinikizo la juu la damu wakati wa ujauzito. Kushindwa huku kulipunguza madhumuni ya Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Vifo vya Uzazi na Watoto Wachanga, kupoteza rasilimali zilizowekezwa katika ufuatiliaji na ukaguzi, na kuchangia kudorora kwa upunguzaji wa vifo vya uzazi.

175. Nilibaini ufuatiliaji usiotesheleza wa mapendekezo yaliyotokana na ukaguzi wa Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Vifo vya Uzazi na Watoto Wachanga. Kati ya Mipango 44 ya utekelezaji iliyotengenezwa ni 25 tu (asilimia 57) ilikuwa na ushahidi wa ufuatiliaji, na kuacha pengo la asilimia 43. Hali hii ilichangiwa na kukosekana kwa utaratibu wa wazi wa ufuatiliaji uliopangwa, pamoja na ukosefu wa mfumo wa ufuatiliaji wa idadi, utegemezi wa taarifa zisizo za kielektroniki, majukwaa ya utoaji taarifa yaliyogawanyika ~~(MPDSR,),~~ muundo wa kamati isiyokamilika, uhaba wa wafanyakazi, na miundombinu michache ya TEHAMA. Kwa kuongezea, Wizara ya Afya ilikosa kanzidata ya kitaifa au mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji ili kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Vifo vya Uzazi na Watoto Wachanga katika viwango vyote. Hali hii, ilisababisha hatua zilizokubaliwa kutotekelezwa mara kwa mara, na kusababisha vifo vya uzazi kueendelea, na hivyo kuchelewesha maendeleo yakupunguza vifo vya uzazi na kufikiwa kwa shabaha ya 3.1 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu.

### (c) Utunzaji wa Kumbukumbu za Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Vifo vya Uzazi na Watoto Wachanga Usiojitosheleza

176. Nilibaini kuwa, ni idadi ndogo tu ya vifo vya uzazi vilivyotolewa taarifa ndiyo vilikuwa na nyaraka zilizojitosheleza. Taarifa hizo ni za vifo 37 kati ya 259 katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, 23 kati ya 84 katika Hospitali za Wilaya, na 11 kati ya 15 katika Vituo vya Afya. Hali hii ilikuwa kinyume na Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Vifo vya Uzazi na Watoto Wachanga wa mwaka 2019, ambao unahitaji nyaraka kamili na kuripoti vifo vyote vya uzazi na Watoto wachanga kwa kutumia mbinu za kawaida. Upungufu huu ulichangiwa na uwezo mdogo wa watumishi na ukosefu wa mafunzo kuhusiana na uandaaji wa nyaraka

za Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Vifo vya Uzazi na Watoto Wachanga, usimamizi mrejesho usio thabiti kutoka kwa Wizara ya Afya na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, na kukosekana kwa uwasilishaji sahihi na mifumo jumuishi ya usimamizi wa taarifa. Matokeo yake, takwimu za vifo vya uzazi na watoto wachanga hazikuwa sahihi na za kuaminika, jambo ambalo lilidhoofisha uchambuzi wa mwenendo wa vifo vya uzazi, kupunguza utambuzi wa sababu zinazoweza kuzuilika, na kupunguza ufanisi wa hatua zinazotegemea ushahidi katika maamuzi ya kisera ya kupunguza vifo vya uzazi.

### 3.5.3 Utendaji wa Mfumo wa Rufaa Usiojitosheleza

177. Nilibaini kuwa mfumo wa rufaa nchini Tanzania haukuwa ukifanya kazi ipasavyo. Hii ilitokana na mfumo kuwa na sifa ya uendeshaji usiokamilika katika vituo vya afya. Mfumo huo pia ulikuwa na nyaraka zisizojitosheleza, na usimamizi usiojitosheleza katika ngazi za Halmashauri na Mikoa . Hali hii ilikuwa kinyume na Mpango wa Taifa wa tatu (2021/22–2025/26) na Mwongozo wa Husuma za Kilini za Wajawazito ANC (2018), ambayo inaelekeza kuwapo kwa mfumo wa rufaa uliyopangwa kuanzia ngazi ya zahanati/vituo vya afya kwa huduma za msingi za dharura za uzazi na watoto wachanga hadi hospitali za wilaya/mkoa kwa huduma jumuishi za dharura za Uzazi na watoto wachanga.

178. Utendaji usiojitosheleza wa mfumo wa rufaa uliosababishwa na usambazaji mdogo wa miongozo ya rufaa kwa watumishi na vifaa, mafunzo yasiyojitosheleza kwa watumishi wa afya juu ya taratibu za rufaa na vigezo ambavyo vinaleta upungufu katika maarifa na ujuzi, pamoja na mifumo isiyojitosheleza ya uwajibikaji na usimamizi wa kutosha kutoka katika ngazi za juu za utawala kama vile Mabaraza ya Usimamizi wa Mfumo wa Afya wa Mkoa na Wilaya ambayo hayakusimamia ufuataji wa taratibu na kufanyia kazi changamoto zilizojitokeza.

179. Kwa hivyo, rufaa za dharura za uzazi ziliongeza hatari ya matatizo ya uzazi, na kusababisha kuongezeka kwa magonjwa ya uzazi na viwango vya vifo ambavyo vilipunguza kasi ya utekelzaji wa malengo ya kitaifa chini ya Mpango Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya na Mpango Mkakati wa Taifa wa Tatu wa Huduma za Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto Mchanga, Mtoto na Vijana (2021/22–2025/26), pamoja na maendeleo kuelekea Shabaha ya 3.1 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu.

180. Aidha, nilibaini ufuatiliaji usiojitosheleza wa utendaji wa mfumo wa rufaa za uzazi, kinyume na Mwongozo wa Taifa wa Mfumo wa Rufaana Mfumo wa Tanzania wa UboreshajiUbora, kwani uanzishaji wa rufaa, ukamilifu wake,

na maoni yake hayakufuatiliwa mara kwa mara katika vituo vyote. Ingawa asilimia 96.7 ya rufaa 151,802 zilizoanzishwa katika kipindi cha 2021/22-2024/25 zilikamilika, rufaa 5,075 (asilimia 3.3) hazikujulikana zilipoishia, ikionesha upungufu katika ufuatiliaji na uratibu kati ya vifaa vya kurejelea na kupokea.

181. Changamoto hizi zilichangiwa na kukosekana kwa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya rufaa za uzazi, ujumuishaji mdogo wa vigezo vya rufaa katika ukaguzi wa kawaida wa utendaji, utunzaji wa kumbukumbu na mifumo ya urejeshaji isiyojitosheleza. Kadhalika, changamoto hizi zilisababishwa na ujumuishaji wa kidigitali usiojitosheleza pamoja na vituo vingi kutegemea mifumo ya karatasi na kutotumia kikamilifu Mfumo wa Taarifa za Afya wa Wilaya kwa ajili ya ufuatiliaji kwa wakati. Matokeo yake, tofauti kati ya rufaa zilizoanzishwa na zilizokamilika iliendelea kuwapo, na kuchangia kucheleweshwa wa matibabu, mahitaji ya huduma za dharura za uzazi na watoto wachanga ambayo hayajatimizwa pamoja na kuongezeka kwa hatari kwa afya ya uzazi na watoto wachanga

182. Aidha, nilibaini ucheleweshaji na vikwazo katika awamu zote za mfumo wa rufaa ya uzazi, pamoja na kucheleweshwa kufanya maamuzi, usafirishaji, na kuanzishwa kwa huduma katika vituo vilivyopokea wagonjwa. Muda wa rufaa mara nyingi ulizidi viwango vilivyowekwa, ufuatialiaji wa huduma ulichelewa kwa saa kadhaa au zaidi ya saa 24, usafiri ulichukua saa 1.5 hadi 2 badala ya saa moja, na hatua za dharura mara nyingi zilichelewa kwa zaidi ya dakika 30 baada ya kuwasili. Ucheleweshaji huu ulitokana hasa na magari ya wagonjwa kutofanya na kutoa na vifaa vya kutosha, miundombinu mibovu ya barabara, uhaba wa watumishi na msongamano katika vituo vinavyopokea wagonjwa. Pia, uratibu na makabidhiano duni, utunzaji wa kumbukumbu usiojitosheleza, na ukosefu wa mafunzo ya kurejesha utendaji wa moyo na mapafu na matumizi ya kifaa cha mshtuko wa umeme wa moyo kwa madereva wa gari za wagonjwa. Kutokana na hali hiyo, ucheleweshaji wa rufaa hasa kati ya vituo vya afya umeendelea kuwa chanzo kikuu cha vifo vya mama na watoto wachanga vinavyoweza kuzuilika, na kuathiri maendeleo kuelekea Shabaha ya 3.1 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu.

### 3.5.4 Kampeni za Uhamasishaji na Programu za Elimu Zisizotosheleza kwa Wanawake Wajawazito kuhusu Afya ya Uzazi

183. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, utekelezaji wa mipango ya elimu na uhamasishaji wa afya ya uzazi na Wizara ya Afya, haukutosheleza na haukuwa na usawa katika mikoa mbalimbali. Hali hii ilidhihirishwa na ukweli kwamba

chanjo ilielekezwa katika maeneo ya mijini licha ya maeneo ya vijijini kuwa karibu asilimia 60 ya idadi ya watu kwa sababu uhamasishaji wa mambo ya afya ulitegemea sana vyombo vya habari kama vile runinga na mabango. Hali hii ilitokana na kukosekana kwa mipango ya kila mwaka, mikakati ya kitaifa, na mifumo ya wazi ya hatua za utekelezaji ili kuongoza hatua za ngazi ya jamii.

184. Aidha, tofauti katika ufahamu wa afya ya uzazi ziliendelea kuwapo, hasa kwa wanawake wa vijijini, na kuchangia hatari kubwa za mimba zisizopangwa, kutopangwa vizuri kwa nafasi kati ya watoto wanaozaliwa, na shida za afya ya uzazi zinazoweza kuzuilika.

185. Ukaguzi wangu pia ulibaini kuwapo kwa uhamasishaji na uungwaji mkono usiotosheleza kwa programu za elimu ya afya ya uzazi ngazi ya jamii ili kuongeza uelewa wa umma, maandalizi ya kujifungua, na ushiriki wa wanaume, kinyume na aya ya 5.1.2 ya Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa Tano (2021-2026). Sera na taratibu za afya ya uzazi kwa kiasi kikubwa zilitanguliza huduma za kliniki za kituo juu ya elimu na kinga ya jamii, na kusababisha ufikiaji mdogo zaidi kwa mama wajawazito, mipango isiyojitosheleza ya kujiandaa kwa kuzaliwa, na mikakati isiyoelezewa vizuri na isiyotekelezwa ya ushiriki wa wanaume. Upungufu huu ulisababishwa na ufadhili usiolingana na duni wa kukuza afya kwa kiasi kikubwa kutegemea msaada wa wafadhili na ucheleweshaji wa kupeleka watumishi wa afya ya jamii waliofunzwa chini ya Mpango Jumuishi wa Afya wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii ambapo zaidi ya watumishi 9,000 waliopatiwa mafunzo walibaki bila kuyatumia maarifa waliyoyapata kwa sababu ya vikwazo vya ufadhili na uratibu usioridhisha kati ya Wizara ya Afya na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI. Kutokana na hali hiyo, juhudi za uhamasishaji wa jamii zilicheleweshwa, uendelevu wa programu ulipungua, Watumishi wa Afya Ngazi ya Jamii waliofunzwa walipoteza morali na kuacha kazi, na maendeleo katika kuimarisha ujuzi wa afya ya uzazi, maandalizi, na maamuzi ya pamoja katika ngazi za kaya na jamii yalibaki duni licha ya ahadi za kisera.

186. Ukaguzi huu pia ulibaini kuwa, programu za afya ya uzazi, hususani uhamasishaji wa jamii na hatua za elimu, zilikosa viashiria muhimu vya utendaji vilivyoainishwa wazi ili kupima ufanisi na matokeo yake, jambo ambalo liliathiri usimamizi na uwajibikaji unaozingatia matokeo. Ingawa takwimu za kila mara zilikusanywa kupitia mfumo wa Taarifa za Afya Ngazi ya Wilaya, takwimu hizi ziliangazia zaidi mahitaji ya rasilimali na matokeo ya utoaji wa huduma na hazikupima mabadiliko ya tabia, uelewa wa jamii, maandalizi ya kujifungua, ushiriki wa wanaume, au utekelezaji wa mapendekezo ya Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Vifo vya Uzazi na Watoto Wachanga.

187. Kutokuwapo kwa mfumo wa kina wa matokeo unaounganisha shughuli, matokeo na athari pamoja na upungufu ya mfumo wa Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za Afya, uwezo mdogo wa ufuatiliaji na tathmini, na msisitizo juu ya viashiria vya msingi vya kituo, kulisababisha ufuatiliaji usiolingana wa utendaji katika mikoa yote. Matokeo yake, ufanisi wa elimu ya afya ya uzazi na afua za jamii haukuweza kuthibitishwa, hali iliyozuia ufanyaji maamuzi usiozingatia ushahidi, kudhoofisha uwajibikaji na kipaumbele cha mikakati ya uelewa wa jamii licha ya uwekezaji mkubwa katika huduma ya afya ya uzazi.

## 3.6 Athari za Changamoto Zilizobainika katika Kuyafikia Malengo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu

188. Utoaji wa huduma za afya ya mfumo wa neva kwa watoto usijitosheleza, unadhoofisha ufikiwaji wa Lengo la 3 la Maendeleo Endelevu (Afya Njema na Ustawi) na Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, hasa yale yanayolenga kupunguza vifo vinavyoweza kuzuilika na kuboresha maisha ya watoto na maendeleo ya rasilimaliwatu. Upatikanaji mdogo wa huduma bobezi za mfumo wa fahamu, uwezo mdogo wa uchunguzi, na upungufu wa watumishi waliofunzwa husababisha kuchelewa kwa utambuzi na usimamizi wa hali ya mfumo wa fahamu, na kusababisha ulemavu unaoweza kuepukika, magonjwa ya muda mrefu, na vifo vya watoto. Changamoto hii inapunguza maendeleo kuelekea Shabaha ya 3.2 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu kuhusu kuzuia vifo vinavyoweza kuzuilika vya watoto wachanga na watoto na inazuia malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ya kuwa na idadi ya watu wenye afya na tija inayoweza kuchangia maendeleo ya taifa.

189. Utoaji usiojitoshelezawa dawa muhimu uliathiri moja kwa moja matokeo ya afya na uimara wa mfumo wa afya. Jambo hili liliathiri Shabaha ya 3.8 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu kuhusu Huduma ya Afya kwa Wote na vipaumbele vya ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo waa Taifa wa Miaka Mitano kuhusu upatikanaji wa huduma bora za afya na za bei nafuu. Ukosefu wa akiba ya madawa, usambazaji usiojitosheleza, na utegemezi wa wasambazaji wa nje vilivuruga mwendelezo wa huduma. Pia, uliongeza gharama za nje ya mfuko, na kupunguza imani ya umma katika vituo vya afya. Hali hii ilipunguza ufanisi wa hatua za kuzuia na kutibu magonjwa, kuleta vikwazo katika kupunguza magonjwa na vifo, na kupunguza kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano katika kuimarisha mifumo ya dawa na

uzalishaji wa ndani ili kuhakikisha upatikanaji wa kuaminika wa dawa za kuokoa maisha.

190. Utoaji wa wa huduma za afya ya uzazi zisizojitosheleza ikiwa pamoja na uhaba wa watumishi wenye ujuzi, huduma za dharura za uzazi, mifumo ya rufaa, na ufadhili ni kikwazo kikubwa katika kufikia Shabaha ya 3.1 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu kuhusu kupunguza vifo vya uzazi na ahadi za Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa za kuwa na usawa, huduma bora ya mama na watoto wachanga. Ucheleweshaji wa huduma, usafiri duni wa dharura, na huduma duni huongeza vifo vya uzazi na watoto wachanga vinavyoweza kuzuilika, hasa katika maeneo ya vijijini na yale yasioyofikiwa kirahisi. Kwa pamoja, upungufu huu unapunguza maendeleo ya kitaifa kuelekea Lengo la 3 la Malengo ya Maendeleo Endelevu. Pia, yanaongeza ukosefu wa usawa wa kiafya, na kudhoofisha matokeo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kwa kuongeza gharama za afya zinazoweza kuepukika, kupunguza tija, na kukwamisha maendeleo jumuishi ya kijamii na kiuchumi.

ISO 9001:2015 Certified

## SURA YA NNE

## UTOAJI WA HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII NA HUDUMA ZA KISHERIA KWA WANANCHI

### 4.1 Utangulizi

191. Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na Utoaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii na Huduma za Kisheria kwa Wananchi. Pia, inafafanua maeneo ya ukaguzi, taasisi za serikali zilizohusishwa katika ukaguzi, uhusiano wa ukaguzi na Malengo ya Maendeleo Endelevu pamoja na Mpango wa tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano, na athari zake.

192. Kaguzi za ufanisi zilihusishwa katika sura hii ni pamoja na:

(a) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Upatikanaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria kwa Wananchi Wasiojiweza; na

(b) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Chakula, Makazi na Malezi kwa Wazee.

#### 4.1.1 Usuli

193. Utoaji wa msaada wa kisheria nchini Tanzania umejikita katika Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21, ambayo inafafanua kuwa wananchi wasiojiweza ni wale wasiomudu gharama za huduma za kisheria binafsi. Msaada wa kisheria una lengo la kuhakikisha kuwa msaada unatolewa katika makundi yanayohitaji ili haki iweze kupatikana. Jitiada za utoaji wa msaada wa kisheria zilianza mwaka 1969 kama juhudi za wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na baadaye zikapanuka kuwa mfumo kamili. Mfumo huu ulirasimishwa kupitia Sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017, ambayo inatambua msaada wa kisheria kama haki ya msingi, na tangu wakati huo umeendelea kukua na kuimarika.

194. Kiutawala, Wizara ya Katiba na Sheria inahusika kusimamia masuala ya haki za binadamu na utoaji wa msaada wa kisheria. Msajili wa msaada wa kisheria anawajibika kusajili, kusimamia na kukagua watoa huduma, wakati Bodi ya Ushauri ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria inatoa mwongozo wa sera na kusikiliza rufaa dhidi ya maamuzi ya Msajili. Mahakama ya Tanzania pia ina jukumu muhimu, ambapo majaji na mahakimu wamepewa mamlaka ya kutoa msaada wa kisheria katika mashauri ya jinai na ya madai pale ambapo haki

inahitajika. Aidha, Jeshi la Polisi na Huduma za Magereza kisheria zina wajibu wa kuanzisha mifumo inayowezesha upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa watu walioko mahabusu. Watoa huduma za msaada wa kisheria wamegawanyika katika makundi mawili: Watoa huduma waliosajiliwa kama vile Taasisi zisizo za Kiserikali, asasi za kiraia, na wasaidizi za kisheria, na watoa huduma kwa mujibu wa sheria ikiwemo Chama Cha Wanasheria Tanganyika, ambao wapo chini ya Sheria maalumu za Bunge na wamepewa msamaha wa ufuataji wa taratibu za usajili.

195. Sambamba na hilo, Tanzania inakabiliwa na ongezeko la kimahitaji kwa wazee nchini. Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003, iliyorejewa 2024, mtu anachukuliwa kuwa ni mzee akiwa na umri wa kuanzia miaka 60 na kuendelea. Umri huu unatumika katika misamaha ya huduma za afya, pensheni, na Mifumo ya Uhamishaji wa Fedha. Kihistoria, wazee walihudumiwa na familia zao, lakini utandawazi na uhamiaji mijini umepunguza jukumu hili, na kuwaacha wazee wengi wakiwa wapweke, wakitelekezwa, na kukosa mahitaji ya msingi.

196. Juhudi za Serikali za kuwasaidia wazee zilianza katika miaka ya 1970 kwa kuanzisha nyumba za wazee, ambazo awali zilihusishwa na vituo vya wagonjwa wa ukoma. Sera ya Taifa ya Wazee ililenga kukuza ustawi, kulinda haki, na kuimarisha mifumo ya familia na jamii katika kuwahudumia.

197. Hata hivyo, changamoto bado zipo, hasa katika ubora wa huduma za kijamii na miundombinu iliyopo kwa ajili ya wazee. Changamoto hizi zinaongezeka kutokana na mabadiliko ya idadi ya watu yaliyosababisha matarajio ya ukomo wa maisha kuongezeka kutoka miaka 52.8 mwaka 2000 hadi miaka 66.8 mwaka 2021, huku idadi ya wazee ikiongezeka kutoka milioni 2.5 mwaka 2012 hadi takribani milioni 3.5 mwaka 2022.

### 4.1.2 Utoaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii na Huduma za Kisheria kwa Wananchi kama Unavyohusishwa na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

198. Sehemu hii inaelezea kuhusu utoaji wa huduma za ustawi wa jamii na huduma za kisheria kwa wanachi zinavyohusiana na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Maelezo ya kina yametolewa hapa chini.

## (a) Utoaji wa huduma za ustawi wa jamii na msaada wa kisheria kwa wananchi unavyohusiana na malengo ya maendeleo endelevu

199. Utoaji wa huduma za ustawi wa jamii na huduma za kisheria kwa wananchi unahusiana kwa karibu na lengo namba 16 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (Amani, Haki na Taasisi Imara), kuhakikisha kwamba makundi yaliyotengwa wakiwemo wale wasio na uwezo wa kifedha wanapata haki kupitia mamlaka yaliyotolewa kwa mahakama, na kukuza utawala wa sheria katika ngazi ya kitaifa na kimataifa kama ilivyoainishwa katika shabaha 16.3. Ulinganifu huu pia unahusiana na lengo namba 5 (Usawa wa Kijinsia) na lengo namba 10 (Kupunguza Ukatili wa Kijamii na Kiuchumi), kwani watoa msaada wa kisheria wanaosimamiwa na Wizara ya Katiba na Kisheria wanasaidia jamii katika masuala muhimu kama vile ukatili wa majumbani, mirathi, umiliki wa ardhi, taratibu za kifamilia, na mengineyo.

200. Vilevile, utoaji wa huduma za kijamii kwa wazee ni muhimu katika kufanikisha lengo namba 1 (shabaha 1.3: Ulinzi wa Kijamii), linalotaka kuwapo kwa mifumo ya kitaifa inayolinda maskini na watu walio hatarini. Pia, utoaji wa huduma za kijamii kwa wazee unasaidia kufanikisha lengo namba 3 (shabaha 3.8: Upatikanaji wa Huduma za Afya kwa Wote) kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu za afya na ulinzi wa kifedha.

## (b) Huduma za Ustawi wa Jamii na Huduma za Kisheria kwa Wananchi zinavyohusiana na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano

201. Juhudi za kutoa huduma za kisheria zimelenga kutekeleza moja kwa moja Mpango wa tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano, ambao unatambua utawala bora, utawala wa sheria, na uwajibikaji kama nguzo za maendeleo endelevu. Sambamba na hilo, Mpango mkakati wa Wizara ya Katiba na Sheria chini ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano unalenga kutoa huduma za msingi za kijamii kwa wazee wote wasio na msaada katika nyumba za wazee kufikia Juni, 2026. Bodi ya Ushauri ya Kitaifa ya Huduma za Msaada wa Kisheria pia inaimarisha mfumo huu kwa kutoa mwongozo wa sera na kulinda msaada wa kisheria kama haki ya kipaumbele inayojenga imani ya wananchi katika mfumo wa haki.

202. Chini ya lengo la Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano la *"kufanikisha ushindani na uendelezaji wa viwanda kwa ajili ya maendeleo ya binadamu,"* juhudi za serikali zinalenga kutoa huduma ya makazi na afya kwa takribani wazee milioni 3.5. Hatua hizi ni muhimu ili kulinda haki

na ustawi wao. Kwa pamoja, hatua hizi zinaonesha dhamira ya Tanzania ya kujenga maendeleo jumuishi, ambapo upatikanaji wa haki na ulinzi wa kijamii unasaidiana katika kujenga jamii yenye usawa na ustahimilivu.

### 4.1.3 Mikakati na Juhudi za Serikali katika Utoaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii na Huduma za Kisheria kwa Wananchi


203. Huduma za msaada wa kisheria nchini Tanzania zinatambuliwa kama haki ya msingi chini ya Sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017, ambapo huduma hizi zimesambazwa kupitia madawati 184 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na maafisa 446 ili kuunga mkono Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano. Hatua muhimu katika kutekeleza ni pamoja na Kampeni ya Mama Samia ya Msaada wa Kisheria (2023), inayolenga kuongeza uelewa kuhusu migogoro ya ardhi na ukatili wa kijinsia, pamoja na kuwapo wa jukwaa la kidijitali la *Hakisheria* kwa uratibu rahisi wa ufuatiliaji.

204. Kwa upande wa huduma za kijamii kwa wazee, huduma hizi zinaongozwa na Sera ya Taifa ya Wazee (iliyorekebishwa 2024) na zinajikita katika vituo vilivyo katika nyumba 13 za umma za wazee kama maeneo yao ya usalama. Msaada zaidi kwa wazee umekua ukijumuisha ruzuku za fedha taslimu kupitia programu ya TASAF, bima ya afya kwa wote, na agizo la mwaka 2021 linalozitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga asilimia 3 ya mapato kwa ajili ya ustawi wa jamii.

ISO 9001:2015 Certified

**Kielelezo Na. 14** kinatoa muhtasari wa juhudi zilizofanywa katika utoaji wa huduma za ustawi wa jamii na huduma za kisheria kwa wananchi;

**Kielelezo Na. 14: Juhudi za Serikali katika Utoaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii na Huduma za Kisheria**




*Chanzo:* Sheria Zilizopitiwa, Sera, Mipango na Mikakati Inayosimamia Utoaji wa Huduma za Kisheria kwa Wananchi na Huduma za Kijamii kwa Wazee, 2025

## 4.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

### 4.2.1 Malengo ya Ukaguzi

205. Kutathmini ufanisi wa Serikali ya Tanzania kupitia Wizara zake na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutoa huduma muhimu za msaada wa kisheria na huduma za kijamii kwa makundi yaliyo hatarini, hususani watu wasio

na uwezo na wazee wasio na msaada, kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wote na kiwango cha maisha kinachokubalika

206. Hasa, nilitathmini iwapo:

(a) Wizara ya Katiba na Sheria imetoa huduma za msaada wa kisheria kwa watu wasio na uwezo nchini Tanzania kwa lengo la kuhakikisha haki kwa wananchi wote; na

(b) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi maalumu, pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, zilikuwa zikitoa kwa ufanisi huduma za kijamii kwa wazee wasio na msaada ili kuhakikisha wanapata kiwango cha maisha kinachokubalika.

### 4.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

207. Ukaguzi wangu wa huduma za msaada wa kisheria ulilenga kuingalia Wizara ya Katiba na Sheria, chini ya Msajili wa Huduma za Msaada wa Kisheria kwa kipindi cha Miaka minne ya Fedha (2021/22–2024/25). Lengo mahususi lilikuwa kutathmini upatikanaji, utekelezaji, na ubora wa huduma zinazotolewa kwa watu wasiojiweza, pamoja na uratibu kati ya wadau. Wigo wa ukaguzi ulihusisha watoa huduma waliosajiliwa (mashirika yasiyo ya kiserikali na wasaidizi wa kisheria) pamoja na watoa huduma za kisheria kama vile Chama cha Wanasheria Tanganyika. Uchaguaji wa mikoa ulizingatia jiografia kwa kufuata vigezo maalumu kama idadi ya watu na idadi ya watoa huduma ili kulinganisha upatikanaji wa huduma katika maeneo ya mijini, pembezoni mwa miji, na vijijini.

208. Pia, ukaguzi wangu kwenye utoaji wa huduma za jamii kwa wazee ulihusisha majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi maalumu pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kipindi cha Miaka mitano ya Fedha (2020/21–2024/25). Katika ukaguzi huu nilitathmini nguzo nne kuu: utambuzi wa wazee wanaostahili kupata huduma, usimamizi wa nyumba za kulelea wazee, ukamilifu wa huduma za msingi zinazotolewa, na ufanisi wa ufuatiliaji na usimamizi. Wigo wa ukaguzi ulihusisha jumla ya nyumba 13 za kulelea wazee zinazomilikiwa na Serikali kwa upande wa Tanzania Bara.

## 4.3 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Upatikanaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria kwa Watu Wasio na Uwezo

209. Katika ukaguzi huu nilibaini kuwa upatikanaji wa msaada wa kisheria nchini haukutolewa kwa usawa kimikoa, na haukuweza kukidhi mahitaji makubwa ya zaidi ya wananchi milioni 30 wanaoishi chini ya viwango vya umasikini. Nilibaini pia utofauti mkubwa kati ya maeneo ya mijini na vijijini, ambapo miji mikubwa kama Dar es Salaam ilikuwa na upatikanaji mkubwa wa huduma za msaada wa kisheria ikiwa na watoa huduma zaidi ya 28. Mikoa yenye uhitaji mkubwa, kama vile Kagera na Ruvuma ilihudumiwa na watoa huduma wachache, ambao walikuwa kati ya wanne hadi saba. Nilibaini pia kanda ya mashariki ilikuwa na takriban asilimia 30 ya watoa huduma waliosajiliwa, hali inayochangiwa na miundombinu bora na kuwapo kwa wafadhili wengi mijini wakati Kanda ya Magharibi ikiwa na asilimia 4.2 pekee.

210. Matokeo ya ukaguzi yalizingatia maeneo manne muhimu: upatikanaji na urahisi wa kufikia huduma za msaada wa kisheria, ufanisi wa utoaji wake, uimara wa mifumo ya kuhakikisha ubora, pamoja na kiwango cha uratibu wa wadau.

### 4.3.1 Kutokuwiana kwa Upatikanaji na Ufikiwaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria Nchini

211. Nilibaini kuwa upatikanaji na ufikiwaji wa huduma za msaada wa kisheria nchini haukuwa sawa bali ulijikita katika maeneo machache, na haukukidhi mahitaji makubwa ya wananchi wasiojiweza. Ingawa kuna mfumo wa kitaifa uliowekwa kupitia Sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017, upangaji wa kimfumo na changamoto za kitaasisi vimesababisha mamilioni ya wananchi walio katika mazingira hatarishi, hususani wale wa maeneo ya vijijini, kukosa nafasi ya kufikiwa na msaada wa kisheria unaojitosheleza. Hali hii ilidhihirika kupitia:

#### (a) Utofauti wa Kijiografia Kati ya Maeneo ya Mijini na Vijijini


212. Nilibaini kuwa watoa huduma za msaada wa kisheria, ambao ndio nguzo kuu ya utoaji wa huduma hizi, wamejikita zaidi katika maeneo ya mijini, huku maeneo mengi ya vijijini yakiwa na watoa huduma wachache (kati ya 1 hadi 3) katika ngazi ya mkoa. Hali hii haiendani na Kifungu cha 7(1)(f) cha Sheria ya Msaada wa Kisheria, 2017 ambacho kinamtaka Msajili kufanya uhamasishaji wa uelewa kwa umma na kuwezesha upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria. Ili kuonesha zaidi ukubwa wa mahitaji ya huduma ambayo hayajafikiwa, nilitumia takwimu za wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii kama kiashiria

cha idadi ya wananchi wasiojiweza. Ulinganisho huu ulidhihirisha pengo kubwa kati ya wingi wa kaya zilizo katika mazingira magumu na idadi ndogo ya watoa huduma za msaada wa kisheria waliopo katika mikoa husika.

213. Kanda ya Mashariki, hasa Dar es Salaam, ilikuwa na jumla ya karibu asilimia 30 ya watoa huduma za msaada wa kisheria waliojisajili, ikinufaika na miundombinu ya mijini, wingi wa watu, pamoja na ukaribu na taasisi za kisheria na programu za wafadhili. Eneo hili lilionekana kuwa na mitandao bora ya usafirishaji, uelewa mkubwa wa wananchi wa masuala ya kisheria, na lilikuwa karibu na taasisi za kisheria, jambo linalofanya huduma za msaada wa kisheria kuwa endelevu zaidi.

214. Kwa upande mwingine, maeneo ya vijijini na pembezoni kama vile kanda ya Magharibi, Kusini, na sehemu za kanda ya Kaskazini bado hazikuwa na huduma za kutojitosheleza, jambo linaloonesha tofauti kubwa katika upatikanaji wa msaada wa kisheria. **Kielelezo Na. 15** unaonesha mgawanyo huu katika kanda saba ya kiutawala nchini.

**Kielelezo Na. 15: Mtawanyiko wa Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria Kikanda Nchini**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Orodha ya Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria Waliosajiliwa na Wizara ya Katiba na Sheria wa Mwaka 2025

215. **Kielelezo Na. 15** kinaonesha kuwa Kanda ya Mashariki inaongoza kwa upatikanaji wa msaada wa kisheria, ambapo Dar es Salaam pekee ina watoa huduma 28 wa msaada wa kisheria, jambo linaloonesha upendeleo mkubwa wa huduma katika maeneo ya mijini. Kanda ya ziwa inashika nafasi ya pili ikiwa na wasaidizi wa sheria 34 katika mikoa sita, hata hivyo mkoa wa Simiyu haukuwa na mtoa huduma za msaada wa sheria. Kanda ya nyanda za juu kusini zilikuwa na upatikanaji wa wastani wa watoa huduma, huku kanda ya kati na Kaskazini zikiwa na watoa huduma wachache zaidi licha ya umuhimu wake wa kimkakati. Kanda ya Magharibi (Kigoma) ilikuwa na kiwango cha chini kabisa cha upatikanaji wa watoa huduma cha asilimia 4.2, ikibainisha mgawanyo usio na usawa wa rasilimali katika kanda na mikoa mbalimbali.

### (b) Kusuasua katika Usajili na Usimamizi wa Watoa Huduma za Kisheria

216. Nilibaini kuwa Wizara ya Katiba na Sheria haikuweza kufikia malengo ya usajili wa Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria katika miaka yote minne ya fedha kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25. Wajibu wa kufikia malengo ya usajili wa wasaidizi wa sheria uliwekwa katika Mpango Mkakati wa Wizara ya Katiba na Sheria (2021/22–2024/25). Mpango huu, ulitaka wizara kusajili watoa huduma wa msaada wa sheria wote kila mwaka. Kiashiria namba 29 cha Matokeo ya Ufuatiliaji kwa kipindi hicho kilihitaji Wizara ya Katiba na Sheria kusajili wasaidizi wa sheria wote waliopo nchini kwa asilimia 100 kama kipimo cha utendaji kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma za msingi za msaada wa sheria. Malengo chini ya Kiashiria cha 29 yalihitaji kusajili wasaidizi wa sheria 165 Mwaka wa Fedha 2020/21, 175 Mwaka wa Fedha 2021/22, 185 Mwaka wa Fedha 2022/23, 195 Mwaka wa fedha 2023/24, na 105 Mwaka wa Fedha 2024/25. Aidha, kiashiria hicho hicho kilihitaji Wizara ya Katiba na Sheria kusajili wanasheria wasaidizi, kwa malengo ya 620 Mwaka wa Fedha 2020/2021, 2,120 Mwaka wa Fedha 2021/22, 2,620 Mwaka wa Fedha 2022/23, 3,120 Mwaka wa Fedha 2023/24, na 3,620 Mwaka wa Fedha 2024/25.

217. Aidha, nilibaini kuwa ufuatiliaji na uthibitishaji wa usajili wa watoa huduma za msaada wa sheria ulifanywa na Wizara ya Katiba na Sheria kwa njia zisizo kidigitali (matumizi ya madaftari). Njia hizi hazikuweza kujumuisha taarifa kuhusu upatikanaji wa huduma au wigo wa huduma. Nilibaini pia kuwa Wizara ya Katiba na Sheria haikufanya tathmini ya kitaifa ya upatikanaji wa msaada wa sheria kati ya Mwaka wa Fedha 2021/22 na 2024/25, kama inavyotakiwa na Sheria ya Msaada wa Kisheria sura ya 21. Hii ilifanya kuiacha wizara bila taarifa muhimu za kupanga na kugawa rasilimali kwa ufanisi (watoa huduma na wasaidizi wa kisheria). Usajili wa watoa huduma wa sheria uliongezeka kutoka 26 Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 110 kufikia Mwaka wa

Fedha 2023/24, kisha ukashuka hadi 5 Mwaka wa Fedha 2024/25, huku usajili wa wasaidizi wa kisheria ukifikia kilele cha 742 Mwaka wa Fedha 2022/23 na kushuka hadi sifuri Mwaka wa Fedha 2024/25. Pia, niliona utunzaji wa kumbukumbu ukiwa haujitoshelezi, zaidi ya usajili 1,000 uliokwisha muda uliachwa bila kushughulikiwa. Uchakataji wa maombi ulizidi muda wa kisheria wa siku 21, na mara nyingine ulichukua miezi kukamilika, huku utekelezaji wa sheria ukiwa hauridhishi, ambapo baadhi ya watoa huduma wasaidizi wa sheria waliendelea kufanya kazi hadi siku 1,200 baada ya usajili wao kuisha muda wake. Changamoto hizi zilipunguza upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria nchini kote.

218. Nilibaini kuwa upungufu huo kwa kiasi kikubwa ulitokana na kushindwa kwa Wizara kujumuisha malengo mahsusi katika mipango ya utekelezaji ya kila mwaka pamoja na mifumo ya matumizi ya fedha ya muda wa kati ambayo ni mipango ya bajeti inayopangwa kwa kipindi cha miaka mitatu hadi mitano. Hakukuwa na fungu maalumu la bajeti kwa ajili ya usajili, ukaguzi wa uthibitisho, au uundaji wa rejesta ya kidijitali. Zaidi ya hayo, jukwaa la kidijitali la "HakiSheria" lililokusudiwa kurahisisha usajili lilikuwa halijakamilika. Hadi wakati wa ukaguzi, mfumo huu wa "hakisheria" haukuwa na mfumo wa ukumbusho wa moja kwa moja kwa mamlaka za idhini na pia haukuwa na kipengele cha mrejesho kwa waombaji.

### (c) Vikwazo vya Kimuundo na Kiufundi katika Ufikiwaji wa Msaada wa Kisheria

ISO 9001:2015 Certified

219. Nilichunguza muda unaotumika katika kushughulikia usajili wa watoa huduma na wasaidizi wa msaada wa sheria na kubaini uchelewaji katika ushughulikia maombi ya usajili, kinyume na kipengele cha 5 cha aya ya 6.1 ya Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa Wizara ya Katiba na Sheria wa mwaka 2020, ambacho kinataka maombi yashughulikiwe ndani ya siku 21 za kazi. Niligundua kuwa, ushughulikiwaji wa usajili ulichukua kati ya mwezi mmoja hadi minne, bila taarifa rasmi kutolewa kwa waombaji wakati wa kusubiri. Ucheleweshaji huu ulitokana na sababu zifuatazo;

#### (i) Upungufu wa Kimuundo na Kiutawala

220. Nilibaini kuwa kabla ya Mwaka wa Fedha 2024/25 maombi ya msaada wa kisheria yalikuwa yakiwasilishwa katika Wizara ya Katiba na Sheria kwa nhjia ya mkono. Lakini hata hivyo hakukua na mfumo wa kufuatilia kutoka hatua ya uwasilishaji hadi utoaji wa vyeti. Ingawa wizara ya Wizara ya Katiba na Sheria ilianzisha jukwaa la kidijitali la "Hakisheria" ili kurahisisha usajili, lakini mfumo huu ulikuwa haujaanza kutumika.

**(ii) Uhaba wa Rasilimaliwatu**

221. Ofisi ya Msajili imekuwa ikifanya kazi na watumishi wachache kulinganisha na mahitaji, jambo lililopunguza uwezo wake wa kutoa huduma za msaada wa kisheria. Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 na 2022/23, kulikuwapo watumishi wawili pekee kati ya kumi wanaohitajika, hali iliyodhihirisha upungufu wa asilimia 80. Idadi ya watumishi iliongezeka kidogo Mwaka wa Fedha 2023/24 hadi kufikia wanne, lakini bado kulikuwa na pengo la asilimia 60. Kufikia Mwaka wa Fedha 2024/25, idadi ilipanda hadi watumishi saba, ikibakisha upungufu wa asilimia 30.

**(iii) Kukosekana kwa Tathmini ya Upatikanaji wa Msaada wa Sheria Kitaifa**

222. Wizara ya Katiba na Sheria haikufanya tathmini ya kitaifa kuhusu upatikanaji wa msaada wa sheria kati ya Mwaka wa Fedha 2021/22 na 2024/25. Nilibaini kuwa, Wizara haikutekeleza tathmini hiyo kama inavyotakiwa na kifungu cha 5 na 26 cha Sheria ya Msaada wa sheria sura ya 21. Badala yake, ilitegemea rejista ya mikono iliyokuwa ikifuatilia tu masuala ya uthibitisho, bila kuonesha kiwango cha upatikanaji wa huduma. Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Msaada wa sheria (2020-2025) haukutekelezwa, na hivyo kuacha wizara bila taarifa muhimu za kupanga na kugawa rasilimali kwa ufanisi. Usajili wa watoa huduma na wasaidizi wa sheria haukuwa thabiti, usajiri huu ulibainika kupanda kutoka 26 hadi 110 kufikia Mwaka wa Fedha 2023/24, kisha ukashuka hadi 5 Mwaka wa Fedha 2024/25; wakati huo huo, usajili wa wasaidizi wa kisheria ulifikia 742 Mwaka wa Fedha 2022/23 na kushuka hadi sifuri Mwaka wa Fedha 2024/25. Zaidi ya hayo nilibaini kuwa, utunzaji wa kumbukumbu ulikuwa haujitoshelezi, huku zaidi ya usajili wa watoa huduma 1,000 uliokwisha muda wake ukiachwa bila kushughulikiwa.

ISO 9001:2015 Certified

### 4.3.2 Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria Usio na Ufanisi na Utoshelevu

223. Nilibaini kuwa, kutokana na kukosekana kwa sera ya kitaifa ya msaada wa sheria, Wizara ya Katiba na Sheria haikuwa na mfumo thabiti wa kuongoza uundaji, upanuzi na usimamizi wa huduma za msaada wa kisheria. Hakukuwa na tamko la wazi la serikali kuhusu malengo ya upatikanaji wa msaada wa kisheria, makundi ya kipaumbele, mikakati ya ufadhili, majukumu ya wadau, au viwango vya kupima utendaji. Hali hii ilisababisha huduma kutolewa kwa njia isiyo na mshikamano, kwani miradi mingi ya msaada wa kisheria imekuwa ikitegemea ufadhili wa wahisani na kuendeshwa kwa msingi wa mradi, bila mwongozo wa kitaifa. Sababu zilizobainika za utoaji wa msaada wa sheria usio na ufanisi na toshelevu ni pamoja na;

**(a) Kukosekana kwa Njia za Kutambua Watu Wasiojiweza**

224. Wizara ya Katiba na Sheria haikuwa na mfumo wa pamoja wa kutambua watu wasiojiweza ili kupatiwa msaada wa sheria nchini. Badala yake, kila mtoa huduma za msaada wa kisheria alitumia vigezo vyake binafsi. Mara nyingi vigezo hivo vimekua vikiongozwa na masharti ya wafadhili au maamuzi ya kihisia. Hali iliyosababisha mgawanyo usio sawa wa rasilimali na uwezekano wa kutowafikia watu wanaohitaji msaada kwa dhati. Hii ilikuwa kinyume na kifungu cha 21(3) cha Sheria ya Msaada wa Sheria ya Mwaka 2017, ambacho kinataka tathmini rasmi ifanywe ili kuhakikisha kuwa watu wanaopewa msaada kweli wanakidhi vigezo vya kutambuliwa kama “wasiojiweza.”

**(b) Uwezeshaji Usiojitosheleza kwa Maafisa wa Dawati la Msaada wa Kisheria**

225. Ingawa serikali iliweza kuanzisha madawati ya msaada wa kisheria katika Halmashauri 184, madawati haya yamekuwa hayafanyi kazi ipasavyo kutokana na ukosefu wa fedha za uendeshaji. Maafisa wa dawati hawakutengewa bajeti yao kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwemo ziara, kampeni za uhamasishaji, au kutatua/kujibu hoja na malalamiko ya wananchi. Matokeo yake, maafisa wengi ambao mara nyingi ni maafisa wa maendeleo ya jamii hutumia muda wao kushughulikia majukumu ya kiutawala yasiyo na uhusiano na msaada wa sheria kama walivyopangiwa.

**(c) Vikwazo vya Kiutawala katika Mfumo wa Utoaji Taarifa za Msaada wa Kisheria**

226. Nilibaini kuwa, kulikuwaupungufu mkubwa katika mnyororo wa utoaji taarifa. Pamoja na kwamba watoa huduma za msaada wa kisheria na maafisa dawati walikuwa wakifanya kazi katika ngazi ya jamii, taarifa walizokusanya hazikutumika katika kupanga mikakati ya kitaifa. Ripoti zilipelekwa moja kwa moja wizarani kwa msajili wa msaada wa sheria, bila kupitia Wasajili Wasaidizi wa ngazi ya mkoa, jambo lililosababisha uholela wa kiutawala na kuzuia udhibiti wa ubora katika ngazi za chini.

### 4.3.3 Udhaifu katika Uhakiki wa Ubora na Ukaguzi

227. Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Katiba na Sheria haikusimamia, kufuatilia wala haikupima ubora wa huduma za msaada wa kisheria zilizotolewa na watoa huduma na wasaidizi wa kisheria kote nchini. Hali hii ilikuwa kinyume na kifungu cha 26 cha sheria ya Msaada wa kisheria Sura ya 21, ambacho kinawataka Msajili na wasajili wasaidizi ngazi za mkoa kufuatilia na kutathmini

shughuli pamoja na ubora wa huduma zinazotolewa na watoa huduma za msaada wa kisheria. Baadhi ya changamoto zilizobainika katika uhakiki wa ubora na ukaguzi ni pamoja na:

**(a) Ubora wa Huduma za Msaada wa Kisheria Nchini Tanzania Usiodhibitiwa**

228. Ufanisi wa utoaji wa huduma uliendelea kuathirika kutokana na ukaguzi usiojitosheleza, kutofanyiwa uchambuzi wa taarifa za huduma, upungufu wa rasilimaliwatu, pamoja na ukosefu wa fedha za kusimamia shughuli ngazi ya mikoa. Kwa wastani, Wizara ya Katiba na Sheria ilishindwa kutekeleza zaidi ya asilimia 40 ya kaguzi ilizopanga kila mwaka. Nilibaini kuwa, hali hii ilisababishwa na kufanyika kwa ukaguzi usiokidhi viwango na mafunzo yasiyojitosheleza kwa watoa huduma. Matokeo yake, wasaidizi wa kisheria wasio na sifa stahiki waliendelea kutoa huduma zisizo na ubora, na katika baadhi ya matukio, watoa huduma walitoza ada kinyume cha sheria.

**(b) Kutokutekelezwa kwa Maelekezo ya Bodi ya Ushauri**

229. Nilibaini kuwa, kifungu cha 39 cha Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21 (Marejeo ya 2023), kinamtaka Msajili kuandaa na kuwasilisha ripoti ya utendaji ya mwaka katika Bodi ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa Mwaka wa Fedha. Bodi ya Ushauri wa msaada wa Kisheria ina jukumu kupitia na kutolea maelekezo taarifa hiyo. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Katiba na Sheria mara kwa mara ilishindwa kutekeleza maelekezo ya Bodi, hususani yale yanayohusu ukaguzi wa mashirika ya watoa msaada wa kisheria yanayofanya kazi bila usajili. Nilibaini kuwa, katika mikutano mitatu mfululizo ya bodi, wizara ilielekezwa kufuatilia watoa huduma wanaofanya kazi bila usajili au kinyume cha sheria, lakini agizo hili halikuwahi kutekelezwa.

230. Sababu zilizochangia kutotekeleza maelekezo ya Bodi ni pamoja na ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya usimamizi wa kikanda, kipaumbele kidogo kilichotolewa kwenye bajeti kwa shughuli za kila siku kama ukaguzi wa wasaidizi wa kisheria na vituo vya msaada wa kisheria, pamoja na kukosekana kwa mifumo ya ufuatiliaji iliyo sanifishwa. Matokeo yake, niliona hatari ya kutolewa huduma za kisheria zisizo na viwango, ukiukwaji wa haki za wananchi, kupungua kwa imani ya umma kwa huduma za msaada wa kisheria, na unyonyaji wa kifedha kinyume cha sheria kwa watu wasiojiweza.

### (c) Kutofanyika kwa Zoezi la Ukaguzi wa Watoa Huduma kama Inavyopaswa

231. Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa asilimia 43 ya watoa hudiuma za msaada wa kisheria waliosajiliwa waliondolewa kwenye mpango wa ukaguzi, na utekelezaji wa mpango wa kaguzi zilizopangwa haukuzidi asilimia 40. Hali hii ilikuwa kinyume na Kanuni za 37 na 38 za Kanuni za Msaada wa Kisheria za mwaka 2018, ambazo zinamtaka msajili msaidizi, au mtu aliyeidhinishwa kukagua ofisi za watoa huduma za msaada wa kisheria angalau mara moja kila mwaka. Nilibaini kutofanyika kwa ukaguzi kama ilivyotakiwa kulisababisha changamoto kama vile wahitaji wa huduma za kisheria kutozwa ada kinyume cha sheria, kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 20(6) cha Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21. Aidha, baadhi ya wasaidizi wa huduma za kisheria walibainika wakitoa huduma bila kuwa na ithibati halali au mafunzo stahiki, jambo lililohatarisha utoaji wa ushauri wa kisheria usio na viwango.

### (d) Upungufu wa Rasilimali katika Usimamizi wa Ubora

232. Nilibaini kuwa kulikuwa na changamoto katika kudumisha viwango vya ubora, jambo ambalo lilihusishwa na upungufu wa rasilimaliwatu na fedha ndani Wizara ya Katiba na Sheria, kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 10** na **Jedwali Na. 11**.

**Jedwali Na. 10: Hali ya Rasilimaliwatu katika Ofisi ya Msajili wa Msaada wa Huduma za Kisheria ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria (2021/22 - 2023/24)**

| Wafanyakazi | Mwaka wa Fedha | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/2022 | 2022/2023 | 2023/2024 | 2024/2025 |
| Wanaohitajika | 10 | 10 | 10 | 10 |
| Waliopo | 02 | 02 | 04 | 07 |
| Upungufu (%) | 80 | 80 | 60 | 30 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Hali ya Rasilimaliwatu katika Wizara ya Katiba na Sheria, 2025

233. **Jedwali Na. 10** linaonesha kuwa idadi ya watumishi katika Ofisi ya Msajili wa Msaada wa Huduma za Kisheria imeendelea kubaki chini ya mahitaji. Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 na 2022/23, kulikuwa na watumishi wawili pekee kati ya kumi waliohitajika, hali inayoashiria upungufu wa asilimia 80. Idadi ya watumishi iliongezeka hadi wanne katika Mwaka wa Fedha 2023/24 (upungufu wa asilimia 60), na kufikia saba katika Mwaka wa Fedha 2024/25, hivyo kupunguza pengo hadi asilimia 30.

234. Pia, nilibaini kuwa kulikuwa na mgao mdogo wa fedha kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 11**, jambo lililochangia zaidi kupunguza uwezo wa Ofisi ya Msajili katika kusimamia na kudumisha ubora wa huduma za msaada wa kisheria.

**Jedwali Na. 11: Fedha Zilizotengwa kwa ajili ya Huduma za Msaada wa Kisheria katika Wizara ya Katiba na Sheria kwa Kipindi cha 2021/22 - 2024/25**

| Mwaka wa Fedha | Bajeti (Sh.) | Fedha Zilizotolewa (Sh.) | Fedha Zilizotolewa (%) |
|---|---|---|---|
| 2021/22 | 330,440,000 | 0 | 0 |
| 2022/23 | 715,176,000 | 1,327,880,000 | 185 |
| 2023/24 | 2,650,439,224 | 2,982,269,500 | 112 |
| 2024/25 | 17,674,292,824 | 17,674,292,824 | 100 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kwenye Mpango wa Bajeti wa Muda kati na Bajeti za Wizara kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25, 2025

235. **Jedwali Na. 11** linaonesha kuwa kati ya Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25, mgao na utolewaji wa fedha kwa ajili ya huduma ya msaada wa kisheria haukuwa thabiti. Mwaka wa fedha 2021/22, hakuna fedha zilizotolewa licha ya bajeti kuidhinishwa, jambo linaloashiria ukosefu wa kipaumbele katika masuala ya huduma za kisheria. Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 fedha zilizotolewa zilizidi bajeti iliyoithinishwa kwa asilimia 85 na Mwaka wa Fedha 2023/24 kwa asilimia 12, hali iliyochangiwa na kuwapo kwa msaada wa serikali kupitia kampeni ya msaada wa sheria (Kampeni ya Mama Samia).

### 4.3.4 Uratibu Usiojitosheleza Katika Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria

236. Mipango ya Mkakati na Mipango ya Kila Mwaka ya Wizara ya Katiba na Sheria haikuzingatia ipasavyo uratibu katika sekta ya huduma ya msaada wa kisheria. Ingawa Mpango Mkakati uliweka malengo ya udhibiti na uratibu, mipango ya kila mwaka ilijikita zaidi kwenye mikutano na makongamano. Matokeo yake, takribani asilimia 40 pekee ya shughuli za uratibu zilizopangwa ziliweza kutekelezwa. Baadhi ya sababu zilizosababisha uratibu usiojitosheleza katika utoaji wa msaada wa kisheria ni pamoja na:

**(a) Kutokuwapo kwa Muunganiko Kati ya Malengo ya Mkakati na Mipango ya Utekelezaji**

237. Nilibaini upungufu katika namna ambavyo Wizara ya Katiba na Sheria inapanga zoezi la uratibu kwenye eneo la huduma za msaada wa kisheria.

Pamoja na kwamba Mpango Mkakati wa 2021/22–2025/26 uliweka malengo ya kuboresha “Upatikanaji wa Haki na Uratibu wa Sekta,” mipango ya utekelezaji ya kila mwaka haikujumuisha mikakati na hatua mahsusi za kufanikisha malengo hayo. Katika kipindi cha miaka minne, bajeti, ya wizara haikuweka shughuli za utekelezaji zinazolenga kufanikisha lengo la kujumuisha shughuli za huduma za msaada wa kisheria. Pia, hakukuwa na mwongozo wa kitaifa au mifumo ya uratibu iliyotengenezwa ili kuimarisha ushirikiano wa wadau, jambo lililosababisha changamoto katika upangaji wa mipango kila mwaka. Matokeo yake, shughuli za utoaji huduma za msaada wa kisheria zilikosa taratibu za pamoja na za viwango, huku uratibu ukiathiriwa na ukosefu wa uwazi katika utaratibu wa utoaji taarifa kati ya watoa huduma za sheria na wasaidizi wa Msajili, ambao wote waliripoti moja kwa moja kwa Msajili.

## 4.4 Matokeo ya Jumla ya Ukaguzi kuhusu Utoaji wa Huduma za Chakula, Makazi na Malezi kwa Wazee

238. Upatikanaji wa huduma za chakula, makazi na malezi kwa wazee unaonesha kuwa, idadi ya wazee waliopo katika nyumba za wazee ni ndogo sana ikilinganishwa na idadi ya wazee wasio na msaada ambao wangenufaika na huduma hizo. Huduma za chakula, makazi na malezi kwa wazee hazikutolewa kwa kiwango cha kutosha katika maeneo mbalimbali nchini, kinyume na kifungu cha 5.2 cha Sera ya Taifa ya Wazee (2003), kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 12**.

ISO 9001:2015 Certified

**Jedwali Na. 12: Upatikanaji wa Huduma za Malezi ya Wazee Kila Mkoa**

| Mkoa | Idadi ya Wazee katika Nyumba za Wazee | Jumla ya Wazee Wasio na Msaada |
|---|---|---|
| Tanga | 35 | 26206 |
| Arusha | 13 | 8654 |
| Kilimanjaro | 11 | 58314 |
| Manyara | 8 | 7027 |
| Lindi | 10 | 10701 |
| Ruvuma | 0 | 19454 |
| Mtwara | 0 | 16585 |
| Morogoro | 26 | 38623 |
| Dar es Salaam | 45 | 344 |
| Pwani | 0 | 27282 |
| Kigoma | 26 | 60557 |
| Mwanza | 25 | 37496 |
| Shinyanga | 32 | 23825 |
| Kagera | 37 | 9364 |
| Mara | 69 | 44239 |
| Geita | 0 | 20371 |
| Simiyu | 0 | 51316 |
| Singida | 27 | 27120 |
| Dodoma | 92 | 10380 |
| Tabora | 26 | 31244 |

| Mkoa | Idadi ya Wazee katika Nyumba za Wazee | Jumla ya Wazee Wasio na Msaada |
|---|---|---|
| Mbeya | 0 | 16167 |
| Rukwa | 0 | 49531 |
| Katavi | 0 | 6640 |
| Iringa | 6 | 13100 |
| Songwe | 0 | 6632 |
| Njombe | 0 | 12586 |

***Chanzo:*** Takwimu za Makazi ya Wazee, 2025

239. **Jedwali Na. 12** linaonesha takwimu za wazee wasio na msaada katika mikoa mbalimbali ya nchi. Idadi ya wazee hawa inatofautiana, ikianzia wazee 344 katika Mkoa wa Dar es Salaam hadi kufikia wazee 60,557 katika Mkoa wa Kigoma. Hata hivyo, ikilinganishwa na upatikanaji wa huduma za kijamii na makazi ya wazee katika nyumba maalumu, nilibaini kuwa jumla ya wazee wasio na msaada waliotambuliwa nchini ni 633,758, lakini ni wazee 488 pekee wanalipata huduma hizo (220 katika nyumba za umma na 268 katika nyumba binafsi).

240. Hali hii inasababisha changamoto katika utoaji wa huduma za chakula, makazi na malezi kwa wazee, ambazo sababu zake zimeelezwa kama ifuatavyo:

### 4.4.1 Upungufu katika Utambuzi na Uhakiki wa Wazee Wasio na Msaada

241. Nilibaini kuwa, mbinu zilizotumika kutambua na kuripoti hali ya wazee wasio na msaada hazikuwa thabiti. Hali hii ilijitokeza kwa sababu utofauti wa mbinu zilizotumika katika mamlaka za serikali za mitaa na maafisa ustawi wa jamii katika utambuzi wa wazee katika jamii. Nilibaini pia mamlaka nyingi za serikali za mitaa ziliendelea kutegemea takwimu za zamani au viashiria visivyo na uhakika, jambo lililosababisha kuwapo kwa takwimu zisizo sahihi na ambazo hazioneshi mabadiliko ya mara kwa mara katika idadi ya wazee.


242. Hii ilikuwa kinyume na matakwa ya Sera ya Taifa ya Wazee (Sehemu ya 4.2 na 3.7) inayozitaka mamlaka za serikali za mtaa kufanya tathmini ya kina ya mahitaji ya wazee katika jamii zao ili kuhakikisha mahitaji ya msingi yanatambulika na kutathminiwa ipasavyo. Mbinu zilizotumika zilisababisha matokeo yasiyo sahihi kwa sababu idadi ya wazee hubadilika mara kwa mara kutokana na mambo kama vile vifo, madiliko ya kiuchumi au wazee kurudi kwa ndugu zao. Hakukuwa na mamlaka ya serikali za mitaa iliyokusanya takwimu za msingi, ambayo ndiyo njia inayokubalika zaidi katika kuzalisha taarifa sahihi.

243. Hali hii ilisababishwa na;

**(a) Upungufu Katika Taarifa za Uchunguzi wa Kijamii**

244. Ripoti za uchunguzi wa kijamii, ambazo kimsingi zinapaswa kuongoza katika kuandaa mpango wa huduma kwa wazee zilikua hazijitoshelezi. Mamlaka ya serikali za mtaa nyingi zilitegemea zaidi mahojiano ya mdomo pekee badala ya kufanya uthibitisho wa kimazingira au vipimo vya kitabibu. Kila mamlaka ilitegemea uelewa na uzoefu wake binafsi katika kuandaa ripoti hizi, jambo lililosababisha tofauti kubwa katika maudhui ya ripoti kutoka mamlaka moja hadi nyingine, na hata kati ya ripoti moja na nyingine, kulingana na uzoefu wa afisa ustawi wa jamii aliyeendesha uchunguzi. **Kielelezo Na. 16** kinaonesha kwa uwazi kiwango cha upungufu uliopo katika ripoti hizi za kijamii.

**Kielelezo Na. 16: Kiwango cha Taarifa Katika Ripoti za Utafiti wa Kijamii**




***Chanzo***: Uchambuzi wa Mafaili Binafsi ya Wazee Kutoka Nyumba za Wazee Zilizotembelewa, 2025

245. **Kielelezo Na. 16** inaonesha ripoti za uchunguzi wa kijamii, ambazo zinapaswa kukusanya taarifa muhimu kabla ya kuomba wazee wapokelewe katika nyumba za malezi, zilionekana kuwa na upungufu. Uchambuzi unaonesha kuwa, vipengele muhimu havikuwapo katika ripoti zilizowasilishwa pamoja katika maombi kupokelewa. Asilimia 86 ya ripoti hazikuonesha uthibitisho wa taarifa zilizokusanywa wakati wa mawasiliano ya awali na maafisa ustawi wa jamii. Ripoti 193 (asilimia 88) hazikuwa na taarifa za kitabibu wala ushahidi wa

vipimo vya afya. Asilimia 80 ya uchunguzi haukujumuisha ziara au uhakiki wa moja kwa moja katika makazi ya wazee au uthibitisho wa hali ya maisha yao. Asilimia 70 ya mafaili hayakuwa na taarifa kuhusu wanafamilia, ndugu, au ushahidi wa ufuatiliaji wa familia.

246. Ukosefu wa taarifa hizi ulisababisha mnyororo wa taarifa kuvunjika, na kuleta ugumu katika kuwaunganisha tena wazee na familia zao baada ya kupokelewa katika nyumba za malezi. Hali hii inadhihirishwa na kiwango cha chini sana cha mafanikio ya kuwarejesha wazee kwa ndugu zao, ambapo ni asilimia 2.3 pekee ya wazee waliweza kuunganishwa tena na familia zao katika kipindi cha miaka mitano.

### (b) Upokeaji wa Wazee Bila Vibali Halali

247. Aya ya 15.0(i) ya Mwongozo wa Uanzishaji na Usimamizi wa Nyumba za Wazee, 2019, afisa ustawi wa jamii anayesimamia nyumba za wazee anatakiwa kuhakikisha kuwa kila mzee anayepokelewa katika nyumba hizo anapata kibali kutoka kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii wakati wa kupokelewa au mara tu baada ya kupokelewa.

248. Hata hivyo, nilibaini kuwa, wazee wengi wanapokelewa kwa kulazimishwa kupitia viongozi wa mitaa kwa ajili ya makazi ya dharura, bila kufuatwa taratibu za kisheria. Mara nyingi maafisa husika hawafuatilii kupata vibali vinavyohitajika baada ya kupokelewa.

ISO 9001:2015 Certified

249. **Jedwali Na. 13** linaonesha idadi ya wazee walioko sasa katika nyumba za malezi bila kibali cha Kamishina wa Ustawi wa Jamii.

**Jedwali Na. 13: Tathmini ya Vibali Vilivyotolewa kwa ajili ya Makazi ya Wazee Katika Nyumba Zilizotembelewa**

| Nyumba ya Wazee | Jumla ya Wazee | Idadi ya Wazee wenye Vibali | Idadi ya Wazee Wasio na Vibali | Asilimia ya Wazee wasio na Vibali |
|---|---|---|---|---|
| Sukamahela | 13 | 3 | 10 | 77 |
| Nunge | 15 | 2 | 13 | 87 |
| Kilima | 21 | 0 | 21 | 100 |
| Bukumbi | 25 | 2 | 23 | 92 |
| Nyabange | 11 | 0 | 11 | 100 |
| Kolandoto | 16 | 0 | 16 | 100 |
| Magugu | 8 | 0 | 8 | 100 |
| Njoro | 11 | 0 | 11 | 100 |
| Misufini | 16 | 0 | 16 | 100 |
| Mwanzage | 12 | 0 | 12 | 100 |
| Fungafunga | 20 | 0 | 20 | 100 |
| Ipuli | 26 | 0 | 26 | 100 |
| Kibirizi | 26 | 0 | 26 | 100 |

| Nyumba ya Wazee | Jumla ya Wazee | Idadi ya Wazee wenye Vibali | Idadi ya Wazee Wasio na Vibali | Asilimia ya Wazee wasio na Vibali |
|---|---|---|---|---|
| **Jumla** | **220** | **7** | **213** | **96.62** |

***Chanzo***: Uchambuzi wa Wakaguzi kwenye Ripoti za Upokeaji wa Wazee, 2025

250. Kutokana na uchambuzi wa **Jedwali Na. 13** kati ya makazi 13 ya wazee yaliyotembelewa, ilibainika kuwa kati ya wazee 220 waliopokelewa, wazee 213 sawa na asilimia 96.62 hawakuwa na vibali vya makazi vilivyotolewa na Kamishna wa Ustawi wa Jamii katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

**(c) Kutokufanya Tathmini ya Awamu ya Pili na ya Kitaalamu baada ya Wazee Kupokelewa**

251. Nilibaini kuwa, baada ya wazee kupokelewa katika nyumba zao, hawakufanyiwa uchunguzi maalum kama inavyotakiwa katika mwongozo wa kitaifa. Hii ilikuwa kinyume na Kifungu cha 7.0 cha Mwongozo wa Uanzishaji na Usimamizi wa Nyumba za Wazee, 2019, ambacho kinataka wazee kuchunguzwa maalum wa kiafya mara tu wanapopokelewa. Ukaguzi ulibaini kuwa:

**(i) Viwango vya Chini vya Tathmini kwa Wazee**

252. Kupitia mapitio ya mafaili ya upokeaji wa wazee na mazungumzo na maafisa wa nyumba zilizotembelewa, ilibainika kuwa ni makazi matatu pekee kati ya 13 (Kolandoto, Ipuli, na Kibirizi) ndio yalifanya na kuweka kumbukumbu tathmini ya pili kuhusu afya na hali ya kimwili ya wazee wakati wa kupokelewa. Hii ni sawa na asilimia 9 ya nyumba za wazee pekee ambazo wakazi wake walifanyiwa tathmini ya pili ya kiafya walipopokelewa.

253. Hivyo, hakukuwa na uhakika wa hali ya jumla ya afya ya wazee waliopokelewa, na hivyo kukosekana msingi wa kuandaa mpango wa huduma binafsi za afya kwa kipindi chote cha makazi yao katika nyumba zao.

**(ii) Ukosefu wa Huduma Binafsi kwa Wazee**

254. Mapitio ya mafaili ya upokeaji na mazungumzo na maafisa wa nyumba za wazee, yalibaini kwamba wazee hupokea huduma za jumla bila kuzingatia mahitaji yao binafsi ya kiafya, kimwili, au kijamii. Nilibaini kua ni asilimia tisa pekee (wazee 20 kati ya 220) waliokuwa wakikaa katika nyumba za serikali waliwahi kufanyiwa tathmini ya pili. Pia, nilibaibi kuwapo kwa taarifa za uchunguzi wa kijamii zisizo kamili, ambapo ripoti za awali kutoka serikali za mtaa mara nyingi hazikujitosheleza ili kuunda mpango wa huduma binafsi. Bila

tathmini hizi, wazee wenye changamoto za kiafya mara nyingi hawakupata huduma hadi hali yao ilipokuwa mbaya, kwani dalili zao hazikudhibitiwi kwa kufuata mpango maalum.

**(d) Upokeaji wa Wazee Wasiokusidiwa**

255. Kupitia mapitio ya kumbukumbu za uandikishaji na ripoti za thathmini ya kijamii kutoka nyumba za wazee, nilibaini kuwa, jumla ya wazee 17 kutoka nyumba 13 nilizozitembelea walikuwa na sifa zilizowaondolea uhalali wa kukaa katika nyumba hizo. Kwa kuwa mchakato wa utambuzi ulikuwa dhaifu, nyumba za wazee zilitumika kwa ajili ya kuhifadhi watu wasiokusudiwa. Baadhi ya wazee waliopokelewa hawakukidhi vigezo vya kupokelewa, kinyume na Kifungu cha 5.0 cha Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Nyumba za Wazee nchini Tanzania, 2019, ambao unawataka wakazi wawe wametimiza umri wa kuazia miaka 60 na masharti mengine yaliyowekwa. Hali hii ilisababisha kupunguza ustawi na heshima ya wakazi wote kwenye nyumba za wazee. Pia, hii iliongeza hatari kwa wazee waliopo, kwani baadhi ya wakazi wasiokusudiwa walikuwa na changamoto za kitabia au kiafya. Mfano halisi ni katika nyumba za Magugu na Sukamahela, ambapo ziliripoti kupokea wagonjwa wa akili wenye tabia za vurugu waliotolewa kutoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe.

### 4.4.2 Usimamizi Usio na Ufanisi wa Nyumba za Wazee

256. Ukaguzi ulibaini kuwa usimamizi wa nyumba za wazee ulikuwa haujitoshelezi na haukuwa na ufanisi, hali iliyopunguza ubora wa huduma na malezi yaliyotolewa. Hii ilikuwa kinyume na Kifungu cha 4.0 cha Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Nyumba za Wazee (2019), ambacho kinazitaka nyumba za wazee kuwa na miundombinu maalum inayokidhi mahitaji ya wazee. Masuala yaliobainika yalikua;

**(a) Usanifu wa Majengo na Mazingira Yasiyoridhisha**

257. Nilibaini kuwa kati ya nyumba 13 nilizotembelea hakukuwa na nyumba iliyokidhi viwango vya usanifu wa majengo kwa ajili ya kuhudumia wazee. Majengo mengi yalijengwa katika miaka ya 1960 na 1970 kwa ajili ya wagonjwa wa ukoma, na hayajabadilishwa ili kukidhi mahitaji maalum ya wazee. Matokeo yake nyumba zilirithiwa zikiwa na dosari kama; nyumba kukosa mwanga na hewa duni, sakafu zilizochakaa na zisizo salama, zinazoongeza hatari ya kuanguka kwa wazee. Pia, kulikua na vyoo visivyofaa kwa matumizi ya wazee, na ukosefu wa maji ya bomba. Sababu kuu za dosari hizi zilikua kuwapo kwa upungufu katika uandaaji wa mipango, bajeti, na utekelezaji wa programu za

matengenezo na ukarabati. Usanifu usiyojitosheleza. Hali hii iliathiri faraja na ustawi wa wazee, na kudhoofisha heshima na hadhi yao wanapokuwa katika nyumba za malezi.

**(b) Upungufu Katika Ukarabati na Matengenezo**

258. Ukaguzi ulibaini kuwa katika kipindi cha miaka mitatu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum iliweka bajeti ya shilingi milioni 820 kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za wazee. Bajeti hii ilihusisha nyumba za makazi tano pekee kati ya 13 zilizokuwa zinahitaji matengenezo, sawa na asilimia 38 ya makazi yote ya wazee. Hata hivyo, kati ya makazi matano yaliyopangwa kukarabatiwa, ni makazi ya sehemu moja pekee ya Ipuli yalikarabatiwa. Kushindwa kutekeleza mpango huu kulitokana na kutotolewa kwa bajeti iliyotengwa, jambo lililosababisha kuendelea kuwapo kwa miundombinu na mazingira ambayo yalikuza hatari ya kutofanyika kwa usafi hivyo kuibuka kwa mazalia ya wadudu na wanyama waharibifu, pamoja na hali duni ya usafi wa mazingira.

**(c) Urasimishaji wa Ardhi na Uvamizi**

259. Nilibaini kuwa, nyumba nyingi za wazee hazikuwa na hati za umiliki, hali ambayo iliyosababisha migogoro ya mara kwa mara. Kati ya makazi 13 ya wazee yaliyotembelewa, makazi ya wazee nane (sawa na asilimia 61.5) hayakuwa na hatimiliki za ardhi. Zaidi ya hapo, kulikuwa na migogoro inayoendelea katika makazi saba kati ya 13 (asilimia 54) ya wazee, huku migogoro iliyotatuliwa ikiripotiwa katika makazi ya sehemu moja pekee ya Magugu (asilimia 20). Makazi toka sehemu 3 (sawa ana asilimia 23) hazikuripoti migogoro yoyote ya ardhi. Aidha, ukosefu wa uzio na mipaka iliyo wazi umesababisha jamii zinazozunguka kuvamia maeneo ya makazi ya wazee. Katika baadhi ya maeneo, uvamizi huu umechukua sura ya kudumu, ikiwemo kujengwa kwa nyumba za makazi na hata makaburi ndani ya maeneo ya nyumba za wazee, kama ilivyobainika katika makazi ya wazee Nunge na Kibirizi.

**(d) Upungufu wa Rasilimaliwatu na Kiwango Kikubwa cha Kazi**

260. Katika ukaguzi huu nilibaini pengo kubwa kati ya watumishi waliopo na mahitaji halisi katika nyumba za makazi ya wazee. Kufikia Januari 2025, kulikuwa na watumishi 78 pekee waliokuwa wakihudumia nyumba zilizopo katika makazi 13 ya serikali, sawa na asilimia 33 ya mahitaji ya watumishi 236. Hii inaonesha upungufu wa takribani asilimia 67 ya watumishi wanaohitajika. Zaidi ya hapo, watumishi waliopo hawakuwa na mafunzo maalum ya

kushughulikia mahitaji ya wazee, jambo lililopunguza ubora wa huduma zinazotolewa. Ukaguzi ulibaini pia wataalam waliopungua walikua ikiwemo wataalam wa lishe, wataalamu wa viungo, na wahasibu. Hali hii ilisababisha majukumu mazito kwa watumishi wachache waliopo. Kwa mfano, muuguzi mmoja anahudumia hadi wazee 56, kinyume na uwiano unaotakiwa wa 1:30 (mhudumu mmoja wazee 30), na mtumishi mmoja wa kufua nguo anahudumia wazee 112, kinyume na uwiano wa 1:30. Kwa ujumla, mchanganyiko wa ukosefu wa wataalamu na uwingi wa kazi kwa watumishi wachache unapunguza ustawi, heshima, na hadhi ya wazee wanaoishi katika nyumba hizi.

### 4.4.3 Upungufu wa Huduma za Kijamii kwa Wazee Wasio na Uwezo Katika Nyumba za Wazee

261. Licha ya jitihada zinazoendelea za serikali na uongozi wa nyumba za wazee, nilibaini changamoto katika ukamilifu na ubora wa huduma za kijamii zinazotolewa kwa wazee waliopokelewa. Hali hii ni kinyume na Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Nyumba za Wazee (2019) ambao unataka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kutoa huduma kamili za kijamii, ikiwemo chakula na lishe, huduma za afya, makazi, mavazi, msaada wa kisaikolojia na afya ya akili, usalama na ulinzi. Changamoto zilizobainishwa ni kama ifuatavyo;

#### (a) Huduma za Chakula na Lishe Zisizojitosheleza

ISO 9001:2015 Certified

262. Katika ukaguzi huu nilibaini kuwa, milo inayotolewa katika nyumba za wazee ni ya kujirudiarudia, yenye wingi wa vyakula vya wanga na haina virutubisho muhimu vinavyohitajika kwa afya ya wazee. Nyumba nyingi zimekuwa zikitoa mlo wa chai, mkate, wali, ugali na maharage kwa kujirudiarudia, hali inayosababisha wazee hawa wapate vyakula vinavyotia nguvu mwilini na kukosa vyakula vya protini, vitamini na madini. Sababu kuu ya changamoto hii ilikuwa vikwazo vya kifedha, ambapo licha ya ongezeko dogo la bajeti ya huduma za chakula kwa wazee kati ya Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi 2024/25, mgao wa kila siku umekuwa mdogo na hauendani na bei za soko za bidhaa muhimu za chakula pamoja na mahitaji ya lishe ya wazee. Aidha, asilimia ya fedha zilizopitishwa na kutolewa kwa nyumba za wazee imepungua kutoka asilimia 54 Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi asilimia 18 Mwaka wa Fedha 2023/24, na kisha kuongezeka kidogo hadi asilimia 49 Mwaka wa Fedha 2024/25. Hali hii imezinyima nyumba za wazee uwezo wa kutoa mlo kamili na wenye uwiano sahihi wa virutubisho.

### (b) Upungufu Katika Huduma za Afya na Usalama

263. Ukaguzi wangu umebaini kuwa, huduma za afya katika nyumba za wazee zilikwamishwa na ukosefu wa bima ya afya, upungufu wa watumishi wa kitaalamu, na usafi hafifu wa miundombinu. Nilibaini kuwa, ni nyumba nne pekee za wazee wa Nunge (asilimia 73), Fungafunga (asilimia 100), Kolandoto (asilimia 100), na Ipuli (asilimia 96) zilitoa bima ya afya kwa wazee. Hata hivyo, mfuko wa bima ya afya kwa wazee ulionekana kutotosha kwani haukuweza kugharimia magonjwa sugu na hali hatarishi kama vile kuvunjika kwa mifupa, upasuaji, na matatizo ya moyo. Hali hii ilitokana na uratibu usiojitosheleza kati ya nyumba za wazee na maafisa wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, hali iliyosababisha changamoto katika ufikiwaji wa huduma za matibabu kwa wazee waliokuwa wanaumwa.

### (c) Upungufu wa Vifaa vya Msaada na Usalama

264. Ukaguzi ulibaini upungufu mkubwa wa vifaa vinavyohitajika ili kuhakikisha wazee wanapata uhuru na usalama wa kujihudumia. Hali hii ni kinyume na aya ya 4(viii) ya Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Nyumba za Wazee (2019), ambayo inaitaka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya msaada vya kutosha katika nyumba za wazee. Upungufu ulionekana kwenye vifaa vya kutembea, vifaa vya kuona, vifaa vya kusikia, na vifaa vya mifupa na viungo.

ISO 9001:2015 Certified

265. Matokeo yake imesababisha kupungua kwa uhuru na uwezo wa wazee kutembea, kuongezeka kwa hatari ya madhara ya kimwili na ajali, kuongezeka kwa kazi hivyo kusababisha kuchoka kwa wahudumu hatimaye kuchangia kudorora kwa ustawi na hadhi ya wazee.

### 4.4.4 Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Kijamii kwa Wazee Usiojitosheleza

266. Nilibaini kuwa, huduma za kijamii kwa wazee hazikusimamiwa ipasavyo na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Hii ilikua kinyume na aya ya 3.1.13 ya Mwongozo wa Taifa wa Ufuatiliaji na Tathmini, Wizara inatakiwa kufuatilia utoaji wa huduma za kijamii kwa kuweka viashiria mahsusi vinavyoweza kupimwa ili kubaini utendaji wa kila nyumba za wazee. Miongoni mwa upungufu ulioonekana katika ufuatiliaji na usimamizi wa huduma za kijamii kwa wazee ni kama ifuatavyo;

### (a) Mfumo wa Kupima Utendaji Usioridhisha

267. Nilipitia Mpango Mkakati wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu wa Mwaka wa Fedha 2021/22–2025/26 na kubaini kuwa, kulikuwa na viashiria 15 vya matokeo vilivyowekwa katika mpango huo ili kupima utekelezaji wa malengo makuu matano. Hata hivyo, kati ya viashiria hivyo 15, hakuna kilichoandaliwa kupima utendaji wa Wizara katika kutoa huduma za kijamii kwa wazee. Kwa hiyo, hakukuwa na viashiria vya moja kwa moja vya kimkakati kwa kitengo kinachohusika na huduma za wazee. Idara ya Ustawi wa Jamii (hasa sehemu inayoongozwa na Kamishna Msaidizi) haina uwajibikaji wa malengo yake, jambo ambalo linaathiri vibaya mgawanyo wa rasilimali.

### (b) Kukosekana kwa Usimamizi Saidizi

268. Licha ya kuwa na asilimia 97 ya watumishi wanaohitajika katika makao makuu ya Idara ya Ustawi wa Jamii, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum haikutoa mwongozo kuhusu makazi ya wazee. Wizara haikufanya usimamizi wowote katika vituo vyote 13 vya serikali vya huduma kwa wazee kwa kipindi cha miaka minne toka Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25 licha ya kuwapo kwa mipango. Hii ilitokana na ufuatiliaji wa makazi ya wazee kuachwa mara kwa mara na badala yake kipaumbele kilielekezwa kwenye shughuli zingine, kama vile kusimamia makazi ya watoto.

ISO 9001:2015 Certified

### (c) Kukosekana kwa Taarifa Jumuishi na Ukosefu wa Teknolojia

269. Nilibaini kuwa, mfumo wa taarifa uliopo kwa sasa haukua faafu jambo linalofanya iwe vigumu kuwa na kanzidata ya taifa iliyo ya kisasa. Kukosekana kwa mfumo juumuishi wa taarifa za usimamizi ndani ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa ajili ya kukusanya, kuchakata na kuunganisha taarifa kutoka taasisi za huduma kwa wazee nchini kunapunguza uwezo wa Wizara kudumisha kanzidata ya taifa iliyo ya kisasa kuhusu hali, uwezo na utendaji wa makazi ya wazee. Matokeo yake, utoaji taarifa usiojumuishi huleta hatari ya kua na taarifa zisizo thabiti, zisizokamilika au zilizopitwa na wakati. Masuala mengine yaliyobainika kuhusiana na utoaji taarifa yalikuwa.

#### (i) Wamiliki Binafsi wa Makazi ya Wazee Kutokutoa Taarifa ya Vituo Vyao

270. Nilibaini kuwa, baada ya idhini za kuanzishwa na kuendeshwa kwa makazi binafsi ya wazee kutolewa na Kamishna, taasisi hizi zinatakiwa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa makazi ya wazee (kila robo mwaka) kwa

Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Makazi yanayomilikiwa na watu binafsi mara nyingi yalishindwa kuwasilisha taarifa zinazohitajika kila robo mwaka mara tu baada ya kupata vibali vya uendeshaji. Hii ni kinyume na Mwongozo wa 16 wa Miongozo ya Kuanzishwa na Uendeshaji wa Makazi ya Wazee (2019) unaoitaka wizara kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma bora za kijamii, jambo linalohitaji mfumo wa utoaji taarifa ili kupima ubora wa huduma na kuhakikisha utekelezaji wa masharti.

**(ii) Kuchelewa kwa Mawasiliano**

271. Nilibaini kuwa, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu haina Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Usimamizi wa kukusanya, kuchakata na kuunganisha taarifa kutoka taasisi za huduma kwa wazee nchini kote. Matokeo yake, usimamizi wa taarifa umeendelea kufanywa nje ya mfumo, jambo linalopunguza ufanisi, usahihi na maamuzi ya haraka. Kutokutumia mifumo kulisababisha ucheleweshaji mkubwa. Ukaguzi ulirekodi tukio moja ambapo ombi la taarifa lilichukua hadi siku 71 kupata majibu.

**(iii) Pengo la Uwajibikaji**

272. Nilibaini kuwa, asilimia 100 ya viashiria vya matokeo vya Wizara havizingatii mahitaji mahususi ya huduma za kijamii kwa wazee. Mapitio ya mpango mkakati wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu (2021/22–2025/26) yanaonesha kuwa, kulikuwa na viashiria 15 vya matokeo vilivyoendana na malengo makuu matano. Hata hivyo, hakukuwa na viashiria vinavyopima utendaji wa wizara katika kutoa huduma za kijamii kwa wazee.

### 4.4.5 Athari za Changamoto Zilizobainika katika Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano

273. Serikali imetekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha huduma za kijamii na huduma za kisheria kwa wananchi. Hata hivyo, licha ya mpango wa kimkakati wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano, kulikuwa na changamoto kadhaa za kimfumo zinazohatarisha kufanikisha kikamilifu malengo haya, kama ilivyoainishwa hapa chini;

274. Ukaguzi wa ufanisi kuhusu Upatikanaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria umebaini tofauti kubwa katika upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria nchini. Huduma zimeendelea kujikita zaidi maeneo ya mijini kama Dar es Salaam, na kuacha maeneo ya vijijini bila kuhudumiwa ipasavyo. Hali hii inadhoofisha kufikia lengo namba 10 (Kupunguza Usawa) na 16 (Amani, Haki na Taasisi Imara) la Malengo ya Maendeleo Endelevu. Hii imesababisha kuwanyima mamilioni ya maskini wa vijijini haki ya kupata huduma za msaada wa kisheria. Uwezo usiojitosheleza wa taasisi, ulioonekana kupitia kiwango kidogo cha usajili wa wasaidizi wa kuduma za kisheria Mwaka wa Fedha 2024/25 na upungufu wa watumishi kwa asilimia 80 katika ofisi ya Msajili. Hii imeathiri kufikika kwa malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano ya kujenga rasilimaliwatu na taasisi. Aidha, kukosekana kwa kipimo cha viwango vilivyokubalika husababisha mgawanyo usio sahihi wa rasilimali, jambo linalokwenda kinyume na lengo namba 1 (Kukomesha Umaskini) la Malengo ya Maendeleo Endelevu, huku vikwazo vya kifedha, ikiwemo ada zinazotozwa kwa msaada wa kisheria badala ya kutolewa bure, vinaathiri moja kwa moja maskini na kuondoa imani kwa mifumo ya haki pamoja na kutofikiwa kwa malengo ya Mpango wa Tatu na wa Tano wa Maendeleo ya Taifa wa Maendeleowa Miaka Mitano.

275. Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Huduma za Wazee umeonesha upungufu unaohatarisha lengo 1 (Kukomesha Umaskini) na lengo 3 (Afya Bora na Ustawi) ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Chini ya Shabaha 1.3, ulinzi wa kijamii ulikuwa mdogo sana, ambapo programu za wizara zilifikia asilimia 0.08 pekee ya wazee wasio na msaada waliotambuliwa ikilinganishwa na asilimia 100 ya Mpango Mkakati wa kupunguza umaskini. Chini ya Shabaha 3.8, nilibaini kuwa asilimia 68.6 ya wazee wanaoishi kwenye makazi ya wazee hawakuwa na bima ya afya, huku waliokuwa na bima wakikabiliwa na mchakato mrefu wa msamaha, hali iliyopunguza upatikanaji wa huduma za afya kwa wote. Ukarabati wa miundombinu chini ya Mpango wa Miaka Mitano ya Maendeleo ya Taifa haukutekelezwa ambapo kati ya makazi 13 yaliyolengwa, moja tu (Ipuli) ndilo lililokarabatiwa licha ya shilingi milioni 820 za Kitanzania kuidhinishwa. Malengo ya kimkakati ya kufanikisha upatikanaji wa huduma za kijamii kwa asilimia 100 ifikapo mwaka 2026 hayataweza kufikiwa kutokana na kukosekana kwa viashiria vya utendaji na usimamizi usio madhubuti.

276. Ingawa Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 inahimiza kutungwa kwa sheria ya kulinda haki za wazee, Wizara ilishindwa kutekeleza takwa hili kwa zaidi ya miaka 22. Hali hii inaonesha pengo kati ya sera na utekelezaji, huku upungufu wa rasilimali fedha kama vile kutolewa kwa asilimia 18 tu ya bajeti iliyoidhinishwa Mwaka wa Fedha 2023/24 ukikwamisha maendeleo. Aidha,

uhaba mkubwa wa watumishi (kwa asilimia 67) pamoja na ukosefu wa wataalamu wenye ujuzi stahiki umeathiri ubora wa huduma, na hivyo kudumaza utekelezaji wa ajenda ya maendeleo ya rasilimaliwatu chini ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT
ISO 9001:2015 Certified

## SURA YA TANO

## USIMAMIZI WA UHIFADHI WA NAFAKA ZA KIMKAKATI

### 5.1 Utangulizi

277. Sura hii inahusu matokeo ya ukaguzi wa ufanisi unaohusiana na usimamizi wa hifadhi ya nafaka za kimkakati. Inaelezea maeneo ya ukaguzi, Wizara na taasisi za serikali zilizohusika katika ukaguzi, uhusiano wa ukaguzi na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya maendeleo endelevu na matokeo yake.

### 5.1.1 Usuli

278. Hifadhi ya nafaka za kimkakati ni akiba ya nafaka inayosimamiwa na serikali kwa lengo la kuhakikisha usalama wa chakula kwa kutoa kinga dhidi ya uhaba unaosababishwa na majanga ya asili, kubadilika kwa bei, au dharura zingine[1]. Nchini Tanzania, nafaka za kimkakati zinazohifadhiwa ni mahindi, mtama mwekundu, na mpunga. Mahindi yanahifadhiwa kwa wingi, na zaidi ya nusu ( yaani asilimia 52) ya jumla ya chakula cha nishati Lishe inatoka kwenye nafaka na kwamba ndani ya kundi hili, mahindi ndio chanzo kikuu, na huchangia asilimia 59 ya nafaka zote[2].

ISO 9001:2015 Certified

279. Awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo wa mwaka 2017 inabainisha kuwa kilimo ndio msingi wa ukuaji wa uchumi wa Tanzania, maendeleo ya viwanda, na usalama wa chakula, ikichangia takribani asilimia 29.1 ya pato la ndani la Taifa, asilimia 65.5 ya ajira, asilimia 65 ya malighafi za viwandani, na asilimia 30 ya mapato ya mauzo ya nje. Licha ya uzalishaji wa kutosha wa chakula kitaifa, Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Mazao baada ya Mavuno wa mwaka 2018 unaangazia uhaba wa chakula unaoendelea katika sehemu za mikoa ya Pwani, maeneo yenye hali ya ukame hasa ukanda wa kati na kaskazini-magharibi. Uhaba huu unachangiwa kwa kiasi kikubwa na upungufu katika mifumo baada ya mavuno, ikiwa pamoja na upotezaji mkubwa wa nafaka unaosababishwa na utunzaji mbaya, uhifadhi na usafirishaji duni, upungufu katika uuzaji, na uwezo mdogo wa usindikaji[3].

[1] https://en.wikipedia.org/wiki/Strategic_grain_reserve
[2] Taarifa ya akiba ya chakula (Balance Sheets Report) (Mei, 2019)
[3] Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Nafaka Baada ya Kuvuna (2019 -2029)

### 5.1.2 Uhusiano kati ya Usimamizi wa Uhifadhi wa Nafaka za Kimkakati na Malengo ya Maendeleo Endelevu Pamoja na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano

280. Sehemu hii inatoa ufafanuzi wa namna usimamizi wa uhifadhi wa nafaka za kimkakati unavyoendana na Malengo ya maendeleo endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

### 5.1.3 Uhusiano wa Usimamizi wa Uhifadhi wa Nafaka za Kimkakati Unavyoendana na Malengo ya Maendeleo Endelevu

281. Usimamizi wa uhifadhi wa Nafaka za Kimkakati unaendana na Lengo la 2 la Malengo ya maendeleo endelevu, ambayo inakusudia kumaliza njaa, kuhakikisha usalama wa chakula, kuboresha lishe, na kukuza Kilimo ili kuwa endelevu ifikapo 2030. Shabaha Na. 2.1 na 2.2 la Lengo la 2 zinalenga haswa kuhakikisha upatikanaji wa chakula kwa watu wote, hasa maskini na watu walio katika mazingira magumu, pamoja na watoto wachanga, kupata chakula salama, chenye lishe na cha kutosha mwaka mzima ifikapo 2030.

282. Shabaha hizi zinataka usimamizi mzuri wa hifadhi za nafaka za kimkakati ili kuhakikisha upatikanaji wa chakula cha kutosha. Kuongezeka kwa hifadhi ya nafaka za kimkakati kunasaidia upatikanaji wa chakula, ambacho husaidia kupunguza viwango vya utapiamlo, kuongeza afya kwa ujumla, sambamba na kiashiria 2.2.2 cha shabaha Na 2.2 la Lengo Na. 2. Hivyo, hii inachangia kufikia shabaha Na. 2.1 ya Lengo la 2 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo 2030.

#### (a) Uhusiano wa Usimamizi wa Uhifadhi wa Nafaka za Kimkakati na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano

283. Mwelekeo wa kimkakati wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, 2021/22-2025/26, ulikuwa na mpango wa kujenga vihenge 56 vyenye uwezo wa Tani 190,000 na maghala tisa yenye uwezo wa Tani 60,000. Lengo lilikuwa kuongeza uwezo wa kuhifadhi chakula kutoka Tani 501,000 hadi Tani 700,000.

### 5.1.4 Mikakati na Juhudi za Serikali Katika Usimamizi wa Hifadhi ya Nafaka za Kimkakati

284. Serikali imeanzisha mikakati mbalimbali ya kuimarisha usimamizi wa hifadhi ya nafaka za Kimkakati kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na.** 14.

**Jedwali Na. 14: Mikakati Inayohusiana na Usimamizi wa Hifadhi ya Nafaka**

| Jina la Mkakati | Lengo la Mkakati |
|---|---|
| Mkakati wa Pili wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (2015/16-2024/25) | Kufanya mabadiliko ya sekta ya kilimo ili kuleta tija katika kuboresha maisha bora, chakula, na usalama wa lishe. |
| Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Nafaka baada ya Mavuno (2019-2029) | Kupunguza upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno, ambao hufanya kati ya asilimia 30 na asilimia 40 ya jumla ya uzalishaji kila mwaka |
| Mpango Mkakati wa Wizara ya Kilimo 2020/21 – 2025/26 | Ili kuimarisha uwezo wa kuhifadhi mazao ya kilimo nchini kwa kuimarisha maghala na miundombinu inayohusiana, ili kuongeza uwezo wa kitaifa wa kuhifadhi chakula (Kwa ajili ya Umma na Kibinafsi) kutoka Tani 3,031,106 hadi Tani 4,000,000 ifikapo 2026, na kuongeza Uwiano wa utoshelevu wa Chakula kutoka asilimia 125 hadi asilimia 150 ifikapo Juni 2026. |
| Mpango Mkakati wa Wakala wa Kitaifa wa Hifadhi ya Chakula 2021/22 -2025/26 | Kuhakikisha hifadhi ya chakula ni toshelevu kulingana na mahitaji ya taifa ya chakula, kwa kupanua miundombinu ya kuhifadhia, teknolojia, na kuimarisha ununuzi wa chakula. |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Mikakati ya Usimamizi wa Shughuli za Kimkakati za Hifadhi ya Nafaka nchini Tanzania, 2025

NATIONAL AUDIT OFFICE NAOT ISO 9001:2015 Certified

## 5.2 Malengo ya Ukaguzi na Mawanda

### 5.2.1 Malengo ya Ukaguzi

285. Lengo la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini kama Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula na Wizara ya Kilimo wanasimamia kwa tija na ufanisi hifadhi ya nafaka za kimkakati ili kuhakikisha utoshelevu wa upatikanaji wa chakula na uhakika wa bei.

286. Mathalani, ukaguzi ulilenga kutathmini kama:

(i) Mchakato wa ununuzi ulisimamiwa ipasavyo ili kuhakikisha kuwa na hifadhi ya kutosha ya nafaka na inadumishwa;

(ii) Vihenge na Maghala ya nafaka na miundombinu yake ilisimamiwa ipasavyo ili kuhakikisha ubora na wingi wa nafaka zilizohifadhiwa unadumishwa;

(iii) Kulikuwa na njia madhubuti za utoaji wa nafaka zilizohifadhiwa ili kuleta unafuu wakati wa dharura na uuzaji ili kuondoa nafaka za zamani; na

(iv) Kulikuwa na uratibu mzuri na wa kutosha kati ya Wizara ya Kilimo, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, na wadau wengine katika kusimamia hifadhi ya nafaka za kimkakati.

### 5.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

287. Wakaguliwa wakuu walikuwa ni Wizara ya Kilimo na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula. Ukaguzi ulilenga kuangalia mchakato wa ununuzi kama ulikuwa umejitosheleza ili kuwa na upatikanaji wa kutosha wa akiba ya nafaka; utoshelevu wa miundombinu ya kuhifadhi nafaka; mbinu zilizowekwa za uondoaji na urudishiaji wa nafaka ikiwa pamoja na kuwa na unafuu wa bei wakati wa dharura na ubadilishaji wa akiba ya nafaka iliyohifadhiwa kwa muda mrefu; na uratibu mzuri na wa kutosha kati ya Wizara ya Kilimo, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, na wadau wengine katika kusimamia hifadhi ya nafaka za kimkakati. Ukaguzi huu ulihusisha kipindi cha miaka minne ya fedha, kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25. Kipindi hiki kililengwa ili kutathmini utekelezaji wa mpango wa uwekezaji wa miaka 10 wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, unaoishia Mwaka wa Fedha wa 2023/24.

## 5.3 Matokeo ya Ukaguzi

NAOT ISO 9001:2015 Certified

288. Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi juu ya usimamizi wa hifadhi ya nafaka za kimkakati

### 5.3.1 Usimamizi Usiyojitosheleza wa Mchakato wa Ununuzi ili Kudumisha Akiba ya kutosha ya Nafaka za Kimkakati

289. Kupitia mapitio niliyofanya katika Mpango wa Ununuzi wa Mwaka na ripoti za utekelezaji kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/25, nilibaini kuwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula alifikia wastani wa asilimia 58 ya malengo yake ya ununuzi wa nafaka. Pia, nilibaini dosari katika matumizi ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi wa nafaka na kusababisha utegemezi wa mikopo ya kibiashara kutoka kwa benki za biashara. Utegemezi huo ulisababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa ununuzi ya nafaka kutoka wastani wa Shilingi 496,120 hadi Shilingi 813,496 kwa tani.

290. Zaidi ya hayo, mchakato wa ununuzi wa nafaka ulionesha upungufu katika usimamizi wa ubora. Hii ni kutokana na kuwapo kwa wadudu na viashiria vingine vya ubora; kutowapo kwa wafanyikazi walioteuliwa kwa ajili ya kudhibiti ubora wakati wa shughuli za ununuzi; na miundombinu duni ya kuhifadhia nafaka, ambayo ilifanya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kuhifadhi nafaka nje ya ghala lililoteuliwa. Maelezo ya kina ya kila upungufu uliobainishwa ni kama ifuatavyo:

**(a) Kutokutumika kwa Fedha Zilizotengwa kwa Ajili ya Ununuzi wa Nafaka kwa Ufanisi**


291. Ukaguzi huu ulibaini kuwa, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula hakutumia fedha zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi wa nafaka kwa ufanisi. Hii ni kinyume na Agizo namba 2.4.5 la Sheria ya Mashirika (Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula) (Uanzishaji), 2016, ambalo linahitaji Wakala, kudhibiti vizuri matumizi ya rasilimali zote za kifedha. Hii ilisababisha yafuatayo;

**(i) Kuongezeka kwa Gharama ya Ununuzi wa Nafaka kwa Tani[4] Kila Mwaka**

292. Uchambuzi wangu juu ya fedha zilizotumika kwenye ununuzi wa nafaka ulibaini kuwa, gharama za ununuzi zilizidi bei zilizoainishwa katika mipango ya ununuzi ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ambazo zilikuwa shilingi 500,000 kwa tani. Maelezo ya uchanganuzi wa gharama iliyotumika kati ya 2020/21-2024/25 yameoneshwa kwenye **Kielelezo Na. 17**.

[4] Gharama kwa tani ni pamoja na kuhusisha posho kwa watumishi, ambapo ni bei ya mazao shambani

**Kielelezo Na. 17: Ulinganifu wa Gharama Iliyotumika kwa Tani na Kiasi Kilichonunuliwa**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa wa Wakaguzi wa Taarifa za Ununuzi wa Nafaka , 2020/2021-2024/2025, 2025

293. **Kielelezo Na. 17** kinaonesha kuwa, ununuzi kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/21 na 2021/22 ulikuwa na ufanisi ukilinganisha na gharama halisi zilizotumika zikiwa chini ya shilingi 400,000 kwa tani moja. Hii ilikua chini ya bei iliyokadiriwa kwa shilingi 100,000. Hata hivyo, katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, kulikuwa na ongezeko la gharama kwa tani hadi kufikia shilingi 770,111 licha ya kiasi kidogo kununuliwa ukilinganisha na miaka iliyopita. Vilevile, katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, gharama ya juu zaidi kwa tani ambayo ilikuwa shilingi 831,509, licha ya kiasi kikubwa kununuliwa. Pia, katika Mwaka wa Fedha wa 2024/25 gharama ilikuwa shilingi 702,826, na kiasi kilichonunuliwa kiliongezeka.

294. Nilibaini kuwa, tofauti ya bei ya ununuzi wakati wa msimu wa ununuzi ilitokana na maagizo tofauti yaliyotolewa na Wizara ya Kilimo, ambayo yalibadilisha bei iliyopangwa katikati ya shughuli za ununuzi wa nafaka. Zaidi ya hayo, mapitio ya taarifa za utekelezaji kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/23 na 2023/24 ilionesha kuwa wakala uliweka bei elekezi kuwa kati ya shilingi 600,000 hadi 750,000 kwa tani ya kipimo.

295. Hivyo, Wakala alitumia matumizi yasiyopangwa kwa ajili ya ununuzi wa nafaka zaidi ya bajeti uliyopangwa. Hii inapunguza thamani ya pesa na kupunguza matokeo yaliyotarajiwa ya ununuzi wa nafaka, na kuathiri ufikiaji wa malengo yaliyowekwa ya ununuzi wa nafaka.

### (ii) Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula Kutumia Kiasi cha Ziada cha Shilingi bilioni 7.86 Kwa Ajili ya Utunzaji wa Nafaka

296. Kupitia mapitio ya ripoti ya matumizi ya mapato ya kipindi cha kuazia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25 nilibaini kuwa, gharama zilizotumika katika ununuzi wa nafaka zilikuwa zaidi ya bajeti iliyopangwa. Nilibaini kuwa, wakala alitumia shilingi bilioni 16.16 kati ya bajeti iliyopangwa ya shilingi bilioni 8.3 kwa miaka mitatu. Hii ilionesha ongezeko la gharama kwa shilingi bilioni 7.86, ikiwakilisha asilimia 197 ya bajeti iliyoidhinishwa. Maelezo ya kiasi kilichopangwa na kiasi kilicho tumika kimeoneshwa katika **Jedwali Na.**15.

**Jedwali Na.15: Uchambuzi wa Bajeti na Kiasi Kilichotumika katika Shughuli za Ununuzi wa Nafaka Mwaka 2022/23-2024/25**

| Kanda | Kiasi kilichopangwa (Sh. milioni) | Kiasi Kilichotumika (Sh. milioni) | Utofauti (Sh. milioni) |
|---|---:|---:|---:|
| Songea | 1,361 | 3,640 | 2,279 |
| Mpanda | - | 154 | 154 |
| Kipawa | 128 | 629 | 501 |
| Sumbawanga | 1,685 | 4,718 | 3,033 |
| Shinyanga | 326 | 249 | (77) |
| Arusha | 764 | 1,044 | 280 |
| Songwe | 1,388 | 2,402 | 1,014 |
| Dodoma | 1,298 | 891 | (407) |
| Makambako | 1,358 | 2,443 | 1,085 |
| **Jumla** | **8,309** | **16,169** | **7,862** |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kwenye Mpango wa Bajeti wa Muda kati kutoka Miaka ya Fedha 2020/21 hadi 2024/25 na Wakaguzi, 2025

ISO 9001:2015 Certified

297. **Jedwali Na.15** linaonesha kuwa katika kanda sita kati ya tisa zilikuwa na matumizi yanayozidi bajeti zao zilizopangwa, ikionesha matumizi ya kupita kiasi katika shughuli za utunzaji wa nafaka. Hasa, Songea, Sumbawanga, Songwe, Makambako na Kipawa walirekodi matumizi makubwa zaidi ya bajeti. Kinyume chake, Dodoma na Shinyanga waliripoti matumizi halisi chini ya bajeti iliyopangwa, ambayo inaashiria kupunguzwa kwa kiasi cha ununuzi au ufanisi katika uendeshaji katika kanda hizi.

298. Uchambuzi wangu ulibaini kuwa kuongezeka kwa gharama kulisababishwa na upangaji duni wa kiasi cha nafaka kitakachonunuliwa kwa kila mwaka. Matokeo yake, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, ilianzisha vituo vya kukusanya nafaka katika maeneo yenye uzalishaji mdogo na kubadilisha bei ya ununuzi wa nafaka wakati wa mchakato wa ununuzi.

### (b) Kiasi cha Nafaka Zilizonunuliwa Kilikuwa Chini ya Lengo la Ununuzi wa Nafaka kwa Asilimia 38

299. Mapitio ya ripoti za utekelezaji za Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, kwa kipindi cha kuazia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25 nilibaini kuwa pamoja na kuwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ilipanga kununua jumla ya tani 1,491,451 za nafaka kwa miaka 5, ni tani 931,174 tu, sawa na asilimia 62 ya nafaka, zilinunuliwa. Hii ilikuwa chini ya lengo la kila mwaka la nafaka iliyopangwa kununuliwa katika mipango ya ununuzi ya kila mwaka kwa asilimia 38. Sababu ya kutofikia lengo ilihusishwa na kutotolewa kwa kiasi chote cha fedha zilizopangwa. Mapitio ya ripoti za matumizi ya fedha kwa miaka ya fedha kuazia 2020/21 hadi 2024/25 nilibaini kuwa, sababu ya kutofikiwa kwa lengo lililowekwa, ilitokana na wakala kutopata fedha yote kama ilivyopangwa. Vilevile, nilibaini kuwa, kiwango cha utoaji wa fedha kwa kipindi cha miaka mitano ya fedha kutoka 2020/21 hadi 2024/25 kilikuwa shilingi Bilioni 993.29 kati ya shilingi Trilioni 1.94 sawa na asilimia 51.2 ya bajeti.


300. Upungufu huu uliathiri uwezo wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kufikia malengo yake ya kila mwaka ya ununuzi. Pengo la ufadhili lilionekana zaidi katika Mwaka wa Fedha wa 2020/21, ambapo chini ya asilimia 20 ya bajeti iliyopangwa ilitolewa, na kudhoofisha juhudi za ununuzi wa nafaka za kimkakati na kuto kuwa na kinga ya kutosha dhidi ya uhaba unaosababishwa na majanga mbalimbali.

ISO 9001:2015 Certified

### 5.3.2 Utekelezaji Usiyojitosheleza wa Mikakati Inayohusiana na Hifadhi ya Nafaka za Kimkakati na Usalama wa Chakula

301. Katika kupitia Ripoti za Utekelezaji wa Robo Mwaka za Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kuanzia Mwaka wa Fedha 2019/20 hadi 2023/24, nilibaini kuwa, kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2020/21 hadi 2023/24, hifadhi ya nafaka zilizokuwapo mwishoni mwa mwaka ilikuwa chini ya kiwango kinachotakiwa cha tani 150,000. Hii ni kinyume na aya ya 3.4 ya mpango mkakati wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula wa 2020/21 hadi 2025/26 ambao unataka kiwango cha akiba ya mwisho cha nafaka kisiwe chini ya tani 150,000. **Kielelezo Na. 18** kinaonesha hali ya ufikiaji wa kiwango kilichowekwa.

**Kielelezo Na. 18: Hali ya Ufikiaji wa Kiwango cha Akiba ya Chakula Kilichotakiwa Kuwapo Kila Mwisho wa Mwaka**




***Chanzo***: Uchambuzi wa Takwimu za Ripoti Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula za Utekelezaji za Robo Mwaka na Wakaguzi kuazia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025, 2025

302. **Kielelezo Na.18** kinaonesha mwenendo wa kiasi cha nafaka zilizohifadhiwa katika kila Mwaka wa Fedha unapoishia kutoka Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25. Takwimu zinaonesha kuwa kwa miaka minne ya fedha kutoka 2020/21 hadi 2023/24 kiasi-ishia kilikuwa chini ya kiwango kilichotakiwa cha tani 150,000. Takwimu zinaonesha kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2023/24, nafaka iliyohifadhiwa ilikuwa chini sana, na tofauti ya tani 104,825 chini ya kiwango kinachotakiwa.

ISO 9001:2015 Certified

303. Akiba ya nafaka ni muhimu katika kuleta utulivu wa mfumuko wa bei ya chakula na kuwa kama kinga dhidi ya upungufu wa chakula nchini. Pale ambapo akiba inakuwa ipo ya kutosha, serikali inaweza kuingiza sokoni nafaka iliyokuwa imehifadhiwa pale inapotokea kuwa na mavuno kidogo, ukame, au mnyonyoro wa usambazaji mazao unakumbwa na changamoto, na hivyo kuzuia kasi ya ongezeko la bei ya chakula. Kinyume chake, akiba isipokuwa ya kutosha huongeza bei, kwani usambazaji wa chakula unapokuwa mdogo huongeza gharama na kuongeza shinikizo la mfumuko wa bei. Uchambuzi wa athari za upatikanaji wa akiba ya kufunga mwaka (salio-azia) ya mwaka unaofuata na mfumuko wa bei vimewasilishwa katika **Error! Reference source not found.**

**Jedwali Na. 16: Uhusiano kati ya Viwango vya Akiba na Mfumuko wa Bei ya Chakula**

| Mwaka wa Fedha | Akiba Ishia (Tani) | Mufumuko wa Bei ya Chakula katikati ya Mwaka (%) |
|---|---|---|
| 2020/21 | 52,724 | 3.8 |
| 2021/22 | 107,384 | 4.7 |
| 2022/23 | 141,576 | 5.9 |
| 2023/24 | 45,175 | 7.8 |
| 2024/25 | 340,479 | 0.9 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wagakuzi katika taarifa za Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO)[5] na Ripoti za Utekelezaji za Robo Mwaka za Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula NFRA (2020/21-2024/25), 2025

304. **Jedwali Na. 16** linaonesha uhusiano kati ya viwango vya hifadhi ya chakula na mfumuko wa bei ya chakula katikati ya mwaka katika miaka mitano ya fedha. Kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2022/23, akiba iliongezeka kutoka tani 52,724 hadi tani 141,576, lakini mfumuko wa bei ulipanda kutoka asilimia 3.8 hadi asilimia 5.9, na kuonesha kuwa akiba iliyoongezeka haikuleta utulivu wa bei mara moja kwani bado ilikuwa chini ya kiwango kinachotakiwa cha tani 150,000. Mnamo 2023/24, akiba ilishuka hadi Tani 45,175, sanjari na kiwango cha juu zaidi cha mfumuko wa bei cha asilimia 7.8, ikiangazia hatari ya bei ya vyakula kupanda pale akiba ya chakula inapokuwa chini ya kiwango kinachotakiwa. Kinyume chake, mnamo 2024/25, akiba iliongezeka hadi tani Tani 340,479, na mfumuko wa bei ulishuka hadi asilimia 0.9, ikionesha kuwa akiba ya kutosha ya chakula hupunguza mfumuko wa bei ya chakula na kuimarisha bei ya vyakula sokoni.

ISO 9001:2015 Certified

305. Mbali na hilo, kutokana na ongezeko la kiasi cha nafaka kilichohifadhiwa kutoka Mwaka wa Fedha wa 2020/21 hadi 2023/23, mfumuko wa bei ulikuwa ukiongezeka. Hii ilitokana na matumizi ya kiwango kinachohitajika cha akiba kilichopitwa na wakati cha tani 150,000, ambacho kilianzishwa mwaka 1976, kwa kutumia idadi ya watu milioni 15, na haijarekebishwa ili kuendana idadi ya sasa ya watu. Kulingana na sensa ya 2022 idadi ya watu imefikia hadi milioni 61.7. Kutofikiwa kwa kiwango kilichopangwa cha akiba ya chakula kulitokana na upungufu wa malengo ya ununuzi yaliyowekwa na Wakala wa Kitaifa wa Hifadhi ya Chakula.

[5] https://www.fao.org/faostat/en/#data/CP // Ilitembelewa tarehe 9 Novemba 2025 Saa mbili usiku

### 5.3.3 Usimamizi Usiyojitosheleza wa Miundombinu ya Kuhifadhia Mazao

306. Nilifanya tathmini ya usimamizi wa miundombinu ya uhifadhi wa nafaka, nikijikita kwenye vifaa kama vile maghala, vihenge, na vibanda vya kuhifadhi kwa muda. Tathmini yangu ilibaini yafuatayo:

(a) **Upungufu wa Asilimia 57 wa Kuhifadhi Nafaka**

307. Katika kupitia ripoti za utekeleza za Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kutoka Mwaka wa Fedha wa 2023 hadi 2024, nilibaini kuwa, wakala kwa sasa ana uwezo wa kuhifadhi takriban tani 303,000, ikiwa ni upungufu wa asilimia 57 dhidi ya uwezo uliokusudiwa wa tani 700,000. Pengo hili haliendani na malengo yaliyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula wa kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2025/26.

308. Upungufu wa ufikiaji wa uwezo unaotakiwa wa uhifadhi ulichangiwa hasa na utekelezaji usiokamilika wa Mradi wa Upanuzi wa Vihenge na Maghala ya kuhifadhia nafaka ambao ulilenga kuongeza uwezo wa kuhifadhi hadi tani 165,000. Hii ilitokana na upungufu katika usimamizi wa mkandarasi wakati wa utekelezaji wa majukumu ya kimkataba chini ya makubaliano kati ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula na mkandarasi.

309. Kutofikiwa kwa uwezo unaohitajika wa kuhifadhi nafaka kulisababisha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kujenga vibanda vya muda vya kuhifadhia nafaka na kutumia sekta binafsi kutoa sehemu/vibanda vya ziada vya kuhifadhia. Hii ilidhihirika zaidi katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, kipindi ambacho wakala alinunua jumla ya tani 340,002.218 ya nafaka, ikizidi uwezo wake wa kuhifadhi kwa tani 37,002.218.

310. Matumizi ya vibanda vya muda vya kuhifadhi nafaka kulisababisha Wakala wa Taifa kutumia gharama za ziada za shilingi bilioni 2,453,632,888 kwa kukodisha vifaa vya kuhifadhi chakula kutoka taasisi binafsi, ambayo iliathiri rasilimali-fedha.

**(b) Uhakiki Usiojitosheleza wa Ubora wa Nafaka Zinazohifadhiwa**

311. Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa hatua za udhibiti ubora, kama vile kuhifadhi nafaka kwa muda usiozidi miaka mitatu, kuhakikisha mazingira mazuri ya kuhifadhi nafaka, na udhibiti wa wadudu kwenye nafaka iliyohifadhiwa katika maghala, hazikutekelezwa ipasavyo. Hasa, nafaka zilihifadhiwa kwa zaidi ya muda uliopendekezwa wa miaka mitatu. Hii ilikuwa kinyume na aya ya 3.4.3 ya

Mpango wa Uwekezaji wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula 2014/15-2023/24, ambayo inaweka sera ya kudumisha hifadhi ya chakula chini ya miaka 3, na baada ya hapo itakuwa vigumu kuhifadhi nafaka ikiendelea kuwa katika hali nzuri. Kiasi cha nafaka zilizokaa zaidi ya miaka mitatu ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 17.**

**Jedwali Na. 17: Nafaka Zilizokaa Zaidi ya Muda Unaotakiwa**

| Kanda | Kiasi cha Nafaka (Tani) Kilichokaa zaidi ya Muda unatakiwa katika Miaka ya Fedha Tofauti | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Arusha | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Dodoma | 199.500 | 1,440.625 | 30.212 | 0 | 212.202 |
| Kipawa | 0 | 393.405 | 0 | 4,406.358 | 10,822.311 |
| Makambako | 0 | 10,427.177 | 0 | 0 | 0 |
| Songwe | 0 | 577.432 | 0 | 0 | 371.191 |
| Shinyanga | 200.341 | 4,101.813 | 0 | 5,719.112 | 5,594.372 |
| Songea | 2,717.441 | 4,003.546 | 0 | 0 | 0 |
| Sumbawanga | 0 | 11,697.107 | 63 | 4,128.185 | 4,128.185 |
| **Jumla** | **3,117.282** | **32,641.105** | **93.212** | **14,253.655** | **13,266.315** |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa ya Maendeleo na Ripoti za Robo Mwaka, 2020/21-2024/2025, 2025

312. **Jedwali Na. 17** linaonesha kuwa kiasi cha akiba ya nafaka iliyokaa zaidi ya muda ulioelekezwa ilirekodiwa katika maeneo yote isipokuwa Arusha, ambayo haikuwa na Nafaka ziliyokaa zaidi katika kipindi kinachotakiwa, kwa miaka yote mitano ya fedha. Kinyume chake, ukanda wa Sumbawanga ulionesha kiwango kikubwa zaidi cha nafaka zilizokaa zaidi ya miaka mitatu, ambacho ni tani 11,697.107 kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 na zaidi ya tani 4,000 kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 na 2024/25. Wakati huo huo ukanda wa Kipawa, ulionesha ongezeko la nafaka zilizokaa zaidi ya miakaka mitatu kutoka tani 393.405 kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi tani 10,822.311 kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, ikionesha kupungua kwa ufanisi katika mauzo ya nafaka na usimamizi wa nafaka.

313. Hali hii kwa kiasi kikubwa ilisababishwa na kutofuatwa kwa kanuni inayoelekeza nafaka za kwanza kuingia ndiyo ziwe za kwanza kutoka wakati wa shughuli za kuingiza na kutoa nafaka. Kanuni hii ni muhimu wakati wa kutoa nafaka za zamani na kuhifadhi nafaka mpya ili kutunza ubora wa nafaka. Kuhifadhi nafaka zaidi ya kikomo kilichopendekezwa cha miaka 3 kulisababisha kupungua kwa ubora, haswa kwa sababu ya kuongezeka kwa wadudu, unyevunyevu, na sababu zingine za mazingira, hivyo kusababisha upotevu wa mapato. Uchambuzi wangu kwenye taarifa za nafaka za Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kutoka Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 hadi 2024/2025,

ulibainisha kuwa upotevu wa mapato unaohusishwa na kupungua kwa ubora wa nafaka za chakula, ulikuwa ni shilingi bilioni 4.43 kwa tani 8,046.7 za mahindi.

314. Hasara hii inatokana na kuuza mahindi yaliyopungua ubora kwa bei pungufu, kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula , ikilinganishwa na thamani ya awali ya ununuzi.

**(c) Matengenezo Yasiyojitosheleza ya Miundombinu ya Kuhifadhia Nafaka na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula**

315. Mapitio ya ripoti za ununuzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 na ripoti za ubora za kila mwezi za kipindi kama hicho yalibaini kuwa, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula alikuwa na miundombinu ya ghala yenye uwezo wa kuhifadhi tani 295,000. Lakini, kwa sababu ya matengenezo yasiyojitosheleza, maghala/vihenge vyenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 57,000 havikutumika, na hivyo kupungua kwa uwezo wa kuhifadhi hadi tani 238,000. Upungufu huu unakiuka masharti ya Sheria ya Uanzishaji wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, 2008, na Mwongozo wa Uendeshaji (2015), ambapo vyote vinamtaka Wakala kudumisha miundombinu na kuwa na miundombinu inayofanya kazi ya uhifadhi ili kulinda usalama wa hifadhi ya nafaka ya kitaifa. **Jedwali Na. 18** linatoa uchambuzi wa kina.

**Jedwali Na. 18: Uchakavu wa Maghala na Uwezo Halisi Unaoweza Kutumika hadi Mwaka 2024/25**

| Kanda | Ukubwa wa Ghala Liliochakaa (Tani) | Ukubwa wa Ghala Unaotumika (Tani) |
|---|---|---|
| Arusha | - | 58,000 |
| Dodoma | 9,000 | 31,500 |
| Kipawa | 20,000 | 33,500 |
| Makambako | - | 22,000 |
| Songwe | 1,000 | 16,000 |
| Shinyanga | 4,500 | 15,500 |
| Songea | - | 32,000 |
| Sumbawanga | 22,500 | 29,500 |
| **Jumla** | **57,000** | **238,000** |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kwenye Ripoti ya Ununuzi ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula Julai 2024/2025, 2025

316. **Jedwali Na. 18**, inaonesha kanda ya Arusha, Makambako, na Songea hayakuripoti kuchakaa kwa miundombinu ya ghala, na hivyo kutumia uwezo wao wote wa kuhifadhi nafaka. Kinyume chake, kanda ya Dodoma, Kipawa, na

Sumbawanga ilionesha maghala yao kuchakaa zaidi, na kusababisha kupungua kwa kiasi kikubwa cha uwezo wao wa kuhifadhi nafaka.

317. Katika Mwaka wa Fedha wa 2024/25, Wakala wa Taifa wa Kuhifadhi Chakula iliongeza wigo wa ununuzi wa nafaka ulipanuliwa na kufikia jumla ya tani 572,000. Aidha, kutokana na kupungua kwa uwezo wa kuhifadhi nafaka, wakala alilazimika kutumia hema za kuhifadhia nje ya ghala, ambayo yalisababisha nafaka kuwa kwenye mazingira hatari, kama vile unyevu na wadudu ambavyo vilihatarisha ubora wa akiba ya nafaka iliyohifadhiwa.

318. Kwenye mapitio ya ripoti ya Juni 2025 ya hesabu za akiba ya nafaka iliyopo, nilibaini kuwa, shehena yenye jumla ya tani 19,055.63 huko Songwe, Kakozi, Ileje na Makambako zilihifadhiwa katika vituo visivyo na ubora ikiwa pamoja na vibanda vya wazi na vibanda visivyo na paa. Mazao yaliyokuwa yamehifadhiwa yalikuwa na thamani ya takribani shilingi bilioni 13.3, kulingana na bei ya ununuzi ya shilingi 700,000 kwa tani. Pia, shehena hizi zilikuwa zimeanza kupoteza ubora kwa sababu ya kuwekwa wazi muda mrefu. Kupungua ubora kunahusianishwa moja kwa moja na ukosefu wa miundombinu ya kutosha na ya kudumu ya kuhifadhi nafaka, na kusababisha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kuhifadhi nafaka nje na katika mazingira hatarishi.

### 5.3.4 Uratibu Usiyojitosheleza kati ya Wadau na Wizara ya Kilimo Katika Kusimamia Uhifadhi wa Nafaka za Kimkakati

ISO 9001:2015 Certified

319. Mapitio ya nyaraka ya uanzishaji wa wakala ilibainika uratibu usiyojitosheleza kati ya Wizara ya Kilimo na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, na kusababisha wote kufanya shughuli ya aina moja. Hii ilikuwa kinyume na Mkakati wa Kitaifa wa Kusimamia Mazao baada ya Mavuno, chini ya Lengo F la mkakati, ambalo linasisitiza kuimarisha uwezo wa kitaasisi, uratibu, ushirikiano, na ushiriki wa wadau kati ya wadau wa usimamizi wa mazao baada ya mavuno ili kuimarisha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Mazao baada ya Mavuno.

320. Uchambuzi wa takwimu kutoka kwa Ripoti ya Viashiria vilivyounganishwa na Malipo, (Kiashiria Na. 5.2) ya Juni 2025 nilibaini kuwa taasisi zote mbili zilikuwa zikifanya kazi sambamba na idara zinazohusika na kusimamia miundombinu ya uhifadhi na kazi za uuzaji. Kwa mfano, Wakala wa Taifa wa Uhifadhi wa Chakula na Wizara ya Kilimo zilikuwa na idara zilizopewa jukumu la kutafuta masoko ya ndani na kimataifa ya nafaka, bila kuwa na mipaka kulingana na nyaraka zao za uanzishaji kuhusu wajibu huu.

321. Hii ilisababisha wadau wote kama Wizara Ya Kilimo na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya chakula wote kufanya kazi ya aina moja na kusababisha matumizi yasiyofaa ya rasilimali za umma, na kupungua kwa ufanisi wa uendeshaji. Kukosekana kwa mfumo wa kitaasisi uliofafanuliwa wazi unaoelezea majukumu na wajibu wa wahusika yaani Wizara ya Kilimo na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kumechangia changamoto ya miundombinu ya kuhifadhia chakula.

### 5.4 Athari za Changamoto Zilizobainika katika Kuyafikia Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

322. Shabaha ya 2.1 na 2.2 ya Lengo Na. 2 la Malengo ya Maendeleo Endelevu zinalenga haswa kuhakikisha upatikanaji wa chakula salama, chenye lishe na cha kutosha mwaka mzima ifikapo 2030 kwa watu wote, hasa maskini na watu walio katika mazingira magumu, pamoja na watoto wachanga. Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano unalenga kuongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka hadi Kufikia tani 700,000 ili kuongeza usalama wa chakula nchini.

323. Nilibaini kuwa, hadi Mwaka wa Fedha 2024/2025, uwezo wa kuhifadhi nafaka ulikuwa Tani 303,000, ambayo ni sawa na asilimia 43 ya lengo lililowekwa. Hii imesababisha Wakala wa Taifa wa Uhifadhi wa Chakula kutumia uhifadhi wa muda mfupi, ambao iliongeza gharama za uendeshaji. Pia, nilibaini kuwa, Wakala wa Taifa wa Uhifadhi wa Chakula hakufikia kiwango cha nafaka za kimkakati kinachotakiwa kuwapo unapomaliza mwaka ili kuleta utulivu wa bei na kuwezesha ufikiaji wa chakula kwa wote wakati wa uhaba wa chakula. Hii ilionesha hatari za kutofikia malengo yaliyowekwa ya kuongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka hadi Tani 700,000 kulingana na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ifikapo 2025/26 ili kuhakikisha upatikanaji wa chakula kama ilivyooneshwa katika Lengo la 2 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo 2030.

## SURA YA SITA

## USIMAMIZI WA USALAMA MAHALI PA KAZI NA UTOAJI WA HUDUMA ZA FIDIA KWA WAFANYAKAZI

### 6.1 Utangulizi

324. Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi kutoka kwenye ripoti za ukaguzi wa ufanisi unaohusiana na usimamizi wa ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi, na utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi. Aidha, sura hii inachambua uhusiano wa ukaguzi huu na Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Ukaguzi wa ufanisi uliohusika katika sura hii unajumuisha Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi; na Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi.

#### 6.1.1 Usuli kuhusu Usimamizi wa Usalama Mahali pa Kazi na Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi

325. Ili sehemu ya kazi ikaguliwe, ni lazima isajiliwe na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kanzidata ya Mfuko wa Fidia wa kwa Wafanyakazi, kuna sehemu za kazi 48,906 zilizosajiliwa, idadi ambayo ni ndogo ikilinganishwa na makadirio ya maeneo 219,371 yaliyotambuliwa kama sehemu za kazi na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, ambayo ni mmoja wa wadau wakuu katika utambuzi wa sehemu za kazi. Aidha, mapitio ya Kanzidata ya Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi inayohusiana na usajili wa sehemu za kazi inaonesha kuwa, kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Wakala wa Usalama Mahali pa Kazi ulitambua sehemu za kazi 1,472 katika Taasisi za Umma kufikia Juni 2025. Hata hivyo, ni Taasisi 260 tu kati ya hizo (sawa na asilimia 18) zilisajiliwa kwa mafanikio na Wakala. Ripoti ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ya Mwaka 2024/25 pia inaonesha mwelekeo wa kuongezeka kwa ajali mahali pa kazi na magonjwa yatokanayo na kazi, ambapo matukio yaliongezeka kutoka 1,783 (asilimia 39) kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 hadi kufikia matukio 2,730 katika Mwaka wa Fedha 2020/21.

326. Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi pia unakabiliwa na changamoto zinazokwamisha utendaji kazi wake. Suala moja kuu ni uelewa mdogo wa umma kuhusu mfuko na faida zake miongoni mwa wafanyakazi. Jambo jingine ni kuchelewa kushughulikia madai na ulipaji wa fidia usioridhisha. Changamoto hizi zinachangia ucheleweshaji wa msaada unaohitajika kwa wafanyakazi walioumia na familia zao. Kutozingatia kwa waajiri katika kuwasilisha michango

yao ya kila mwezi kwenye mfuko pia kunadhoofisha utulivu wa kifedha wa Mfuko.

### 6.1.2 Uhusiano wa Usimamizi wa Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi na Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano

327. Sehemu hii inaonesha uhusiano wa usimamizi wa ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi pamoja na utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi, na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, kama inavyoelezwa hapa chini.

#### (a) Uhusiano wa Usimamizi wa Ukaguzi wa Usalama Mahali pa Kazi na Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi na Malengo ya Maendeleo Endelevu

328. Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi una uhusiano na utekelezaji wa Lengo la 8 la Malengo ya Maendeleo Endelevu, Shabaha ya 8.8, ambayo inatoa wito wa kulinda haki za kazi na kukuza mazingira salama ya kazi kwa wafanyakazi wote, ikiwa pamoja na makundi yaliyo katika mazingira magumu. Ukaguzi wa afya na usalama mahali pa kazi pia una uhusiano na utekelezaji wa Lengo la 3 la Malengo ya Maendeleo Endelevu, shabaha ya 3.9, inayolenga kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo na magonjwa yanayosababishwa na kemikali hatari, uchafuzi wa mazingira, na huduma zisizo salama za maji, usafi wa mazingira, na usafi wa mwili.

329. Vilevile, Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi una uhusiano na utekelezaji wa Lengo la 8 la Malengo ya Maendeleo Endelevu, Shabaha ya 8.8, ambayo inatoa wito wa kulinda haki za kazi na kukuza mazingira salama ya kazi kwa wafanyakazi wote, ikiwa pamoja na makundi yaliyo katika mazingira magumu. Utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi pia una uhusiano na utekelezaji wa Lengo la 1 la Malengo ya Maendeleo Endelevu, Shabaha ya 1.3 inayosisitiza kuhusu utekelezaji wa mifumo na hatua muafaka za kitaifa za hifadhi ya jamii kwa wote.

### (b) Uhusiano wa Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi na Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano

330. Uhusiano wa ukaguzi wa ufanisi katika ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi pamoja na utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi, na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano umeelezwa katika **Jedwali Na. 19** hapa chini.

**Jedwali Na. 19: Uhusiano wa Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi Pamoja na Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano**

| Jina la Ukaguzi | Mpango wa Taifa wa Maendeleo | Eneo la Kipaumbele | Sekta | Hatua za Kuchukua |
|---|---|---|---|---|
| Ukaguzi wa Ufanisi katika Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi | Mpango wa III | Usalama wa Umma, Sheria na Utaratibu | Maendeleo ya Rasilimaliwatu | Uimarishaji wa Usalama wa Umma, Sheria na Utaratibu |
| Ukaguzi wa Ufanisi katika Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi | Mpango wa III | Maendeleo ya Jamii | Maendeleo ya Rasilimaliwatu | Uboreshaji na ulindaji wa maslahi na mazingira ya kazi ya wafanyakazi katika sekta zote |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa wakaguzi kwa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, Mwaka 2025

### 6.1.3 Mikakati na Jitihada za Serikali Katika Usimamizi wa Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi na Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi


### (a) Mikakati ya Serikali Katika Usimamizi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi na Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi

331. Ili kuhakikisha usimamizi madhubuti wa ukaguzi wa usalama mahali pa kazi, ukaguzi wa afya katika maeneo ya kazi na utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi, Serikali, kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, ziliweka mikakati mbalimbali iliyotoa mwelekeo wa kufikia usalama wa maeneo

NATIONAL AUDIT OFFICE NAOT ISO 9001:2015 Certified

ya kazi na huduma za fidia kwa wafanyakazi. Baadhi ya mikakati hiyo imeorodheshwa katika **Kielelezo Na. 19.**

**Kielelezo Na. 19: Mikakati katika Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kwa Mikakati ya Serikaliwa Mwaka

332. Vilevile, mikakati ya serikali inayozingatia usimamizi wa ukaguzi wa afya na usalama mahali pa kazi ni pamoja na: kusimamia usajili wa maeneo ya kazi, kufanya ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi katika maeneo ya kazi, na kuratibu na taasisi zingine kusimamia maeneo ya kazi kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi; na kuandaa pamoja na kufuatilia utekelezaji wa sera za kazi ikijumuisha afya na usalama mahali pa kazi kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano.

### (b) Jitihada za Serikali Katika Usimamizi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi na Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi

333. Ili kuhakikisha afya na usalama mahali pa kazi, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/25, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi iliendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuhakikisha kuwa maeneo ya kazi yanasajiliwa kwa mujibu wa

Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi Na. 5 ya mwaka 2003. Katika kutekeleza jukumu hili, serikali imejikita katika kuhakikisha kuwa maeneo yote ya kazi nchini yanafikika na kusajiliwa, kutoa elimu kwa waajiri kuhusu umuhimu wa usajili kwa mujibu wa mahitaji ya kisheria, na kuboresha mfumo wa usajili kwa kuufanya kuwa wa haraka, rahisi na rafiki kwa mtumiaji.

334. Vilevile, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia huduma za fidia kwa wafanyakazi, inaendelea kutoa fidia kwa wafanyakazi wanaopata majeraha yatokanayo na kazi, magonjwa yatokanayo na kazi na kutoa msaada kwa wategemezi katika matukio ya vifo vinavyohusiana na kazi. Huduma za fidia kwa wafanyakazi zinaimarishwa kupitia usajili wa waajiri na ukusanyaji wa michango, malipo ya mafao, shughuli za uwekezaji, uelimishaji wa umma, na utoaji wa huduma za utengamao.

## 6.2 Malengo ya Ukaguzi na Mawanda ya Ukaguzi

### 6.2.1 Malengo ya Ukaguzi

335. Lengo kuu la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini iwapo Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano, na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi zilisimamia kwa ufanisi ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi, na kutoa kwa ufanisi huduma za fidia kwa wafanyakazi pamoja na wanufaika wao husika katika matukio ya majeraha, magonjwa, au vifo vinavyotokana na kazi. ISO 9001:2015 Certified

336. Ukaguzi hasa ulijikita katika kutathmini iwapo:

(a) Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano zilisimamia kwa ufanisi ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi ili kudhibiti ajali, magonjwa, na vifo vinavyotokana na kazi; na
(b) Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi unasimamia kwa ufanisi utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi na wanufaika wao husika katika matukio ya majeraha, magonjwa, au vifo vilivyotokana na kazi.

### 6.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

337. Kwa upande wa Ukaguzi wa Usimamizi wa Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Taasisi kuu zilizokaguliwa ni Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi. Ukaguzi huu ulitathmini ukamilifu wa daftari la usajili katika maeneo ya kazi, ufanisi wa

taratibu za kubadilishana taarifa na taasisi zingine za umma katika kusaidia ukaguzi wa maeneo ya kazi, utoshelevu wa mipango ya ukaguzi, vitendea kazi, na rasilimali, pamoja na muda uliotumika, ufikiaji, na ubora wa ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi. Ukaguzi ulihusisha miaka minne ya fedha, kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2025/26.

338. Aidha, Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi, mkaguliwa mkuu alikuwa ni Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Ukaguzi huo ulilenga kutathmini ufanisi wa michakato ya usimamizi wa madai, kuanzia uwasilishaji, tathmini hadi upitishaji na utoaji wa fidia kwa wanufaika waliokusudiwa. Ukaguzi huu pia ulitathmini kiwango cha usajili wa waajiri wanaostahili, waajiri wanaochangia, wanufaika, pamoja na utaratibu uliopo wa kuhamasisha uelewa miongoni mwa wafanyakazi na waajiri. Ukaguzi huu ulihusisha miaka minne ya fedha, kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25.

## 6.3 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi


339. Nilibaini upungufu katika usimamizi wa ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi. Masuala makuu yaliyobainika ni pamoja na kuongezeka kwa kiwango cha vifo vinavyotokea maeneo ya kazi, usajili usioridhisha wa maeneo ya kazi, na utekelezaji duni wa ukaguzi wa kisheria kama ulivyofafanuliwa hapa chini:

ISO 9001:2015 Certified

### 6.3.1 Kuongezeka kwa Viwango vya Vifo Mahali pa Kazi kwa Asilimia 22

340. Nilibaini kuwa kuanzia Mwaka wa Fedha 202/22 hadi 2024/25, kulikuwa na mabadiliko ya idadi ya vifo vilivyotokana na kazi kutoka 76 hadi 161 katika Mwaka wa Fedha 2022/23, kabla ya kushuka hadi vifo 76 katika Mwaka wa Fedha 2023/24, na kisha kupanda hadi vifo 93 katika Mwaka wa Fedha 2024/25, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 20.**

**Kielelezo Na. 20: Mwenendo Usio thabiti wa Kupungua kwa Vifo Mahali pa Kazi**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Ripoti za Utekelezaji kutoka Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25

341. **Kielelezo Na. 20** kinaonesha kuwa vifo mahali pa kazi vilivyoripotiwa na Wakala wa Usalama Mahali pa Kazi havijapungua kwa mfululizo katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25, badala yake vimekuwa vikibadilika. Idadi ya vifo vitokanavyo na kazi vilivyorekodiwa viliongezeka kutoka 76 Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 161 Mwaka wa Fedha 2022/23, ikiwa ni zaidi ya mara mbili katika kipindi cha miaka miwili. Baada ya kilele hicho, idadi ya vifo ilishuka hadi 76 kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, kisha ikapanda tena hadi 93 Mwaka wa Fedha 2024/25, jambo linaloashiria mwelekeo usio thabiti badala ya uimara. Pamoja na jitihada za Wakala wa Usalama Mahali pa Kazi za kupunguza ajali na vifo mahali pa kazi, mienendo ya vifo mahali pa kazi unaendelea kubadilika, jambo ambalo linasisitiza uhitaji wa hatua madhubuti zaidi za kisera na juhudi endelevu katika utekelezaji wa sheria.

### 6.3.2 Usajili Usioridhisha wa Maeneo ya Kazi katika Kusaidia Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi

342. Nilibaini usajili usioridhisha wa maeneo ya kazi uliofanywa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi, licha ya kuwapo wa mipango ya kuyaibua maeneo hayo kupitia Makubaliano ya Mashirikiano, Mikataba ya Kubadilishana Taarifa, matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kijiografia, na uhamasishaji wa usajili wa mtandaoni, kama ilivyoainishwa katika lengo C la Mpango Mkakati wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi wa mwaka 2021 hadi 2026. Hali hii ni Kinyume na Kifungu cha 15 na 16 cha Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003, ambayo inaipa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi mamlaka ya kuyaibua na kuyasajili maeneo yote ya kazi ili kuhakikisha yanazingatia viwango vya usalama na afya vinavyotakiwa. Maelezo ya kina kuhusu masuala haya ni kama ilivyoelezwa hapa chini:

#### (a) Usajili Usioridhisha wa Maeneo ya Kazi

343. Nilibaini kuwa Wakala wa Usimamizi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi haukusajili asilimia 79 ya maeneo ya kazi 179,196 yaliyoibuliwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Hali hii ni kinyume na Kifungu cha 17 (5) cha Sheria ya Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya mwaka 2003, ambacho kinakataza wamiliki wa maeneo ya kazi kuendesha shughuli zao bila kusajiliwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi. Aidha, nilibaini kuwa bado kuna ongezeko la maeneo ya kazi ambayo hayajasajiliwa, kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na. 20.**

**Jedwali Na. 20: Ongezeko la Maeneo ya Kazi ambayo Hayakusajiliwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi**

| Miaka ya Fedha | Idadi ya Maeneo ya Kazi yaliyotambuliwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu | Maeneo ya Kazi yalisajiliwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi | Pengo la Usajili | Asilimia ya Pengo la Usajili |
|---|---|---|---|---|
| 2023/2024 | 87,556 | 28,238 | 59,318 | 67.7 |
| 2024/2025 | 179,196 | 37,382 | 141,814 | 79.1 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi Mwaka 2025

344. **Jedwali Na. 20** linaonesha kuwa, ikilinganishwa na Takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu, idadi ya maeneo ya kazi ambayo hayakusajiliwa iliongezeka kutoka asilimia 67 Mwaka wa Fedha 2023/24 hadi asilimia 79 Mwaka wa Fedha 2024/25. Mwenendo huu unaonesha juhudi bado zinahitajika kufanywa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi katika kufanya usajili wa maeneo ya kazi nchini. Aidha, mapitio ya hali ya usajili wa maeneo ya kazi yameonesha kuwa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi imetambua maeneo ya kazi 1,472 katika taasisi za umma kufikia Juni 2025. Hata hivyo, ni Taasisi 260 pekee kati ya hizo, sawa na asilimia 18 zilizosajiliwa kikamilifu na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi, huku maeneo mengine ya kazi yakiwa hayajasajiliwa, jambo linaloashiria maeneo yanayohitaji maboresho.

ISO 9001:2015 Certified

345. Usajili usioridhisha wa maeneo ya kazi umetokana na ushirikiano usiotosheleza kati ya Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Kituo cha Uwekezaji Tanzania, Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania, na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni katika kubadilishana taarifa za maeneo ya kazi. Hali hii inazuia ufanisi wa taarifa na juhudi za usajili wa maeneo ya kazi.

346. Usajili mdogo wa taasisi za umma umesababisha Taasisi hizo ambazo hazijasajiliwa kutojumuishwa katika ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha uzingatiaji wa viwango vya usalama na afya mahali pa kazi, jambo linalowaacha wafanyakazi katika maeneo ya kazi yasiyosajiliwa katika hatari ya vihatarishi visivyotambuliwa, na kuongeza uwezekano wa kutokea kwa ajali na magonjwa yatokanayo na kazi.

**(b) Kutotozwa Tozo kwa Maeneo ya Kazi Yanayoendesha Shughuli Zake bila Cheti cha Usajili kutoka Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi**

347. Nilibaini kuwa, maeneo ya kazi 11,578 yaliyokuwa hayana vyeti vya usajili hayakutozwa faini, kinyume na Kifungu cha 17(5) cha Sheria ya Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya mwaka 2003, kinachoielekeza Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi kutoza faini ya kuanzia shilingi milioni 1 hadi shilingi milioni 5 kwa maeneo ya kazi ambayo hayajasajiliwa ili kulazimisha usajili wa maeneo hayo.

348. Kukosekana kwa mifumo ya ukaguzi wa mara kwa mara au mbinu za uhakiki wa kubaini maeneo ya kazi ambayo hayajasajiliwa kumesababisha usajili usioridhisha wa maeneo ya kazi. Hali hii ilichangiwa pia na changamoto ya uhaba wa wakaguzi wa kukagua maeneo ya kazi. Matokeo yake, maeneo mengi ya kazi yameendelea kuendeshwa bila cheti cha usajili cha Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi na hayakutozwa faini. **Jedwali Na. 21** linaonesha ongezeko la maeneo ya kazi ambayo hayakusajiliwa nchini, pamoja na kiasi cha faini ambazo hazikutozwa.

**Jedwali Na. 21: Faini ambazo Hazikukusanywa kutoka kwenye Maeneo ya Kazi Yasiyo na Vyeti vya Usajili**

| Miaka ya Fedha | Maeneo ya Kazi ambayo hayakusajiliwa (a) | Kiwango cha chini cha faini (Sh.) (b) | Kiasi cha faini ambacho hakikukusanywa (a x b) |
|---|---|---|---|
| 2020/21 | 439 | 1,000,000 | 439,000,000 |
| 2021/22 | 1,691 | 1,000,000 | 1,691,000,000 |
| 2022/23 | 2,662 | 1,000,000 | 2,662,000,000 |
| 2023/24 | 3,747 | 1,000,000 | 3,747,000,000 |
| 2024/25 | 3,039 | 1,000,000 | 3,039,000,000 |
| **Jumla** | **11,578** | | **11,578,000,000** |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Kanzidata ya Wakala wa Usalama Mahali pa Kazi na Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003

349. **Jedwali Na. 21** linaonesha kuwa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi haukutoza faini ya takriban shilingi bilioni 11.578 kwa wamiliki wa maeneo ya kazi walioshindwa kusajili maeneo yao ya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya mwaka 2003.

350. Kutotekelezwa kwa faini kunadhoofisha takwa la kisheria la usajili wa maeneo ya kazi, na hivyo kuyaruhusu maeneo ambayo hayajasajiliwa kuendelea kufanya kazi kinyume na viwango vya Afya na Usalama Mahali pa Kazi. Hali hii imeikosesha fursa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya kukusanya

fedha ambazo zingeweza kutumika kuongeza uwezo wake wa kufanya ukaguzi na kusaidia programu za usalama mahali pa kazi. Jambo hili, kwa upande mwingine linadhoofisha jukumu la msingi la Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi la kuhakikisha mazingira salama ya kazi, na hivyo kutengeneza hatari ya uzingatiaji usioridhisha wa vihatarishi vya usalama na afya mahali pa kazi.

### 6.3.3 Utekelezaji Usioridhisha wa Mipango ya Ukaguzi wa Kisheria Unaofanywa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi


351. Nilibaini kuwa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi hakutekeleza kwa ufanisi ukaguzi wake wa kisheria, kinyume na mahitaji ya Ibara ya 2 ya Mkataba wa Shirika la Kazi Duniani Na. 81, unaotaka ukaguzi wa kazi katika maeneo ya viwanda uhusishe maeneo yote ya kazi ambayo masharti ya kisheria yanayohusu hali ya kazi na ulinzi wa wafanyakazi wanapokuwa kazini yanapaswa kusimamiwa na wakaguzi wa kazi. Upungufu mahususi umefafanuliwa hapa chini:

#### (a) Ukaguzi Usioridhisha wa Maeneo ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Yaliyosajiliwa

352. Nilibaini kuwa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi alikagua wastani wa asilimia 31.3 ya maeneo ya kazi yaliyosajiliwa, jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya Kifungu cha 6 (2) cha Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 21.**

ISO 9001:2015 Certified

**Kielelezo Na. 21: Ukaguzi Usioridhisha wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi katika Maeneo ya Kazi Yaliyosajiliwa**





***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Usajili na Ukaguzi wa Mahali pa Kazi unaotekelezwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi wa Mwaka 2025

353. **Kielelezo Na. 21** kinaonesha kuwa, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi wamefanya ukaguzi katika maeneo ya kazi yaliyosajiliwa kwa chini ya asilimia 60. Kiwango cha juu zaidi cha ukaguzi wa maeneo ya kazi kilirekodiwa katika Mwaka wa Fedha 2023/24, wakati katika Mwaka wa Fedha 2024/25, idadi ya maeneo ya kazi yaliyokaguliwa ilipungua hadi asilimia 23 ikilinganishwa na idadi ya maeneo yaliyosajiliwa. Hata hivyo, nilibaini kuwa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi wanakabiliwa na upungufu wa asilimia 66 wa wakaguzi wanaohitajika (wakaguzi 123 kati ya 365), jambo linaloashiria kuwa nguvu kazi iliyopo inatosheleza kwa asilimia 33.7 tu ya wakaguzi wanaohitajika. Jambo hili lilibainika kuathiri ufanisi wa muda na ukamilifu wa ukaguzi wa maeneo ya kazi.

**(b) Kuchelewa kwa Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi baada ya Usajili**

354. Nilibaini kuwa maeneo ya kazi hayakukaguliwa ndani ya siku 30 baada ya usajili kama inavyotakiwa na Ibara ya 5.3.1 ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi wa Mwaka 2023, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 22.**

**Kielelezo Na. 22: Muhtasari wa Kuchelewa Kufanyika kwa Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi baada ya Usajili**





***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kwenye Kanzidata ya Usajili wa Maeneo ya Kazi, 2025

355. **Kielelezo Na. 22** kinaonesha kuwa idadi kubwa zaidi ya maeneo ya kazi yaliyochelewa kufanyiwa ukaguzi wa kwanza baada ya usajili ilikuwa kati ya siku 31 hadi 365, kukiwa na ucheleweshaji wa hadi siku 335, wakati idadi ndogo zaidi ya maeneo ya kazi yaliyofanyiwa ukaguzi wa kwanza ilikuwa kati ya siku 1461 hadi 1830, kukiwa na ucheleweshaji wa hadi siku 1800. Ucheleweshaji huu unadhoofisha lengo kuu la usajili, ambalo ni kuwezesha uhakiki wa mapema wa uzingatiaji wa viwango vya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

356. Aidha, nilibaini ongezeko la idadi ya maeneo ya kazi yaliyosajiliwa hivi karibuni ambayo hayakukaguliwa baada ya usajili wake, kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 23.**

**Kielelezo Na. 23: Idadi ya Maeneo ya Kazi Ambayo Hayakukaguliwa**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kwenye Kanzidata ya Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi wa Mwaka 2025

357. Kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 23,** idadi ya maeneo ya kazi ambayo hayakukaguliwa iliendelea kuwa juu katika kipindi cha miaka minne iliyopita, ikianzia maeneo 989 hadi 1,552 kati ya Mwaka wa Fedha 2021/22 na Mwaka wa Fedha 2024/25. Ucheleweshaji wa ukaguzi wa maeneo ya kazi umetokana na kutowapo kwa mikakati madhubuti ya Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya kukabiliana na ongezeko la majukumu ya kazi yanayotokana na kuongezeka kwa maeneo mapya yaliyosajiliwa kwenye mipango ya ukaguzi ya kila mwaka. Matokeo yake, maeneo mapya ya kazi ambayo hayajakaguliwa yaliendelea kufanya kazi kwa miezi kadhaa bila usimamizi wowote wa kisheria wa masuala ya Usalama na Afya mahali pa kazi.

### 6.3.4 Afua Zisizotosheleza katika Kusaidia Usimamizi wa Ukaguzi wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi Katika Maeneo ya Kazi

358. Nilibaini kuwa, afua za usimamizi zilizotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano hazikuwa na ufanisi katika kusaidia jukumu la Wizara la usimamizi wa utekelezaji wa usalama na afya mahali pa kazi na katika kufikia malengo ya kitaifa ya usalama na afya, kama inavyooneshwa hapa chini:

**(a) Kukosekana kwa Usimamizi wa Ukaguzi wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi unaopaswa Kufanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano**

359. Nilibaini kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano, haikuandaa wala kuanza kutumia mfumo thabiti wa ufuatiliaji na tathmini kwa

ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi na utendaji wa ukaguzi wa afya na usalama mahali pa kazi nchini. Hali hii ni kinyume na Ibara ya 3 ya Sura ya 5 ya Sera ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2009, inayotaka Ofisi ya Waziri Mkuu kutengeneza mfumo wa ufuatiliaji na tathmini uliodhabitiwa, wa kimfumo, na ulioainishwa vyema baada ya kuandaa afua mkakati za utekelezaji wa Sera. Uchambuzi zaidi wa taarifa kutoka kwenye Ripoti za Ufuatiliaji na Tathmini za Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Ripoti za Utendaji za Mwaka ulionesha kuwa, Ripoti hizo hazikugusia usimamizi wa ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi.

360. Sababu kuu za hali hii ni kukosekana kwa utaratibu maalum na wa kimfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa utekelezaji wa Sera ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, ajira na Mahusiano, na ukosefu wa uwazi kuhusu jukumu la usimamizi la Waziri Mkuu kuhusiana na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi katika Mpango Mkakati wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Hali hii inaizuia Ofisi ya Waziri Mkuu katika mamlaka yake ya kufuatilia utekelezaji wa Sera na Ukaguzi kwa ufanisi. Matokeo yake, kwa sasa Ofisi ya Waziri Mkuu inategemea uwajibikaji wa ndani wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi kwa Bodi yake ya Wakurugenzi, bila kuwa na usimamizi wa ziada wa nje.

## 6.4 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi

ISO 9001:2015 Certified


361. Nilibaini upungufu katika utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi. Masuala makuu niliyobaini ni pamoja na kupungua kwa asilimia ya madai yaliyolipwa fidia, ucheleweshaji wa uchakataji wa madai, kutosajiliwa kwa waajiri wote waliobainishwa, kutowasilishwa kwa tozo kutoka kwa waajiri waliosajiliwa wasiozingatia sheria, na kukosekana kwa ufanisi katika kutangaza huduma za fidia, kama inavyofafanuliwa hapa chini:

### 6.4.1 Kupungua kwa Kiwango cha Madai Yaliyolipwa Fidia

362. Nilibaini kuwa, kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ulilipa fidia kwa asilimia 67 ya madai yaliyosajiliwa ya wafanyakazi waliopata majeraha, au kuugua magonjwa yatokanayo na kazi, au kufariki dunia wakati wa utekelezaji wa majukumu yao Tanzania Bara, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 24.** Hali hii ni kinyume na matakwa ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura Na. 263, inayoelekeza kuwa lengo la kuanzishwa kwa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ni kutoa fidia kwa wafanyakazi kutokana na ulemavu au kifo kilichosababishwa na au kutokana na

majeraha waliyopata au magonjwa waliyoambukizwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

**Kielelezo Na. 24: Kiwango cha Madai Yaliyolipwa Fidia Ikilinganishwa na Madai Yaliyosajiliwa Kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Kumbukumbu za Usajili, Uchakatajiwa Madai na Malipo ya Madai kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25, 2025

363. **Kielelezo Na. 24**, kinaonesha kuwa kiwango cha malipo ya madai yaliyosajiliwa kilishuka kutoka asilimia 81 katika Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi asilimia 53 Mwaka wa Fedha 2024/25. Kushuka kwa asilimia ya madai yaliyolipwa ikilinganishwa na madai yaliyosajiliwa imesababishwa na mambo kadhaa, kama inavyofafanuliwa hapa chini:

ISO 9001:2015 Certified

**(a) Ongezeko la Asilimia 33 la Idadi ya Madai Yaliyosajiliwa**

364. Nilibaini kuwa idadi ya madai yaliyosajiliwa iliongezeka kutoka 3,693 Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 4,920 kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 33. Ongezeko hili la madai lilisababisha uhitaji mkubwa wa uchunguzi, jambo ambalo lilisababisha kuchelewa kwa upitishaji wa malipo ya madai hayo.

**(b) Kukataliwa kwa Madai Yaliyosajiliwa na Ongezeko la Madai Yasiyoshughulikiwa**

365. Nilikuta kuwa, mfuko ulikataa madai yaliyosajiliwa kutoka asilimia 17 kwa Mwaka fedha 2021/22 hadi asilimia 10 Mwaka wa Fedha 2024/25 kwa sababu mbalimbali, ikiwemo yale yaliyowasilishwa bila ushahidi wa kutosha na yale yaliyowasilishwa nje ya muda wa kisheria wa miezi 12. Mapitio ya takwimu za madai yaliyokataliwa kwa miaka ya fedha 2021/22 hadi 2024/25 yanaonesha kuwa, asilimia 1.24 ya madai yaliyokataliwa yalitokana na kuwasilishwa nje ya muda wa kisheria wa miezi 12. Kupungua kwa madai yaliyolipwa pia

kulichochewa na ongezeko la madai yasiyoshughulikiwa kutoka asilimia moja katika mwaka wa fedha 2021/22 hadi asilimia 25 katika mwaka wa fedha 2024/25.

**(c) Utendaji wa Shughuli za Usimamizi na Tathmini ya Madai katika Ofisi Ndogo ya Makao Makuu na Ofisi ya Kanda ya Dododma Pekee**

366. Nilibaini kuwa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi unatekeleza shughuli za tathmini ya madai ndani ya Kitengo cha Tathmini ya Madai katika Ofisi Ndogo ya Makao Makuu Dar es Salaam na Ofisi ya Kanda ya Dodoma pekee, licha ya kuanzishwa kwa Ofisi tisa za Mikoa/Kanda zinazoongozwa na Wakuu wa ofisi hizo. Aidha, nilibaini kuwa, kuwapo kwa utendaji wa ofisi hizi haumo katika Muundo wa Majukumu na Taasisi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi uliopitishwa na Mheshimiwa Rais tarehe 5 Novemba 2018 na kuwasilishwa kwa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi tarehe 15 Novemba 2025 na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.


367. Utekelezaji usioridhisha wa usimamizi na tathmini ya madai katika Ofisi za Mikoa/Kanda za Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ulitokana zaidi na kukosekana kwa chombo kinachofafanua kisheria kuanzishwa kwa ofisi hizo, ikiwemo majukumu, mfumo wa utoaji taarifa, mipango kazi, na bajeti zake. Hali hii ilisababisha ucheleweshaji wa kuidhinisha na kulipa madai.

### 6.4.2 Kuchelewa kwa Ushughulikiwaji wa Madai

ISO 9001:2015 Certified

368. Nilibaini ucheleweshaji katika kushughulikia na kuidhinisha malipo ya madai yaliyowasilishwa na wafanyakazi waliopata majeraha au magonjwa yatokanayo na kazi kuanzia Mwaka wa fedha 2021/22-2024/25. Hii ilikuwa kinyume na aya ya 10 ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi wa mwaka 2020, ulioweka muda wa malipo ya ulemavu wa muda, ulemavu wa kudumu, na fidia ya mkupuo kwa wafanyakazi waliojeruhiwa kuwa ndani ya siku 30 za kazi baada ya kupokea maombi ya madai yanayostahili yakiwa na nyaraka kamili. **Kielelezo Na. 25** kinaonesha wastani wa idadi ya siku ambazo Wakala wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi hutumia kushughulikia madai tangu tarehe ya kusajiliwa kwake.

**Kielelezo Na. 25: Wastani wa Siku Zinazotumiwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi Kushughulikia Madai Kamili na Halali**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Madai Yaliyolipwa kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi 2024/2025, 2025

369. **Kielelezo Na. 25** kinaonesha kuwa wastani wa muda uliotumika kushughulikia madai kamili na halali ulikuwa siku 54 katika Mwaka wa Fedha 2021/22, uliongezeka hadi siku 126 katika Mwaka wa Fedha 2022/23, na kupungua hadi siku 62 katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, ambazo zote zilikuwa juu ya kiwango cha siku 30 za kazi. Hata hivyo, kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, siku 28 zilizotumika zilikidhi viwango vilivyowekwa katika Mkataba wa Huduma kwa Mteja.

370. Kuchelewa kwa ushughulikiwaji wa madai katika hatua mbalimbali za uchakataji kumeathiri ufanisi wa jumla wa mfumo wa fidia. Kipindi kirefu kati ya usajili wa dai na malipo kumepunguza uwezo wa Mfuko kutoa msaada wa kifedha kwa wakati kwa wafanyakazi walioumia kazini, na hivyo kudhoofisha lengo la Mfuko, ambalo ni kutoa huduma za fidia kwa wafanyakazi waliokidhi vigezo.

371. Aidha, nilibaini kuwa, ucheleweshaji huo katika ushughulikiwaji wa madai ulitokana na mambo yafuatayo:

**(a) Zaidi ya Asilimia 40 ya Madai Yalihitaji Uchunguzi kwa Kutembelea Eneo la Kazi**


372. Nilibaini kuwa, takriban asilimia 40 ya madai yote yaliyoshughulikiwa yalihitaji uchunguzi wa kutembelea eneo la Kazi badala ya uchunguzi wa mezani. Kwa mujibu wa maofisa, hatua hii kimsingi huchukua muda mrefu, kwani inahitaji kutembelea maeneo ya kazi na kufanya mahojiano ili kuhakiki madai na kuzuia udanganyifu.

### (b) Kuwapo kwa Muda Mrefu kuanzia Usajili wa Madai hadi Kushughulikiwa Kwake

373. Kuchelewa kwa ushughulikiwaji wa madai pia kulitokana na wastani wa muda kuanzia usajili wa dai hadi nyaraka zote zinapowasilishwa na mwajiri, mfanyakazi, au mtu mwingine yeyote anayehusika na madai hayo. Nyaraka zote muhimu zinapowasilishwa kikamilifu, madai hayo huchukuliwa kuwa halali kwa ajili ya kushughulikiwa na Mfuko na huitwa "dai lililo tayari kwa mafao."

374. Nilibaini kuwa kwa madai yaliyolipwa katika miaka ya fedha 2021/22 hadi 2024/25, kwa wastani, ilichukua siku 180 kuanzia usajili hadi wakati dai lilipokuwa na nyaraka kamili, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 26.**

**Kielelezo Na. 26: Muda Unaotumika kuanzia Usajili hadi Hatua ya Dai Lililo Tayari kwa Mafao**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Madai Yaliyolipwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kwa Miaka ya Fedha 2021/22-2024/25, 2025

375. **Kielelezo Na. 26** kinaonesha kuwa kwa miaka ya fedha 2021/22, ilichukua siku 166, siku 225 kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, siku 196 kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, na siku 133 kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 kwa mhusika kuwasilisha kikamilifu nyaraka zinazohitajika ili madai yawe tayari kufanyiwa kazi. Ucheleweshaji huu wa uwasilishaji wa nyaraka zinazohitajika ulitokana na usimamizi usiotosheleza wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi katika mahitaji ya uwasilishaji wa nyaraka na uelewa mdogo wa taratibu za madai miongoni mwa waajiri na wafanyakazi.

### 6.4.3 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi Kutokusajili Waajiri Wote Waliobainishwa

376. Nilibaini kuwa kwa miaka ya fedha 2021/22 hadi 2024/25, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi iliwabaini waajiri wasiosajiliwa 12,982, lakini ilifanikiwa kusajili waajiri 4,676 pekee, ikiwa ni sawa na asilimia 36 ya waajiri waliobainika kutosajiliwa na Mfuko. Hali hii ilikuwa kinyume na matakwa ya Kanuni ya 9(1) ya Kanuni za Fidia kwa Wafanyakazi za mwaka 2016, inayomtaka kila mwajiri, ndani ya siku 30 za kalenda tangu tarehe ya kumuajiri mfanyakazi wa kwanza, kuwasilisha maelezo yake ya usajili kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi.

377. Kiwango kidogo cha usajili wa waajiri ikilinganishwa na wale walioibuliwa kilitokana na usimamizi na ufuatiliaji usio na ufanisi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi katika kuhakikisha kuwa waajiri walioibuliwa wanasajiliwa rasmi na maofisa wanaohusika katika ngazi za Makao Makuu na Ofisi za Kanda. Pia, kukosekana kwa malengo halisi ya usajili yanayozingatia takwimu za uibuaji kumechangia kutotosheleza kwa idadi ya usajili wa waajiri.

378. Matokeo yake, hali hii inasababisha idadi kubwa ya waajiri walioendelea kuendesha shughuli zao nje ya mfumo wa usajili wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, jambo ambalo liliathiri moja kwa moja uwezo wa mfuko wa kukusanya michango na kutoa mafao ya fidia kwa wafanyakazi katika sekta mbalimbali. Aidha, usajili mdogo wa waajiri unazuia ukuaji wa idadi ya waajiri wanaochangia na wanufaika.

### 6.4.4 Tozo za Riba Kutokuwasilishwa Kutoka kwa Waajiri Waliosajiliwa Wasiozingatia Sheria

379. Nilibaini kuwa, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi haukuweza kukusanya tozo za riba kutoka kwa waajiri wasiozingatia sheria, jambo ambalo ni kinyume na Kanuni ya 13(7) ya Kanuni za Mfuko za Mwaka 2016 kama zilivyofanyiwa marekebisho na Kanuni za Fidia kwa Wafanyakazi za Mwaka 2021 (Tangazo la Serikali Na. 668 lililochapishwa tarehe 10/09/2021), inayomtaka mwajiri kulipa kiasi kisichozidi asilimia mbili ya kiasi ambacho hakijalipwa kama riba kutoka tarehe ambayo malipo hayo yalipaswa kufanyika, na kiasi hicho cha riba kitadaiwa kama deni kwa Mfuko kutoka kwa mwajiri. Wakati wa ukaguzi, ilibainika kuwa, waajiri ambao hawakuchangia kwenye Mfuko walikuwa na madeni ya riba ambayo hayakukusanywa, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 22.**

**Jedwali Na. 22: Tozo za Riba Ambazo Hazijawasilishwa kutoka kwa Waajiri Wasiozingatia Sheria**

| Miaka ya Fedha | Sekta ya Umma | | Sekta Binafsi | | Jumla ya Riba Ambayo Haikukusanywa |
|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya Wafanyakazi | Riba Ambayo Haikukusanywa (Sh. "000") | Idadi ya Wafanyakazi | Riba Ambayo Haikukusanywa(Sh. "000") | (Sh. "000") |
| **2021/22** | 60 | 102,793 | 6,651 | 779,376 | 882,169 |
| **2022/23** | 93 | 132,235 | 9,167 | 809,361 | 941,596 |
| **2023/24** | 181 | 147,012 | 21,622 | 885,571 | 1,032,583 |
| **2024/25** | 230 | 72,747 | 25,205 | 347,243 | 419,990 |
| **Jumla** | | **454,786** | | **2,821,552** | **3,276,338** |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa wakaguzi kuhusu tozo za riba ambazo hazikuwasilishwa kwenye Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kutoka Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25, 2025"

380. **Kielelezo Na. 22** kinaonesha kuwa, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi haukuweza kukusanya riba kiasi cha shilingi milioni 454.79 kutoka kwa waajiri wa sekta ya umma na Shilingi bilioni 2.82 kutoka kwa waajiri wa sekta binafsi, na kufanya jumla ya riba ambayo haikukusanywa kuwa shilingi bilioni 3.276 kwa miaka ya fedha minne iliyokaguliwa kuanzia 2021/22 hadi 2024/25. Ilibainika kuwa tozo za riba ambazo hazijawasilishwa zilifikia kilele cha shilingi milioni 885.571 katika sekta binafsi kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 kutokana na kuongezeka kwa idadi ya waajiri wasiozingatia sheria, jambo lililosababishwa na usimamizi usiojitosheleza wa notisi za madai kwa waajiri waliosajiliwa.

381. Usimamizi usiotosheleza wa malipo ya riba ulisababisha ucheleweshaji au kushindwa kwa waajiri kuwasilisha michango yao kwenye Mfuko. Aidha, nilibaini kuwa, kufikia tarehe 30 Juni, 2024/25, jumla ya shilingi bilioni 3.99 haikukusanywa na mfuko kama michango kutoka kwa waajiri wa sekta ya umma na sekta binafsi.


### 6.4.5 Utoaji wa Elimu ya Uelewa Usio na Ufanisi kuhusu Huduma za Fidia Zinazotolewa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi

382. Nilibaini kuwa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ulifanya kwa nadra matembezi kwa waajiri au mialiko kwa ajili ya shughuli za kuongeza uelewa kuhusu huduma za fidia ziotolewazo na Mfuko. Utaratibu huu ni kinyume na Kifungu cha 13(g) cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263, na Ibara

ya 3.5(i) ya Muundo wa Majukumu na Taasisi wa Mfuko wa Mwaka 2018, inayotaka Mfuko kuhamasisha uelewa wa umma kuhusu haki na wajibu wa wafanyakazi, wategemezi, na waajiri, na kutekeleza programu za elimu kwa umma kupitia Kitengo chake cha Uhusiano wa Umma.

383. Aidha, nilibaini kuwa licha ya kuwapo kwa mipango ya uhamasishaji, asilimia 75 ya wafanyakazi waliohojiwa katika mikoa sita iliyotembelewa walielezea uhitaji wa kampeni za uelewa kuhusu huduma za Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi wenzao, jambo linaloashiria kasoro katika ufikiaji na mawasiliano kuhusu huduma za mfuko, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 27.**

**Kielelezo Na. 27: Maeneo Yanayopendekezwa kwa ajili ya Maboresho ya Huduma za Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Maswali Yaliyoulizwa kwa Wafanyakazi kwa Waajiri Waliotembelewa katika Mikoa iliyochaguliwa, 2025


ISO 9001:2015 Certified

384. **Kielelezo Na. 27** kinaonesha kuwa asilimia 75 ya wafanyakazi kutoka mikoa sita iliyotembelewa waliomba kampeni za uhamasishaji kwa waajiri na wafanyakazi kuhusu huduma za Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Asilimia 25 iliyobaki walipendekeza maboresho katika huduma zingine za Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, kama vile kuhakikisha fidia inatolewa kwa wakati na inayotosheleza kwa wafanyakazi walioathiriwa na majeraha na magonjwa yatokanayo na kazi. Hali hii inaashiria pengo la uelewa kuhusu masuala ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kama ilivyofafanuliwa hapa chini:

### (a) Uelewa Mdogo wa Taratibu za Madai

385. Nilibaini kuwa kwa wastani, asilimia 60 ya wafanyakazi walikuwa hawafahamu taratibu ambazo mtu anapaswa kufuata anapodai mafao ya fidia kutoka Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Kiwango cha wafanyakazi waliohojiwa katika kila mkoa uliotembelewa imeoneshwa katika **Kielelezo Na. 28.**

**Kielelezo Na. 28: Uelewa wa Wafanyakazi kuhusu Taratibu za Madai**




***Chanzo:*** Maswali Yaliyosambazwa kwa Wafanyakazi wiliopo kwa Waajiri katika Mikoa ya Iliyotembelewa, 2025

386. Kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 28**, uelewa wa taratibu za kudai mafao ya fidia kutoka Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ulitofautiana katika mikoa mbalimbali. Asilimia kubwa zaidi ya wafanyakazi wasiofahamu taratibu hizo ilirekodiwa katika Mkoa wa Dodoma (asilimia 75), ikifuatiwa na Mbeya (asilimia 70) na Pwani (asilimia 54). Viwango vya wastani vya uelewa vilionekana katika mikoa ya Arusha na Tabora, ambapo asilimia 50 na 52 ya waliohojiwa, walikuwa hawafahamu kuhusu taratibu hizo. Mkoa wa Mwanza ulirekodi asilimia kubwa (asilimia 55) ya wahojiwa waliokuwa wanafahamu taratibu za madai kuliko wale wasiofahamu, kukiwa na utofauti wa asilimia tano.

387. Ukosefu wa mipango madhubuti ya uhamasishaji, malengo yaliyo wazi, na viashiria vya utendaji vilidhoofisha juhudi za Mfuko katika ngazi za makao makuu na kanda katika utoaji elimu za uelewa. Hali hii imesababisha uelewa mdogo wa huduma za mfuko miongoni mwa wafanyakazi na waajiri.

### 6.5 Athari za Changamoto Zilizobainika katika kuyafikia Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

388. Serikali imetekeleza mikakati mbalimbali ili kuimarisha usalama mahali pa kazi, ukaguzi wa afya, na utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi waliopata majeraha, magonjwa, au vifo vitokanavyo na kazi. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini upungufu katika utekelezaji, jambo linalokwaza ufikiaji wa

malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu, kama ilivyoainishwa hapa chini:

389. Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi ulionesha ongezeko la kiwango vya vifo kazini, usajili usioridhisha wa maeneo ya kazi, kutotozwa kwa faini kwa maeneo ya kazi yanayoendeshwa bila Cheti cha Usajili cha Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi, na kukosekana kwa usimamizi wa ukaguzi wa Usalama na Afya mahali pa Kazi. Hali hii inakinzana na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, inayotaka kuimarishwa kwa usalama wa umma, sheria, na utaratibu. Aidha, matokeo ya ukaguzi wangu yalionesha changamoto katika kufikia Lengo la 8 la Maendeleo Endelevu, Shabaha ya 8.8, inayotaka kulindwa kwa haki za kazi na kuhamasisha mazingira salama ya kazi kwa wafanyakazi wote.

390. Vilevile, Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Fidia ulibaini upungufu katika ulipaji wa madai ya fidia, ucheleweshaji wa ushughulikiwaji wa madai, usajili usioridhisha wa waajiri wanaostahili, changamoto katika utekelezaji wa tozo za riba kwa waajiri waliosajiliwa wasiozingatia sheria, na utoaji wa uelewa usio na ufanisi kwa waajiri na wafanyakazi kuhusu huduma za fidia. Upungufu huu unazuia juhudi za nchi katika kufikia, hususani Shabaha ya 8.8, inayotaka kulindwa kwa haki za kazi na kuhakikisha maeneo salama ya kazi kwa wafanyakazi wote, wakiwemo makundi yaliyo katika mazingira hatarishi na wahamiaji, pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu, hususani Shabaha Na. 9.4 na 9.5, zinazotaka kuimarisha maendeleo endelevu na matumizi bora ya rasilimali.

## SURA YA SABA

## UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI

### 7.1 Utangulizi

391. Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi katika ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi ya Udhibiti wa Huduma za Maji. Vilevile, inaelezea eneo la ukaguzi, taasisi za serikali zilizohusishwa katika ukaguzi, na uhusiano wa ukaguzi na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na matokeo yake.

### 7.1.1 Usuli

392. Sekta ya maji na usafi wa mazingira, ni msingi kwa afya ya jamii, utuzaji wa mazingira na maendeleo ya uchumini. Licha ya kuwa na umuhimu mkubwa katika maisha ya watu na maendeleo ya nchi, huduma za maji na usafi wa mazingira bado hazijatolewa vya kutosha. Hadi mwaka 2023, ni asilimia 72 tu ya watu waliopata huduma za msingi za maji ya kunywa, wakati upatikanaji wa huduma za maji safi na salama ulifikia asilimia 45 katika maeneo ya mijini na asilimia 24 katika maeneo ya vijijini[6]. Udhibiti wa huduma za maji ni muhimu ili kuhakikisha ufikiaji wa huduma za maji safi na salama, bei nafuu za huduma na uendelevu wa huduma. Kutokana na huduma ya usambazaji wa maji kutolewa na taasisi moja na kutoa na ushindani, udhibiti wa huduma hii hulinda watumiaji, kukuza ufanisi, na kuhakikisha viwango vya kiufundi na vya ubora vinafikiwa[7] .

393. Nchini Tanzania, huduma za usambazaji wa maji na usafi wa mazingira zinasimamiwa na Sheria ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira, Sura ya 272 na kusimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414. Moja ya majukumu ya Mamlaka hii ni kutoa leseni kwa watoa huduma za maji, kuidhinisha tozo za maji, kufuatilia utendaji wa watoa huduma, na kuhakikisha watoa huduma za maji zenye viwango vinavyotakiwa. Sheria ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira, Sura ya 272 inakamilisha hili kwa kupeleka jukumu la utoaji wa huduma kwa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira. Kufikia mwaka 2024, kulikuwa na jumla ya Mamlaka za Maji na

[6] National Bureau of Statistics (NBS) & UNICEF/WHO Joint Monitoring Programme (JMP) for Water Supply, Sanitation and Hygiene (2023). Progress on household drinking water, sanitation and hygiene 2000–2022: Special focus on gender.
[7] Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo, 2015

Usafi wa Mazingira 82 zilizosajiliwa na kuainishwa kama mamlaka za Mikoa, Wilaya, au Miradi ya Kitaifa.

### 7.1.2 Uhusiano Kati ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Malengo ya Maendeleo Endelevu Pamoja na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano

394. Sehemu hii inatoa ufafanuzi wa namna udhibiti wa huduma za maji unavyoendana na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano kama ifuatavyo:

#### (a) Udhibiti wa Huduma za Maji Unavyoendana na Malengo ya Maendeleo Endelevu

395. Udhibiti wa Huduma za Maji umeunganishwa na Lengo la 6 la Malengo ya Maendeleo Endelevu, ambayo inakusudia kuhakikisha upatikanaji na usimamizi endelevu wa huduma za maji na usafi wa mazingira kwa wote ifikapo 2030. Shabaha namba 6.1 na 6.2 ya Lengo la 6 zinalenga kuhakikisha upatikanaji wa huduma za maji ya kunywa na huduma za usafi wa Mazingira zilizokidhi viwango kwa bei nafuu. Vilevile shabaha namba 6.3 na 6.4 zinalenga kuboresha ubora wa maji kwa kupunguza uchafuzi wa mazingira, kuondoa utupaji wa taka hovyo, na kupunguza utoaji wa kemikali hatarishi, na kupunguza nusu ya sehemu ya maji machafu ambayo hayajatibiwa. Pia, inachangia lengo 3 la mpango wa maendeleo endelevu hasa shabaha namba 3.9, ambalo linalenga kupunguza magonjwa yanayosababishwa na utumiaji wa maji yasiyo salama.

396. Malengo haya yanaangazia umuhimu wa usimamizi mzuri wa usambazaji wa Maji ili kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa maji yenye ubora. Udhibiti wa huduma za maji huhakikisha upatikanaji wa kutosha wa huduma za maji na miundombinu ya kutibu majitaka.

#### (b) Uhusiano Kati ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano

397. Udhibiti wa huduma za maji unaunga mkono Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ambao unalenga kuboresha upatikanaji wa huduma za ubora na endelevu za maji na usafi wa mazingira. Kipaumbele hiki kimejikita katika kupunguza maji yasiyo ya mapato au maji yanayopotea na kupanua huduma ya huduma za maji. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kama chombo cha udhibiti husaidia kufikia malengo haya kwa kuweka na kufuatilia viwango vya utendaji wa Mamlaka za Usambazaji Maji na Usafi wa

Mazingira; na kuwalinda watumiaji wa huduma za maji kupitia upitishaji wa bei/tozo za maji na kuboresha uhakika wa upatikanaji wa huduma.

### 7.1.3 Mikakati na Juhudi za Serikali Katika Udhibiti wa Huduma za Maji

398. Mikakati ya serikali inayohusiana na Udhibiti wa huduma za maji ni pamoja na Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji wa 2021/22 – 2025/26. Pia, juhudi zilizofanywa na serikali zimehusisha uundaji wa kanuni na miongozo mbalimbali zinazosimamia udhibiti wa huduma za maji. Muhtasari wa mikakati ya serikali na juhudi za Udhibiti wa Maji vimeoneshwa katika **Kielelezo Na. 29**.

**Kielelezo Na. 29: Muhtasari wa Mikakati na Juhudi za Serikali Kuhusiana na Udhibiti wa Huduma za Maji**

**Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Umeme na Maji 2021/22 - 2025/26**

- Kuhakikisha ubora, upatikanaji, na uwezo wa huduma za maji na usafi wa mazingira zilizodhibitiwa
- Kukuza uwezo wa kibiashara na Uwezo wa upangaji wa uwekezaji wa watoa huduma
- Kuimarisha ulinzi wa watumiaji wa huduma na mifumo ya ushirikishaji watumiaji wa huduma
- kutekeleza viwango vya mazingira na kiufundi
- Kuimarisha uangalizi wa udhibiti na kuangalia hali ya ufikiaji wa viwango

**Jitihada za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Umeme na Maji ili Kuboresha Udhibiti**

Ili Kuboresha Udhibiti wa Huduma za Maji EWURA ina Kanuni na Miongozo ifuatayo

- Mwongozo wa Mamlaka za Maji kuanda Mpango kazi, 2022;
- Mwongozo wa Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji na Majitaka, 2020
- Kanuni ya uombaji na Uaandaji wa tozo za Maji, 2020
- Kanuni ya Huduma za Usambazaji wa Maji and Usafi wa Mazingira (Utoaji wa Leseni na Ubora wa Huduma), 2020
- Mwongozo wa uendeshaji wa vituo kuteka maji, 2022
- Mwongozo wa uandaaji wa Mpango wa Kupunguza maji yanayopotea/ maji yasiyo na mapato, 2021
- Inspection Manual For Water Utilities, 2020
- Mwongozo wa Ukaguzi wa Mamlaka za Maji- 2020
- Mwongozo wa kupima Utendaji wa Mamlaka za Maji, 2022

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kwenye Mpango Mkakati wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji wa 2021/22-2025/26 na Kanuni na Miongozo Iliyoandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji, 2025

## 7.2 Malengo ya Ukaguzi na Mawanda

### 7.2.1 Malengo ya Ukaguzi

399. Lengo kuu la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini kama udhibiti wa Mamlaka ya Uthibiti wa Nishati na Maji kwenye huduma za maji kupitia utoaji leseni kwa watoa huduma za maji, uaandaaji wa tozo za maji, na ufuatiliaji wa

ubora wa maji na majitaka umechangia kuimarisha udhibiti wa huduma za maji nchini Tanzania, ili kuboresha upatikanaji, ubora, na uendelevu wa huduma za maji na usafi wa mazingira.

400. Mathalani, ukaguzi ulilenga kutathmini kama:

(a) Mchakato wa utoaji leseni wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji umewezesha watoa huduma za maji kutoa huduma bora na za za Maji;

(b) Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji imeweza kupanga, kufuatilia na kuhakikisha bei za maji zilizopitishwa zinatumika kwa utoshelevu na watoa huduma za maji ili kuimarisha upatikanaji wa huduma na uwezo wa kumudu gharama za maji na usafi wa mazingira; na

(c) Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji imefuatilia kwa ufanisi ubora wa maji na huduma za majitaka ili kuthibitisha ufikiaji viwango vinavyohitajika

NATIONAL AUDIT OFFICE

### 7.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

401. Taasisi za iliyokaguliwa ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji. Ukaguzi uliangalia mchakato wa utoaji wa leseni; uandaaji, ufuatiliaji, na utekelezaji wa tozo za maji; na utoshelevu na ufanisi wa ufuatiliaji wa ubora wa maji na majitaka. Ukaguzi huu ulihusisha miaka mitano ya fedha, kuazia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25.

ISO 9001:2015 Certified

## 7.3 Matokeo ya Ukaguzi

402. Sehemu hii inawasilisha matokeo makuu ya ukaguzi wa Udhibiti wa Huduma za Maji. Maelezo ya matokeo ya ukaguzi yametolewa hapa chini;

### 7.3.1 Uangalizi Usiyojitosheleza wa Mamlaka za Huduma za Maji katika Utoaji wa Huduma

403. Ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji haijahakikisha vya kutosha kuwa watoa huduma wanatoa huduma toshelevu za maji na usafi wa mazingira kote nchini. Upungufu huu ulisababisha ubora usiojitosheleza wa maji na pamoja na upatikanaji wake, upotevu wa maji kuwa mkubwa, kutofikiwa kwa upatikanaji wa huduma za majitaka na uimara endelevu wa fedha kwa ajili ya huduma za maji na usafi wa mazingira. Ukaguzi

huu ulichambua Ripoti za Utendaji wa Huduma za Maji kwa kipindi cha miaka minne ya fedha, kutoka 2020/21 hadi 2023/24 na kubainisha upungufu wa utendaji kama inavyoelezwa hapa chini.


**(a) Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji Kutokuimarisha Upatikanaji wa Kutosha wa Huduma za Maji na Usafi kwa Jamii katika Ubhibiti wake**

404. Mapitio ya Taarifa za Utendaji wa Watoa Huduma za Maji kwa Miaka ya Fedha kuazia 2020/21 hadi 2023/24, yalibaini kutofikiwa kwa lengo la upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira katika maeneo ya huduma ya watoa huduma za maji kama ifuatavyo;

**(i) Ongezeko Dogo la Upanuaji wa Upatikanaji wa Maji Katika Maeneo ya Huduma ya Mamlaka za Maji**

405. Mapitio ya ripoti za utendaji wa Huduma kwa miaka minne ya fedha, yalibaini kutofikiwa kwa lengo lililowekwa la upatikanaji wa maji katika eneo la mamlaka za maji au watoa huduma za maji. Kwa ujumla, ripoti inaonesha kuwa, mamlaka za maji hazijaweza kupanua huduma katika maeneo yao na kuweza kufikia asilimia 84 ya watu katika eneo la huduma kama inavyotakiwa katika mwongozo wa upimaji wa utendaji kazi wa Mamlaka za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya 2022. **Kielelezo Na. 30** kinaonesha idadi ya mamlaka za maji na asilimia ya huduma za maji ambazo zilipata zaidi ya au sawa na asilimia 84 katika kuwafikia watu katika maeneo yao ya huduma.

**Kielelezo Na. 30: Idadi ya Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Zilizofanikisha Utoaji Huduma za Maji kwa Asilimia 84 katika Maeneo Yao ya Huduma**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti za Utendaji wa Mamlaka za Maji kutoka 2020/2021 hadi 2024/2025, 2025

406. **Kielelezo Na. 30** kinaonesha kuwa, katika miaka minne ya fedha, asilimia kubwa ya Mamlaka za Maji zilizofikisha asilimia 84 ya watu wanaopata maji katika maeneo yao ya huduma zilianzia asilimia 8 hadi asilimia 24. Utendaji wa juu zaidi ulikuwa Mwaka wa Fedha 2020/21, na wa chini kabisa Mwaka wa Fedha 2022/23. Takwimu zinaonesha kushuka kutoka Mwaka wa Fedha wa 2020/21 hadi 2021/22, kutoka asilimia 24 hadi 11, ambayo ilikuwa kabla ya kutolewa kwa mwongozo wa 2022, na ongezeka kutoka Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi 2023/24, kutoka asilimia 8 hadi 9. Licha ya kuonesha mwenendo kuongezeka wa kuwafkia wananchi, bado kuna upungufu katika kufikisha huduma ya maji.

407. Kutopatikana kwa huduma za maji kwa asilimia 84 katika eneo la mamlaka za maji kulisababishwa na kuunganishwa kwa mamlaka na kupanua eneo la huduma la mamlaka za maji. Mapitio ya taarifa za Mamlaka za maji nilibaini kuwa jumla ya mamlaka 43 za maji ziliunganishwa na kupanua maeneo yao ya huduma katika Mwaka wa Fedha wa 2019/20. Hii imesababisha upatikanaji mdogo wa huduma za maji safi na salama kwa jamii na kuongezeka kwa hatari za kiafya. Upungufu huu katika utoaji wa huduma za maji umechangia ucheleweshaji wa kufikia lengo la 6 Mpango wa Maendeleo

endelevu hasa shabaha Na. 6.1, 6.2 na 6.3 ambazo zinalenga upatikanaji wa maji safi.

### (ii) Maendeleo ya Taratibu Katika Kupanua Utoaji wa Huduma za Mifumo ya Matibabu ya Majitaka

408. Mapitio ya ripoti za utendaji wa mamlaka za maji kutoka Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2023/24, yalibaini kuwa baadhi ya mamlaka za maji hazikuwa na mitandao ya majitaka na miundombinu ya kutibu majitaka ndani ya maeneo yao ya huduma. Mitandao ya majitaka na miundombinu ya kutibu majitaka ni muhimu katika kuhakikisha kuwa majitaka yanayotolewa kwenye mazingira yanakidhi viwango vinavyotakiwa. Kutokuwapo kwa miundombinu ya majitaka ni kinyume Kanuni za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (Leseni na Ubora wa Huduma), 2020 ambazo zinahitaji maombi ya leseni yaambatane na ramani ya mpangilio wa mfumo wa maji na majitaka. **Jedwali Na. 23** linaonesha hali ya upatikanaji wa mfumo wa majitaka katika mamlaka za maji.

**Jedwali Na. 23: Upatikanaji wa Miundombinu ya Matibabu ya Majitaka katika Mamlaka za Huduma za Maji**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Mamlaka za Maji safi na usafi wa mazingira zinazopaswa kuwa na Miundombinu ya Majitaka[8] | Idadi ya Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Zenye Miundombinu ya Kutibu Majitaka | % Mamlaka za Maji Zenye Miundombinu ya Kutibu Majitaka |
|---|---|---|---|
| 2020/21 | 84 | 19 | 23 |
| 2021/22 | 83 | 20 | 24 |
| 2022/23 | 78 | 21 | 27 |
| 2023/24 | 76 | 23 | 30 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Ubora wa Majitaka kwenye Ripoti za Utendaji wa Mamlaka za Maji kutoka Mwaka 2020/21 hadi 2023/24, 2025

409. **Jedwali Na. 23** linaonesha kuwa, kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2020/21 hadi 2023/24, kulikuwa na jumla ya mamlaka 76 za maji zinazopaswa kuwa na miundombinu ya majitaka, lakini ni mamlaka 23 tu sawa na asilimia 30 zilikuwa na mifumo ya majitaka, ikiwa pamoja na mitandao ya majitaka na mifumo ya kutibu majitaka. Pia, jedwali linaonesha kuwa kutoka Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2023/24, idadi ya mamlaka za maji zilizo na mifumo ya majitaka ziliongezeka kutoka 19 Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 23 Mwaka wa Fedha

[8] Hii haihusushi Mamlaka za maji za kitafa ambazo huzalisha maji tu na kuziuzia mamalaka zingine[9] Magonjwa yanayosababishwa na unywaji wa maji yenye aseniki. Imesomwa tarehe 04 Oktoba 2025 kwenye Arsenic

2023/24. Hii inaonesha ongezeko la asilimia 7 mamlaka za maji kwa miaka minne ya fedha. Kiwango kidogo cha ufikiaji wa miundombinu ya majitaka kilisababishwa na kutowa na kipaumbele katika ujenzi wa miundombinu ya majitaka ikilinganishwa na miundombinu ya usambazaji wa maji.

410. Kwa sababu ya kukosekana kwa mtandao wa majitaka, jamii/wananchi wanakosa maeneo ya kutupa majitaka yanayozalishwa kutoka majumbani mwao, mwishowe kusababisha utupaji wa taka kwenye maeneo yasiyo rasimi, na kusababisha uchafuzi wa mazingira.


**(b) Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Kutokuboresha Utoaji wa Huduma za Maji Safi na Huduma za Majitaka katika Mamlaka zote za Maji wakati wa Udhibiti**

411. Mapitio yangu ya Ripoti za Utendaji wa Mwaka wa Mamlaka za Maji kutoka Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2023/24, ilionesha kuwa sio Mamlaka zote za maji zilifikia viwango vinavyohitajika vya ubora wa maji na majitaka. Uchambuzi wa kina umewasilishwa hapa chini;

**(i) Maji Yanayosambazwa na Mamlaka za Huduma za Maji Kutokukidhi Viwango Vinavyohitajika vya Ubora wa Maji**

412. Baada ya mapitio ya ripoti za utendaji wa Mamlaka za Maji kutoka Mwaka wa Fedha wa 2020/21 hadi 2023/24, nilibaini kuwa si mamlaka zote za maji nchini zilizotoa maji kwa wananchi yenye ubora unaotakiwa. Uchambuzi wa ripoti za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kuhusu vigezo vya jumla vya ubora wa maji, ikiwa pamoja na kuwapo kwa wadudu wanaotokana na kinyesi, mvurugiko wa maji, klorini bakia, na Kiwango tindikali na Alkali, ulionesha kuwa, huduma za maji hazikufikia viwango vinavyotakiwa. Hali hii ni kinyume na kifungu cha 7(1)(c)(ii) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Huduma za Maji ya mwaka 2006, ambacho kinaitaka mamlaka kufuatilia utendaji wa sekta zinazodhibitiwa kwa kuzingatia viwango vya huduma. Kwa kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji inadhibiti huduma za maji, lazima ihakikishe kuwa, mamlaka za maji zinasambaza maji yenye viwango vinavyohitajika vya ubora wa maji. **Kielelezo Na.31** kinatoa taarifa za ubora wa maji kutoka Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2023/24 kwa ufikiaji wa kiwango kinachotakiwa cha kuwapo kwa wadudu watokanao na kinyesi na ufikiaji wa kiwango cha klorini Bakia.

## Kielelezo Na. 31: Kiwango cha Ufuataji wa Viwango vya Ubora wa Maji




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Uzingatiaji wa Ubora wa Maji katika Ripoti za Mwaka za Utendaji za Mamlaka za Huduma za Maji kwa Kipindi cha 2020/2021 hadi 2023/2024.

413. **Kielelezo Na. 31** Takwimu zinaonesha kuwa, katika kipindi cha miaka yote minne ya fedha kuanzia 2020/21 hadi 2023/24, utekelezaji wa viwango vya ubora wa maji haukufikiwa kikamilifu na mamlaka zote za maji kwenye kuwapo kwa wadudu watokanao na kinyesi na Klorini bakia. Ufikiajia wa ubora mkubwa ulikuwa kwenye kuwapo kwa wadudu watokanao na kinyesi katika Mwaka wa Fedha wa 2021/22, kwa kufikia asilimia 73 ya mamlaka na kiwango cha chini kilikuwa asilimia 12 ya mamlaka kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 kwa mamalaka za maji za mikoa na wilaya. Ufikiaji wa viwango vya Klorini bakia ulikuwa chini ya asilimia 10 ya mamlaka katika miaka yote minne ya fedha na ufikiaji wa ubora wa juu ulikuwa Mwaka wa Fedha 2020/21, ambao ulikuwa asilimia sita ya mamlaka zote.

414. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji walibainisha kuwa kiwango cha chini cha ufikiaji wa ubora wa maji kilitokana na utekelezaji duni wa maagizo yanayotolewa na mamlaka ya udhibiti kutokana na kukosekana kwa hela, kama vile ufungaji wa mashine za kuweka klorini. Hivyo, kusababisha upungufu wa ubora wa maji bila kutatuliwa, na mamlaka za ziliendelea kusambaza maji ambayo hayakufikia viwango vinavyohitajika kila wakati, na kuweka afya ya jamii inayotumia maji hayo ambayo hayajafikia viwango katika hatari ya kuathiriwa na magonjwa yanayoenezwa na maji.

## (i) Utekelezaji Usioridhisha wa Viwango vya Utoaji wa Majitaka Miongoni Mwa Mamlaka za Huduma za Maji Zinazodhibitiwa

415. Mapitio ya Ripoti za Utendaji wa Mamlaka za Maji kutoka Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2023/24 yalionesha kuwa, ufikiaji wa viwango vya ubora wa majitaka ulikuwa chini ya kiwango kwa kipindi chote. Hii ni kinyume na viwango vya Tanzania vinavyotolewa na Shirika la Viwango Tanzania namba TZS 860:2006, ambacho kinaweka viwango vya juu vya 30mg/l kwa mahitaji ya oksijeni ya biokemikali na 60mg/l kwa mahitaji ya oksijeni ya kemikali. Matokeo ya uchambuzi yaliyowasilishwa katika **Jedwali Na. 24** yanaonesha kuwa, kati ya asilimia 36 na asilimia 56 ya mamlaka za maji zilizo na huduma za majitaka zilikidhi viwango vya mahitaji ya oksijeni ya biokemikali na mahitaji oksijeni ya Kemikali kila mwaka.

**Jedwali Na. 24: Ufikiaji wa Viwango vya Ubora wa Majitaka**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Mamlaka za Maji safi na usafi wa mazingira zinazopaswa kuwa na Miundombinu ya majitaka | Idadi ya Mamlaka za Maji safi na usafi wa mazingira zenye Miundombinu ya Majitaka Zilizokaguliwa | Idadi ya Mamlaka za Maji safi na usafi wa mazingira zilizofikia Viwango vya BOD na COD vinavyotakiwa | % ya Idadi ya Mamlaka za Maji safi na usafi wa mazingira zilizofikia Viwango vy BOD na COD vinavyotakiwa |
|---|---|---|---|---|
| 2020/21 | 84 | 9 | 5 | 56 |
| 2021/22 | 83 | 11 | 4 | 36 |
| 2022/23 | 73 | 11 | 6 | 55 |
| 2023/24 | 76 | 11 | 4 | 36 |
| 2024/25 | - | - | - | - |

ISO 9001:2015 Certified

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ufikiaji wa Ubora wa Majitaka kwenye Ripoti za Utendaji wa Mamlaka za Maji kutoka Mwaka 2020/21 hadi 2023/24, 2025

**Jedwali Na. 24** linaonesha kuwa, katika miaka minne ya fedha kutoka Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2023/24, kiwango cha juu zaidi cha kufikia ubora wa majitaka kilikuwa asilimia 56 ya mamlaka za maji na zenye mitandao ya majitaka. Mwaka 2020/21, asilimia 56 ya mamlaka za maji zilizo na miundombinu ya majitaka zilikidhi viwango vya mahitaji ya oksijeni ya biokemikali na mahitaji Oksijeni ya Kemikali. Ufikiaji wa ubora ulipungua hadi asilimia 36 Mwaka wa Fedha 2021/22, kisha ukaongezeka hadi asilimia 55 Mwaka wa Fedha 2022/23, kabla ya kushuka tena hadi asilimia 36 Mwaka wa Fedha 2023/24. Ingawa idadi ya mamlaka za maji zilizo na mitandao ya majitaka iliongezeka kutoka tisa Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 11 Mwaka wa Fedha 2023/24, Ongezeko hili halikuongeza ufikiaji wa ubora wa majitaka.

416. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ilionesha kuwa kutofikia viwango ubora wa majitaka kunategemea utoshelevu wa miundombinu ya kutibu majitaka kulingana na kiasi cha majitaka yanayoingia kwenye mabwawa ya majitaka. Utembeleaji wa mabwawa ya kutibu maji ya Kurasini yaliyopo chini ya DAWASA ulibaini kuwa, mabwawa yalikuwa yamejaa bila kuondoa taka zilizo jaa, na kuathiri uwezo wa mabwawa kusafisha majitaka kufikia viwango vinavyotakiwa. Matokeo yake, mabwawa yalikuwa yakifanya kazi kwa ufanisi mdogo, na matokeo ya vipimo vya Mahitaji ya oksijeni ya biokemikali na mahitaji oksijeni ya kemikali yalionesha kutofikia viwango vinavyotakiwa.

417. Hali hii ya kutiririsha majitaka ambayo hayajafikia viwango vya ubora vinavyohitajika vya 30 mg/l kwa mahitaji ya oksijeni ya biokemikali na 60 mg/l kwa mahitaji ya oksijeni ya kemikali, huchangia uchafuzi wa mazingira na kuhatarisha afya ya umma kupitia uchafuzi wa vyanzo vya maji na mifumo ikolojia inayozunguka maeneo majitaka yanakotiririkia.

### 7.3.2 Utoaji Leseni Usiyojitosheleza wa Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira

418. Nilibaini kuwa, pamoja na kuwa mamlaka zote 83 za huduma za maji zilipewa leseni kati ya 2020/21 na 2024/25, uwiano wa mamlaka zilizokuwa na miundombinu ya kutibu majitaka hadi Mwaka wa Fedha 2023/24 ilikuwa asilimia 30 pekee kati ya 76 ukiacha mamlaka za kitaifa ambazo huzalisha maji na huziuzia mamlaka za maji. Hii inaonesha kuwa asilimia 70 ya mamlaka zilizopatiwa leseni hazikuwa na mifumo ya kutibu majitaka.

419. Hii ilikuwa kinyume na Kanuni za Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira (Leseni na Ubora wa Huduma), 2020, ambazo zinahitaji uwasilishaji wa ramani za mifumo ya maji na majitaka kama sehemu ya masharti ya maombi ya leseni. Hii inaonesha kuwa mamlaka za maji zinatakiwa kuwa na miundombinu ya majitaka kama moja ya vigezo vya utoaji leseni. Hivyo, inaonesha kuwa mamlaka za maji zilipewa leseni bila kukidhi vigezo vinavyohitajika. Hali hiyo ilichangiwa zaidi na uwekezaji mdogo katika miundombinu ya majitaka na utekelezaji duni wa masharti ya leseni. Matokeo yake, jamii katika maeneo hayo zinakosa maeneo kwa ajili ya majitaka pale mashimo ya majitaka yanapokuwa yamejaa, na kusababisha uchafuzi wa mazingira.

### 7.3.3 Upangaji wa Bei za Maji, Ufuatiliaji wa Maagizo ya Bei za Maji na Utekelezaji Wake Usioridhisha

420. Wakati wa ukaguzi nilibaini upungufu katika mchakato wa upangaji na mapitio ya bei za maji, ikiwemo kutozingatia uwezo wa wananchi kumudu tozo/gharama wakati wa upangaji bei, upungufu katika kuzingatia gharama halisi, kuendelea kutumia bei za Maji zilizoisha Kipindi chake halali, na ufuatiliaji na utekelezaji wa bei za maji na masharti yaliyoambatana na bei iliyopitishwa kama ilivyoelezewa hapa chini;

**(a) Tathmini Isiyokamilika ya Mahitaji ya Mapato Wakati wa Upangaji wa Bei za Huduma za Maji**

421. Wakati wa Ukaguzi nilibaini kuwa, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji haikuweza kuandaa, kufuatilia au kusimamia utekelezaji wa tozo/gharama za maji kikamilifu. Kati ya maamuzi ya bei za maji toka mamlaka za maji 15 zilizopitishwa katika kanda nne zilizotembelewa kwa miaka ya fedha ya 2020/21 hadi 2024/25, makosa makubwa yalibainika. Mamlaka 10 za mamlaka za maji, uandaaji wa tozo zake hazikuhusisha ipasavyo gharama za fidia ya uchakavu au kushuka kwa thamani ya miundombinu, mamlaka moja ya maji haikuweka marejesho ya hela ya uwekezaji, na mamlaka zote 15 za maji zilishindwa kufanya marekebisho ya vipindi vya awali/nyuma. Upungufu huu unadhoofisha urejeshaji wa gharama za uwekezaji na kuongeza hatari ya viwango vya bei/tozo za maji ambazo wananchi hawatazimudu. Hii ni kinyume na aya ya 3 ya Jedwali la Pili la Kanuni (Maombi ya tozo za huduma za Maji na Uandaaji wa viwango vya tozo), 2020 ambayo inataka gharama za kufidia uchakavu au kushuka kwa thamani kujumuishwa ipasavyo na kukokotolewa kwa msingi wa thamani ya mali kwa kutumia mbinu ya mstari wa moja kwa moja na kuendana na muda uliobaki wa kutumika kwa miundombinu husika.

**(b) Bei za Maji Zilizoidhinishwa Kuendelea Kutumika zaidi ya Kipindi Chake Halali**

422. Kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha kuazia 2020/21 hadi 2024/25, nilibaini kuwa Mamlaka za Maji ziliendelea kutumia tozo za maji ambazo zimeisha muda wake bila kubadilishwa au kuhuishwa. Kwa kuwa mamlaka za maji zinaruhusiwa kuomba bei za maji ambazo zitatumika zaidi ya mwaka mmoja na kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu; kutowasilishwa kwa maombi ya bei mpya baada ya bei ya awali kuisha muda wake kulisababisha matumizi ya muda mrefu ya tozo za maji zilizoisha muda wake. Hii ni kinyume na Kanuni ya 26 (a) ya Kanuni ya Uombaji na Uandaaji wa Tozo za Maji, 2020 ambayo inahitaji bei ya maji

iliyooidhinishwa kutumika kwa miaka mitatu tu. Idadi ya Mamlaka za maji zilizoendelea kutumia tozo zilizoisha muda wake katika kanda nne zilizotembelewa zimeoneshwa katika **Jedwali Na. 25.**

**Jedwali Na. 25: Namba ya Mamlaka za Maji Zilizokuwa Zinatumia Tozo Zilizoisha Muda wake katika Kanda nne Zilizotembelewa**

| Jina la Kanda | Idadi ya Mamlaka za Maji safi na usafi wa mazingira kaitka Kanda iliyotembelewa | Ida ya Mamlaka za Maji zinzotumia Tozo zilizoisha Muda wake | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Mashariki | 10 | 6 | 6 | 7 | 7 | 8 |
| Ziwa | 15 | 5 | 10 | 15 | 14 | 14 |
| Nyanda za Juu Kusini | 20 | 16 | 15 | 10 | 17 | 17 |
| Kaskazini | 14 | 9 | 13 | 8 | 7 | 7 |
| **Jumla** | **59** | **36** | **44** | **40** | **45** | **46** |
| Asilimia ya Mamlaka za maji zilizokuwa zinatumia tozo zilizoisha muda wake | | 61 | 74 | 68 | 76 | 78 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Rejista ya Leseni za Mamlaka za Maji na Tozo Zinazotumika Kutoka Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25), 2025


ISO 9001:2015 Certified

423. **Jedwali Na. 25** lilionesha kuwa hadi Mwaka wa Fedha 2024/25, mamlaka za maji 46 takribani asilimia 78 ya Mamlaka za maji ziliendelea kutumia tozo zilizoisha muda wake. Pia, Jedwali linaonesha kuwa kati ya miaka ya fedha ya 2020/21 na 2024/25, asilimia 61 hadi asilimia 78 ya mamlaka za maji zilikuwa zikitumia tozo zilizoisha muda wake.

424. Mamlaka 46 za huduma za maji katika kanda zilizotembelewa ziliendelea kutumia tozo zilizoisha muda wake hadi 2024/25, kutokana na kusitishwa kwa mchakato wa mapitio na Waziri husika, hasa kwa kuzingatia uwezo wa wananchi kumudu gharama, jambo lililoathiri uamuzi wa mapitio hayo. Hii ilisababisha malaka za maji kuendelea kutumia tozo ambazo hazina uhalisia. Kupitia mapitio ya uwiano wa gharama za uendeshaji na makusanyo yatokanayo na mauzo ya maji na uwiano wa gharama za uendeshaji wa kazi wa mamlaka za maji ikijumuisha na ulipaji wa madeni na gharama za kupungua kwa thamani ya miundombinu na mapato yatokanayo na mauzo ya maji kwa

miaka ya fedha 2020/21 hadi 2023/24, nilibaini mambo yafuatayo kama yalivyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 32.**

**Kielelezo Na. 32:Mamlaka za Maji safi na Usafi wa Mazingira Zilizofikia Uwiano Unaotakiwa kuazia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2023/24**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti ya Utendaji wa Mamlaka za Maji kutoka Mwaka 2020/21 hadi 2023/24, 2025

ISO 9001:2015 Certified

425. **Kielelezo Na. 32** kinaonesha kwamba, katika kipindi cha miaka minne, uwiano wa matumizi na mapato yatokanayo na mauzo ya maji na uwiano wa gharama za uendeshaji ukijumulisha na ulipaji wa mikopo na gharama za kufikidia uchakavu wa miundombinu ulikuwa chini ya asilimia 65. Mwaka wa 2021/22 ulirekodi uwiano wa matumizi wa juu wa asilimia 61, na miaka ya 2020/21 na 2021/22 ilirekodi uwiano wa uendeshaji wa juu wa asilimia 24. Hii inaashiria kuwa katika Mwaka wa Fedha 2021/22, takribani asilimia 61 ya gharama za uendeshaji wa huduma za maji zililipwa kupitia mapato ya mauzo ya maji, huku katika miaka mingine mapato yaliyopatikana yalikuwa chini ya asilimia 50.

426. Mapitio ya Ripoti za Utendaji wa Mamlaka za Huduma za Maji kwa miaka ya fedha 2020/21 hadi 2023/24 yalionesha kuwa kushindwa kufikia viwango vya urejeshaji gharama kulisababishwa zaidi na gharama kubwa za kufidia uchakavu au upunguaji wa thamani pamoja na miundombinu chakavu. Mazungumzo na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji yalibainisha kuwa, kusitishwa kwa marekebisho ya bei katika miaka ya 2019/2020 na 2023/2024 kuliathiri uwezo wa WSSAs kupata mapato ya kutosha, kwani mamlaka hizo

ziliendelea kutumia viwango vya bei vilivyopitwa na wakati ambavyo havikuakisi gharama halisi za uendeshaji. Mnamo tarehe 2 Septemba 2025, Wizara ya Maji ilitoa barua (Kumb. Na. BC. 9/186/01-F/79) ikielekeza Wakurugenzi Wakuu wote wa Mamlaka za maji kuwasilisha mipango ya biashara kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kwa ajili ya mapitio mapya ya bei. Hatua hii ilikusudiwa kuwezesha mamlaka husika kuomba viwango vipya vya bei baada ya mipango yao ya biashara kuidhinishwa.

**(c) Ufuatiliaji na Usimamiaji Usio wa Kutosha na Kutotekelezwa kwa Maagizo ya bei/tozo Pamoja na Masharti Yake**

427. Nilibaini kuwa, ufuatiliaji na utekelezaji wa maagizo ya bei za maji ulikuwa mdogo. Hii ilitokana na ukosefu wa taarifa za utekelezaji wa masharti ya tozo, ambapo katika Mwaka wa Fedha wa 2020/21 mamlaka moja kati ya mamlaka 91 za maji ziliwasilisha taarifa na katika Mwaka wa Fedha wa 2021/22, ni mamlaka nne tu kati ya 90 zilizowasilisha taarifa, na hakuna mamlaka ya maji iliyowasilisha taarifa kuanzia 2022/23 hadi 2024/2025. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji haikutoa vyeti vya uthibitisho kwa mamlaka za maji zilizowasilisha taarifa, wala barua zozote za onyo kwa mamlaka za maji ambazo hazikuwasilisha taarifa. Aidha, kiwango cha ukaguzi wa mamlaka kilibaki kuwa cha chini, ambapo asilimia 32 ya mamlaka za maji bei zao zilizoidhinishwa zilikuwa hazijaisha muda wake zilitakiwa kufuatiliwa kwa kipindi cha 2020/21 hadi 2024/25 lakini hazikufuatiliwa, hususani mamlaka za Daraja la III na zile za kipindi cha mpito.

ISO 9001:2015 Certified

428. Hii ni kinyume na Kanuni ya 65 ya Kanuni za Maombi ya Bei na Uandaaji wa Bei za Huduma za Maji, 2020, ambayo inataka mamlaka za maji kuwasilisha taarifa za kila mwaka zinazoelezea jinsi mamlaka za maji zilivyotekeleza masharti yaliyoambatana na bei za maji zilizoidhinishwa. Sheria pia inataka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kutathmini taarifa hizo na kutoa cheti, barua za onyo, au agizo la kuzingatia ili kufuata sheria, kanuni, au masharti yaliyowekwa.

429. Sababu ya kutotoa barua za onyo katika kipindi hicho ilitokana na kusitishwa kwa upitishaji wa bei mpya za maji, jambo lililoathiri utekelezaji wa masharti ya bei kwa ufanisi. Hii ilisababisha utekelezaji wa masharti ya maagizo yanayoambatana na utekelezaji wa bei, ambapo nilibaini utekelezaji kuwa kati ya asilimia 49 na 61 kwa kipindi cha kuazia miaka ya fedha 2020/21 hadi 2024/25. Kwa sababu hiyo, maboresho yaliyokusudiwa katika upatikanaji wa huduma za maji wakati wa utekelezaji wa bei zilizopitishwa hayakufikiwa.

### 7.3.4 Ukaguzi Kufanyika Pasipokufuatilia Vigezo Vyote ili Kuhakikisha Ufikiaji wa Viwango vya Ubora wa Maji

430. Ukaguzi ulibaini kuwa, ukaguzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kuhusu ubora wa maji haukuwa wa kutosha, kwani si vigezo vyote vilivyotajwa katika Mpango wa Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji vilipimwa wakati wa ukaguzi. Katika mamlaka nne za maji zilizotembelewa, mamlaka moja ya maji, yaani Chunya, haikuwa na Mpango wa Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji wakati wa ukaguzi uliofanyika Oktoba 2025, kwani bado mpango ulikuwa haujapitishwa. Mamlaka tatu zilizobaki za maji zilikuwa na Programu za Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji. Mapitio ya Programu za Ufuatiliajia wa Ubora wa Maji, ulibaini kuwa, kuna baadhi ya vipimo vilivyowekwa kwenye programu ya ufuatiliaji wa ubora wa maji havikupimwa na mamlaka wakati wa ufuatiliaji wa ubora wa maji. Vigezo ambavyo havikupimwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji, ambavyo vimejumuishwa katika Mipango ya Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji na mamlaka husika, vimeoneshwa katika **Jedwali Na. 26.**

**Jedwali Na. 26: Vigezo vya Ubora wa Maji ambavyo Havikupimwa wakati wa Ukaguzi wa Ubora wa Maji na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

| Jina la Mamlaka ya Maji | Vigezo ambavyo Havikupimwa vya Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji kwa Kipindi cha 2020/21 hadi 2024/25 |
|---|---|
| Mwanza | Aluminiamu, Aseniki, Amoniamu, Rangi ya Maji, Sianidi, Kromiamu, Kadmiumu, Floridi, Chuma, Manganizi, Zinki na Salfeti |
| Moshi | Manganizi, Chuma na Naitreti |
| DAWASA | Amoniamu, Kalisiamu, Alkali, Ugumu wa Maji, Salfeti, Bariamu, Zebaki, Aseniki, Mabaki ya zebaki, Kromi na kemikali zinazoundwa wakati klorini inapotumika kusafisha maji na Chembechembe zake |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Vigezo Vilivyopimwa katika Ripoti za Maabara ya Ubora wa Maji kutoka 2020/21 hadi 2023/24 na EWURA; na Mpango wa Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji kutoka kwa Mamlaka za Maji Zilizotembelewa, 2025.

431. **Jedwali Na. 26** linaonesha kuwa vigezo vingi ambavyo havikupimwa vinaangukia katika kundi la metali nzito nazisizo za kikaboni, ambazo zina hatari kubwa kiafya, ikiwa pamoja na kusababisha saratani kwa watumiaji wa maji, matatizo ya neva, uharibifu wa figo na ini, methemo-globinemia kwa watoto wachanga, na flurosis kama ilivyoelezewa na Shirika la Afya Duniani[9]. Hii ilisababishwa na kutofuata mpango ulioidhinishwa wa ufuatiliaji wa ubora wa

[9] Magonjwa yanayosababishwa na unywaji wa maji yenye aseniki. Imesomwa tarehe 04 Oktoba 2025 kwenye Arsenic

maji wakati wa uchaguzi wa vitu/viezo vya kwenda kupima wakati wa ufuatiliaji wa ubora wa maji.

## 7.4 Athari za Changamoto Zilizobainika katika Kuyafikia Malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

432. Shabaha namba 6.1 na 6.2 ya lengo Na.6 katika Malengo ya Maendeleo Endelevu zinalenga kusimamia viwango vya usalama wa maji na upatikanaji wa maji kwa bei nafuu Pamoja na huduma ya usafi wa mazingira. Zaidi ya hayo, shabaha namba 6.3 na 6.4 kutoka kwenye lengo kuu namba 6 ya malengo ya Maendeleo Endelevu zinalenga kuboresha ubora wa maji kwa kupunguza uchafuzi wa mazingira, kuondoa utupaji hovyo wa taka, na kupunguza utoaji wa kemikali hatarishi na kupunguza nusu ya sehemu ya majitaka ambayo hayajatibiwa. Pia, inachangia Malengo ya Maendeleo Endelevu lengo Na. 3 hasa shabaha Na. 3.9, ambalo linalenga kupunguza magonjwa yanayosababishwa na maji. Pia, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano unalenga kuboresha upatikanaji wa huduma bora, kupunguza maji yasiyo na gharama na kupanua wigo wa huduma.

433. Nilibaini kuwa, kwa miaka ya fedha ya 2020/21 hadi 2023/24, maji yaliyotolewa kwa jamii hayakufikia viwango vinavyohitajika kwa vigezo vyote vilivyopimwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji hasa, klorini bakia. Viwango vinavyotakiwa havikufikiwa na Mamlaka zote za maji. Zaidi ya hayo, katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24, ni asilimia 9 tu ya mamalaka za maji 82 zilifikia viwango vya upatikanaji wa huduma katika maeneo yao. Hii inaonesha hatari ya kutofikia malengo yaliyowekwa ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ifikapo 2025/26 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo mwaka 2030.

## SURA YA NANE

## USIMAMIZI WA MFUMO WA USAFIRISHAJI

### 8.1 Utangulizi

434. Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi kutoka kwenye taarifa za kaguzi za ufanisi zinazohusu usimamizi wa mfumo wa usafirishaji. Pia, inaelezea maeneo yaliyokaguliwa, taasisi zilizokaguliwa na uhusiano wa ukaguzi, na Malengo ya Maendeleo Endelevu, na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na athari za matokeo ya ukaguzi katika kufikia mipango hiyo.

435. Kaguzi hizo ni kama zifuatazo:

(a) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mchakato wa Upangaji wa Maboresho ya Miundombinu ya Barabara;

(b) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Uendeshaji wa Mizani za Barabarani; na

(c) Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Huduma za Usafiri Mijini katika Majiji Makubwa.

ISO 9001:2015 Certified

### 8.1.1 Usuli Kuhusu Usimamizi wa Mfumo wa Usafirishaji

436. Mfumo wa usafirishaji nchini unatawaliwa na miundombinu ya usafiri wa nchi kavu, ambayo hutumika kama nyenzo muhimu ya usafirishaji wa abiria na mizigo na kitovu cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

437. Kupitia miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara, uboreshaji na ukarabati, pamoja na kudhibiti huduma za usafirishaji, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuboresha miundombinu yake ya barabara na utoaji wa huduma ili kuboresha ukuaji wa uchumi, kuimarisha mawasiliano ya kikanda, na kusaidia kupunguza umaskini. Hii imechangia kuwapo kwa mchango mkubwa wa sekta ya barabara katika maendeleo ya taifa, ukiwa ni asilimia 7.8 ya Pato la Taifa na kuzalisha wastani wa dola za Marekani bilioni 2.6 katika mapato ya fedha za kigeni kwa mwaka 2024.

438. Licha ya mafanikio hayo, sekta ya barabara bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazotokana na upangaji usiojitosheleza wa

uboreshaji wa miundombinu, ambao husababisha kuongezeka kwa gharama za ujenzi, mrundikano wa matengenezo yasiyofanyiwa kazi, na ucheleweshaji wa fedha za utekelezaji.

439. Pia, kuendelea kuwapo kwa magari ya mizigo yaliyojaa kupita kiasi kunachangia kuzorota kwa miundombinu ya barabara, na kusababisha kuongezeka kwa gharama za matengenezo, na kuongezeka kwa hatari za kiusalama kwa watumiaji wa barabara.

440. Kwa upande mwingine, huduma za usafiri wa mijini katika miji mikubwa hukumbwa na changamoto zinazohusiana na usalama, msongamano wa magari, na utoaji wa huduma za kusuasua. Kwa mfano, mwaka 2023, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa na ajali 1,733 za barabarani zilizohusisha pikipiki, na kusababisha vifo vya watu 1,647 na majeruhi 2,716, huku vifo vya waendesha pikipiki vikiongezeka kwa asilimia 13.3 kutoka 2022 hadi 2023.

### 8.1.2 Uhusiano Kati ya Usimamizi wa Mfumo ya Ushafirishaji na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

441. Kaguzi za Ufanisi Katika Usimamizi wa Mchakato wa Upangaji wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Barabara; Usimamizi wa Uendeshaji wa Mizani; na Usimamizi wa Huduma za Usafiri Mjini, zinawiana na Lengo la 9 na la 11 la Malengo ya Maendeleo Endelevu, hususani shabaha ya 9.1 na 11.2 mtawalia, kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 27.**

**Jedwali Na. 27: Uhusiano kati ya Usimamizi wa Mfumo wa Usafirishaji na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu**

| Jina la Ukaguzi | Mpango/Malengo | Eneo la Kipaumbele | Hatua |
|---|---|---|---|
| Usimamizi wa Mchakato wa Upangaji wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Barabara | Mpango wa tatu wa Mendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano | Kufungua Miundombinu ya Usafirishaji | • Ujenzi wa Miundombinu ya Barabara; na<br>• Kuimarisha Taasisi za Mafunzo katika Sekta ya Barabara. |
| | Malengo ya Maendeleo Endelevu | Lengo la 11: Kufanya miji na makazi ya watu yawe salama, thabiti na endelevu kwa wote. | • Shabaha ya 11.2: Kufika mwaka 2030, kuwa na mfumo wa usafirishaji uliyo salama, nafuu, unaofikika na endelevu kwa wote. |
| | | Lengo la 9: Kujenga miundombinu | • Shabaha ya 9.1, ifikapo 2030, kuwa na |

| Jina la Ukaguzi | Mpango/Malengo | Eneo la Kipaumbele | Hatua |
|---|---|---|---|
| | | thabiti, kukuza ushirikishaji na maendeleo endelevu ya viwanda, na kukuza uvumbuzi. | miundombinu bora, inayotegemewa, endelevu na thabiti ili kusaidia maendeleo ya kiuchumi |
| Usimamizi wa Uendeshaji wa Mizani | Mpango wa tatu wa Mendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano | Kufungua Miundombinu ya Usafirishaji | • Ujenzi wa Miundombinu ya Barabara; na<br>• Kuimarisha Taasisi za Mafunzo katika Sekta ya Barabara. |
| | Malengo ya Maendeleo Endelevu | Lengo la 9: Kujenga miundombinu thabiti, kukuza ushirikishaji na maendeleo endelevu ya viwanda, na kukuza uvumbuzi | • Shabaha ya 9.1, ifikapo 2030, kuwa na miundombinu bora, inayotegemewa, endelevu na thabiti ili kusaidia maendeleo ya kiuchumi. |
| Usimamizi wa Huduma za Usafiri Kwenye Miji Mikuu | Mpango wa tatu wa Mendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano | Kufungua Miundombinu ya Usafirishaji | • Kupunguza foleni kwenye Majiji Makubwa<br>• Kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika huduma za usafiri wa ardhini; na<br>• Kuimarisha udhibiti wa huduma za usafiri |
| | Malengo ya Maendeleo Endelevu | Lengo la 11: Kufanya miji na makazi ya watu kuwa salama, thabiti na endelevu kwa wote | • Shabaha ya 11.2: Ifikapo 2030, kuwa na mfumo wa usafirishaji ulio salama, nafuu, unaofikika na endelevu kwa wote. |

***Chanzo***: Uchambuzi wa Wakaguzi kwa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa na Malengo ya Mendeleo Endelevu, 2025

### 8.1.3 Mikakati na Juhudi za Serikali katika Usimamizi wa Mfumo wa Usafirishaji Nchini

442. Ili kuhakikisha usimamizi mzuri wa mfumo wa usafirishaji, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeweka mikakati mbalimbali inayotoa mwelekeo katika kufanikisha kuwapo kwa mfumo wa usafirishaji unaofikika, nafuu, salama na endelevu nchini. Mikakati hii imeainishwa katika **Kielelezo Na. 33**.

**Kielelezo Na. 33: Mikakati ya Serikali Iliyowekwa Kusimamia Mfumo wa Usafirishaji**

**Mpango Mkakati wa Wizara ya Ujenzi (2021/22 - 2025/26)**

Kupitia Lengo D: Mpango unalenga kuboresha miundombinu katika sekta ya ujenzi kupitia ujezi wa miundombinu ya barabara na udhibiti wa uzito wa magari ili kuzuia uharibifu wa miundombinu ya barabara

**Mpango Mkakati wa Wizara ya Uchukuzi (2021/22 - 2025/26)**

Mpango huu unalenga kuboresha huduma za usafiri kwa kuimarisha udhibiti huduma katika sekta ya Uchukuzi

**Mpango Mkakati wa OWM-TAMISEMI (2021/22-2025/26)**

Kupitia Lengo D: Mpango unalenga kuboresha utoaji wa huduma kwenye Mikoa na Wilaya kupitia ujenzi na matengenezo ya mtandao wa barabara

NATIONAL AUDIT OFFICE NAOT

***Chanzo***: Uchambuzi wa Wakaguzi Katika Mipango Mikakati Kwenye Usimamizi wa Mfumo wa Usafirishaji

ISO 9001:2015 Certified

443. Aidha, jitihada za serikali katika usimamizi wa mfumo wa usafirishaji ni kama ilivyoelezwa katika **Kielelezo Na. 34.**

**Kielelezo Na. 34: Jitihada za Serikali Katika Usimamizi wa Mfumo wa Usafirishaji**

| Kupunguza Foleni Kwenye Majiji | Kuboresha Miundombinu ya Usafirishaji | Kulinda Mindombinu ya Barabara |
|---|---|---|
| •Kupunguza foleni katika Jiji la Dar es Salaam, Dodoma n.k. Hatua hizi zinajumuisha ujenzi wa barabara za juu, upanuzi wa barabara kuu, ujenzi wa barabara za mzunguko, na miundombinu ya usafiri wa mwendokasi. | •Utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara kwa lengo la kuunganisha mikoa na maeneo mbalimbali ili kuwezesha shughuli za kibiashara na kukuza uchumi. | •Kuandaliwa muongozo wa uendeshaji wa Mizani unaosaidia katika usimamizi wa utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Mizani na Kanuni Zake. |

***Chanzo***: Uchambuzi wa Wakaguzi kwa Juhudi za Serikali Katika Usimamizi wa Mfumo wa Usafirishaji, 2025

## 8.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

### 8.2.1 Malengo ya Ukaguzi

444. Lengo kuu la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini iwapo Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi, na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilisimamia ipasavyo mfumo wa usafirishaji ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za usafiri, za uhakika na endelevu.

445. Malengo mahususi ya ukaguzi yalikuwa kutathmini iwapo:

(a) Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilisimamia ipasavyo mchakato wa upangaji wa uboreshaji wa miundombinu ya barabara;

(b) Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara nchini zilisimamia ipasavyo uendeshaji wa mizani ili kudhibiti magari yanayozidisha uzito; na

(c) Wizara ya Uchukuzi na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilisimamia ipasavyo huduma za usafiri wa umma ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za usafiri mijini, zilizo za uhakika na endelevu.

NATIONAL AUDIT OFFICE NAOT ISO 9001:2015 Certified

### 8.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

446. Katika Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Mchakato wa Upangaji wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Barabara, Wakaguliwa wakuu walikuwa ni Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI. Ukaguzi huu ulilenga kutathmini utambuzi wa mahitaji ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara, kuweka kipaumbele kwa mahitaji, kukusanya rasilimali za kuwezesha uboreshaji wa miundombinu, na kupanga kwa ajili ya utekelezaji wa Uboreshaji wa Miundombinu. Ukaguzi ulihusisha kipindi cha miaka minne ya fedha, kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25

447. Aidha, Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Uendeshaji wa Mizani, Wakaguliwa wakuu walikuwa ni Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara Nchini. Ukaguzi ulilenga kutathmini iwapo Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara Nchini walisimamia ipasavyo sheria za mizani kwa makosa yote yanayofanywa na wasafirishaji, uanzishaji na utekelezaji wa hatua za kuimarisha uendeshaji wa mizani, kutekeleza matengenezo na urekebishaji wa vifaa vya mizani, uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya uendeshaji wa mizani. Ukaguzi huu ulihusisha kipindi cha miaka minne ya fedha, kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25.

448. Aidha, nilitathmini ufanisi wa huduma za usafiri mijini katika majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, na Mbeya, ambapo Wizara ya Uchukuzi na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI walikuwa wakaguliwa wakuu. Katika kipengele hiki nilitathmini upangaji wa huduma za usafiri mijini, kiwango ambacho huduma hiyo inahakikisha ufikivu, na kiwango ambacho mifumo ya kitaasisi na udhibiti inasaidia kikamilifu uratibu na udhibiti wa huduma ya usafiri. Pia, nilitathmini matumizi ya miundombinu iliyopo, usimamizi wa msongamano wa magari, pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya huduma za usafiri mijini. Mawanda ya ukaguzi yalihusisha miaka mitano ya fedha kuanzia 2020/21 hadi 2024/25.

## 8.3 Matokeo ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Usimamizi wa Mchakato wa Upangaji wa Maboresho ya Miundombinu ya Barabara

449. Nilibaini upungufu katika usimamizi wa mchakato wa upangaji wa maboresho ya miundombinu ya barabara ili kuhakikisha uimarishaji wa ufikikaji. Tathmini yangu ya uboreshaji wa barabara za mikoa na za wilaya chini ya Wakala wa Barabara Nchini na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini mtawalia, imebaini kuwa, shughuli za kila mwaka za uboreshaji wa miundombinu hazikusababisha kikamilifu uboreshaji wa hali ya jumla ya barabara za mikoa na wilaya.

450. Aidha, tathmini yangu kuhusu hali ya barabara za mikoa na wilaya (2021/22-2024/25) imebaini kuwa, licha ya maboresho ya barabara yaliyofanyika kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25, asilimia ya barabara za mikoa zilizo katika hali nzuri ilipungua kutoka asilimia 28 Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi asilimia 17 kwa Mwaka wa Fedha 2024/25. Barabara za mikoa zilizo katika hali mbaya zilibaki kuwa asilimia 9 kwa miaka mitatu ya fedha (2021/22-2023/24), kisha ikaongezeka hadi asilimia 15 Mwaka wa Fedha 2024/25. Matokeo ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara yalionekana kidogo katika asilimia ya barabara zilizo katika hali ya kawaida, ambayo iliongezeka kutoka asilimia 63 Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi asilimia 67 Mwaka wa Fedha 2024/25.

451. Barabara za wilaya zilizo katika hali mbaya zilipungua kutoka asilimia 45 kwa Mwaka kwa Fedha 2021/22 hadi asilimia 37 kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, kisha ikabaki vilevile Mwaka wa Fedha 2023/24, kabla ya kupungua kidogo hadi asilimia 36.8 Mwaka wa Fedha 2024/25. Wakati huo huo, barabara za wilaya zilizo katika hali nzuri ziliongezeka kutoka asilimia 19 Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi asilimia 30 Mwaka wa Fedha 2022/23, lakini zilipungua hadi asilimia 28 Mwaka wa Fedha 2023/24 na kuongezeka kidogo hadi asilimia 29 kwa Mwaka wa Fedha 2024/25. Licha ya kupungua kwa barabara za wilaya zilizoorodheshwa kuwa katika hali mbaya, malengo yaliyokusudiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini, ambayo yalikuwa ni kupunguza asilimia ya barabara zilizo katika hali mbaya kutoka asilimia 41 Mwaka wa Fedha 2021/22 na hadi asilimia 25 Mwaka wa Fedha 2024/25, hayakufikiwa.

452. Upungufu huu ulitokana na upangaji usiotosheleza wa maboresho ya miundombinu ya barabara kama ilivyofafanuliwa hapa chini:

### 8.3.1 Utambuzi na Uainishaji Usiotosheleza wa Mahitaji ya Maboresho ya Miundombinu ya Barabara

453. Nilibaini yafuatayo katika uainishaji wa mahitaji ya maboresho ya miundombinu ya barabara.

#### (a) Ukosefu wa Utaratibu Rasmi wa Utambuzi wa Maboresho ya Miundombinu ya Barabara

454. Mapitio ya Mpango Mkakati (2021/22-2025/26) wa Wakala wa Barabara Tanzania na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania, yalibaini kuwa Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilikuwa hazijaweka mfumo madhubuti wa utambuzi wa mahitaji ya miundombinu ya barabara. Hasa, Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa

na Serikali za Mitaa hazikuweka utaratibu maalumu wa kuibua miradi ya ujenzi wa barabara, hivyo kupunguza upatikanaji wa misingi iliyo wazi na yenye lengo la kuamua ujenzi wa barabara.


455. Aidha, ubainishaji wa mahitaji uliokuwapo ulijikita katika shughuli za matengenezo ya barabara pekee, ambapo Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini Tanzania na Wakala wa Barabara Tanzania walikuwa na Mfumo wa Matengenezo ya Barabara za Wilaya na Mfumo wa Usimamizi wa Matengenezo ya Barabara, mtawalia, kama nyenzo za kuchakata mahitaji ya matengenezo ya mitandao ya barabara, huku kukikosekana kwa mfumo maalum kwa ajili ya kutambua mahitaji ya ujenzi wa barabara (ujenzi kwa kiwango cha lami).

456. Aidha, katika kuandaa Mpango Mkakati wa Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2025/26, miradi ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara ilijumuishwa katika mpango kama mahitaji yaliyoainishwa. Hata hivyo, mahitaji hayo hayakuwa na tathmini ya mahitaji ili kuonesha mambo muhimu kama vile hali ya barabara, wingi wa matumizi, umuhimu wa kuunganishwa, na masuala ya kijamii na kiuchumi yalivyotathiminiwa vya kutosha katika kupendekeza majitaji hayo. Hali hii ilikuwa kinyume na Kifungu cha 6(f) cha Sheria ya Barabara za Taifa Sura ya 167, kinachozitaka mamlaka za barabara kufanya tathmini ili kurahisisha upangaji, uendelezaji na uboreshaji wa miundombinu ya barabara. Hali hii ilisababisha kukosekana kwa msingi madhubuti wa kupanga vipaumbele vya miradi ya kuboresha miundombinu ya barabara, kwani taarifa za awali muhimu kama vile wingi wa magari, umuhimu wa kiuchumi, na tija ya kijamii ya mahitaji ya barabara yaliyoibuliwa hazikuainishwa ipasavyo ili kuweka kipaumbele kwa miradi ya ujenzi wa barabara.

### (b) Uzingatiaji Usiojitosheleza wa Mahitaji ya Matengenezo Katika Upangaji wa Maboresho ya Miundombinu ya Barabara

457. Mapitio yangu ya Mipango ya Mwaka ya Wakala wa Barabara Tanzania na Mipango Kazi ya Wakala wa Brabara Vijijini na Mijini kwa miaka ya fedha 2021/22–2024/25 , yalibaini kuwa Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hazikuhakikisha kwa ufanisi kuwa mahitaji ya matengenezo ya barabara yanaakisiwa ipasavyo katika mipango. Aidha, nilibaini kuwa malengo ya kila mwaka ya matengenezo ya barabara za mikoa yalionesha mwelekeo wa kushuka katika kushughulikia mahitaji ya matengenezo yaliyokuwapo, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 34.**

**Kielelezo Na. 35: Kiwango cha Mahitaji ya Matengenezo ya Barabara Kilichoshughulikiwa na Mpango wa Mwaka wa Matengenezo ya Barabara**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi Katika Mipago Kazi ya Mwaka wa Wakala wa Barabara Tanzania (2021/22-2024/25)

458. **Kielelezo Na. 35** kinaonesha kuwa Matengenezo ya Barabara za mikoa yaliyopangwa yalikuwa ni asilimia 97.8 na asilimia 91.7 ya mahitaji yaliyoainishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 na 2022/23, mtawalia. Hata hivyo, kiwango ambacho mahitaji yaliyoainishwa yalijumuishwa katika mpango wa mwaka wa matengenezo yaliyopangwa kilipungua kutoka asilimia 97.8 hadi asilimia 40.5 Mwaka wa Fedha 2023/24 na asilimia 34.9 Mwaka wa Fedha 2024/25. Hii inamaanisha kuwa asilimia 59.5 ya mahitaji ya matengenezo ya barabara za mikoa yaliyoibuliwa hayakushughulikiwa katika mipango ya matengenezo ya Mwaka wa Fedha 2023/24, huku kiasi hicho kikifikia asilimia 65.1 katika Mwaka wa Fedha 2024/25, jambo linaloashiria kuongezeka kwa mrundikano wa matengenezo ya barabara za mikoa ambayo hayakufanyiwa kazi.

459. Aidha, Mapitio yangu ya Ripoti za Mwaka za Matengenezo za Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini kwa Miaka ya Fedha 2021/22–2024/25 nilibaini kuwa, kwa wastani, ni asilimia 26 za mahitaji ya matengenezo ya barabara za wilaya yaliyoibuliwa yalijumuishwa katika Mipango ya Mwaka ya Matengenezo. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, uzingatiaji wa mahitaji ya matengenezo katika Mpango wa Mwaka wa Matengenezo ulikuwa asilimia 24, ulipanda hadi asilimia 26 kwa miaka ya fedha 2022/23 na 2023/24, na kisha kufikia asilimia

27 Mwaka wa Fedha 2024/25. Hali hii inaashiria kuwa takriban asilimia 73 hadi asilimia 76 ya mahitaji yaliyopo ya matengenezo ya barabara za wilaya hayakujumuishwa katika Mpango wa mwaka wa Matengenezo. Hii inaashiria kuongezeka kwa mrundikano wa kazi za matengenezo ya barabara, jambo linalosababisha kuzorota kwa hali ya barabara.

460. Uzingatiaji usiotosheleza wa mahitaji ya matengenezo ulitokana na matumizi ya ukomo wa bajeti badala ya kutoa kipaumbele kulingana na mahitaji halisi ya shughuli za matengenezo. Kama nilivyobaini wakati wa mapitio ya Mpango wa Mwaka (2021/22-2024/25) wa shughuli za matengenezo ya barabara, malengo ya mwaka yalipangwa kulingana na ukomo wa bajeti uliotolewa, huku kukiwa hakuna uzingatiaji wa mahitaji ya matengenezo yaliyopo ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyopangwa yanahakikisha uendelevu wa uboreshaji wa miundombinu ya barabara.

### 8.3.2 Upangaji Usiojitosheleza wa Vipaumbele Katika Kuchagua Miradi ya Kutekeleza katika Kuboresha Miundombinu ya Barabara

461. Nilibaini kuwa Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hazikuhakikisha kuwa upangaji wa vipaumbele vya mahitaji ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara yaliyopo unafanyika kwa tija. Aidha, Mpango Mkakati wa Wakala wa Barabara Tanzania (2021/22–2024/26) unabainisha hitaji la maboresho ya barabara ili kukidhi mahitaji ya kijamii na kiuchumi ya nchi. Pia, mpango ulibainisha kama utekelezaji wa mahitaji hayo ulikumbwa na changamoto ya uhaba wa fedhaa. Mpango huo unatambua uboreshaji wa miundombinu ya barabara kama uwezeshaji mtambuka kwa sekta za kilimo, viwanda, madini, biashara, utalii, maendeleo ya mijini, na huduma za kijamii.

462. Hata hivyo, licha ya kuwapo kwa mahitaji ya uboreshaji na upungufu wa fedha, mapitio yangu ya miradi ya ujenzi wa barabara iliyopangwa kwa miaka ya fedha 2021/22 hadi 2024/25, pamoja na upembuzi yakinifu uliopangwa, yalibaini kuwa miradi ya ujenzi wa barabara za mikoa na wilaya haikuibuliwa kupitia uchambuzi wa vipaumbele. Miradi iliibuliwa kulingana na maelekezo, mahitaji, na mawasilisho kutoka ofisi za mikoa. Hata hivyo, mchakato huu wa uibuaji ulikosa tathmini ya kimfumo ya vigezo muhimu, ikiwa pamoja na miundombinu iliyopo, hali ya barabara, umuhimu wa kiuchumi, athari za kijamii, na tija ya kifedha. Hali hii ilikuwa kinyume na kifungu cha 6(2)(a) cha Sheria ya Barabara, Sura ya 167, kinachoielekeza Wizara ya Ujenzi kuendeleza barabara kwa mujibu wa programu ya kitaifa ya uwekezaji na maendeleo ya barabara. Vigezo hivi vilikuwa muhimu ili kuhakikisha kuwa

miradi ya uboreshaji wa miundombinu inatoa thamani bora na inaendana na vipaumbele vya maendeleo ya kitaifa.

463. Upangaji wa vipaumbele usio na tija ulitokana na ukosefu wa zana sanifu ya kupanga vipaumbele kwa ajili ya miradi ya Ujenzi wa barabara, ambayo ingetoa vigezo vilivyo wazi na utaratibu maalumu wa kufanya tathmini, kupanga madaraja, na kuchagua miradi kulingana na vigezo kama vile hali ya barabara, umuhimu wa kiuchumi na kijamii, usalama, na gharama nafuu.

464. Kutokana na hali hiyo, mfumo huu wa uchaguzi wa miradi unazidisha hatari ya rasilimali chache kuelekezwa kwenye barabara zenye umuhimu mdogo, huku miradi ya yenye tija zaidi ikisalia bila kufanyiwa kazi, na hivyo kuathiri maendeleo ya nchi kuelekea kupata mfumo endelevu wa usafirishaji.

465. Upangaji wa vipaumbele uliishia kwenye shughuli za matengenezo kutokana na kuwapo kwa zana za upangaji vipaumbele vya matengenezo kama vile Mfumo wa Matengenezo ya Barabara za Wilaya chini ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini na Mfumo wa Usimamizi wa Matengenezo ya Barabara, chini ya Wakala wa Barabara Tanzania.

### 8.3.3 Ukusanyaji Usiotosheleza wa Rasilimali kwa ajili ya Kuboresha Miundombinu ya Barabara

466. Nilibaini yafuatayo kuhusiana na ukusanyaji wa rasilimali kwa ajili ya miradi ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara:

#### (a) Utengaji wa Fedha Usio na Ufanisi kwa ajili ya Uboreshaji wa Miundombinu ya Barabara

467. Tathmini yangu kuhusu mwenendo wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara za mikoa na wilaya kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25 ilibaini kuwa Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa hazikutenga fedha ipasavyo kwa ajili ya shughuli hizo. Hali hii ilikuwa kinyume na aya ya 5.11.2.2 ya Sera ya Taifa ya Usafirishaji ya Mwaka 2003, inayoelekeza kuwa, ili kuhakikisha upangaji na ufadhili wa kutosha wa miundombinu ya barabara mijini, mamlaka za barabara zinapaswa kuibua na kutenga rasilimali ikiwa pamoja na zinazotoka sekta binafsi.

468. Kupitia Mpango Kazi wa Mwaka wa Wakala wa Barabara Nchini (2021/22-2024/25) nilibaini kuwa, kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, jumla ya Shilingi bilioni 94.64 zilitengwa kwa ajili ya shughuli za uboreshaji wa

miundombinu ya barabara za mikoa, kiwango ambacho kilipungua kwa shilingi bilioni 89.6 mnamo mwaka wa fedha 2022/23, kikifuatiwa na shilingi bilioni 87.27 katika miaka ya fedha 2023/24 na 2024/25, mtawalia.

469. Kwa upande mwingine, uchambuzi wa fedha zilizotengwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara za wilaya, ulionesha kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ilitenga shilingi bilioni 716.8 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara za wilaya kwa Mwaka wa Fedha 2021/22. Hata hivyo, licha ya kuongezeka kwa mahitaji ya maboresho ya barabara, fedha zilizotengwa zilipungua hadi shilingi bilioni 704.9 kwa mwaka wa fedha 2022/23 na Sh. 704.7 bilioni kwa mwaka wa fedha 2023/24, kiwango ambacho kilibaki vilevile kwa mwaka wa fedha 2024/25.

470. Kupungua kwa kiwango cha fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara kulitokana na matumizi ya ukomo wa bajeti badala ya kutoa kipaumbele kulingana na mahitaji halisi ya shughuli za uboreshaji wa miundombinu ya barabara. Nilibaini kuwa Malengo ya Mpango wa Mwaka (2021/22–2024/25) ylipangwa kulingana na ukomo wa bajeti uliotolewa, huku kukiwa na uzingatiaji mdogo wa mahitaji ya maboresho yaliyopo ili kuhakikisha kuwa maboresho yaliyopangwa yanahakikisha uendelevu wa miundombinu ya barabara.

471. Utaratibu huu ulipunguza uwezo wa Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kupanga na kutekeleza hatua muhimu za uboreshaji wa barabara ili kuakisi mahitaji halisi. Hali hii ilisababisha miundombinu ya barabara kuendelea kuharibika, kama ilivyobainika kupitia kupungua kwa idadi ya barabara za mikoa zenye hali nzuri.

**(b) Fedha Zilizotengwa Kwa Ajili ya Uboreshaji wa Miundombinu ya Barabara Kutokutolewa Kikamilifu**

472. Nilibaini kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya uboreshaji wa barabara za mikoa hazikutolewa kikamilifu. Kupitia mapitio ya Taarifa za Utendaji za Mwaka wa Fedha (2021/22-2024/25) za Wakala wa Barabara Tanzania na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini, nilibaini kuwa fedha zilizotengwa na Wizara ya Ujenzi kwa ajili ya uboreshaji wa barabara za mikoa zilitolewa kikamilifu katika miaka miwili kati ya minne ya fedha iliyokaguliwa, huku viwango vya utoaji vikiwa ni asilimia 116 na asilimia 104 mnamo Mwaka wa Fedha 2021/22 na 2023/24 mtawalia.

473. Aidha, katika miaka ya fedha ya 2022/23 na 2024/25, fedha zilizotolewa kwa ajili ya kufanikisha uboreshaji wa miundombinu ya barabara za mikoa

zilikuwa asilimia 51 na asilimia 88, mtawalia, ya fedha yote iliyotengwa kwa mwaka husika.

474. Vilevile, fedha zilizotengwa na Ofisi ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa ajili ya maendeleo ya barabara za wilaya chini ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini hazikutolewa kikamilifu, ambapo kiwango cha juu cha utoaji kilirekodiwa Mwaka wa Fedha 2021/22 kwa asilimia 93, na kupungua hadi asilimia 86 katika Mwaka wa Fedha 2022/23. Katika miaka miwili ya fedha iliyobaki, utoaji wa fedha ulikuwa asilimia 78 Mwaka wa Fedha 2023/24 na asilimia 57 Mwaka wa Fedha 2024/25. Hii inamaanisha kuwa utoaji wa fedha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara haukuwa thabiti, jambo ambalo linaashiria upungufu katika mipango ya kifedha ili kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali kwa wakati na kusaidia shughuli za uboreshaji wa miundombinu ya barabara.

475. Hali hii ilikuwa ni kinyume na Kanuni ya 11(1) ya Kanuni za Barabara (Ufadhili na Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi) za Mwaka 2013, inayozitaka Wizara ya Ujenzi na OWM - TAMISEMI kutenga rasilimali kwa ajili ya kazi za maendeleo kulingana na mpango wa uwekezaji wa muda mrefu na bajeti ya mwaka iliyoidhinishwa na Bunge.

476. Mapitio ya Barua yenye kumbukumbu namba CD.145/569/01A/96 kutoka kwa Wakala wa Barabara Nchini kwenda Wizara ya Ujenzi kuhusu hali ya malimbikizo ya malipo ya miradi ya uboreshaji wa barabara, Nilibaini kuwa kutotolewa kwa fedha kikamilifu zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu ya barabara kumesababisha ongezeko la malimbikizo ya madai ya malipo ambayo hayajalipwa yanayohusiana na uboreshaji wa miundombinu ya barabara.

477. Aidha, kufikia Juni kwa mwaka wa fedha 2021/22, malipo yaliyokuwa yakidaiwa kwa ajili miradi ya uboreshaji wa barabara chini ya Wakala wa Barabara Nchini yalikuwa Shilingi trilioni 0.633, ambapo yaliongezeka hadi Shilingi trilioni 0.701 kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, kisha shilingi trilioni 1.295, na hatimaye kufikia Shilingi trilioni 1.221 kwa mwaka wa fedha 2023/24 na 2024/25 mtawalia.

478. Aidha, nilibaini kuwa ucheleweshaji wa utoaji wa fedha haukukwamisha tu maendeleo ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara, bali pia ulisababisha serikali kuingia gharama za ziada kutokana na tozo za riba kwenye malipo yaliyochelewa au tofauti za viwango vya kubadilishia fedha za kigeni, kwa kuwa malipo yalifanyika kwa fedha za kigeni. Kwa mfano, wakati wa ukaguzi huu,

miradi minne kutoka mikoa iliyotembelewa ilikuwa na madai ya riba ya Shilingi bilioni 5.6 kutokana na kuchelewa kwa malipo. Miradi hiyo ilikuwa ni barabara ya Nachingwea–Nanganga na Chunya–Makongorosi, ambazo zilipata tozo za riba za Shilingi bilioni 2.984 na shilingi milioni 824.86 mtawalia, na barabara ya Nsalaga–Ifisi Jijini Mbeya na barabara ya mzunguko ya Dodoma awamu ya kwanza ambazo zilirundika tozo za riba ya shilingi milioni 764.51 na shilingi bilioni 1.03 mtawalia.

479. Kukosekana kwa ufanisi katika utoaji wa fedha kulitokana na makadirio ya bajeti yasiyohalisi kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara, kwani ilibainika kuwa kiasi kilichopangwa kwenye bajeti hakikuakisi mahitaji ya fedha katika mradi kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara. Jambo linaloashiria kuwa makadirio ya mahitaji ya fedha wakati wa maandalizi ya bajeti haukuwa na ufanisi. Hali hii ilisababisha mzigo katika utoaji wa fedha, kwani kiasi kikubwa cha fedha kilichoombwa hakikuakisiwa katika bajeti iliyoidhinishwa.

## 8.4 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Usimamizi wa Uendeshaji wa Mizani

480. Nilibaini changamoto katika Usimamizi wa Uendeshaji wa Mizani, zinazohusiana na ufanisi wa uendeshaji, usimamizi wa kisheria, Matengenezo ya vifaa vya Mizani, pamoja na uratibu wa shughuli za mizani, kama ilivyoelezwa hapa chini:

ISO 9001:2015 Certified

### 8.4.1 Uendeshaji wa Mizani Usiojitosheleza ili Kupunguza Muda wa Upimaji wa Uzito wa Magari

481. Nilibaini yafuatayo yanayoathiri ufanisi wa uendeshaji wa Mizani:

#### (a) Kukosekana kwa Uwezo wa Mifumo ya Mizani Kuwasiliana na Kubadilishana Taarifa

482. Kupitia uhakiki uliofanyika kwenye mizani 10 zilizotembelewa na wakaguzi, nilibaini kuwa mifumo ya kwenye mizani ilikuwa haisomani, huku kukiwa hakuna ubadilishanaji wa taarifa kati ya mizani zilizopo katika kituo kimoja (kwa mfano, mizani ya upande wa mashariki na magharibi). Utaratibu huu ni kinyume na Kifungu cha 13 (1) na (2) cha Sheria ya Udhibiti wa Uzito wa Magari, ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ya Mwaka 2016, inayozitaka nchi wanachama kuanzisha na kusimamia mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa ajili ya mtandao wa barabara, hususani kwa ajili ya usimamizi wa mizani, na mifumo hiyo iweze kusomana ndani ya mtandao wa mizani wa kikanda.

483. Ingawa Wakala wa Barabara Tanzania ulitumia programu za kompyuta kama vile T-Load, Tan-Weight, na Smart Scale kwenye vituo vya mizani, mifumo hii ilikabiliwa na changamoto za utangamano na uwezo wa kuwasiliana. Kutokana na hali hiyo, gari lililosajiliwa upande mmoja wa kituo (kwa mfano, Mashariki/Kaskazini), taarifa zake za usajili moja kwa moja hazikuweza kunaswa upande wa pili (Magharibi/Kusini) ndani ya mtandao mmoja wa barabara.

484. Nilibaini kuwa kutowasiliana kwa mifumo ya uendeshaji wa mizani kulitokana na usanifu usiojitosheleza wa mifumo ya TEHAMA pamoja na Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara Tanzania kushindwa kuratibu uanzishaji wa mfumo wa TEHAMA wa uendeshaji wa mizani, ambao unaweza kusaidia vituo vya mizani kusomana na ambao ungeweza kuunganishwa na usajili wa wasafirishaji ili kuwezesha unasaji wa taarifa za awali katika vituo vya mizani.

485. Hali hii inasababisha urudufu wa kazi, taratibu za upimaji uzito nje ya mifumo, na muda mrefu wa utoaji huduma, jambo ambalo husababisha msongamano wa magari usio wa lazima wakati wa usajili. Kutokana na msongamano huo, waendesha mizani walilazimika kufanya uhakiki wa magari nje ya mifumo yaani mizani na kurekodi takwimu za uzito kwenye madaftari kama ilivyoshuhudiwa katika Mizani za Vigwaza Kaskazini na Kusini, ambapo mnamo Septemba 2025, kati ya magari 35,015 yaliyopimwa, magari 12,512 yalifanyiwa uhakiki nje ya mfumo kwa kutumia madaftari, ikiwa in sawa ana asilimia 35.7 ya magari yote yaliyohakikiwa.

ISO 9001:2015 Certified

**(b) Usimamizi Usiojitosheleza wa Mfumo wa Kusimamia Takwimu wa Duku Kusababishia Hasara Serikali ya Shilingi bilioni 5.089**

486. Nilibaini kutokuwepo kwa ufanisi katika usimamizi na utekelezaji wa mfumo wa mizani wa kusimamia takwimu wa Duku. Mfumo huo uliundwa ili kuwezesha ufuatiliaji wa mizani ukiwa mbali, kuongeza uwazi, na kusaidia usambazaji wa takwimu kwa wakati kupitia usimamizi wa pamoja wa takwimu za uzito na picha za kamera za ufuatiliaji.

487. Mapitio yangu ya mkataba namba TRD/HQ/1031/2015/16, nilibaini kuwa mnamo tarehe 29 Aprili 2016, Wakala wa Barabara Nchini, kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi, waliingia mkataba na mzabuni kwa ajili ya usanifu na ufungaji wa mfumo huo katika vituo 13 vya mizani, vikiwemo Vigwaza, Mikese, Nala, Njuki, Himo, Mikumi, Mpemba, Mingoyo, Mutukula na Nyakahura kwenye mtandao wa barabara kuu, ukiwa na thamani ya Shilingi bilioni 7.780.

488. Kupitia uhakiki niliofanya katika vituo vilivyochaguliwa wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa katika vituo 13 ambavyo mfumo huo mpya ulikuwa umewekwa, baadaye uliondolewa, huku Wakala wa Barabara Nchini akirejea kwenye kutumia mfumo wa mwanzo wa T-LOAD, ambao hauna uwezo wa kufuatilia shughuli za mizani ukiwa mbali.

489. Hali hii ilitokana na upangaji usijitosheleza wa mkataba katika kuhakikisha umiliki kamili wa mfumo uliotekelezwa. Kutokana na hali hiyo, shughuli za mizani zinaendelea kutegemea mifumo isiyounganishwa, jambo ambalo huathiri usimamizi wa takwimu, utoaji wa taarifa, na usimamizi wa sheria, hususani ukusanyaji wa faini kutoka kwa magari yaliyozidisha uzito, ambao kwa sasa unategemea mfumo isiyo ya TEHAMA. Aidha, jambo hili linaashiria hasara ya Shilingi bilioni 5.089 zilizolipwa kwa ajili ya mfumo uliowekwa lakini baadaye ukaondolewa.

### (c) Kutokuwiana kwa Kasi ya Kuwasili kwa Magari na Uwezo wa Kupima Uzito

490. Kupitia uhakiki na mapitio ya mawasiliano ya maoni ya madereva, nilibaini kuwa ushoroba wa Barabara Kuu ya Tanzania -Zambia ulikabiliwa na msongamano wa magari, hasa katika vituo vya mizani kama Vigwaza na Mpemba. Msongamano wa magari katika kituo cha mizani ulfika takribani mita 700 kutoka eneo la mizani.

ISO 9001:2015 Certified

491. Hali hii ni kinyume na aya ya 1.4 (v) ya Mwongozo wa Wakala wa Barabara Tanzania wa Uendeshaji wa Mizani wa mwaka 2018, chini ya malengo ya udhibiti wa uzito wa magari, unaomtaka Wakala wa Barabara Nchini kupunguza msongamano unaosababishwa na malori mazito yanayokwenda polepole, na hivyo kuongeza ufanisi wa muda na gharama katika usafirishaji wa bidhaa zinazopita kuelekea nchi jirani.

492. Upungufu huu ulitokana na:

***Eneo la Mizani kuwa Upande Mmoja wa Barabara*** ; Nilibaini kuwa uwekaji wa miundombinu ya mizani ilichangia msongamano wa magari katika vituo kadhaa vya mizani. Hii ni kwa sababu mizani zilijengwa upande mmoja tu wa barabara, mkabala na upande wenye mzunguko mkubwa wa magari. Katika muktadha huu, mpangilio uliopo wa miundombinu ya mizani unazuia ugeuzaji wa magari, hasa wakati wa msongamano wa magari mengi. Hali hii inasababisha misururu mirefu ya magari yanayosubiri kupimwa.

***Kutumia Muda Mrefu Katika Upimaji wa Magari Kutokana na Kutokuwa na Mifumo inayojitosheleza;*** Kupitia uhakiki niliofanya kwenye mizani nilizotembelea, nilibaini kuwa mifumo ya uendeshaji inayotumika, ambayo ni T-Load, Smart Scale, na Tan-Weight, inahitaji uingizaji wa takwimu kwa mfumo wa karatasi kwa ajili ya taarifa muhimu za magari kama vile mpangilio wa ekseli za magari, maelezo ya dereva, na usajili wa mizigo, kabla ya zoezi la upimaji kukamilika. Hivyo basi, mchakato huo ulisababisha muda mrefu wa upimaji, misururu mirefu ya magari kwenye njia za kuingilia, na msongamano ndani ya eneo la kituo.

### 8.4.2 Usimamizi Usiojitosheleza wa Taratibu za Kisheria kwa Magari Yaliyozidisha Uzito

493. Nilibaini upungufu ufuatao katika utekelezaji wa taratibu za kisheria kwa magari yaliyokutwa na makosa:

**(a) Ufatiliaji Usioridhisha wa Tozo za Uharibifu wa Barabara Zilizofikia Shilingi bilioni 1.618**

494. Nilibaini kuwa magari yaliyotozwa faini kwa makosa ya kuzidisha uzito yaliruhusiwa kuendelea na safari bila kuzuiliwa. Hali hii ilisababisha malimbikizo ya tozo za kuzidisha uzito yaliyofikia Shilingi bilioni 1.618 kufikia tarehe 30 Septemba 2025. Utaratibu huu ni kinyume na Kanuni ya 13(1) ya Kanuni za Udhibiti wa Uzito wa Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki za Mwaka 2018. Kanuni hii inataka gari lililozidisha uzito kuzuiliwa hadi pale msafirishaji atakapolipa tozo za kuzidisha uzito.

495. Mapitio yangu ya Ripoti za Kila Mwezi za Mizani, nilibaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2025, jumla ya vyombo vyenye makosa 187 viliruhusiwa kuendelea na safari. Kati ya hivyo,163 viliruhusiwa bila kuwapo kwa makubaliano yoyote rasmi ya kulipa tozo za uharibifu wa barabara. Hali hii ilisababisha mrundikano wa tozo iliyofikia Shilingi bilioni 1.618.

496. Nilibaini kuwa kutolipwa kwa tozo hizi za uharibifu wa barabara kulitokana na:

- ***Mfumo Usio na Ufanisi wa Kumbukumbu na Usimamizi wa Takwimu***: Nilibaini kuwa si madeni yote yaliyoingizwa kwenye kumbukumbu za kila mwezi na za udhibiti wa mahesabu. Nilibaini hili wakati wa mapitio yangu ya kumbukumbu za risiti za mizani na ripoti za kila siku za mwaka 2025, kutoka vituo vitatu vya Luhimba, Mpemba na Msimba, ambapo malimbikizo

ya makosa yenye thamani ya shilingi milioni 41.557 hayakuingizwa wala kuripotiwa kwenye taarifa hizo.

- ***Ukusanyaji Usiojitosheleza wa Taarifa na Maelezo ya Magari katika Vituo vya Mizani;*** Nilibaini kutozingatiwa kwa taratibu zilizowekwa za upimaji katika vituo vya mizani vilivyotembelewa. Aidha, katika vituo 10 vya mizani vilivyokaguliwa, nilibaini kuwa kati ya magari/malori 70 yaliyokaguliwa, magari 18 yalipimwa bila kuhakiki taarifa za madereva na magari husika. Taarifa hizi ni muhimu kwa utekelezaji wa sheria kwani hutumika kama dhamana ya awali kwa magari yaliyotozwa faini ya kuzidisha uzito na hivyo kuwezesha uwajibikaji kwa magari yanayotoroka. Hii, kwa upande mwingine, hupunguza matukio ya tozo za uharibifu wa barabara kutolipwa au kukwepwa.

- ***Ukosefu wa Utaratibu Madhubuti wa Kufuatilia Ukusanyaji wa Malimbikizo ya Tozo za Uharibifu wa Barabara:*** Nilibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania anategemea zaidi kutoa notisi na barua za ukumbusho kwa wasafirishaji waliotenda makosa. Utaratibu huu haukuleta msukumo wa kisheria au uhakika wa malipo ya kiasi cha malimbikizo.

**(b) Udhibiti Usiojitosheleza wa Njia za Kukwepa Mizani na Njia za Mchepuko kutoka Vituo vya Mizani**

497. Mapitio yangu ya Ramani ya Mizani Toleo la Mei 2024, nilibaini kuwa usambazaji wa mizani katika mtandao wa barabara za kitaifa hautoshelezi, jambo linaloacha sehemu zingine za mtandao wa barabara bila ufuatiliaji na kuruhusu wasafirishaji kukwepa vituo vya mizani. **Jedwali Na. 28** linaonesha mtandao wa barabara wa kitaifa, ikijumuisha sehemu za barabara zisizofuatiliwa, zinazoweza kutumika kama njia za kukwepa, na michepuko ya mizani.

ISO 9001:2015 Certified

**Jedwali Na. 28: Uchambuzi wa Uwepo wa Michepuko na Njia za Kukwepa Mizani**

| Ukanda wa Barabara | Njia Zinazoweza Kutumika Kukwepa Mizani |
|---|---|
| Arusha – Sirari | • Kukwepa mizani kwa kutumia barabara za mikoa kupitia Manyara au Ziwa Natron<br>• Njia inayounganisha Arusha na Mpaka wa Kenya |
| Morogoro - Mbeya | • Umbali mrefu kati ya mizani moja na nyingine unaikadiriwa kwenye ukanda huu<br>• Njia ya Kilosa au za ndani za Iringa-Mafinga |
| Pwani ya Kusini | • Kuwapo kwa Maeneo mengi yanayoruhusu magari kukwepa mizani katika barabara ya Mtwara - Newala au Lindi – Ruangwa |
| Nyanda za Juu Kusini | • Njia inayounganisha Mbeya hadi Mpaka wa Malawi<br>• Kuwapo kwa Idadi kubwa ya Barabara za Mikoa zinazoruhusu magari kukwepa mizani<br>• Kijiji cha Ilunda – Kijiji cha Idofi (Inayounganisha Makambako - Njombe Njia Kuu na Makambako – Mafinga) |
| Songea - Tunduru | • Kukosekana kwa Mizani kwa ajili ya kudhibiti magari ya mizigo yanayopita mpaka wa Msumbiji<br>• Umbali mrefu kati ya mizani moja na nyingine unaokadiriwa kuwa km 260 |
| Kanda Ya Kati (Dodoma) | • Barabara ya Decca - Bango – Njia Nne<br>• Barabara ya Hospitali ya Manispaa- Sheli ya Kesi - Mnadani<br>• Sabasaba (mpaka Cho cha Uhasibu) – Sepuka – Kizaga - Singida - Malendi (Tabora ) - km 77+400<br>• Itigi (Mzunguko wa Itigi – Chaya Tabora) – Barabara ya Mbeya km 7+500 mpaka Mlongoji makutano kwenda Rungwa |

***Chanzo:* Uchambuzi wa Wakaguzi katika Ramani ya Mizani Toleo la Mei 2024, 2025**

498. **Jedwali Na. 28** linaonesha mtandao wa barabara za kitaifa ikijumuisha sehemu za barabara zisizofuatiliwa, ambazo zinaweza kutumika kama njia za kukwepa, na michepuko ya mizani. upungufu huu katika usambazaji wa mizani unatoa mwanya kwa magari yaliyozidisha uzito kukwepa vituo vya mizani kupitia barabara zisizofuatiliwa.

499. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, nilibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania, kupitia Mpango Mkakati wake wa Mwaka wa Fedha 2021/22–2025/26, chini la Lengo C, alipanga kujenga angalau mizani mipya 13 kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25. Hata hivyo, nilibaini kuwa kufikia Mwaka wa Fedha 2024/25, ni vituo vya mizani 6 kati ya 13 vilivyopangwa ndivyo vilivyojengwa. Hali hii inaashiria udhibiti mdogo wa njia zinazoweza kutumika kukwepa mizani. Kutokana na hali hiyo, magari yaliyozidisha uzito yana uwezekano mkubwa wa kusababisha uchakavu wa kupitiliza na uharibifu wa haraka wa lami katika mitandao hii ya barabara isiyofuatiliwa.

500. Nilibaini kuwa changamoto hii ilitokana na kutowapo kwa Mpango Kabambe wa Mizani wa Taifa ambao ungeweza kuainisha umbali bora wa uwekaji mizani kulingana na mifumo ya barabara na vihatarishi vilivyopo.

### 8.4.3 Ukarabati na Uhakiki Usiyojitosheleza wa Mitambo ya Mizani ili Kuhakikisha Usahihi Katika Upimaji wa Uzito

501. Nilibaini changamoto zifuatazo katika ukarabati na uhakiki wa Mitambo ya Mizani:

(a) **Kutokufuatwa kwa Mipango ya Ukarabati wa Kinga**

502. Mapitio yangu ya nyaraka za ukarabati wa mizani na vyeti vya usahihi kwa mizani zilizotembelewa nilibaini kuwa Wakala wa Barabara Tanzania haukuandaa mipango ya mara kwa mara ya ukarabati kinga na uhakiki. Kulikuwa na mpango wa uhakiki wa kila baada ya miezi mitatu tu kwa ajili ya mizani zisizohamishika au baada ya matengenezo makubwa, kulingana na aya ya 4.1 ya Mwongozo wa Uendeshaji wa Mizani wa Wakala wa Barabara Tanzania wa mwaka 2018.

503. Hii ili maanisha kuwa wakala alikosa mfumo rasmi wa kuratibu, kufuatilia, na kuweka kumbukumbu za shughuli za ukarabati wa kawaida na uhakiki wa mizani, zikiwemo mizani zisizohamishika, na zile zinazohamishika.

504. Kutokana na hali hiyo, ukarabati wa miundombinu ya mizani ulifanyika tu baada ya kutokea kwa hitilafu kubwa, badala ya kufanyika kupitia mpango madhubuti wa ukarabati wa kinga. Utaratibu huu ni kinyume na aya ya 4.6 ya Mwongozo wa Uendeshaji wa Mizani wa Mwaka 2018 wa Wakala wa Barabara Tanzania, inayopendekeza ukarabati wa kawaida na ukaguzi kufanyika angalau mara moja kwa wiki.

505. Kukosekana kwa ukarabati wa kinga kulisababisha kuharibika kwa mitambo kusikotarajiwa, jambo ambalo lilikwamisha shughuli za mizani kutokana na matengenezo makubwa. **Jedwali Na. 29** linatoa maelezo ya ukarabati wa dharura uliofanyika katika mizani zilizochaguliwa.

**Jedwali Na. 29: Idadi ya Matengenezo ya Dharura katika Mizani Zilizochaguliwa**

| Mkoa | Jina la Mizani | Idadi ya Matengenezo | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | |
| Dar es Salaam | Kurasini | 2 | 3 | 1 | 5 | 11 |
| Pwani | Vigwaza | - | 4 | 12 | 8 | 24 |
| Lindi | Mingoyo | - | 2 | 5 | 4 | 11 |
| Tanga | Horohoro | 4 | 5 | 4 | 6 | 19 |
| Arusha | Kimokouwa | - | 10 | 16 | 8 | 34 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi Katika Ripoti za Mwezi za Mizani Kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25

506. **Jedwali Na. 29** linaonesha kuwa mizani za Vigwaza, Kimokouwa, na Horohoro ilirekodi kiwango cha juu cha matengenezo 6 hadi 16 kila mwaka, ambayo ni sawa na idadi ya hitilafu zilizotokea. Uharibifu huu husababisha msongamano wa magari na kupunguza ufanisi wa mizani.

### (b) Kutokuwapo kwa Uhakiki na Uidhinishaji wa Mitambo ya Mizani

507. Wakati wa mahojiano yangu na maafisa wa Wakala wa Barabara Tanzania katika vituo vya mizani vilivyotembelewa, nilibaini kuwa Wakala wa Barabara Nchini hakuhakikisha kuwa vifaa vya mizani vinafanyiwa uhakiki na kuidhinishwa ufanisi wake kabla ya kufungwa. Mitambo ya mizani ilikosa nyaraka za uhakiki na uidhinishaji katika vituo vyote 10 vya mizani vilivyotembelewa.

NATIONAL AUDIT OFFICE ISO 9001:2015 Certified

508. Aidha, utaratibu huu ulikuwa kinyume na Kifungu cha 4 (1) (b) cha Sheria ya Viwango, Sura Na. 130. Kifungu hicho kinaelekeza kuwa mitambo ya majaribio na uhakiki wa vifaa vya usahihi, vipimo, na zana za kisayansi, kwa ajili ya kubaini usahihi wake kwa kulinganisha na viwango husika, lazima iidhinishwe na Waziri wa Viwanda na Biashara kulingana na mapendekezo ya Bodi ya Wakurugenzi, na hii ndiyo huamua pia utoaji wa vyeti.

509. Licha ya kutowapo kwa uhakiki wa ufanisi na uidhinishaji wa vifaa vya mizani, nilibaini kuwa hakukuwa na taratibu maalumu kwa ajili kuwezesha uthibitishaji wa ubora wa vifaa kabla ya kufungwa. Hii iliashiria kuwa wakati wa matengenezo, Wakala wa Barabara, alitegemea zaidi maelezo ya vifaa kutoka kwa wazabuni badala ya uzingatiaji wa uidhinishaji wa Shirika la Viwango Tanzania.

510. Hali hii ilihatarisha muda wa kudumu wa vifaa vilivyofungwa, jambo ambalo liliathiri utendaji wa mizani kutokana na kuharibika mara kwa mara, kama ilivyoainishwa.

### 8.4.4 Uratibu, Ufuatiliaji na Mikakati ya Tathmini Isiotosheleza katika Uendeshaji wa Mizani

511. Nilibaini kutowapo kwa uratibu wa katika usimamizi wa udhibiti wa uzito wa magari kati ya Wizara ya Ujenzi na mamlaka zingine za udhibiti, vikiwemo Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Shirika la Viwango Tanzania, Jeshi la Polisi na Wizara ya Uchukuzi. Aidha, kati ya miaka ya fedha ya 2021/22 na 2024/25, Wizara ya Ujenzi ilifanya mikutano miwili tu ya kisekta, na hakuna hata mmoja uliojadili maswala ya udhibiti wa uzito wa magari.

512. Hali hii ilikuwa kinyume na aya ya 2.5.5 ya Mpango Mkakati wa Wizara ya Ujenzi wa Mwaka wa Fedha 2021/22–2025/26, unaoitaka Wizara kuimarisha uratibu miongoni mwa wizara na taasisi kupitia mipango ya kisekta.

513. Uratibu huu usio na ufanisi ulitokana na kutowapo kwa mwongozo wa wazi wa usimamizi na uratibu wa kisheria ili kuongoza ushirikiano wa taasisi mbalimbali katika udhibiti wa uzito wa magari. Vile vile, hakukuwa na miongozo rasmi, au mipango ya kitaasisi iliyoainisha kwa uwazi majukumu, wajibu, taratibu za utoaji taarifa, au mifumo ya uwajibikaji miongoni mwa wadau wakuu, yaani Wizara ya Ujenzi, Wakala wa Barabara Tanzania, na mamlaka zingine za udhibiti.

514. Kutokana na hali hiyo, juhudi za usimamizi wa sheria haukuratibiwa vizuri, usambazaji wa taarifa ulikuwa mdogo, na utumiaji wa kanuni za uzito wa magari haukuwa thabiti miongoni mwa wadau, jambo ambalo lilidhoofisha ufanisi wa jumla wa shughuli za udhibiti uzito wa Magari.

515. Aidha, kutokana na uratibu usiojitosheleza, nilibaini kuwapo kwa magari yenye muundo ambao hautambuliwi katika Kanuni za Udhibiti wa Uzito wa Magari za Jumuiya ya Afrika Mashariki za mwaka 2018. Kanuni hizi zinatoa maelezo ya mipangilio yote ya magari inayoruhusiwa pamoja na uzito wa ekseli na ukomo wa uzito wa jumla wa gari unaokubalika.

516. Kwa kuwa mifumo ya uendeshaji wa mizani imesanifiwa kulingana na aina za magari zilizoorodheshwa kwenye Mwongozo wa Uendeshaji wa Mizani na Sheria za Afrika Mashariki pekee, magari haya hayawezi kupimwa katika vituo vya Mizani, kwa kuwa ukomo wao unaoruhusiwa haujulikani na haujaainishwa katika Mwongozo wa Uendeshaji wa Mizani.

## 8.5 Matokeo ya Ukaguzi Katika Usimamizi wa Huduma za Usafiri Mijini katika Majiji Makubwa

517. Katika tathmini yangu ya huduma za usafiri wa mijini katika majiji makubwa, nilibaini kuwa uhakika wa huduma hizo uliathiriwa na kuenea kwa shughuli zisizo rasmi ambazo hazikuwa na ratiba maalumu wala viwango vya huduma vinavyodhibitiwa. Watumiaji mara nyingi walikumbana na muda wa kusubiri usiotabirika na hali mbaya ya vyombo vya usafiri. Aidha, nilibaini upungufu katika upangaji wa huduma za usafiri mijini, na usimamizi wa mfumo wa mabasi yaendayo haraka kama ilivyofafanuliwa hapa chini:

### 8.5.1 Upangaji na Udhibiti Usioridhisha wa Huduma za Usafiri wa Umma Mijini

518. Nilibaini yafuatayo katika Upangaji na Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Umma Mijini.

#### (a) Ukuaji Mdogo wa Usafiri Rasmi wa Umma na Kuongezeka kwa Utegemezi wa Vyombo vya Usafiri Vyenye Uwezo Mdogo

519. Nilibaini kuwa, mfumo wa utoaji leseni na udhibiti wa watoa huduma umekuwa ukivutia watoa huduma wasio rasmi wa usafiri wa mijini. Aidha, nilibaini kuwa, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, imekuwa ikitoa leseni kwa watoa huduma za usafiri wa mijini wanaotumia vyombo vyenye uwezo mdogo wa kubeba abiria vikiwemo bajaji na pikipiki kinyume na Aya 5.7.2.2 ya Sera ya Taifa ya Usafirishaji ya Mwaka 2003 inayohimiza usafiri wa umma wa watu wengi kwa kutilia mkazo uingizaji na utoaji wa leseni kwa magari ya abiria yenye uwezo mkubwa kuanzia abiria 30 kwa mabasi madogo hadi abiria 90 kwa mabasi makubwa.

520. Uchambuzi wa Taarifa za Leseni za Usafirishaji kwa robo ya nne, ukijumuisha miaka ya fedha 2020/21 hadi 2024/25 ulionesha kuwa usafiri wa umma wa watu wengi haukusajiliwa wala kupewa leseni. Hata hivyo, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini imekuwa ikitoa leseni kwa watoa huduma za usafiri wa umma wenye vyombo vyenye uwezo mdogo, jambo lililosababisha ongezeko kubwa la asilimia 95 kufikia Mwaka wa Fedha 2024/25.Kati ya Mwaka wa Fedha 2020/21 na 2024/25, usajili wa pikipiki uliongezeka kwa asilimia 145 kutoka 18,408 hadi 45,078, na kuzifanya kuwa aina ya usafiri wa mijini uliyopewa leseni zaidi.

521. Kinyume chake, vyombo vyenye uwezo mkubwa wa kubeba abiria kwa ajili ya usafiri wa umma vilipungua. Aidha, Magari ya huduma ya huduma za

jamii yalipungua kwa asilimia 55, mabasi ya daladala kwa asilimia 19, na mifumo ya usafiri wa watu wengi, kama vile huduma za usafiri wa mabasi yaendayo haraka ilishuka hadi asilimia sifuri, ikiashiria uwekezaji mdogo na usaidizi usioridhisha wa kitaasisi.

522. Nilibaini kuwa hali hii ilitokana na upangaji na uratibu usiojitosheleza miongoni mwa Mamlaka za Udhibiti wa Usafiri na kukosekana kwa mikakati jumuishi ya usafiri wa mijini ili kuwezesha uhimizaji na uboreshaji huduma rasmi za umma. Matokeo yake, miji mikubwa inakabiliwa na hali mbaya ya mchanganyiko wa magari barabarani, inayosababisha msongamano mkubwa wa magari, muda mrefu wa kusafiri na ongezeko la ajali za barabarani, ambavyo huwa vinaathiri upatikanaji wa usafiri bora na salama mijini.

### (b) Mipango Kabambe ya Miji Mikubwa Kutokuendana na Mpango Kabambe wa Taifa wa Usafiri

523. Mapitio yangu ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Usafiri (2020/21–2024/25) katika majiji ya Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, na Mwanza yalibaini ucheleweshaji wa mara kwa mara, usimamizi usioridhisha, ukosefu wa utengamano na utekelezaji usioridhisha wa hatua zilizopangwa. Juhudi muhimu ikiwemo upanuzi wa miundombinu ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam, kuwapo kwa njia maalum za usafiri wa umma, kuwapo kwa vituo vikuu vya usafiri vinavyounganisha njia mbalimbali, mipango ya kupunguza msongamano, na uunganishaji wa mfumo wa barabara na vivuko, hazikutekelezwa kikamilifu. Hali hii ilikuwa kinyume na matakwa ya aya ya 2.3 na 2.4 ya Sera ya Taifa ya Usafirishaji ya mwaka 2003, inayotaka mipango kabambe ya usafiri wa mijini iwiane na mikakati ya kitaifa ya usafiri ili kuhakikisha mifumo jumuishi, yenye ufanisi na endelevu. Pia, inatoa wito wa kuendeleza mifumo ya usafiri wa aina mbalimbali, ikiwa na taratibu za wazi za utekelezaji katika ngazi ya jiji. **Jedwali Na. 30** linatoa uchambuzi wa kina wa mpango kabambe wa usafiri katika miji mikubwa iliyotembelewa.

**Jedwali Na. 30: Uchambuzi wa Kina wa Mipango Kabambe ya Usafirishaji Katika Miji Mikubwa**

| Mikoa | Tathmini ya Jumla (2020/21-2024/25) | Athari za Changamoto |
|---|---|---|
| Dar es Salaam | Utekelezaji wa mpango haukuwa thabiti, ukikumbwa na changamoto kama vile ucheleweshaji wa Awamu ya II ya Miundombinu ya Magari yaendayo haraka, uunganishaji mdogo wa miundombinu ya aina mbalimbali za usafirishaji, ujumuishaji mdogo wa barabara za kutoka na kuingia kwenye njia kuu. | Kuendelea kuwapo kwa foleni ambayo inaathiri ufikivu wa huduma za usafiri mjini, pamoja na muunganiko mdogo wa njia za usafiri zinazopatikana katika jiji la Dar es Salaam, na kutofikiwa kwa malengo ya ufanisi. |

| Mikoa | Tathmini ya Jumla (2020/21-2024/25) | Athari za Changamoto |
|---|---|---|
| Mbeya | Malengo muhimu kama vile kuwapo kwa njia maalum za usafiri wa umma, Miundombinu inayounganisha aina mbalimbali za usafiri, na kuhakikisha utendaji kazi wa mpango kabambe wa usafiri, yalicheleweshwa na mengine kutotekelezwa kabisa, huku kukiwa na ushiriki mdogo wa wadau wa huduma ya usafiri. | Kuendelea kuwapo kwa ufanini mdogo wa huduma ya usafiri wa umma, msongamano vya vyombo vya usafiri mijini na kutowapo kwa uratibu wa kimkakati. |
| Arusha | Uhuishaji wa Mpango Kabambe wa usafirishaji na mpango wa kuondoa msongamano ulichelewa. Pia, uzingitiaji wa mahitaji ya wasioa tumia vyombo vya moto ulikuwa mdogo. | Ongezeko la msongamano, kuenea kwa watoa huduma ya usafiri wasio rasmi. |
| Mwanza | Uunganishaji wa barabara na vivuko, upangaji wa njia, na uboreshaji wa vituo vilikabiliwa na ucheleweshaji au usimamizi usioridhdisha; Mipango wa awali ya huduma ya usafiri wa mabasi yendayo haraka na mipango jumuishi ilichelewa kutekelezwa. | Muunganiko mdogo na huduma za usafiri zisizotabirika. |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi Katika Mpango wa Usafirishaji wa Mwaka 2020/21 – 2025/26, 2025

524. **Jedwali Na. 30** linaonesha upungufu katika utekelezaji wa mipango kabambe ya usafiri katika miji mikubwa minne. Upungufu huu unajumuisha miradi ambayo haijatekelezwa kama vile njia maalumu za usafiri wa umma, muunganisho wa mifumo ya usafiri, pamoja na ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi iliyopangwa, kama vile kuunganisha barabara na kivuko jijini Mwanza na utekelezaji wa Mradi wa Mabasi yaendayo haraka awamu ya pili jijini Dar es Salaam.

525. Upungufu huu ulitokana na kutotafsiriwa ipasavyo kwa Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya Mwaka 2003 na Mipango ya Taifa ya Usafiri kuwa mipango inayotekelezeka katika ngazi ya miji, pamoja na kutoingizwa kwa vipaumbele katika hatua za mipango mikuu.

526. Kukosekana kwa uwiano huo kulisababisha msongamano wa kudumu, upatikanaji mdogo na kuongezeka kwa huduma zisizo rasmi za usafiri, hali ambayo ilidhoofisha ufikiaji wa malengo ya kitaifa ya usafiri na kuongeza ukosefu wa ufanisi katika kudhibiti msongamano wa magari mijini.

### 8.5.2 Kutoridhisha kwa Upatikanaji wa Huduma za Usafiri wa Umma wenye Uhakika na Gharama Nafuu

527. Nilibaini kuwa, huduma za usafiri katika miji mikubwa hazikidhi mahitaji ya idadi ya watu inayoongezeka, huku kukiwa na changamoto kubwa katika upatikanaji wa usafiri wa uhakika na gharama nafuu kama ilivyofafanuliwa hapa chini:

**(a) Kutozingatia kwa Upatikanaji na Ujumuishi wa Huduma za Usafiri Mijini**

528. Nilibaini kuwa misingi ya usanifu jumuishi haikuingizwa kwa utaratibu maalumu katika michakato ya upangaji na uandaaji wa bajeti za usafiri mijini. Mathalani, kulikuwa na ushirikishaji mdogo wa mashirika yanayowakilisha watu wenye mahitaji maalumu na makundi maalumu wakati wa hatua za usanifu, utekelezaji na tathmini ya Miradi.

529. Katika Jiji la Dar es Salaam, vituo vya treni za abiria na stendi za mabasi kwa usafiri wa mjini vilikosa miundombinu maalumu kama vile miundombinu ya watu wenye mahitaji maalumu maalumu , njia za watembea kwa miguu, na vivuko. Aidha, kulikuwa na changamoto katika miundombinu ya mwanga, alama kwa ajili ya wenye ulemavu wa macho, na majukwaa kwa ajili ya kuwezesha upakiaji au ushushaji wa abiria, hali inayovifanya vituo hivyo kutowa rafiki kwa watumiaji walio na mahitaji maalumu.

ISO 9001:2015 Certified

530. Vilevile, mapitio yangu ya mipango ya miji yalionesha kuwa, misingi ya usanifu jumuishi haukuzingatiwa katika uandaaji wa mipango na bajeti kwa ajili ya huduma za usafiri wa mijini, kwa Wizara ya Uchukuzi, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini na OWM - TAMISEMI pamoja na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Nilibaini changamoto hizi wakati nilipotembelea miji iliyochaguliwa wakati wa ukaguzi, ambapo niliona kuwa treni za mjini za abiria na daladala hazikuwa na miundombinu kama vile njia za walemavu, viti maalumu vya kukalia walemavu na mfumo wa matangazo ya sauti. Kukosekana kwa miundombinu hiyo kuliathiri uwezekano wa ufikiaji wa huduma za usafiri mijini kwa watu wenye mahitaji maalumu, kama vile walemavu, wazee na abiria wengine wasiojiweza.

531. Hali hii ilisababishwa na michakato ya usajili na utoaji leseni kwa vyombo wa usafiri, inayosimamiwa na Mamlaka za Udhibiti Usafiri wa Ardhini na Mamlaka ya Mapato Tanzania, ambazo zilifanya usajili wa magari na leseni za uendeshaji bila kuzingatia ipasavyo kuwapo kwa miundombinu kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalumu katika magari yanayosajiliwa. Matokeo yake, jambo hili limezuia uwezo wa kutembea kwa watu wenye ulemavu, wazee,

wanawake, na watoto; hali iliyochangia kuendelea kutengwa kijamii na kuzuia fursa za kiuchumi, huduma za afya, na elimu kwa makundi yaliyotengwa.

**(b) Upatikanaji Usiojitosheleza wa Huduma za Usafiri katika Maeneo ya Pembezoni mwa Mji**

532. Nilibaini kuwa huduma za usafiri zilijikita zaidi katikati mwa jiji, bila kuzingatia mahitaji ya wakazi wanaoishi pembezoni, na hivyo kusababisha huduma finyu na kupungua kwa upatikanaji wa huduma za usafiri kwa jamii za maeneo ya pembezoni.

533. Kupitia mapitio yangu ya Ripoti za Mwaka za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, kumbukumbu za vikao vya Bodi na Taarifa kutoka kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Barabara na Reli kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25, nilibaini kuwa, kulikuwa na tabia ya baadhi ya watoa huduma kufupisha au kubadilisha njia kinyume cha taratibu, kwa kuyapa kipaumbele maeneo yenye wasafiri wengi huku wakiyaacha maeneo ya pembezoni mwa mji. **Jwedwali Na. 31** linaonesha idadi ya kesi zilizorekodiwa za watoa huduma kubadilisha njia.

**Jedwali Na. 31: Idadi ya Kesi za Watoa Huduma Waliokamatwa Wakiwa Wamebadili Njia Walizosajiliwa Kutoa Huduma**

| Jiji/ Mwaka wa Fedha | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mbeya Jiji | 0 | 18 | 24 | 25 | 6 | 73 |
| Dar es Salaam | 0 | 7 | 1 | 0 | 46 | 54 |
| Mwanza Jiji | 2 | 3 | 83 | 187 | 401 | 676 |
| Arusha Jiji | 0 | 4 | 11 | 25 | 51 | 91 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi Katika Mlalamiko ya Wasafiri 2020/21-2024/25, 2025

534. **Jedwali Na. 31** Linaonesha kuwa Jiji la Mwanza lilikumbwa na ongezeko la kesi za kufupisha au kubadilisha njia, kutoka kesi 2 kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 401 kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, hivyo kufanya jumla ya kesi kuwa 676. Aidha, Jiji la Arusha lilikuwa na jumla ya kesi 91, ikifuatiwa na Mbeya, kesi 73 na Dar es Salaam yenye jumla ya kesi 54 kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25. Tatizo hili, lilisababishwa na tabia ya watoa huduma kutaka kuongeza mapato, kwa kuangalia maeneo yenye wasafiri wengi hivyo huathiri upatikanaji wa huduma ya usafiri katika maeneo ya pembezoni.

**(c) Usimamizi Usiojitosheleza wa Kanuni za Nauli**

535. Nilibaini kuwa udhibiti wa nauli zilizoidhinishwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, katika majiji yote yaliyokaguliwa ulikuwa haujitoshelezi. Mabasi

ya abiria hutoza nauli mara kwa mara zaidi ya viwango vilivyoidhinishwa. Ukiukwaji huu ulijitokeza katika kipindi chote cha Mwaka wa Fedha wa 2022/2023–2023/24. Aidha, ukiukaji wa nauli ulikuwa umeenea hasa katika maeneo yenye uhitaji mkubwa, kama vile katikati mwa jiji na muda wenye wasafiri wengi.

536. Hii ilichangiwa na ufuatiliaji usiojitosheleza ili kubaini watoa huduma ambao wanatoza nauli bila ya kuzingatia kiwango kilichoidhinishwa, kama nilivyobaini kuwa ufuatiliaji uliokuwa unafanyika ulikuwa wa baada ya matukio. Pia, changamoto hii ilichangiwa na ushirikiano mdogo kati ya Mamlaka ya Udhibiti na Askari wa Usalama Barabarani ili kuhakikisha wanaokiuka taratibu zilizowekwa wanashughulikiwa. Kwa pamoja, mambo haya yalisababisha utekelezwaji usio thabiti na kuondoa imani ya umma katika udhibiti wa nauli.

537. Hii ilikuwa ni kinyume na matakwa ya Kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu ya Mwaka 2019, kinachoitaka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini kusimamia nauli katika sekta ya usafirishaji ili kuhakikisha haki, unafuu na uendelevu wa kiuchumi.

**(d) Mgawanyiko Kati ya Maendeleo ya Miundombinu ya Usafiri na Mwenendo wa Ukuaji wa Miji**

538. Nilibaini kuwa miundombinu ya usafiri iliyopo haikusaidia kikamilifu ukuaji wa/au mahitaji ya kiteknolojia mpya yanayoweza kutokea katika sekta ya usafirishaji. Aidha, upanuzi na uboreshaji wa miundombinu haukufanyika kikamilifu, ili kuendana na kasi ya ukuaji wa mji, ongezeko wa umiliki wa vyombo vya usafiri, na ongezeko la matumizi ya mifumo ya TEHAMA.

539. Hii ilikuwa kinyume na matakwa ya Sera ya Taifa ya Uchukuzi (2003), Mpango Mkakati wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (2021–2025), na Malengo ya Maendeleo Endelevu, Lengo Namba 11, ambayo kwa pamoja yanaweka kigezo kwamba miundombinu ya usafiri inapaswa kuendelezwa sanjari na upanuzi wa miji, ukuaji wa idadi ya watu, na maendeleo ya kiteknolojia ili kuhakikisha usalama, na kufikika kwake.

540. Mapitio yangu ya ya Taarifa ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardthini ya Utendaji Katika Sekta ya Uchukuzi ya Mwaka 2023, nilibainii kuwa ukuaji mkubwa wa mji katika jiji la Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya haukulingana na uwekezaji katika miundombinu ya usafiri. Kwa mfano, kati ya Mwaka wa Fedha 2020 na 2023, eneo la majiji haya liliongezeka kwa asilimia 27 wakati ongezeko la miundombinu mipya ya barabara za mjini lilikuwa ni 8.5. **Jedwali Na. 32** linatoa ulinganisho wa ukuaji wa jiji dhidi ya upanuzi wa

miundombinu ya usafiri kwa mwaka 2020 hadi 2025, likionesha zaidi pengo lililopo la miundombinu.

**Jedwali Na. 32: Ulinganisho Kati ya Ukuaji wa Jiji na Utanuzi wa Miundombinu ya Usafirishaji**

| Jiji | Ukuaji wa Jiji (%) | Ukuaji wa Miundombinu (%) | Uwiano Kati ya Ukubwa wa Eneo na Urefu wa Barabara ($km^2$/km) |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 21 | - | - |
| Arusha | 25.8 | 8.1 | 4.3 $km^2$/km |
| Mbeya | 24.2 | 7.3 | 4.9 $km^2$/km |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi Katika Taarifa ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Juu ya Utendaji Katika Sekta ya Usafirishaji ya Mwaka 2023, 2025

541. **Jedwali Na. 32** linaonesha kwamba wakati miji inapanuka kwa viwango cha asilimia 21, 25.8 na 24.2, kwa Miji ya Dar es Salaam, Arusha, na Mbeya mtawalia, maendeleo ya miundombinu hayakuendana na kasi ya ukuaji wa miji hiyo. Kiwango cha ukuaji wa miundombinu kilikuwa kwa asilimia 8.1 kwa Arusha na asilimia 7.3 kwa Mbeya, huku kiwango cha ukuaji wa Miundombinu kwa Dar es Salaam kikiwa hakijabainishwa. Kwa kuzingatia uwiano uliopo kati ya ukubwa wa eneo na urefu wa barabara ambao ni 4.3 $km^2$/km na 4.9 $km^2$/km kwa Arusha na Mbeya mtawalia, kiwango cha ufikiwaji wa usafiri kiko chini sana kulinganisha na kiwango pendekezwa cha kilomita za mraba 1.5 hadi 2 kwa kila kilomita 1 ya barabara katika maeneo ya miji yenye watu wengi (Viwango vya Ufikiaji vya Benki ya Dunia vya Mwaka 2015). Pengo hili linaonesha uratibu na uwekezaji usiojitosheleza katika miundombinu ya usafiri.

542. Pia, hali hii iliyonesha utanuzi usiojitosheleza wa miundombinu, hasa katika barabara za kuwezesha kufikia huduma ya usafiri, na uboreshaji wa vituo vya usafiri. Upungufu huu ulionekana hasa katika maeneo ya pembezoni mwa miji, ambapo msongamano wa watu ulikuwa unazidi watu 5,000 kwa kilomita moja ya mraba, lakini barabara ilibaki kuwa chini ya kilomita moja kwa eneo la kilometa za mraba 2.5.

543. Sababu kuu ya changamoto hizi katika ukuaji wa miundombinu ilikuwa ni kutowapo kwa mipango jumuishi ya miji, ambapo nilibaini kuwa Wakala wa Udhibiti Usafiri Ardhini, mamlaka za serikali za mitaa, na Wakala wa Barabara Tanzania na Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini hazikushirikiana kikamilifu katika utekelezaji wa miradi ya mindombinu. Mgawanyiko huu unasababisha kutofanyika kikamilifu kwa uboreshaji wa miundombinu ya usafiri katika miji.

544. Aidha, changamoto hizi zilisababisha, usafiri wa umma kuendelea kukabiliwa na msongamano, na ufikiaji mdogo katika maeneo mapya ya miji.

Hii ilisababisha muda mrefu wa safari, gharama kubwa za usafiri, na matumizi ya huduma za usafiri zisizo rasmi.

### 8.5.3 Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Mrejesho Usiojitosheleza wa Wizara Husika

545. Nilibaini kuwa huduma za usafiri wa Mijini zimekuwa hazijitoshelezi kutokana na uzingatiaji mdogo wa ratiba, upatikanaji mdogo wa magari, uendeshaji usio salama na huduma zisizoridhisha kwa wateja. Masuala haya yalichangiwa na upungufu katika ufuatiliaji wa huduma kama yalivyoelezwa hapa chini.

#### (a) Kutokuwapo kwa Ufuatiliaji na Tathmini ya Huduma za Usafiri wa Mijini Unaofanywa na Wizara ya Uchukuzi na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI

546. Nilibaini kuwa Wizara ya Uchukuzi na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI hawakufanya tathmini za mara kwa mara katika mamlaka za serikali za mitaa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini juu ya utoaji wa huduma za usafiri mjini. Hii ilikuwa kinyume na matakwa ya Aya ya 6.1 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ambao unazitaka wizara kufanya tathmini za mara kwa mara, ya matokeo ya huduma za usafiri zinazoratibiwa na mamlaka za serikali za mitaa, na Vyombo vya Udhibiti kama vile Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini ili kuwezesha uboreshaji wa huduma na kuhakikisha uwajibikaji.

547. Ufuatiliaji na tathmini isiyojitosheleza katika huduma za usafiri mjini ulisababishwa na ukosefu wa mipango wa wazi na ratiba ya ufautiliaji na tathmini kuwezesha utaratibu wa kufanya ufuatiliaji na tathmini.

548. Kutokana na hali hiyo, usimamizi wa huduma za usafiri mijini ulikabiliwa na changamoto, ikiwa pamoja na ufanisi mdogo wa huduma, na kutojitosheleza kwa viwango vya huduma inayotolewa. Ukosefu wa tathmini za mara kwa mara ulidhoofisha uwajibikaji na kupunguza uwezo wa wizara kutambua upungufu na kuendeleza uboreshaji wa huduma ya usafiri mijini.

#### (b) Kukosekana kwa Mfumo Jumuishi wa Taarifa ili Kuwezesha Ufuatiliaji Wenye Ufanisi

549. Nilibaini kuwa, kufikia Septemba 2025, hakukuwa na mfumo jumuishi wa usimamizi wa taarifa za huduma za usafiri wa mijini, ikiwa pamoja na huduma za usafiri wa mwendokasi na huduma ya usafiri wa treni za mjini. Aidha, takwimu za abiria, mapato, kumbukumbu za usalama, utendaji wa huduma, na maoni ya wateja, zilikuwa zikikusanywa kwa muundo uliogawanyika kupitia

taasisi mbalimbali kama vile Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri, Kitengo cha Usalama Barabarani, mamlaka za serikali za mitaa, na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni, bila ya kuoanisha au kuunganisha mifumo yao ya taarifa.

550. Hii ilikuwa kinyume na Aya ya 4.2.3 ya Sera ya Taifa ya Uchukuzi, 2003, ambayo inazitaka wakala za usafirishaji kuanzisha mifumo jumuishi ya usimamizi wa taarifa. Pia, inasisitiza kuwapo kwa Taarifa za kuaminika, na zinazoweza kufikiwa ili kuwezesha uandaaji wa mipango, udhibiti na utoaji taarifa juu ya utendaji katika huduma za usafiri mjini.

551. Kutokuwapo kwa mfumo jumuishi kulichangiwa hasa na uratibu usiojitosheleza, uwekezaji mdogo katika miundombinu inayotumia TEHAMA na uwezo mdogo wa kiufundi wa kutekeleza itifaki za kusambaza taarifa.

552. Changamoto hii ilisababisha taarifa za utendaji katika utoaji wa huduma za usafiri kutolingana na kutokuwa za uhakika, na hivyo kudhoofisha uandaaji wa mipango bora na ufanyaji maamuzi. Pia, ilichelewesha uwezekano wa kubaini maeneo yenye changamoto katika utoaji wa huduma za usafiri kama vile waendeshaji wa chini, maeneo yenye ajali, na uzembe katika uendeshaji. Zaidi ya hayo, ilileta hatari ya rasilimali kupotea kupitia juhudi zilizorudiwa za ukusanyaji wa taarifa.

### 8.5.4 Upangaji na Uendeshaji Usiojitosheleza wa Mfumo wa Usafiri wa Mabasi ya Mwendokasi

NAOT ISO 9001:2015 Certified

553. Nilibaini changamoto zinazoathiri ufanisi katika usimamizi wa huduma ya mabasi ya mwendokasi, kama ilivyoelezwa hapa chini:


#### (a) Uungwanishaji Usiojitosheleza wa Huduma ya Mwendokasi na Huduma Nyingine za Usafiri

554. Kupitia uhakiki niliofanya kwenye utoaji wa huduma za usafiri mjini, nilibaini kuwa njia za usafiri katika jiji la Dar es Salaam, ikiwa pamoja na vituo vya usafiri wa mwendokasi, hazikuunganishwa kikamilifu au kuratibiwa na huduma zingine za usafiri. Kwa mfano, huduma za Usafiri wa Vivuko hazikuoanishwa kikamilifu na huduma za usafiri wa mwendokasi. Wakati huo huo, sehemu za kupakia na kushushia abiria kwa daladala na pikipiki mara nyingi hazikuunganishwa kikamilifu na huduma za usafiri wa mwendokasi. Zaidi ya hayo, kadi za kielektroniki zilizokuwa zinatumika katika usafiri wa mwendokasi haikuunganishwa na huduma zingine za usafiri.

555. Hii ilikuwa kinyume na matakwa ya aya ya 3.2.3 ya Sera ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya Mwaka 2009, ambayo inaeleza kuwa miundombinu ya usafiri wa mijini lazima ijumuishe aina zote za usafiri zinazotumika, Pia, iratibiwe na iwe rafiki kwa mtumiaji kwa kumwezesha kuhama kutoka aina moja ya usafiri kwenda nyingine bila vikwazo na kuimarisha ufanisi wa mtandao wa usafiri.

556. Aidha, changamoto hii ilisababisha msongamano na kuchelewa kwa wasafiri. **Kielelezo Na.36** Kinaonesha muda uliotumiwa na abiria katika kusubiri mabasi ya mwedokasi na muda unaotumika kusafiri hadi mwisho wa safari.

**Kielelezo Na. 36: Muda Uliotumiwa Kusuburia Usafiri wa Mabasi ya Mwendokasi Katika Kuchukua Abiria na Muda Yanaotumia Kufika Mwisho wa Safari**




***Chanzo:*** **Uchambuzi wa Wakaguzi Katika Taarifa za Wakala wa Babasi Yaendayo Haraka**, 2025

557. **Kielelezo Na. 36** kinaonesha changamoto katika uendeshaji wa huduma ya mabasi ya mwendokasi ikiwa pamoja na abiria kusubiri usafiri kwa muda mrefu na kutumia muda mrefu wa kusafiri kwenye njia kuu kama vile Kimara-Gerezani na Mbezi Luis-Muhimbili. Hii inaashiria hitaji la kuboreshwa kwa ratiba ya basi, na udhibiti wa huduma ili kuimarisha upatikanaji wa huduma.

558. Hii ilikuwa kinyume na aya ya 2.4.7 ya Mpango Mkakati wa Wakala wa Mabasi Yandayo Haraka, (2021/22–2025/26), ambayo inahitaji wakala wa mabasi yaendayo haraka, kuhakikisha mabasi ya kutosha yanapatikana ili

kukidhi mahitaji ya umma na kupunguza msongamano. Zaidi ya hayo, viwango vya kimataifa vya usafiri wa mabasi ya mwendokasi vinapendekeza basi moja kila baada ya dakika 3-5 kwa saa za kilele.

559. Changamoto hizi zilitokana na kutowepo kwa uratibu na mipango ya pamoja miongoni mwa wadau husika, pamoja na kutowapo kwa sera jumuishi ya usafiri na uwekezaji usiojitosheleza katika miundombinu.

560. Muunganisho usiojitosheleza wa miundombinu ya aina tofauti za usafiri hupunguza ufanisi wa huduma ya mwendokasi ambayo ilitumika kama usafiri muhimu mijini. Hii iliathiri matumizi ya huduma ya mwendokasi, hasa miongoni mwa wasafiri ambao walihitaji kusafiri maeneo ambayo yako zaidi ya mahali ambapo mwendokasi inaishia, na hivyo kusababisha kuendelea kutegemea magari ya kibinafsi na usafiri usio rasmi wa umma.

**(b) Kuendelea Kutegemea Ukusanyaji wa Nauli Kwa Njia Zisizo za Kimfumo**

561. Wakati wa ziara ya tarehe 9 Septemba 2025 katika vituo vya mwendokasi, jijini Dar es Salaam, nilibaini kuwa nauli zilikusanywa kwa mkono kama ilivyodhihirishwa kwa kuwapo kwa tiketi ambazo zilikuwa tayari zimechapishwa. Tathmini zaidi ya ripoti za ufuatiliaji za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Mwaka 2024, nilibaini kuwa, ingawa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka alianzisha mfumo wa tiketi za kielektroniki, mfumo huo haukufanya kazi, huku programu ya kwenye simu ya UDART, iliyokuwa ikitumiwa na abiria kwa ununuzi wa tiketi, ikiripotiwa kutowa thabiti na mara kwa mara haifanyi kazi.

562. Hii ilikuwa kinyume na aya ya 3.5.7 ya Mpango Mkakati wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, ambayo inasisitiza uwekaji wa mfumo ili kuimarisha ukusanyaji wa nauli, usalama na ufuatiliaji. Hii ililenga kuboresha ufanisi, kulinda mapato, na kuhakikisha usalama wa wafanyakazi, wasafiri na miundombinu halisi.

563. Kuendelea kutegemea ukusanyaji wa nauli kwa mikono kulisababishwa na ucheleweshaji wa utumiaji na utekelezaji kamili wa mfumo jumuishi wa kielektroniki katika huduma za mabasi ya mwendokasi pamoja na udhibiti usiojitosheleza wa utoaji wa huduma, pamoja na upungufu katika ufuatiliaji unaofanywa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini.

564. Ingawa Sera na Mifumo ya Kimkakati ilisisitiza matumizi ya mifumo, utekelezaji wake haukuwa dhabiti kutokana na upatikanaji mdogo wa kadi za kielektroniki na udhibiti wa ndani usiojitosheleza katika ukusanyaji wa nauli.



ISO 9001:2015 Certified

Upungufu huu ulichangiwa na kukosekana kwa muunganisho wa nauli katika njia zote za usafiri, uhaba wa miundombinu ya tiketi katika vituo vikubwa, iliyosababisha watoa huduma kutotumia mifumo licha ya matakwa ya kiudhibiti.

## 8.6 Athari za Changamoto Zilizobainshwa katika Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

565. Pamoja na kwamba serikali iliendeleza jitihada mbalimbali za kuboresha usimamizi wa mfumo wa usafirishaji, kaguzi za ufanisi katika usimamizi wa mchakato wa upangaji wa maboresho ya miundombinu ya barabara, usimamizi wa uendeshaji wa mizani za barabarani na usimamizi wa huduma za usafiri mijini katika majiji makubwa ulibaini upungufu unaoathiri kufikiwa kwa malengo ya serikali. Hasa, upungufu huu uliathiri kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, kama ilivyoelezwa hapa chini.

### 8.6.1 Athari Katika Malengo ya Maendeleo Endelevu

566. Usimamizi usiojitosheleza wa mchakato wa kupanga uboreshaji wa miundombinu ya barabara, uendeshaji wa mizani, na huduma za usafiri wa mijini katika majiji makubwa umeathiri moja kwa moja kufikiwa kwa Shabaha ya 11.2 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa kupunguza ufikiaji wa miundombinu ya barabara na huduma za usafiri mijini.

567. Aidha, upungufu kama vile kutowa na utaratibu maalumu na vipaumbele vilivyoainishwa ili kuwezesha kuchagua barabara ambazo zitajengwa, pamoja na utoaji usiojitosheleza wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya barabara, kama yalivyobainika katika usimamizi wa mchakato wa upangaji wa maboresho ya miundombinu ya barabara, yalichangia uboreshaji usiojitosheleza wa miundombinu hivyo kusababisha kuendelea kuzorota kwa hali ya miundombinu ya barabara.

568. Pia, hali ya miundombinu ya barabara iliathiriwa pia na upungufu uliobainishwa katika usimamizi wa shughuli za mizani. Upungufu huo ni pamoja na udhibiti duni wa njia zinazoweza kutumika kukwepa mizani, pamoja na utumiaji mdogo wa mifumo ya TEHAMA katika uendeshaji wa mizani. Aidha, upungufu huu huleta mwanya wa kuendelea kuwapo kwa magari yaliyozidisha uzito ambayo huharibu miundombinu ya barabara.

569. Zaidi ya hayo, upangaji duni na udhibiti wa huduma za usafiri wa mijini katika majiji makubwa, ulisababisha kutopewa kipaumbele kwa mahitaji ya makundi maalumu katika upangaji wa huduma za usafiri mjini na muunganiko mdogo wa miundombinu ya aina zote za usafirishaji zilizopo.

570. Kwa ujumla, upungufu huo uliobainishwa, ulipunguza juhudi za serikali za kuhakikisha kuwa miundombinu ya usafiri pamoja na huduma za usafiri wa mijini, zinafikika na kutegemewa, hivyo kuathiri kufikiwa kwa Shabaha ya 11.2 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Shabaha hii inatoa wito wa utoaji na upatikanaji wa mifumo ya usafiri salama, nafuu, inayofikika na endelevu kwa wote, kuboresha usalama barabarani, hasa kwa kupanua usafiri wa umma, kwa kuzingatia hasa mahitaji ya wale walio katika mazingira hatarishi, wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na wazee.

### 8.6.2 Athari za Changamoto Zilizobainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano

571. Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa unaathiriwa na usimamizi usiojitosheleza wa upangaji wa maboresho ya miundombinu ya barabara na utoaji wa huduma za usafiri, pamoja na uendeshaji usiojitosheleza wa mizani. Upungufu uliobainika ni kama vile; utambuzi usiojitosheleza wa mahitaji ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara, kutowa na utaratibu maalumu wa kuchagua miradi ya barabara ya kutekeleza, udhibiti duni wa huduma za usafiri, na udhibiti mdogo wa magari yaliyozidisha uzito. Vyote hivi vinazuia kufikiwa kwa shabaha kuu za Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa. Shabaha hizo ni pamoja na kupunguza msongamano katika miji mikubwa pamoja na kufungua huduma za usafiri kupitia uboreshaji wa miundombinu ya usafirishaji.

## SURA YA TISA

## UTUNZAJI WA MAZINGIRA

### 9.1 Utangulizi

572. Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi kuhusu utunzaji wa mazingira. Pia, inatoa maelezo ya eneo lililokaguliwa, malengo na mawanda ya ukaguzi, mikakati na jitihada za serikali, uhusiano wake na Malengo ya Maendeleo Endelevu pamoja na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na athari zilizotokana na kaguzi.

573. Kaguzi zilizohusishwa katika sura hii ni pamoja na;

(a) Ukaguzi wa Ufanisi katika Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi nchini Tanzania;
(b) Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Shughuli za Urejeshaji Misitu; na
(c) Ukaguzi wa Ufanisi katika Utekelezaji wa Miradi ya Nishati Jadidifu.

#### 9.1.1 Usuli

574. Tanzania inakabiliwa na athari kubwa za mabadiliko ya tabianchi zinazohatarisha ukuaji wa uchumi na maisha ya jamii, huku gharama za kukabiliana na athari hizo zikikadiriwa kufikia asilimia 1–2 ya Pato la Taifa kila mwaka ifikapo mwaka 2030[10]. Ili kukabiliana na changamoto hizi, nchi iliandaa Mkakati wa Kwanza wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Mwaka 2012, na baadaye mpango huu uliboreshwa kupitia Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi wa Mwaka 2021–2026 ili kuimarisha jitihada za kukabiliana na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, pamoja na kuhakikisha kuwa sekta zote zinajumuisha masuala ya tabianchi kwenye shughuli zao za kila siku. Hata hivyo, Tanzania inaendelea kushuhudia ongezeko la athari za mabadiliko ya tabianchi, ikiwemo kuongezeka kwa joto, ukame wa mara kwa mara, mvua kubwa, mafuriko, na kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo[11].

575. Aidha, misitu ya Tanzania inayochukua takribani eneo la hekta milioni 48.1 na ni muhimu kwa mifumo ya ikolojia, maisha ya jamii, na uchumi wa taifa,

[10] https://unfccc.int/sites/default/files/NDC/202206/TANZANIA_NDC_SUBMISSION_30%20JULY%202021.pdf

[11] https://www.taees.org/wp-content/uploads/2021/09/NCCRS-2021-2026_-Final_PK.pdf

lakini nchi hupoteza takribani hekta 376,970 kila mwaka kutokana na shuguli za kilimo, uchomaji wa misituni, matumizi ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia, pamoja na matumizi ya misitu yasiyo endelevu. Licha ya kuwapo kwa sera na mikakati ya kitaifa ya uhifadhi na urejeshaji wa misitu, uharibifu wa misitu unaendelea, na hivyo kutishia malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ya kupunguza nusu ya uharibifu wa misitu ifikapo Mwaka wa Fedha 2025/26, pamoja na lengo la 15.2 la Malengo ya Maendeleo Endelevu kuhusu usimamizi endelevu wa misitu na urejeshaji wa mandhari yaliyoharibiwa. Hali hii inaonesha haja ya mipango madhubuti ya upandaji, urejeshaji na usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu.

576. Vilevile, maendeleo ya taratibu katika ukuaji wa sekta ya nishati jadidifu zinaibua wasiwasi juu ya upotevu wa fursa za kuwa na nishati ya uhakika, kupunguza gharama, na kuboresha upatikanaji wa umeme vijijini. Mapitio ya hotuba za Waziri wa Nishati (2020–2024) yanaonesha kuwa, licha ya Tanzania kuwa na vyanzo vingi vya nishati jadidifu kama vile jua, upepo, maji, na joto-ardhi, bado inategemea kwa kiasi kikubwa nishati itokanayo na mabaki ya viumbe, hususani gesi asilia katika uzalishaji wa umeme. Hadi kufikia Mei 2022, asilimia 60.27 ya umeme katika gridi ya taifa ulizalishwa kwa kutumia gesi asilia, huku asilimia 33.91 ikitokana na umeme wa maji, na asilimia 0.62 tu ikitokana na biomasi, wakati vyanzo vingine vya nishati jadidifu kama jua na upepo vikichangia kwa kiwango kidogo sana. Aidha, sekta ya nishati jadidifu nchini inaendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo uelewa mdogo kuhusu faida zake, upungufu wa taarifa kuhusu teknolojia za nishati na mbinu bora za matumizi, pamoja na uhaba wa wataalamu wenye ujuzi stahiki.

### 9.1.2 Uhusiano wa Utunzaji wa Mazingira na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano

577. Utunzaji wa mazingira kupitia utekelezaji wa hatua mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, urejeshaji misitu, na miradi ya nishati jadidifu unasaidia kufanikisha malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa kukuza ustahimilivu kwenye mabadiliko ya tabianchi, kuhifadhi mifumo ya ikolojia, na kuwezesha ukuaji wa uchumi endelevu, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 33** hapa chini.

**Jedwali Na. 33: Uhusiano wa Utunzaji wa Mazingira na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano**

| Jina la Ukaguzi | Mpango | Eneo la Kipaumbele | Hatua za Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| Ukaguzi wa Ufanisi katika Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi | Mpango wa Tatu wa Taifa Maendeleo wa Miaka Mitano | Usimamizi wa Mazingira na Rasilimali Asili | Kuimarisha uwezo wa kitaifa wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza madhara yake |
| | Malengo ya Maendeleo Endelevu | Lengo la 13: Kuchukua hatua za dharura za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na athari zake | Shabaha ya 13.1 inasisitiza juu ya kuimarisha ustahimilivu na uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ifikapo mwaka 2030 |
| | | Lengo la 6: Kuhakikisha upatikanaji na usimamizi endelevu wa maji | Shabaha ya 6.1 inaangazia kufanikisha upatikanaji wa maji safi na salama na kwa gharama nafuu kwa wote ifikapo mwaka 2030 |
| | | Lengo la 2: Kuhakikisha upatikanaji wa chakula cha kutosha, kuboresha lishe, na kuhakikisha kilimo endelevu | Shabaha ya 2.3 inasisitiza kuongeza mara mbili uzalishaji wa mazao ya kilimo na mapato ya wafugaji ifikapo mwaka 2030 |
| Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Shughuli za Urejeshaji Misitu | Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano | Usimamizi wa Mazingira na Maliasili | Kupunguza uharibifu wa ardhi na kuhifadhi viumbe hai |
| | Malengo ya Maendeleo Endelevu | Lengo la 15, Maisha Duniani | Shabaha ya 15.1 inasisitiza kuhakikisha uhifadhi, urejeshaji, na matumizi endelevu ya mifumo ya ikolojia na maji ifikapo mwaka 2030 |
| Ukaguzi wa Ufanisi katika Utekelezaji wa Miradi ya | Mpango wa Tatu wa Taifa Maendeleo wa Miaka Mitano | Usimamizi wa Mazingira na Maliasili | Kukuza teknolojia za nishati jadidifu (gesi asilia, nishati ya jua) na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi |

| Jina la Ukaguzi | Mpango | Eneo la Kipaumbele | Hatua za Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| Nishati Jadidifu | Malengo ya Maendeleo Endelevu | Lengo la 7, Nishati Safi na ya Bei Nafuu | Shabaha ya 7.2 inaangazia kuongeza kiwango cha nishati jadidifu kwenye muunganiko wa vyanzo vya nishati wa nishati ya taifa |
| | | Lengo la 15, Maisha Duniani | Shabaha ya 15.2 inakusudia kupunguza ukataji miti na upotevu wa makazi ya viumbe kwa kuendeleza vyanzo mbadala vya nishati jadidifu |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2025

### 9.1.3 Mikakati na Jitihada za Serikali katika Utunzaji wa Mazingira

578. Serikali imetekeleza mikakati na jitihada mbalimbali za kuhakiksha utunzaji wa mazingira, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 34.**

**Jedwali Na. 34: Mikakati na Jitihada za Serikali katika Utunzaji wa Mazingira**

| Eneo | Mikakati | Jitihada |
|---|---|---|
| Juhudi za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi | • Mpango Kabambe wa Taifa wa Mazingira wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira 2022 - 2032: Mpango huu unatoa njia ya utekelezaji wa changamoto za kimazingira zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.<br>• Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi 2021-2026: Mkakati huu unalenga kuimarisha ustahimilivu wa taifa dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi.<br>• Mpango Mkakati wa Ofisi ya Makamu wa Rais 2021/22 - 2025/26: Mpango huu unatoa njia ya kukabiliana na changamoto za kimazingira zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi. | • Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza madhara yake. Hatua hizi ni pamoja na miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwenye maeneo ya pwani, programu ya kugharimia athari za mabadiliko ya tabianchi, ufuatiliaji wa kuwapo kwa fursa za biashara ya kaboni, na kukuza mbinu endelevu kama vile upandaji miti, matumizi ya majiko-janja ya kupikia yanayopunguza matumizi ya kuni, na kilimo kinachostahimili ukame. |

ISO 9001:2015 Certified

| Eneo | Mikakati | Jitihada |
|---|---|---|
| Shughuli za Urejeshaji Misitu | • Mpango Kabambe wa Taifa wa Mazingira wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032): Mpango huu usisitiza juu ya upandaji miti nchini kote na unazitaka kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka.<br>• Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Misitu (2021–2031): Mkakati huu unalenga kurejesha hekta milioni 5.2 za misitu na kupunguza ukataji miti wa kila mwaka kwa asilimia 70 ifikapo mwaka 2031.<br>• Mkakati wa REDD+: Mkakati huu unahimiza upandaji miti na urejeshaji na usimamizi endelevu wa misitu. | • Serikali, kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI imeandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Misitu (2021–2031) na Mkakati wa Taifa wa Urejeshaji wa Mandhari ya Misitu (2023–2033) ili kuimarisha uhifadhi wa misitu nchini Tanzania. |
| Miradi ya Nishaji Jadidifu | • Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia 2024-2034: Mkakati huu unalenga kufanikisha mustakabali wa nishati safi na jumuishi kwa kuongeza aina za vyanzo vya nishati, kukuza mifumo ya umeme iliyo nje ya gridi ya taifa (off-grid) na kuboresha ufanisi wa nishati katika sekta zote.<br>• Mpango Mkakati wa Wizara ya Nishati 2021 - 2026: Mpango huu unahamasisha uanzishaji wa vyanzo vya umeme wa nishati jadidifu ikiwemo nishati ya jua, upepo na jotoardhi. Ifikapo mwaka 2026.<br>• Mpango Mkakati wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (2022/23 – 2026/27): Kuzingatia ufuatiliaji wa kimfumo wa miradi ya nishati jadidifu ifikapo mwaka 2025. | • Serikali imeweka wazi malengo ya kuongeza mchango wa nishati jadidifu hadi asilimia 75 kupitia uwekezaji katika teknolojia za jua, upepo, maji, na joto-ardhi, na kufanikisha upatikanaji wa huduma za umeme vijijini kwa asilimia 100 na uunganishaji wa asilimia 75 ifikapo mwaka 2030 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Mikakati na Jitihada za Serikali katika Utunzaji wa Mazingira, 2025

ISO 9001:2015 Certified

## 9.2 Lengo na Mawanda ya Ukaguzi

### 9.2.1 Lengo la Ukaguzi

579. Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa kutathmini kama Serikali, kupitia taasisi husika, imehakikisha usimamizi madhubuti wa utunzaji wa mazingira kwa kuendana na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

580. Hususani, ukaguzi wangu ulijikita katika kutathmini iwapo:

(a) Ofisi ya Makamu wa Rais iliweka mikakati madhubuti ya utekelezaji wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kuimarisha ustahimilivu wa nchi dhidi ya athari zake;

(b) Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilisimamia kwa ufanisi utekelezaji wa shughuli za urejeshaji misitu ili kuhakikisha uendelevu wa misitu nchini; na

(c) Wizara ya Nishati na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji zilisimamia ipasavyo miradi ya nishati jadidifu ili kuhakikisha ulinganifu katika vyanzo vya nishati, unaoimarisha usalama na uendelevu wa nishati nchini.

ISO 9001:2015 Certified

### 9.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

581. Ukaguzi wangu kuhusu utekelezaji wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania ulijumuisha Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira pamoja na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Nishati, na Wizara ya Maji. Ukaguzi pia ulilenga kutathmini hali ya utekelezaji wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuzingatia upatikanaji wa rasilimali, utoaji wa taarifa, uratibu, ufuatiliaji, na tathmini ya hatua hizo. Masuala haya yaliangaziwa kwa miaka mitano kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25.

582. Aidha, ukaguzi wangu kuhusu Usimamizi wa Shughuli za Urejeshaji Misitu ulijumuisha Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI). Ukaguzi huu ulitathmini ufanisi wa upangaji, utekelezaji, uratibu, pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za urejeshaji misitu katika kipindi cha miaka minne ya fedha, kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25.

583. Katika ukaguzi wangu wa Usimamizi wa Miradi ya Nishati Jadidifu, taasisi zilizokaguliwa ni pamoja na Wizara ya Nishati na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji. Ukaguzi uliangalia kama Wizara na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji zilisimamia ipasavyo miradi ya nishati jadidifu kupitia maandalizi ya awali ya miradi, utekelezaji wa miradi (ikiwemo ununuzi, ujenzi, na utumiaji wa miradi), uendeshaji wa miradi, pamoja na uratibu na upimaji wa utendaji. Tathmini hiyo ilifanyika kwa miaka minne ya fedha kuanzia 2021/22 hadi 2024/25.

## 9.3 Matokeo ya Ukaguzi katika Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

584. Nimebaini kuwa, utekelezaji wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika sekta za maji, kilimo, na nishati haukuwa wa kutosha. Katika sekta ya maji, asilimia 43 tu ya hatua zilizopangwa ndizo zilizotekelezwa; katika sekta ya kilimo, kiwango cha utekelezaji kilikuwa asilimia 44, huku sekta ya nishati ikionesha wastani wa utekelezaji kwa asilimia 52. Hali hii ilisababishwa na upungufu wa rasilimali, utoaji wa taarifa usio wa kutosha, uratibu usioridhisha, pamoja na ufuatiliaji na tathmini usiojitosheleza. Maelezo zaidi changamoto hizi yametolewa hapa chini.

### 9.3.1 Ofisi ya Makamu wa Rais Kutowezesha Kikamilifu Ukusanyaji wa Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

ISO 9001:2015 Certified

585. Mapitio yangu ya Ripoti ya Tathmini ya Mwaka 2021 ya Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa, na Ripoti ya Utendaji wa Mwaka ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya Mwaka wa Fedha 2022/23 yalibaini kuwa Ofisi ya Makamu wa Raisi - Muungano na Mazingira haikuwezesha ipasavyo ukusanyaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi nchini. Upungufu huu ulijidhihirisha katika ufadhili usiojitosheleza wa jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabiannchi, hali iliyoathiri utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa wakati.

586. Aidha, kulikuwa na uwezo mdogo na mafunzo yasiyotosha katika ngazi ya Serikali za Mitaa, hali iliyowazuia watendaji wa ngazi za halmashauri kupanga, kutekeleza, na kufuatilia ipasavyo hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Pia, nilibaini kuwa urithishaji na matumizi ya teknolojia zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi haukuwa wa kuridhisha. Upungufu huu ulichangia kuchelewa kwa utekelezaji wa hatua za kukabiliana na mabadiliko

ya tabianchi na kupungua katika uwezo wa nchi kulinda ikolojia dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi, kama ilivyoelezwa kwa kina hapa chini:

### (a) Kutokujitosheleza kwa Ufadhili wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

587. Mapitio yangu ya Mpango wa Mkakati wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira wa Mwaka wa Fedha 2021/22–2025/26 yalibaini kuwa, Tanzania inakabiliwa na upungufu wa ufadhili kwa ajili ya utekelezaji wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Hali hii ilidhihirishwa na kuwapo kwa upungufu wa asilimia 68 ya msaada uliotolewa na nchi ya Uingereza kwa Tanzania, katika Mwaka wa Fedha 2020/21 na 2021/22. Kwa upande mwingine, nilibaini kuwa mapato ya Serikali kutoka vyanzo vya nje yalipungua kutoka shilingi trilioni 3.6 hadi shilingi trilioni 2.1 ndani ya kipindi cha miaka mitano nilichokagua.

588. Pia, nilibaini kuwa fedha zilizotolewa na Ofisi ya Makau wa Rais, Muungano na Mazingira ili kuratibu utekelezaji wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hazikuwa za kutosha, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 35**.

**Jedwali Na. 35: Utoaji wa Fedha kwa ajili ya Kuwezesha Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais** - Muungano na Mazingira

| Mwaka wa Fedha | Kiasi Kilichopangwa (Sh. milioni) | Kiasi Kilichotolewa (Sh. milioni) | Kiasi Kilichotolewa (%) |
|---|---|---|---|
| 2021/22 | 207.24 | 206.44 | 99.6 |
| 2022/23 | 398.39 | 240.02 | 60 |
| 2023/24 | 757.61 | 545.48 | 72 |
| 2024/25 | 1,938.80 | 1,298.99 | 67 |
| **Jumla** | 3,302.04 | 2,290.94 | **70** |

***Chanzo*****:** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Mipango ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais (2021/22 – 2024/25) wa Mwaka 2025

589. Taarifa zilizowasilishwa katika **Jedwali Na. 35** zinaonesha kuwa kati ya Mwaka wa Fedha 2021/22 na 2024/25, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira iliongeza kwa kiasi kikubwa cha bajeti yake kwa ajili ya kuratibu shughuli za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kutoka shilingi milioni 207 hadi bilioni 1.94. Hata hivyo, ni asilimia 70 tu ya jumla ya fedha zilizotengwa ndizo zilizotolewa katika kipindi cha miaka minne ya kifedha. Kupitia mahojiano niliyofanya na maafisa kutoka wizara mbalimbali, ikiwemo Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, nilibaini kuwa, utolewaji mdogo wa fedha

ulisababishwa na kutowapo kwa utaratibu madhubuti wa kuhakikisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi yanapewa kipaumbele wakati wa utoaji wa fedha.

590. Utolewaji mdogo wa fedha umesababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuiweka jamii katika hatari za athari za madadiliko ya tabianchi. Hali hii inaweza kuongeza gharama za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa mfano, ukosefu wa fedha za kutosha za kukabiliana na tabianchi katika sekta ya kilimo umesababisha kupungua kwa uzalishaji wa chakula kwa asilimia 20.

### (b) Uwezo na Mafunzo Yasiyojitosheleza kwa ajili ya Utekelezaji Bora wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika Serikali za Mitaa

591. Mapitio yangu ya ripoti za ufuatiliaji na tathmini za mradi wa Mfuko wa Nchi Zinazoendelea katika Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, pamoja na mahojiano na maafisa kutoka Wizara ya Kilimo na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, yalibaini kuwa mafunzo yaliyotolewa kwa waratibu wa mazingira wa wilaya na washiriki wengine kuhusu uandaaji wa vihatarishi na ufuatiliaji katika mradi wa mfuko wa nchi zinazoendelea, hayakujumuisha mazoezi kwa vitendo. Hali hii ilipunguza uwezo wa maafisa wengi wa wilaya kutekeleza ipasavyo hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Hali hii ilitokana na kutotengwa kwa fedha za mafunzo ya vitendo katika bajeti ya mradi, jambo lililopunguza uwezekano wa kuwajenga uwezo wa kutosha katika ngazi za serikali za mitaa.

ISO 9001:2015 Certified

592. Kwa ujumla, upungufu huu ulisababishwa na kukosekana kwa programu ya kitaifa ya kujenga uwezo kwa Maafisa wa Mazingira nchini. Kutokuwapo kwa programu hii kulisababisha ukosefu wa usawa katika kuwajengea maarifa na ujuzi maafisa, ambapo baadhi ya wilaya hupata mafunzo huku nyingine zikibaki bila kupata mafunzo. Changamoto hii ilipunguza ufanisi wa juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuziacha baadhi ya halmashauri zikiwa hazina uwezo wa kutosha wa kujumuisha masuala ya tabianchi katika mipango yake.

### 9.3.2 Utoaji Usiojitosheleza wa Taarifa za Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

593. Nilibaini kuwa kulikuwa na utoaji wa taarifa usiojitosheleza juu ya utekelezaji wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Hali hii ilisababishwa na wadau muhimu, wakiwemo wizara za kisekta, kutowasilisha ripoti zao za utekelezaji wa masuala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi

katika Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira. Vilevile, hali ya utekelezaji ilionekana kuwasilishwa kwa kiasi kidogo sana kupitia Ripoti za Utendaji za Mwaka za wizara husika. Aidha, utoaji wa taarifa kwa wadau kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira kwenda kwa wadau kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi haukuwa wa kutosha.

594. Maelezo ya ziada kuhusu masuala haya yametolewa hapa chini:

**(a) Wizara Zilizokaguliwa Kutokuwasilisha Ripoti zao za Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira**

595. Nilibaini kuwa Wizara ya Nishati, Wizara ya Maji na Wizara ya Kilimo, hazikuwasilisha ripoti ipasavyo katika Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira. Hali hii ni kinyume na kifungu cha 32 (1a) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191, iliyofanyiwa marejeo mwaka 2023, ambacho kinazitaka wizara za kisekta, kupitia Mratibu wa Mazingira wa Sekta, kuwasilisha kwa Mkurugenzi wa Mazingira ripoti kila baada ya miezi sita kuhusu hali ya mazingira, ikiwemo masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

596. Kimsingi, kila wizara ya kisekta ilitakiwa kuwasilisha ripoti mbili kuhusu hali ya mazingira kwa kila Mwaka wa Fedha kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25, lakini hakukuwa na wizara hata moja iliyotekeleza takwa hili. Hali hii ilisababishwa na kutowapo kwa utaratibu wa ndani ya ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira wa kufuatilia hali ya utoaji wa taarifa wa wizara husika. Matokeo yake, uratibu wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi baina ya wadau haukuwa wa kutosha, hali iliyosababisha ucheleweshaji katika kuboresha mipango ya kisekta na kupunguza uwajibikaji katika kushughulikia vipaumbele vya mabadiliko ya tabianchi.

**(b) Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira Kutokuwa na Mfumo wa Kurudisha Maoni Juu ya Taarifa za Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi**

597. Mapitio yangu ya mpango mkakati na mipango ya kila mwaka ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira yalibaini kuwa hakukuwa na utaratibu wa kutoa mrejesho wa hali ya utoaji wa taarifa za masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika wizara za kisekta. Matokeo yake, wizara hizo hazikuweza kutimiza wajibu wao wa kisheria wa kuripoti kuhusu hali ya utekelezaji wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira. Kutokuwapo kwa mfumo wa

mrejesho pia kulizorotesha jitihada za kuboresha hali ya utoaji wa ripoti, kwani kulipunguza fursa za kutatua changamoto, ufuataji wa taratibu, na kuimarisha, ubora na muda wa uwasilishaji wa ripoti.

598. Hali hii ilisababishwa na mawasiliano yasiyojitosheleza kati ya wizara za sekta pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, na upungufu wa mafunz kama ilivyodhihirishwa na kutohusishwa kwa maafisa wa wizara katika programu za mafunzo ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika Mwaka wa Fedha 2023/24.

599. Vilevile, nilibaini kutokuwapo kwa mfumo wa kurejesha taarifa kulizuia ufuatiliaji na tathmini kwa ufanisi, kupunguza fursa za kujifunza, na kupunguza mawasiliano na uratibu, kutotekeleza ipasavyo mipango ya taifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**(c) Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira Kutokuhakikisha Utoaji wa Taarifa za Kutosha kuhusu Masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi**

600. Nilibaini kuwa, utoaji wa taarifa kuhusu hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira katika ngazi za kitaifa na kimataifa, ulikuwa na upungufu kama inavyoelezwa hapa chini.

**(i) Utoaji wa Taarifa Ndani ya Nchi**

ISO 9001:2015 Certified

601. Mapitio yangu ya Taarifa za Utendaji wa Mwaka ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2023/24, yalibaini kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira haikutoa ripoti yoyote kuhusu hali ya mazingira nchini. Hali hii ilikuwa kinyume na aya ya 4.6.2 ya Mpango Mkakati wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira ambayo inasisitiza juu ya utoaji wa ripoti kuhusu hali ya mazingira, ikiwemo hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mara mbili kwa mwaka. Changamoto hii ilisababishwa na uhaba wa watumishi, kwani kulikuwa na watumishi 39 pekee kati ya 56 (sawa na upungufu wa asilimia 17) waliohitajika katika divisheni ya mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais.

**(ii) Utoaji wa Taarifa katika Ngazi ya Kimataifa**

602. Mapitio yangu ya ripoti za Tanzania za “Mawasilisho ya Kwanza na ya Pili ya Kitaifa” kwenda katika Umoja wa Mataifa sehemu ya Mabadiliko ya

Tabianchi yalionesha kuwa, mawasilisho ya kwanza ya Tanzania yalikuwa ni ya taarifa za kutoka mwaka 1993 hadi 2004, huku mawasilisho ya pili yalikuwa ni ya taarifa za kutoka mwaka 1995 hadi 2005 ambayo yaliwasilishwa katika Umoja wa Mataifa mwaka 2014. Zaidi ya hayo, hadi kufikia mwezi Oktoba 2024, miaka kumi baadaye, Tanzania haikuwasilisha ripoti yoyote. Hali hii imeiacha nchi bila taarifa za kisasa juu ya masuala ya mabadiliko ya tabianchi zinazoweza kusaidia juhudi za kuimarisha ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Hii nikinyume na masharti ya Umoja wa Mataifa yanayoitaka Tanzania kuwasilisha ripoti kila baada ya miaka miwili kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa hatua za kukabiliana na kupunguza madhara ya mabadiliko ya tabianchi.

### 9.3.3 Kutojitosheleza kwa Uratibu wa Wadau Wakati wa Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

603. Nilibaini kuwa, kulikuwa na uratibu usiojitosheleza wa wadau muhimu ambao unabainika kupitia utendaji usioridhisha wa Kamati ya Kitaifa ya Kiufundi ya Mabadiliko ya Tabianchi na Kamati Tendaji ya Kitaifa. Pia, hapakuwapo mifumo ya kuimarisha mfuko wa mazingira na kuanzisha Mfumo wa Kitaifa wa Ufadhili wa Mabadiliko ya Tabianchi, pamoja na ukosefu wa mara kwa mara wa mikutano ya kitaifa ya mabadiliko ya tabianchi. Hali hii ilikuwa kinyume na aya ya 4.2 ya Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2021–2026), ambayo inaipa Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira Muungano na Mazingira jukumu la kuratibu usimamizi wa masuala yote ya mazingira nchini.

ISO 9001:2015 Certified

604. Upungufu huu umefafanuliwa kwa kina hapa chini:

**(a) Kutojitosheleza kwa Uratibu wa Kamati ya Kitaifa ya Kiufundi ya Mabadiliko ya Tabianchi na Kamati Tendaji ya Kitaifa ya Mabadiliko ya Tabianchi**

605. Nilibaini kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira haikufanya uratibu wa kutosha wa Kamati ya Kitaifa ya Kiufundi ya Mabadiliko ya Tabianchi na Kamati Tendaji ya Kitaifa ya Mabadiliko ya Tabianchi, kwani mikutano yake haikufanyika ipasavyo. Hali hii ni kinyume na kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191, iliyofanyiwa marejeo mwaka 2023 na Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2021–2026), ambao inaipa Ofisi ya Makamu wa Rais jukumu la kuratibu usimamizi wa masuala yote ya kimazingira nchini.

606. Suala hili lilisababishwa na ukosefu wa rasilimali fedha za kutosha ili kutekeleza shughuli zilizopangwa, jambo lililopunguza utekelezaji wa hatua za

kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Matokeo yake, ufanisi wa utekelezaji wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ulipungua na kuongeza hatari kwa jamii, mifumo ya ikolojia, na sekta za uchumi dhidi ya athari hasi za mabadiliko ya tabianchi.

**(b) Kutokuwapo kwa Mipango ya Uratibu ya Kuimarisha Mfuko wa Mazingira na Kuanzisha Mfumo wa Kitaifa wa Ufadhili wa Mabadiliko ya Tabianchi**

607. Nilibaini kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira haikuratibu ipasavyo wadau mbalimbali ikiwemo wizara za kisekta ili kuimarisha Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Mazingira, kinyume na Kifungu cha 213(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira [Sura ya 191, iliyofanyiwa marejeo mwaka 2023], kinachobainisha masharti ya uimarishaji wa mfuko huo. Nilibaini kuwa hali hii ilisababishwa na kutowapo kwa kanzidata ya wadau na miradi ya mabadiliko ya tabianchi nchini, kutobainishwa kwa mahitaji ya rasilimali, pamoja na kukosekana kwa mfumo wa kufuatilia matumizi ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya masuala ya mabadiliko ya tabianchi kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, hadi kufikia Februari 2025, serikali kupitia Wizara ya Fedha ilikuwa katika hatua za mwisho za kuanzisha Kitengo cha Fedha za Madabiliko ya Tabianchi kitakachohusika na kuhamasisha, kufuatilia na kuratibu fedha za masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika taasisi za serikali, washirika wa maendeleo, sekta binafsi na asasi za kiraia.

608. Pia, nilibaini ukosefu wa mipango ya kifedha ya kuimarisha Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Mazingira, jambo ambalo limechangia ushiriki mdogo na uelewa usiojitosheleza miongoni mwa baadhi ya sekta binafsi kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

609. Hivyo basi, ukosefu wa mifumo endelevu ya kifedha unakwamisha ufadhili wa muda mrefu wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kwani mifumo iliyopo inategemea miradi maalumu badala ya programu za muda mrefu, hali inayopunguza kasi ya kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu hususani yale yanayohusiana na tabianchi.

**(c) Kutokufanyika Ipasavyo kwa Mikutano ya Kitaifa ya Mabadiliko ya Tabianchi**

610. Licha ya juhudi za Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira katika kuhamasisha na kuratibu mipango mbalimbali, ikiwemo mifumo ya mawasiliano ya tabianchi ya serikali na isiyo ya kiserikali, nilibaini kuwa Jukwaa la Kitaifa la Mabadiliko ya Tabianchi la kila mwaka, linalowakutanisha wadau

wote muhimu, halikufanyika ipasavyo. Hali hii ni kinyume na Aya ya 4.2 ya Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi wa Mwaka wa Fedha 2021–2026, unaoitaka Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira kuratibu jukwaa hilo kila mwaka.

611. Pia, tathmini yangu ilionesha kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira iliendesha jukwaa moja tu linalohusiana na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kati ya Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2023/24. Hali hii ilisababishwa na kutowapo kwa mpangilio maalumu wa kuwakutanisha wadau na wahusika wakuu, jambo lililochochea kutotathmini ipasavyo maendeleo ya utekelezaji wa mkakati wa taifa wa mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuhamasisha hatua za kukabaliana na mabadiliko ya tabianchi kupitia ubunifu na matumizi ya teknolojia za kisasa.

### 9.3.4 Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira Kutokufanya Ipasavyo Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

612. Nilibaini kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira haikufuatilia na kutathmini ipasavyo utekelezaji wa hatua za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Hali hii ilidhihirika kutokana na viashiria vya ufuatiliaji na tathmini kutojumuishwa kikamilifu katika mifumo ya kawaida ya ufuatiliaji na tathmini ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira pamoja na kukosekana kwa mfumo wa kukusanya kanzidata kwa ajili ya tathmini na ufuatiliaji. Hali hii ilichochea kutotekelezwa kikamilifu kwa viashiria vilivyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira. Maelezo ya kina juu ya masuala haya yametolewa hapa chini:

#### (a) Kutokujumuishwa Kikamilifu kwa Viashiria Vilivyowekwa katika Mpango Mkakati wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira katika Mipango ya Utendaji ya Kila Mwaka

613. Nilibaini kuwa Mipango ya Utekelezaji ya Mwaka ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira kwa miaka ya fedha kuanzia 2021/22, na 2024/25 haikujumuisha kikamilifu viashiria na malengo ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi vilivyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Mwaka wa Fedha 2021/22–2025/26. Upungufu huu haukua sambamba na aya ya 4.6 ya Mwongozo wa Ujumuishaji wa Malengo ya Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika Sera, Mipango na Programu za Kisekta wa mwaka 2012, unaoielekeza Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira kuweka viashiria

vya utendaji kwa ajili ya kurahisisha ufuatiliaji na tathmini. **Jedwali Na. 36** linaonesha maelezo zaidi.

**Jedwali Na. 36: Ujumuishaji wa Viashiria vya Mpango Mkakati wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira katika Mipango ya Utekelezaji ya Mwaka**

| Viashiria katika Mpango Mkakati | Viashiria katika Mipangomkakati ya kila Mwaka | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/2022 | 2022/2023 | 2023/2024 | 2024/2025 |
| Idadi ya miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza athari zake iliyopangwa na kutekelezwa | Kuwezesha maandalizi ya maandiko matatu ya miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na maandiko matatu ya miradi ya kupunguza athari za tabianchi | Kuandaa maandiko matatu ya miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na maandiko matatu ya miradi ya kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi ili kupata ufadhili | Hakuna | Hakuna |
| Idadi ya programu za uelewa katika hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na upunguzaji wa athari zake | Kuwezesha maandalizi na utekelezaji wa programu ya uelewa kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi | Kuandaa na kutekeleza programu ya uelewa kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi | Hakuna | Hakuna |
| Idadi ya wizara za kisekta, na serikali za mitaa zilizojumuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika mipango na bajeti yao | Kuwezesha ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, Mikakati miningine kama wa programu ya Kupunguza Uzalishaji wa Gesi Ukaa unaotokana na Ukataji na Uharibifu wa Misitu, Ripoti ya Mchango wa Kitaifa wa Kupunguza Uzalishaji wa Gesi chafu na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Mpango wa Taifa wa Hatua | Kupitia miongozo ya Kujumuisha Masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi katika Wizara za Kisekta na Serikali za Mitaa<br><br>Kufuatilia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, Mikakati mingine kama programu ya Kupunguza Uzalishaji wa Gesi Ukaa unaotokana na Ukataji na Uharibifu wa Misitu, Ripoti ya Mchango wa Kitaifa wa Kupunguza Uzalishaji wa Gesi | Kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira [Sura ya 191, iliyofanyiwa marejeo mwaka 2023] katika wizara zote za kisekta na Serikali za Mitaa | Hakuna |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika ngazi za sekta na serikali za mitaa | chafu na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Mpango wa Taifa wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika sekta mbalimbali na serikali za mitaa | | |
| Idadi ya Mashirika ya Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia zinazoshiriki katika hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na upunguzaji wa atharii zake | Hakuna | Hakuna | Hakuna | Hakuna |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Mpango wa Mkakati na Mipango ya Utekelezaji ya Kila Mwaka ya Ofisi ya Makamu wa Rais wa Mwaka 2025

614. Kutokana na **Jedwali Na. 36** nilibaini kuwa, viashiria vilivyowekwa katika Mpango Mkakati wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira havikujumuishwa ipasavyo katika Mipango ya Utekelezaji ya kila Mwaka. Aidha, kiashiria cha kuhakikisha ushiriki wa sekta binafsi na asasi za kiraia katika hatua za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi hakikujumuishwa katika Mipango ya Utekelezaji ya Mwaka ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

ISO 9001:2015 Certified

### (b) Ukosefu wa Mfumo Jumuishi wa Kanzidata kwa ajili ya Kufuatilia Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

615. Uchambuzi wangu wa taarifa za utendaji ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira ulionesha kutowapo kwa mfumo jumuishi wa kanzidata kwa ajili kufuatilia utekelezaji wa hatua za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, licha ya ahadi iliyotolewa awali na ofisi hii kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ya kuanzisha mfumo huo katika Mwaka wa Fedha 2007/2008. Hali hii ilikuwa kinyume na kifungu cha 174 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira [Sura ya 191, iliyofanyiwa marejeo mwaka 2023], ambacho kinaelekeza Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kuanzisha na kuendesha Mfumo wa Taarifa za Mazingira kwa madhumuni ya kukusanya matokeo, takwimu na taarifa kutoka taasisi za umma na binafsi katika shughuli za usimamizi wa mazingira.

616. Kukosekana kwa mfumo jumuishi wa kanzidata kwa ajili usimamizi na kufuatilia utekelezaji wa hatua za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kulihusishwa na ukosefu wa ujuzi wa kiufundi wa kubuni, kutekeleza, na kudumisha mfumo huo. Hali hii inasababisha kuwapo kwa taarifa zisizojitosheleza wakati wa kufanya maamuzi juu ya mafanikio na changamoto zinazohusiana na hatua za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**(c) Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira Kutotoa Taarifa ya Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini**

617. Uchambuzi wangu wa nyaraka pamoja na mahojiano na maafisa kutoka Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji, na Wizara ya Nishati ulionesha kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira haikutoa ripoti ya hali ya usimamizi wa mazingira. Hali hii ni kinyume na kifungu cha 175 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira [Sura ya 191, iliyofanyiwa marejeo mwaka 2023], ambacho kinaelekeza ofisi hii kupitia Mkurugenzi wa Mazingira kuchapisha ripoti kuhusu hali ya usimamizi wa mazingira kila baada ya miaka miwili, ambapo ripoti hiyo inapaswa kuwasilishwa Bungeni.

618. Aidha, uchambuzi wangu zaidi ulionesha kuwa ofisi hii haikutoa ripoti za hali ya usimamizi wa mazingira katika mwaka 2021, 2023, na 2025, kwani ripoti ya mwisho ilikuwa ya mwaka 2019. Hali hii ilipunguza upatikanaji wa taarifa muhimu za mazingira kwa wadau, hasa Bunge, ikiwemo masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Upungufu huu ulitokana na Ofisi ya Makamu wa Rais kutotoa kipaumbele cha kutosha juu ya masuala haya katika mipango na bajeti zake za kila mwaka.

NATIONAL AUDIT OFFICE NAOT ISO 9001:2015 Certified

## 9.4 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Usimamizi wa Shughuli za Urejeshaji Misitu

619. Licha ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 kusisitiza kuimarishwa kwa uhifadhi wa ikolojia ya misitu ili kutoa bidhaa na huduma za kimazingira kwa njia endelevu, nilibaini kwamba Tanzania iliendelea kukumbwa na opotevu wa misitu kwa wastani wa hektari 376,970 kwa mwaka kati ya mwaka 2016 na mwaka 2021, jambo lililosababishwa na shughuli za kilimo, ongezeko la idadi ya watu, matumizi makubwa wa kuni, na malisho holela.

620. Aidha, kati ya Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25 shughuli za upandaji miti katika Serikali za Mitaa zilifikia asilimia 67 hadi 87 ya malengo, na wastani wa kitaifa ukiwa asilimia 80.43 huku kukiwa na kiwango kidogo cha ustawi na ukuaji ambacho ni wastani wa asilimia 50.9 ya miti iliyopandwa,

jambo lililosababishwa na ukosefu wa mifumo ya ufuatiliaji na ukaguzi miti hiyo baada ya upandaji.

621. Changamoto hii ilitokana na upangaji na utekelezaji usiofanisi wa shughuli za urejeshaji misitu, uratibu dhaifu kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, ufuatiliaji na tathmini isiyojitosheleza ya shughuli za urejeshaji misitu zinazotekelezwa na serikali za mitaa. Mambo haya yameelezwa kwa kina hapa chini.

### 9.4.1 Mipango isiyo ya ufanisi ya shughuli za urejeshaji misitu

622. Nilibaini kwamba, mchakato wa upangaji wa shughuli za urejeshaji na uhifadhi wa misitu haukuendelezwa vya kutosha ili kuhakikisha utekelezaji wenye ufanisi wa shughuli za upandaji upya miti, kinyume na aya ya 14.2 cha Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032) ambayo inazitaka wizara za kisekta na serikali za mitaa kuandaa mipango ya kila mwaka na ya kila robo mwaka ili kupanga na kutekeleza shughuli za upandaji miti kwa ufanisi zaidi. Maelezo zaidi kuhusu eneo hili yametolewa hapa chini.

**(a) Mikakati ya Urejeshaji Misitu Isiyojitosheleza**

623. Tathmini yangu ya mikakati ya shughuli za urejeshaji misitu nchini ilibaini kwamba mikakati hii haikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na maeneo yaliyoathirika zaidi na ukataji miti. Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Wizara ya Maliasili na Utalii walitegemea lengo la kila mwaka la kupanda miti milioni 1.5 kwa kila halmashauri, bila kuzingatia tofauti zilizopo katika ukubwa wa misitu na viwango vya upotevu wa misitu kwa kila halmashauri nchini.

624. Zaidi ya hayo, mapitio yangu ya Ripoti ya Utambuzi na Ufuatiliaji wa Ukubwa wa Msitu ya Mwaka 2021 yalibaini tofauti katika ukubwa wa misitu na viwango vya ukataji miti kote nchini. Mikoa ya Ruvuma ilikuwa na kiwango cha juu zaidi cha upotevu wa misitu, ikifuatiwa na Lindi, Tabora, na Morogoro. Licha ya tofauti hizi, ukaguzi ulibaini kwamba malengo ya urejeshahi misitu kwa kupanda miti milioni 1.5 kwa kila halmashauri bila kuzingitia utofauti wa ukubwa na upotevu wa misitu kwa kila halmashauri yalikuwa kinyume na aya ya 2.1 cha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Misitu ya Taifa (2021 – 2031), ambayo inasisitiza juu ya ufanyikaji wa uchambuzi wa hali za misitu ili kusaidia katika utengenezaji wa mikakati na malengo ya usimamizi wa misitu inayojitosheleza.

625. Pia, nilibaini kutozingatia vichocheo vya upotevu wa misitu katika mikakati ya urejeshaji misitu. Hii ilidhihirishwa na juhudi za urejeshaji misitu



ISO 9001:2015 Certified

zilizokuwa zinatekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii kutoshughulikia vya kutosha mambo yanayochochea upotevu wa misitu katika mikoa mbalimbali. Hali hii ilitokana na kutokuwapo kwa mfumo rasmi wa uratibu unaohusisha sekta kama ardhi, kilimo na mifugo. Ukaguzi pia ulibaini kuwa, uratibu usiojitosheleza unapunguza ufanisi wa juhudi za urejeshaji misitu wakati wa kushughulikia ukataji miti unaosababishwa na shughuli za kiuchumi katika sekta zingine.

**(b) Mamlaka za Serikali za Mitaa Kutotayarisha Mpango wa Utekelezaji wa Lengo Zililowekewa la Kupanda Miti Milioni 1.5**

626. Mapitio yangu ya mipango ya utekelezaji wa bajeti ya kila mwaka na mahojiano niliyoyafanya na maafisa katika halmashauri sita yalibaini kwamba halmashauri zote sita hazikuandaa mpango wowote wa kusaidia utekelezaji wa lengo la kupanda miti milioni 1.5. Hali hii ni kinyume na aya ya 14.2 ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022–2032), ambayo inazitaka halmashauri kuandaa mipango ya utekelezaji wa upandaji miti kama mojawapo ya shughuli za urejeshaji misitu na hivyo kuathiri ufanisi wa ufikiwaji wa lengo la kupanda miti milioni 1.5.

627. Ukosefu wa mpango wa upandaji miti ulitokana na ufuatiliaji usioridhisha wa shughuli za upandaji miti unaofanywa na OWM - TAMISEMI na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kutokana na hali hii, ukosefu wa mpangokazi ulisababisha kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa, ambapo halmashauri tano kati ya sita zilizotembelewa zilishindwa kufikia malengo yao ya upandaji miti kwa miaka minne mfululizo ya fedha kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25. Aidha, hali hii inapunguza uwezo wa serikali za mitaa wa kubaini na kusimamia changamoto katika uhifadhi na urejeshaji misitu, hivyo kuathiri mafanikio na uendelevu wa juhudi za urejeshaji miti."

**(c) Kutotayarishwa kwa Ufanisi Mipango ya Usimamizi ya Misitu ya Hifadhi**

628. Uchambuzi wangu wa orodha ya hifadhi za misitu ulibaini kwamba, kati ya misitu 2,306 iliyopo nchini, takriban misitu 1,571 sawa na asilimia 68 haikuwa na mpango wa usimamizi wa misitu wa kusaidia katika shughuli za urejeshaji. Hii ina maana kwamba misitu 735 tu, sawa na asilimia 32, ilikuwa na mpango huo. Hali hii ilikuwa kinyume na Kifungu cha 11 cha Sheria ya Misitu, Sura ya 323, ambacho kinataka hifadhi zote za misitu ya taifa, misitu ya serikali za mitaa na ya vijiji kuwa na mpango wa usimamizi wa misitu unaojumuisha utaratibu wa uhifadhi wa misitu, ikiwemo shughuli za urejeshaji .

ISO 9001:2015 Certified

629. Uchambuzi wangu wa ziada kulingana na makundi ya hifadhi za misitu ulionesha upungufu katika uandaaji wa mipango ya usimamizi. Asilimia 58 ya hifadhi zote za misitu za taifa haikuwa na mipango ya usimamizi, asilimia 51 ya misitu ya serikali za mitaa haikuwa na mipango wa usimamizi wa misitu, na asilimia 72 ya misitu ya vijiji haikuwa na mipango hiyo.

630. Kukosekana kwa mipango ya usimamizi wa misitu kwa hifadhi hizi kunamaanisha kwamba misitu hiyo ilisimamiwa bila mfumo maalum wa kusaidia urejeshaji endelevu wa misitu, ikiwemo shughuli za upandaji miti.

### 9.4.2 Utekelezaji wa Shughuli za Urejeshaji Misitu Usiojitosheleza

631. Nilibaini upungufu uliokuwa unaathiri ufanisi na tija ya utekelezaji wa shughuli za urejeshaji misitu. Upungufu huo ulikuwa ni upatikanaji usioridhisha wa miche kwa ajili ya urejeshaji misitu, kufikiwa kwa kiwango kidogo cha malengo ya ukusanyaji mbegu, na hatua zisizojitosheleza za kufuatilia miti baada ya kupandwa ili kuhakikisha ukuaji wake. Maelezo zaidi yametolewa katika sehemu ifuatayo.

#### (a) Upungufu wa Miche kwa ajili ya Shughuli za Urejeshaji wa Misitu

632. Mahojiano yangu na maafisa wa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yalibaini kwamba, wakati wa utekelezaji wa shughuli za urejeshaji misisitu katika halmashauri mbalimbali, miche ilipatikana kutoka vitalu vilivyomilikiwa na Wakala wa Huduma za Misitu. Hali hii ilithibitishwa wakati wa ziara yangu katika halmashauri sita nilizozikagua, ambapo zote zilitegema miche kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Uchambuzi zaidi wa uzalishaji wa miche chini ya Wakala wa Huduma za Misitu ulionesha kwamba miche iliyozalishwa haikutosha kufikia lengo lililokusudiwa la kupanda miti milioni 1.5 katika halmashauri zote 184, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 37.**

**Jedwali Na. 37: Uzalishaji wa Miche Unoafanywa na Wakala wa Huduma za Misitu dhidi ya Mahitaji ya Serikali za Mitaa (2021/22-2024/25)**

| Mwaka | Mahitaji ya Miche katika Halmshauri 184 | Idadi ya Miche Iliyozalishwa na Wakala wa Huduma za Misitu | Upungufu (%) |
|---|---|---|---|
| 2021/22 | 276,000,000 | 33,515,523 | 87.9 |
| 2022/23 | 276,000,000 | 33,068,643 | 88.1 |
| 2023/24 | 276,000,000 | 34,126,916 | 87.7 |
| 2024/25 | 276,000,000 | 35,039,365 | 87.3 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti za Utendaji za Wakala wa Huduma za Misitu za Mwaka 2021/22-2024/25 wa Mwaka 2025

ISO 9001:2015 Certified

633. **Jedwali Na. 37** linaonesha kuwa uzalishaji wa miche kutoka Wakala wa Huduma za Misitu ulikuwa pungufu ya mahitaji yaliyohitajika kwa asilimia 87.9, 88.1, 87.7 na 87.3 katika Miaka ya Fedha 2021/22, 2022/23, 2023/24 na 2024/25 mtawalia. Upungufu huu ulitokana na halmashauri kutotoa kipaumbele katika uanzishaji wa vitalu vya miche kwa ajili ya shughuli za urejeshaji misitu.

634. Kutokana na hali hiyo, upungufu huu uliathiri kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Kati ya halmashauri sita zilizokaguliwa, halmashauri tano hazikufikia lengo la kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka. Ni halmashauri ya Wilaya ya Ushetu pekee iliyofikia lengo hilo, licha ya kutokuwa na kitalu chake cha miche, kwani ilinufaika na msaada uliotolewa na makampuni ya tumbaku ambayo yalianzisha vitalu vya miche ili kuwezesha shughuli za urejeshaji wa misitu wilayani humo.

**(b) Wakala wa Huduma za Misitu Kutotunza Kikamilifu Malengo ya Ukusanyaji Mbegu za Miche Yaliyopangwa**

635. Mapitio yangu ya Mpango Mkakati wa Wakala wa Huduma za Misitu, (2021/22–2024/25) na Ripoti ya Utendaji ya Mwaka wa Fedha 2024/25 yanaonesha kwamba, licha ya ongezeko la vyanzo vya mbegu za miti kutoka hekta 270 Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi hekta 689.5 Mwaka wa Feda 2024/25, mwenendo wa ukusanyaji wa mbegu hizi ulikuwa ukipungua . Hali hii ni kinyume na aya ya 6.3 ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Misitu ya Taifa (2021–2031), ambayo inaitaka Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia Wakala wa Huduma za Misitu, kuhakikisha upatikanaji wa mbegu za miti ili kuunga mkono utekelezaji wa mipango ya urejeshaji misitu.

636. Mahojiano yangu na maafisa kutoka Wakala wa Huduma za Misitu, yalibaini kuwa upungufu wa ukusanyaji wa mbegu ulitokana na idadi ndogo ya wapandaji miti waliobobea katika kupanda na kukusanya mbegu kutoka misituni na kuzipeleka katika vituo vya miche kwa ajili ya uoteshaji.

637. Kutokana na hali hiyo, Wakala wa Huduma za Misitu, ilishindwa kukidhi mahitaji yaliyobainishwa. Ingawa Mpango Mkakati wake wa Miaka ya Fedha 2021/22–2024/25 unabainisha uhitaji wa tani 40 za mbegu kwa mwaka, ukusanyaji halisi wa mbegu ulikuwa kati ya tani 25.3 hadi 29.4 kwa mwaka katika kipindi cha miaka minne ya fedha, kutokana na mbinu za ukusanyaji zisizojitosheleza.

### (c) Ukosefu wa Udhibiti na Utunzaji wa Miche baada ya Kupandwa

638. Mahojiano yangu na maafisa wa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yalibaini kwamba, halmashauri hazikuanzisha mfumo rasmi wa kutunza miche baada ya kupandwa ili kuhakikisha kuwa inastawi vizuri. Hali hii ilithibitishwa kupitia ukaguzi wangu katika halmashauri sita, ambapo nilibaini kwamba hakuna halmashauri yoyote iliyokuwa na mfumo rasmi wa kufuatilia miti iliyopandwa kila mwaka na kuhakikisha inasitawi vizuri. Hali hii ni kinyume na Kifungu cha 20(10) na Kifungu cha 66(2)(c) cha Sheria ya Misitu, Sura ya 323, ambacho kinaitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Wakala wa Huduma za Misitu, na Ofisi ya Waziri - TAMISEMI kupitia serikali za mitaa kufuatilia ukuaji wa miti baada ya kupandwa, ikiwemo utoaji wa mafunzo na ushirikishaji wa jamii.

639. Ukaguzi ulibaini kwamba ukosefu wa kutosha wa mbinu za kufuatilia na kutunza miti baada ya kupandwa ulitokana na kutokuwapo kwa mpango kamili wa upandaji miti unaoeleza namna ya utekelezaji na ufuatiliaji wa shughuli za urejeshaji misitu. Hali hii pia ilisababisha halmashauri kutekeleza malengo ya upandaji miti bila kuzingatia uendelevu na ustahimilivu wa miti iliyopandwa.

## 9.4.3 Uratibu Usiojitosheleza Kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI katika Usimamizi wa Shughuli za Urejeshaji Misitu

NATIONAL AUDIT OFFICE NAOT
ISO 9001:2015 Certified

640. Tathmini yangu ya uratibu katika utekelezaji wa shughuli za urejeshaji misitu ilibaini upungufu katika utoaji wa taarifa za maendeleo ya urejeshaji wa misitu, ushirikiano kati ya serikali za mitaa na Wakala wa Huduma za Misitu, na uratibu wa mchango wa asasi za kiraia katika shughuli za urejeshaji misitu, kama inavyoelezwa hapa chini.

### (a) Kutojitosheleza kwa Utoaji wa Ripoti za Utekelezaji wa Shughuli za Urejeshaji Misitu Nchini

641. Nilibaini kwamba ingawa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ilikuwa imekusanya takwimu za upandaji miti kutoka serikali za mitaa kupitia ombi la Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, takwimu hizo hazikuwasilishwa katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Hali hii ni kinyume na sura ya 7.6.3 ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Misitu wa 2021–2031, ambayo inazitaka taasisi zinazotekeleza sera ya misitu kuandaa ripoti za utendaji kwa vipindi husika, zikieleza mafanikio ya shughuli za urejeshaji misitu.

642. Zaidi ya hayo, nilibaini kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii, ambayo inawajibika kusimamia utekelezaji wa mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Misitu, haikusisitiza uzingatiaji wa utaratibu wa utoaji taarifa uliowekwa. Kutokuwapo kwa utoaji ripoti jumuishi na mijadala ya wadau ya mara kwa mara kulizuia utambuzi na ufumbuzi wa changamoto, ikiwemo ukataji haramu wa miti, uvamizi, na uharibifu wa misitu. Hivyo basi, juhudi za kufikia malengo ya kitaifa ya upandaji miti na uhifadhi wa misitu ziliathiriwa.

643. Pia, nilibaini kwamba Wakala wa Huduma za Misitu, huandaa ripoti za utendaji wa kila mwaka zinazoeleza mafanikio katika shughuli za urejeshaji misitu, ikiwemo uzalishaji wa miche, uandaaji wa mipango ya usimamizi wa misitu na miradi mingine ya uhifadhi. Licha ya ripoti ya Wakala wa Huduma za Misitu kuingizwa kwenye ripoti ya utekelezaji ya kila mwaka ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ripoti hizi hazikujadiliwa katika vikao vya mapitio ya kila mwaka ili kutathmini ufikiwaji wa malengo ya sera, kama inavyohitajika katika mkakati.

**(b) Kutoratibiwa na Kufuatiliwa kwa Ufanisi wa Michango ya Asasi za Kiraia katika Shughuli za Urejeshaji Misitu**

644. Mahojiano yangu na maafisa wa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yalibaini kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI haikufuatilia shughuli za urejeshaji misitu unaofanywa na asasi za kiraia ili kutathmini utendaji wao katika uhifadhi wa misitu. Hali hii ni kinyume na aya ya (vii) ya Mwongozo wa Usimamizi wa asasi za kiraia, 2024, ambayo inaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kuratibu na kufuatilia utendaji wa asasi za kiraia shughuli zake ikiwemo urejeshaji wa misitu.

645. Zaidi ya hayo, kufuatia mazungumzo yangu na asasi za kiraia tatu, nilibaini kwamba shughuli zao ndani ya halmashauri ziliripotiwa rasmi kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalum kila mwaka. Hata hivyo, hakukuwa na utaratibu uliopangwa wa utoaji ripoti kwenda Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, licha ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kuwa na mamlaka ya kusimamia na kufuatilia shughuli za asasi za kiraia, ikiwemo shughuli za urejeshaji misitu katika halmashauri mbalimbali.

646. Pia, nilibaini kwamba uratibu wa asasi za kiraia usiojitosheleza ulitokana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kutokuwa na kanzidata ya asasi zinazotekeleza shughuli zinazohusiana na urejeshaji misitu nchini. Pia, kulikuwa na uratibu usioridhisha kati ya asasi hizi, Maafisa wa Madawati ya asasi za kiraia na maafisa wa misitu katika halmashauri mbalimbali.

647. Uratibu na ufuatiliaji wa asasi za kiraia usiojitosheleza ulisababisha utendaji wao kutotathminiwa, kwani asasi hizi hazikuripoti kwa maafisa wa misitu wa halmashauri husika na ushirikiano baina ya serikali ulitokea zaidi kupitia maombi ya asasi kufanya kazi na jamii badala ya maombi kwa ajili ya usimamizi natathmini, jambo liloleta mazingira magumu wakati wa ufuatilaji wa mchango wa asasi hizi katika shughuli za urejeshaji misitu.

**(c) Ushirikiano Usiojitosheleza kati ya Wakala wa Huduma za Misitu na Serikali za Mitaa katika Utekelezaji wa Shughuli za Urejeshaji Misitu**

648. Mapitio yangu ya mipango ya mwaka na ripoti za utendaji (2021/22–2024/25) kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, na Wakala wa Huduma za Misitu, pamoja na mahojiano na maafisa wa halmashauri nilizotembelea, yalibaini kuwa ushirikiano katika utekelezaji wa shughuli za urejeshaji misitu ulikuwa mdogo. Ushirikiano kati ya taasisi hizi mara nyingi ulifanyika tu wakati wa matukio ya kitaifa kama sherehe za mwenge wa uhuru, siku za kimataifa za upandaji miti, na siku za kimataifa za mazingira. Katika matukio haya, maafisa wa misitu wa Wilaya na wahifadhi wa misitu wa wilaya hufanya shughuli za upandaji miti katika halmashauri zao husika.

649. Ushirikiano usiojitosheleza miongoni mwa wadau ulitokana na Wizara ya Maliasili na Utalii kutofanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango ya urejeshaji misitu inayotekelezwa na Wakala wa Huduma za Misitu na mamlaka za serikali za mitaa, jambo lililopunguza ushirikiano kati ya pande hizo mbili. Hali hii kwa upande mwingine iliathiri utekelezaji wa ufanisi wa Sera ya Misitu ya Taifa, hasa katika kufanikisha malengo ya kitaifa ya urejeshaji miti.

### 9.4.4 Kutojitosheleza kwa Ufuatiliaji na Tathmini wa Shughuli za Urejeshaji Miti Zinazotekelezwa Wakala wa Huduma za Misitu na Serikali za Mitaa

650. Nilitathmini shughuli za ufuatiliaji zinazofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI katika kuangalia hali ya utekelezaji wa Serikali za Mitaa na Wakala wa Huduma za Misitu na kubaini upungufu katika ufuatiliaji wa shughuli hizo. Upungufu uliobainika ulihususiana na uanzishaji wa nyenzo za ufuatiliaji usiojitosheleza, ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za urejeshaji misitu usioridhisha na tathmini ya utendaji wa Wakala wa Huduma za Misitu na serikali za mitaa usiojitosheleza katika kutekeleza malengo ya urejeshaji misitu waliyojiwekea. Changamoto hizi zimetolewa maelezo yake katika sehemu ifuatayo:

**(a) Kutojitosheleza kwa Uandaaji wa Nyenzo za Ufuatiliaji wa Urejehaji na Uhifadhi wa Misitu**

651. Tathmini yangu ya nyenzo za ufuatiliaji ilibaini uandaaji usiojitosheleza wa nyenzo hizi. Hali hii ilionekana kutokana na mapitio yangu ya Mpango Mkakati wa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI wa Miaka ya Fedha 2021/22 – 2025/26, ambapo nilibaini kutowekwa kwa vigezo na viashiria vya utendaji vinavyotumika wakati wa ufutiliaji wa utekelezaji wa shughuli za urejeshaji misitu. Hali hii ni kinyume na aya ya 4.4.1 ya Sera ya Misitu ya Taifa (1998), inayosisitiza taasisi za usimamizi wa misitu kuwa na mikakati ya uhifadhi na usimamizi wa misitu inayojitosheleza ili kuhakikisha usimamizi na uhifadhi bora wa misistu nchini.

652. Kutokuwapo kwa viashiria vya utendaji katika Mpango Mkakati kumezuia uwezo wa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kufuatilia na kutathmini ufanisi wa shughuli za urejeshaji na uhifadhi wa misitu. Kutokana na hali hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI haikuwa na kigezo na msingi wa kubaini changamoto zinazozikumba shughuli za urejeshaji na uhifadhi wa misitu, na hivyo kushindwa kuchukua hatua za haraka ili kutatua changamoto zitazozobainika.

**(b) Kutokufuatilia Utekelezaji wa Shughuli za Urejeshaji Miti**

653. Mapitio yangu ya Ripoti za Utendaji za Kila Mwaka (2021/22–2024/25) za Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, pamoja na mahojiano na maafisa kutoka wizara hizi yalibaini kwamba wizara hizi hazikufatilia kikamilifu utekelezaji wa shughuli za urejeshaji misitu.

654. Ufuatiliaji usiojitosheleza ulitokana na kutoingizwa kwa shughuli za urejeshaji misitu kwenye mipango ya ufuatiliaji, huku kipaumbele cha wizara hizi kikiwa programu za misitu zinazofadhiliwa na wahisani na miradi ya maendeleo. Hali hiyo, imepunguza uwezo wa wizara wa kubaini na kushughulikia changamoto za utekelezaji, kama vile idadi ndogo ya miche inayokua na kustawi baada ya kupandwa, ushirikishaji mdogo wa jamii, uvamizi wa misitu, na ucheleweshaji wa utekelezaji wa mipango ya usimamizi wa misitu.

### (c) Tathmini ya Wizara ya Maliasili na Utalii Pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI katika Utekelezaji wa Shughuli za Urejeshaji Misitu

#### (i) Wizara ya Maliasili na Utalii Kutotathmini Utendaji wa Wakala wa Huduma za Misitu katika Utekelezaji wake wa Shughuli za Urejeshaji Misitu

655. Mapitio yangu ya ripoti za utekelezaji wa kila mwaka kwa Miaka ya Fedha 2021/22 hadi 2024/25 yalibaini kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii haikutathmini ipasavyo utendaji wa Wakala wa Huduma za Misitu, katika shughuli za urejeshaji misitu, ikiwemo kutathmini maendeleo yake dhidi ya hatua za zilizopangwa. Hali hii ni kinyume na aya ya 4.8.1 ya Mpango Mkakati wa Wizara ya Maliasili na Utalii wa Miaka ya Fedha 2021/22 – 2025/26, ambao unaitaka wizara kufanya tathmini ya miradi iliyotekelezwa kila mwaka.

656. Kutokuwapo kwa tathmini kumepunguza uwezo wa wizara kutathmini kiwango cha uchangiaji wa shughuli za urejeshaji misitu katika kuboresha juhudi za uhifadhi wa misitu.

#### (ii) Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI Kutotathmini Utendaji wa Mamlaka za Serkali za Mitaa katika Utekelezaji Katika Shughuli za Urejeshaji Misitu

657. Mapitio yangu ya ripoti za utekelezaji wa Kila Mwaka kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25 yalibaini kwamba tathmini za shughuli za urejeshaji misitu katika Serikali za Mitaa haikufanyika ipasavyo. Hali hii ilipunguza uwezo wa wizara kutathmini maendeleo na ufanisi katika kukuza juhudi za urejeshaji misitu katika halmashauri zote nchini.

658. Aidha, nilibaini kwamba ingawa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ilipokea kila mwaka takwimu za upandaji miti kutoka halmashauri nchini, hata hivyo hakuna uchambuzi wowote uliofanyika kutathmini utendaji wa halmashauri hizo dhidi ya lengo la kupanda miti milioni 1.5 kwa mwaka. Hali hii ilisababishwa na ukosefu wa viashiria kamili vya utendaji kwa ajili ya kupima matokeo ya utekelezaji wa shughuli za urejeshaji misitu. Kwa namna hiyo, hapakuwa na hatua zozote zilizochukuliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI dhidi ya halmashauri ambazo hazikufanya vizuri katika utekelezaji wa lengo hilo.

ISO 9001:2015 Certified

## 9.5 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Nishati Jadidifu

659. Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi yanayohusu usimamizi wa miradi ya nishati jadidifu.

### 9.5.1 Mchango Usiojitosheleza wa Miradi ya Nishati Jadidifu katika Mchanganyiko wa Nishati Uliokusudiwa

660. Nilibaini kuwa mchango wa nishati jadidifu, hususani nishati ya jua, upepo, na jotoardhi, uliendelea kuwa chini sana ya malengo ya kitaifa katika kipindi chote cha Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25. Licha ya maboresho ya hatua kwa hatua katika nishati ya maji yaliyofanya mchango wa maji kufikia asilimia 66.9 kufuatia kuzinduliwa na kuanza kwa sehemu ya uendeshaji wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Mwalimu Julius Nyerere, miundombinu isiyotosheleza ya kusafirisha umeme imesababisha matumizi madogo ya nishati ya maji inayozalishwa.

661. Kwa ujumla, sehemu ya nishati jadidifu (bila kujumuisha miradi mikubwa ya nishati ya maji) ilibaki chini ya asilimia tano, ikilinganishwa na makadirio ya asilimia 15 ya Mpango Kabambe wa Mfumo wa Umeme wa mwaka 2024. Nilibaini kuwa, upungufu katika uzalishaji wa nishati kutoka kwa vyanzo jadidifu yametokana na kuchelewa kwa uendelezaji wa miradi na ukosefu wa ufanisi wa kiutendaji katika sekta mbalimbali za nishati jadidifu.

NAOT
ISO 9001:2015 Certified

662. Mambo yafuatayo pia yamechangia kuwapo kwa kasi ndogo ya ufikiaji wa malengo ya nishati jadidifu ya katika Mchanganyiko wa Nishati ya Taifa:

**(a) Kutoa Kipaumbele kwa Miradi ya Gesi Asilia na Nishati ya Maji**

663. Kupitia Mapitio ya ripoti za Maendeleo za Wizara ya Nishati, nilibaini kwamba, vipaumbele vya kitaifa kati ya mwaka 2021 na 2025 viliendelea kutilia mkazo miradi ya gesi asilia na miradi mikubwa ya maji kama vile Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Mwalimu Julius Nyerere (MW 2,115), Ruhudji (MW 358), Rumakali (MW 222), Malagarasi (MW 49.5), Kikonge (MW 300), na Kakono (MW 87), kwa gharama ya miradi ya nishati jadidifu, hususani nishati ya jua na upepo. Mfumo huu wa uwekezaji unaonesha upendeleo endelevu kuelekea miradi ya gesi na miradi mikuwa ya nishati ya maji, jambo linalokwamisha mseto wa vyanzo vya nishati na kucheleweshа ufikiaji wa malengo ya mchanganyiko wa nishati jadidifu kama yaliyovyofafanuliwa na Mpango Kabambe wa Mfumo wa Umeme wa mwaka 2024.

### (b) Kukosekana kwa Mipango ya Utekelezaji ya Mpango Kabambe wa Mfumo wa Umeme, 2020

664. Mapitio ya Mpango Kabambe wa Mfumo wa Umeme wa mwaka 2020 na Makubaliano ya Kitaifa ya Nishati ya mwaka 2025 yalibaini kuwa mifumo wezeshi ya kuvutia uwekezaji katika nishati jadidifu haikuanza kutumika katika kipindi cha mwaka 2020 hadi mwaka 2025. Kukosekana kwa mikakati ya utekelezaji chini ya Mpango kabambe wa Mfumo wa Umeme kulisababisha pengo kati ya sera na utekelezaji, jambo lililochochea kuchelewa kwa mipango muhimu kama vile Mfumo wa Ununuzi wa Nishati kutoka kwa wazalishaji binafsi wa nishati jadidifu, ambao ulisogezwa mbele hadi mwaka 2026. Hii inaashiria maandalizi madogo ya kitaasisi na uratibu duni katika kutekeleza vipaumbele vya nishati jadidifu.

665. Kutokana na mambo haya, mchango wa nishati jadidifu katika mchanganyiko wa nishati ya taifa ulibaki palepale chini ya asilimia 5, ikiwa ni chini ya lengo la asilimia 15 lililowekwa kwa mwaka 2025. Kuchelewa kuanza kutumika kwa makadirio ya Mpango Kabambe wa Mfumo wa Umeme Nchini kumepunguza kasi ya kuwapo kwa mseto wa vyanzo vya nishati, kumeondoa imani ya wawekezaji, na kukwamisha mwelekeo wa nchi katika mfumo wa nishati thabiti na uliolingana.

### 9.5.2 Kutokamilika kwa Utwaaji wa Maeneo ya Kimkakati Yaliyoibuliwa katika Marekebisho ya Mpango Kabambe wa Mfumo wa Umeme Nchini wa Mwaka 2020

ISO 9001:2015 Certified

666. Nilibaini kuwa maeneo 45 ya miradi ya kuzalisha umeme yaliyoibuliwa chini ya Mpango Kabambe wa Mfumo wa Umeme wa mwaka 2020 hayajatwaliwa rasmi. Maeneo hayo ni kwa ajili ya miradi yenye uwezo wa jumla wa megawati (MW) 5,705.6 kwa ajili ya mipango ya muda mfupi ifikapo mwishoni mwa mwaka 2028, ikijumuisha MW 2,995.6 za nishati ya maji, MW 715 za nishati ya jua, MW 1,000 za upepo, na MW 995 za jotoardhi. Kinyume na ibara ya 4(6) ya kanuni za umeme (Uendelezaji wa Miradi Midogo ya Umeme) za mwaka 2020, hakuna mradi hata mmoja kati ya hiyo uliopiga hatua kuelekea hatua ya kutengwa kwa ardhi au utwaaji wa rasilimali.

667. Aidha, si Shirika la Umeme Tanzania wala mamlaka za serikali za mitaa zilizoweka mipaka katika maeneo yaliyoibuliwa ili kuzuia uvamizi kabla ya utwaaji rasmi. Hali hii inaongeza hatari ya uvamizi na uwezekano wa migogoro ya ardhi. Kukosekana kwa uhakikishaji wa ardhi na uwekaji mipaka kwa wakati unaonesha kuwa Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania hazijatoa kipaumbele katika utwaaji rasmi wa maeneo haya ya kimkakati. Kukosekana

kwa ulinzi wa mapema wa kisheria au wa kiutawala wa ardhi kunaacha maeneo yaliyoibuliwa na Mrabi Kabambe wa Mfumo wa Umeme katika hatari ya kuvamiwa, kuchelewa, kugawiwa upya, na gharama kubwa zaidi ya utekelezaji.

### 9.5.3 Utekelezaji Usioridhisha wa Miundombinu ya Kusafirisha Umeme wa Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Mwalimu Julius Nyerere

668. Nilibaini kuwa miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere haijakamilika, jambo linalokwaza matumizi ya uwezo wa uzalishaji uliowekwa na uimarishaji wa gridi ya taifa, kinyume na Mpango Kabambe wa Mfumo wa Umeme wa mwaka 2020 uliyolenga kukamilisha kwa njia za kusafirisha umeme za Chalinze–Dodoma na Chalinze–Kinyerezi kufikia mwaka 2022. Kwa mujibu wa Mpango Kabambe wa Mfumo wa Umeme na Ripoti ya Maendeleo ya hadi Desemba 2025, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya Kilovoti 400 ya Chalinze–Dodoma, ambayo ni ushoroba muhimu wa usafirishaji umeme wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, ulikuwa umefikia asilimia 55.37. Aidha tarehe ya kutarajiwa kukamilika ni Septemba 2026. Aidha, nilibaini kuwa Wizara ya Nishati inatekeleza mradi wa njia ya kusafirisha umeme ya Kilovoti 400 ya Chalinze–Mkuranga, ambayo itaimarisha zaidi usafirishaji wa umeme kutoka Bwawa la Mwl. Julius Nyerere, na kwamba mradi huo umefikia asilimia 48.07 na unatarajiwa kukamilika kufikia Novemba 2026.


669. Licha ya mradi wa uzalishaji umeme wa Bwawa la Mwl. Nyerere kukamilika na kuwa tayari kwa uendeshaji kamili, miundombinu iliyopo ya usafirishaji umeme imeshindwa kusafirisha jumla ya uwezo uliowekwa wa MW 2,115. Hadi kufikia Desemba 2025, ni mitambo minne tu iliyokuwa ikifanya kazi, ikizalisha takriban MW 940, huku mitambo mitano inayowakilisha takriban asilimia 55 ya uwezo wa bwana ikibaki bila kutumika kutokana na kutotosheleza kwa uwezo wa kusafirisha umeme kwenda kwenye gridi kuu.

670. Kuchelewa kwa ukamilishaji wa miundombinu ya kusafirisha umeme katika mradi wa JNHPP kunatokana na kutotengwa kwa fedha za kutosha kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi ya njia za kusafirisha umeme zilizosanifiwa. Matokeo yake, Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Mwalimu Julius Nyerere limeshindwa kusafirisha uwezo wake wa juu wa uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya mfumo yanapohitajika, na kuacha MW 1,175 za uwezo uliowekwa bila kutumika, kiasi ambacho ni sawa na mitambo mitano, ambapo kila moja una uwezo wa kuzalisha MW 235.

### 9.5.4 Uzalishaji wa Nishati Jadidifu Usiokuwa na Uhakika Kutokana na Mabadiliko katika Matumizi ya Mitambo

671. Nilibaini kuwa, utendaji wa mitambo ya nishati jadidifu, uliopimwa kwa matumizi ya mitambo, ulionesha mabadiliko makubwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2024, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 36.** Matumizi ya mitambo huonesha uwiano wa uzalishaji halisi ikilinganishwa na uwezo wa juu zaidi wa uzalishaji ikiwa mtambo ungefanya kazi kwa uwezo wake wote mwaka mzima, na hivyo hutumika kama kiashiria muhimu cha ufanisi, uhakika, na matumizi ya uwezo uliowekwa. **Kielelezo Na. 37** kinaonesha wastani na mchepuko wa kawaida wa uwezo wa matumizi kwa kila mtambo.

**Kielelezo Na. 37: Kiwango cha Matumizi ya Mitambo ya Kuzalisha Umeme**




***Chanzo:*** **Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Zinazohusu Uzalishaji wa Nishati Jadidifu za Mwaka 2021-2024 wa Mwaka 2025**

672. Kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 37,** vituo vya kufua umeme wa maji vilirekodi viwango vya juu zaidi vya wastani wa matumizi, vikianzia asilimia 40 hadi 48, jambo linalothibitisha mchango wake mkubwa katika uzalishaji wa nishati jadidifu. Kinyume chake, miradi ya nishati ya jua na bayomasi ilionesha mara kwa mara viwango vya chini vya matumizi, vikiwa wastani wa chini ya asilimia 15 katika kipindi chote. Hali hii inaashiria ufanisi mdogo wa kiutendaji na mchango mdogo katika mchanganyiko wa nishati. Wastani wa jumla wa matumizi wa asilimia 21.6 unaonesha kuwa, licha ya kuongezeka kwa uwezo wa uzalishaji uliowekwa, sekta ya nishati jadidifu bado haitumiki kikamilifu.

673. Matokeo zaidi yanaonesha kuwa, ingawa uzalishaji wa nishati jadidifu kitaifa uliongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka Gigawati-saa 2,573 mwaka 2023 hadi Gigawati-saa 6,125 mwaka 2024, ikiashiria uthabiti wa uzalishaji bado ni changamoto. Utegemezi mkubwa wa nishati ya maji, ukichangiwa na mabadiliko makubwa katika matumizi ya mitambo, huongeza vihatarishi kutokana na mabadiliko ya msimu ya mtiririko wa maji na mabadiliko ya tabianchi. Kukosekana kwa mchango thabiti kutoka kwa teknolojia zingine za nishati jadidifu, hususani upepo na jua, kumeongeza zaidi hatari ya kutokuwa na uhakika wa nishati.

### 9.5.5 Ukaguzi Usioridhisha wa Vituo vya Kufua Umeme vyenye Leseni na Vilivyosajiliwa

674. Nilipitia Mipango Kazi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Ripoti ya Utekelezaji, na Ripoti za Ukaguzi kwa Miaka ya Fedha 2021/22 hadi 2024/25 na kubaini kuwa Mamlaka ya Udhibiti Huduma za Nishati na Maji haikufanya ukaguzi wa kutosha wa vituo vya kufua umeme vyenye leseni na vilivyosajiliwa. Kwa wastani, Mamlaka ilikagua asilimia 19 tu ya vituo vyenye leseni na asilimia 3 ya vituo vilivyosajiliwa katika kipindi cha miaka ya fedha minne iliyofanyiwa mapitio kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25.

675. Kumbukumbu zaidi zilionesha kiwango cha chini cha ukaguzi katika Mwaka wa Fedha 2022/23 kwani ni vituo viwili tu vilivyosajiliwa kati ya 34 vilikaguliwa, wakati katika Mwaka wa Fedha 2024/25, hakuna kituo chochote kilichosajiliwa kilichokaguliwa. Hali hii ni kinyume na Kifungu cha 31 cha Sheria ya Umeme ya mwaka 2008, kinachoipa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji mamlaka ya kufuatilia na kudhibiti watoa huduma wote wa nishati wenye leseni, ikijumuisha kufanya ukaguzi baada ya mitambo kuanza kazi ili kuhakikisha uzingatiaji wa viwango vya kiufundi, masharti ya leseni, mahitaji ya usalama, na vigezo vya uhakika wa huduma.

676. Ingawa idadi ya vituo vya kufua umeme vyenye leseni na vilivyosajiliwa iliongezeka kutoka 87 Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 127 Mwaka wa Fedha 2024/25, ukaguzi haukuendana na kasi ya upanuzi wa sekta hiyo. Kwa sababu hii, vituo vingi vinavyofanya kazi haikufanyiwa uhakiki wa kisheria na tathmini za ufuatiliaji wa utekelezaji wa masharti wakati kipindi cha ukaguzi.

## 9.6 Athari za Changamoto Zilizobainika katika kufikia Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

### 9.6.1 Athari za Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Nchini katika Ufikiwaji wa Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

677. Utekelezaji usioridhisha wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika sekta za maji, kilimo, na nishati nchini umeathiri uwezo wa nchi kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu yanayohusiana na sekta hizo. Maendeleo yasiyotosheleza katika maeneo kama vile usimamizi wa rasilimali za maji, kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi na mifumo ya nishati inayostahimili mabadiliko ya tabianchi yameongeza hali ya athari kwa jamii, kupunguza uzalishaji wa kilimo, na kuongeza utegemezi wa vyanzo vya nishati vinavyoathiriwa kwa urahisi na mabadiliko ya hali ya tabia nchi.

678. Upungufu huu unadhoofisha juhudi za kuhakikisha ukuaji wa uchumi endelevu, usalama wa chakula, upatikanaji wa maji safi na nishati, pamoja na ulinzi wa mfumo wa ikolojia, ambayo ni malengo ya msingi ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Aidha, utekelezaji usioridhisha wa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi unakwamisha maendeleo ya kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, hususani yale yanayohusu kutokomeza njaa, uzingatiaji wa maji safi na usafi wa mazingira, nishati nafuu na safi, pamoja na hatua dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

### 9.6.2 Athari za Ukaguzi wa Utendaji kuhusu Usimamizi wa Shughuli za Urejeshaji Upya wa Misitu katika Ufikiwaji wa Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

679. Usimamizi usioridhisha wa shughuli za upandaji upya wa misitu unadhoofisha ufikiwaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa kuharakisha uharibifu wa misitu, kupunguza huduma za mfumo wa ikolojia, na kudhoofisha uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Hali hii inachangia kuendelea kwa ukataji miti, kupotea kwa anuai ya viumbe hai, na kupungua kwa uwezo wa kufyonza hewa ya ukaa, na hivyo kuhatarisha malengo ya uendelevu wa mazingira yaliyowekwa katika ngazi za kitaifa na kimataifa.

680. Zaidi ya hayo, hali hii inahatarisha maisha ya watu wanaotegemea misitu, inaongeza hatari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi, na kuzuia ukuaji wa uchumi endelevu nchini Tanzania. Matokeo yake, inadhoofisha malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na kupunguza kasi ya maendeleo kuelekea Malengo ya Maendeleo Endelevu yanayohusu kupunguza umaskini, uzingatiaji wa usalama wa chakula, nishati safi, hatua dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, na ulinzi wa mfumo wa ikolojia, na hivyo kukwamisha maendeleo ya taifa na ahadi za kimataifa za maendeleo endelevu.

### 9.6.3 Athari katika Kufikia Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Nishati Jadidifu

681. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Mpango wake wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ililenga kupanua upatikanaji wa nishati jadidifu kama sehemu ya lengo lake pana la kuboresha maisha ya watanzania na kusaidia ukuaji wa viwanda. Mpango huo unabainisha nishati ya jua, upepo, bayomasi, na vyanzo vingine vya nishati safi kama suluhisho muhimu kwa ajili ya kufikisha umeme vijijini na kupunguza uharibifu wa mazingira. Aidha, unasisitiza upanuzi wa upatikanaji wa nishati jadidifu kwa jamii zisizofikiwa na huduma za umeme. Vilevile, unahamasisha ushiriki wa sekta binafsi kupitia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi pamoja na vivutio vya uwekezaji, ikijumuisha uhamasishaji na uendelezaji wa teknolojia za nishati jadidifu (kama vile gesi ya viumbe, jotoardhi, gesi ya petroli iliyoshindiliwa, jua, na upepo), hususani kwa kaya za vijijini na mipango ya nishati safi ya kupikia, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

682. Lengo la 7 la Maendeleo Endelevu linasisitiza kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya gharama nafuu, ya uhakika, endelevu, na ya kisasa kwa wote, hususani Shabaha ya 7.2, inayotaka ongezeko kubwa la mchango wa nishati jadidifu katika mchanganyiko wa nishati duniani. Ingawa juhudi za kufikia Lengo la 7 la Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano zimetambuliwa, zinahitaji hatua madhubuti zaidi. Hata hivyo, Serikali inakabiliwa na changamoto za mpito kutoka kwenye vyanzo vya nishati visivyojadidifu kwenda kwenye vyanzo safi na vyenye ufanisi zaidi, kama ilivyobainishwa katika matokeo ya ukaguzi. Licha ya kuwa na uwezo wa kuzalisha nishati jadidifu, kama vile jua, upepo, maji, na jotoardhi, nchi inaendelea kukabiliwa na changamoto katika kuhakikisha kunakuwapo na mchango wa kutosha wa miradi ya nishati jadidifu kwenye mchanganyiko wa nishati uliokusudiwa, utwaaji wa maeneo ya kimkakati yaliyoibuliwa kwa ajili

ya uanzishaji wa nishati jadidifu, na uzalishaji wa nishati jadidifu usiokuwa na uhakika kutokana na mabadiliko katika matumizi ya mitambo.

ISO 9001:2015 Certified

## SURA YA KUMI

## USIMAMIZI WA TARATIBU ZA USHIRIKISHWAJI WA WAZAWA KATIKA SEKTA YA MADINI

### 10.1 Utangulizi

683. Sura hii inatoa matokeo ukaguzi wa ufanisi katika Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini. Vilevile, sura hii inaelezea maeneo ya ukaguzi, wizara na taasisi za serikali zilizohusika katika ukaguzi, uhusiano wa ukaguzi na athari za matokeo yake katika Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

#### 10.1.1 Usuli

684. Mwongozo ya Taifa wa Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta Mbalimbali za Uchumi wa mwaka 2019 unaeleza kuwa ushirikishwaji wa wazawa ni thamani iliyoongezwa katika uchumi kupitia matumizi ya makusudi ya rasilimaliwatu na bidhaa za Kitazania katika ajira, ununuzi, urithishwaji wa teknolojia, uongezaji thamani, na uongezaji wa ujuzi. Licha ya kwamba nchi kuwa na utajiri mkubwa wa madini na gesi asilia, ushiriki wa wazawa katika sekata hii bado ni mdogo.

685. Ili kushughulikia changamoto hii, Serikali ilianzisha Sera ya Kitaifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 inayolenga kupanua wigo wa unufaikaji wa wazawa katika fursa za kiuchumi kulingana na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025. Katika sekta ya madini, Wizara ya Madini ilitekeleza malengo haya kwa kuandaa sera na Sheria ya Madini (Sura ya 123) ya mwaka 2019 na Kanuni za Uwezeshaji wa Wazawa kwenye Sekta ya Madini za mwaka 2018 na marekebisho yake, zinazolenga kuimarisha ushirikishwaji wa wazawa katika sekta hii. Ingawa Serikali imewekeza nguvu katika ushirikishwaji wa wazawa kwenye sekta ya madini, juhudi hizi zimekumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo; ajira chache, ufinyu wa ujuzi, pamoja na urithishwaji wa teknolojia usiojitosheleza[12].

[12] Kinyondo, A. (2024b). Local Content Management in Tanzania's Extractive Sector: How effective is it? The Extractive Industries and Society, DOI: https://doi.org/10.1016/j.exis.2024.101435.

### 10.1.2 Uhusiano wa Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano

686. Usimamizi mzuri wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini unachangia moja kwa moja ufikiaji wa malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa kuimarisha uwajibikaji na kuhakikisha kuwa matumizi ya rasilimali za madini yanaleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Uhusiano wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini na mipango hii umeainishwa hapa chini.

**(a) Uhusiano na Mpango wa Tatu wa Taifa Maendeleo wa Miaka Mitano**

687. Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini una uhusiano wa moja kwa moja na malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ambao unasisitiza juu ya mabadiliko ya kiuchumi na ukuaji wa viwanda na uchumi. Pia, mpango huu unasisitiza juu ya kuimarisha tija katika sekta za kiuchumi, kuimarisha uongezaji thamani, kuongeza ushiriki wa wazawa katika viwanda vya kimkakati, na utengenezaji wa fursa za ajira kwa wazawa. Ukaguzi huu unaendana moja kwa moja na malengo haya kwani umejikita katika kuangalia kama taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini zimesimamiwa ipasavyo ili kuongeza fursa za ajira, ununuzi wa bidhaa na huduma za Kitanzania, urithishwaji wa teknolojia, ukuzaji wa ujuzi wa wazawa na kuongeza thamani za madini nchini.

**(b) Uhusiano na Maendeleo Endelevu**

688. Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini una uhusiano na Malengo ya Maendeleo Endelevu, hasa lengo la 8 linalohimiza utengenezaji fursa za ajira; lengo la 9 linalohimiza ukuaji wa viwanda vya ndani, urithishwaji wa teknolojia, na uongezaji thamani wa bidhaa, pamoja na lengo la 12 linalohimiza usimamizi bora na endelevu wa maliasili.

### 10.1.3 Mikakati na Jitihada za Serikali katika Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini

689. Serikali, kupitia Wizara ya Madini, Tume ya Madini, na Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi imeweka mikakati na jitihada mbalimbali

ISO 9001:2015 Certified

katika usimamizi wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini, kama ilivyobainishwa katika **Jedwali Na. 38.**

**Jedwali Na. 38: Mikakati na Jitihada za Serikali katika Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini**

| Taasisi | Mkakati | Jitihada |
|---|---|---|
| Wizara ya Madini | Mpango Mkakati wa Wizara ya Madini wa Mwaka (2019/20-2023/24) pamoja na Mpango Mkakati wa Mpito wa Mwaka wa Fedha 2024/25 – 2025/26 vinasisitiza juu ya kuimarisha usimamizi wa rasilimali za madini kupitia uundaji na utekelezaji wa mkakati wa uwajibikaji kwa jamii na ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini. | Serikali kupitia Wizara ya Madini imetengeneza mipango mbalimbali ikiwemo Sera na Sheria ya Madini (Sura ya. 123) ya mwaka 2019 |
| Tume ya Madini | Mpango Mkakati wa Tume ya Madini wa Mwaka wa Fedha 2019/20 – 2023/2024 na Mpango Mkakati wake wa Mpito wa Mwaka wa Fedha 2024/25 - 2025/2026 vinalenga kuimarisha uzingatiaji wa wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini, ili kuhakikisha kuwa sekta hii inachangia ipasavyo katika uchumi wa kitaifa. | • Uundaji wa mfumo wa ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini, Mwongozo wa Ukaguzi wa Fedha, Mapitio ya Ushuru na Ushirikishwaji wa Wazawa wa mwaka 2020 na Kanuni za Madini za Ushirikishwaji wa Wazawa za mwaka 2018 |
| Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | Mpango Mkakati wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 2018/19 - 2025/26 unasisitiza juu ya uratibu wa jitihada za serikali katika ushirikishwaji wa wazawa, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, na kufungua fursa mbalimbali za za kiuchumi. Hii inafanywa kwa kutambua na kushughulikia changamoto mbalimbali katika uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na uhusishwaji wa masuala ya ushirikishwaji wa wazawa katika sera, mipango na miradi mbalimbali ya kimkakati. | • Baraza limeandaa Mwongozo wa Taifa wa Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta mbalimbali za uchumi wa mwaka 2019 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Mikakati na Jitihada za Serikali katika Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini, 2025

## 10.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

### 10.2.1 Malengo ya Ukaguzi

690. Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa kufanya tathmini kama Wizara ya Madini, Tume ya Madini pamoja na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wanasimamia ipasavyo taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini ili kuchagiza ushiriki wa wazawa na kuchangia ipasavyo kwenye pato la taifa.

### 10.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

691. Ukaguzi huu ulihusisha Wizara ya Madini, Tume ya Madini pamoja na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Ukaguzi uliangazia mchakato mzima wa usimamizi wa uwezeshaji wa wazawa ikiwemo usimamizi wa utekelezaji wa mipango ya ushirikishwaji wa wazawa, ukuzaji wa uwezo wa wazawa, ufuatialiaji na uratibu katika utekelezaji wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa kwenye sekta ya madini. Tathmini hii ilifanyika kwa muda wa miaka mitano ya fedha, kuanzaia 2020/21 hadi 2024/25.

## 10.3 Matokeo ya Ukaguzi

692. Nilibaini kuwa usimamizi wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini ulichochea ongezeko la asilimia 171 la ajira za wazawa kati ya mwaka 2020 na mwaka 2024. Hata hivyo, kulikuwa na ongezeko la asilimia 63 ya waajiriwa wa kigeni katika kipindi hicho. Zaidi ya hayo, nilibaini utofauti wa mishahara kwani waajiriwa wa kigeni walilipwa mishahara mikubwa zaidi ya waajiriwa wazawa walio katika nyadhifa zinazofanana. Vile vile, nilibaini kuwa kutoka 2020 hadi 2024, jumla ya thamani ya ununuzi wa huduma na bidhaa za kitanzania ilikuwa asilimia 33, wakati thamani ya ununuzi wa huduma na bidhaa za kigeni ilikuwa asilimia 67. Mambo haya yanabanisha Kuwapo kwa changamoto katika usimamizi wa taratibu za uwezeshaji wa wazawa katika sekta ya madini, kama ilivyobainishwa hapa chini.

### 10.3.1 Tume ya Madini Kutotekeleza Ipasavyo Utekelezaji wa Mipango ya Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini


693. Mapitio yangu ya Mipango na Taarifa za Mwaka za Tume ya Madini za kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25 yalibaini kuwa Tume hauikusimamia ipasavyo utekelezaji wa mipango ya ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini. Hali hii ilikuwa kinyume na Kanuni Na. 6 ya Kanuni za

Usimamizi wa Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini za mwaka 2018, zinazoipa Tume ya Madini wajibu wa kusimamia taratibu zote za ushirikishwwaji wa wazawa katika sekta ya madini. Upungufu uliobanika katika eneo hili ni kama ifuatavyo:

**(a) Tume ya Madini Kutofanya Ukaguzi Unaojitosheleza Katika Masuala ya Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini**

694. Uchambuzi wangu wa ripoti za utendaji wa Tume ya Madini kutoka Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25 ulionesha kuwa idadi ya kaguzi ziliofanywa na Tume hazikutosha ikilinganishwa na mipango ya ushirikishwaji wa wazawa iliyoidhinishwa. **Kilelezo Na. 38** kinaonesha hali niliyoibaini.

**Kielelezo Na. 38: Idadi ya Mipango ya Ushirikishwaji wa Wazawa Iliyoidhinishwa dhidi ya Idadi ya Kaguzi zilizofanywa na Tume ya Madini**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa na Mipango ya Mwaka ya Tume ya Madini 2020/21-2024/25 wa Mwaka 2025

695. **Kielelezo Na. 38** kinaonesha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2020/21 idadi ya kaguzi ilikuwa 5 kati ya mipango 532 iliyoidhinishwa; katika Mwaka wa Fedha 2021/22, hakuna ukaguzi uliofanyika licha ya kuwapo kwa mipango 343 iliyoidhinishwa; katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Tume ya Madini ilifanya kaguzi 19 kati ya mipango 652; katika Mwaka wa Fedha 2023/4, Tume ilifanya kaguzi 20 kati ya mipango 789 iliyodhinishwa na katika Mwaka wa Fedha 2024/25, Tume ya Madini ilifanya kaguzi 10 kati ya mipango 1,736 iliyoidhinisha.

696. Udhaifu wa Tume ya Madini katika kufanya kaguzi za ushirikishwaji wa wazawa yalisababishwa na upungufu wa watumishi katika kitengo cha ushirikishwaji wa wazawa. Tume ilikuwa na watumishi 9 kati ya 13

waliohitajika, hivyo kusababisha watumishi waliokuwapo kuwa na kazi nyingi zaidi ya uwezo wao. Hali hii iliongeza hatari ya ukaguzi usiojitosheleza na hivyo kupunguza ufanisi wakati wa utekelezaji wa mipango ya ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini.

**(b) Kamati ya Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini Kutofanya Ziara ili Kukagua Utekelezaji wa Mipango ya Ushirikishwwaji wa Wazawa**

697. Mapitio yangu ya Mipango ya Utekelezaji ya Mwaka ya Tume ya Madini kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25 ilionesha kuwa Kamati ya Ushirikishwaji wa Wazawa haikufanya ziara yoyote ili kukagua utekelezaji wa mipango ya ushirikishwaji wa wazawa. Hali hii ilitokana na uratibu usiojitosheleza kati ya wajumbe wa kamati hiyo, hivyo kuchochea kupunguza uwezo wa Tume kuthibitisha taarifa za ushirikishwwaji wa wazawa zinazotolewa na makampuni ya madini na kuongeza hatari ya kutofuata taratibu za ushirikishwaji wa wazawa zilizowekwa.

**(c) Tume ya Madini Kutopitia Ipasavyo Ripoti za Ushirikishwaji wa Wazawa Zilizowasilishwa na Wamiliki wa Leseni za Madini, Wakandarasi Wakuu Wakandarasi Wadogo na Washirika Wengine**

698. Mapitio yangu ya Ripoti za Utendaji katika Ushirikishwaji wa Wazawa kuanzia mwaka 2020 hadi 2024, yalibaini kuwa Tume ya Madini haikupitia ripoti hizi ipasavyo ili kujiridhisha usahihi wa taarifa zake. Hali hii ni kinyume na Kanuni ya 38, (1) na (2) ya Kanuni za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini za mwaka 2018 na marekebisho yake, ambazo zinaitaka tume kupitia ripoti hizi ndani ya siku 50 za kazi baada ya kuwasilishwa kwake. **Jedwali Na. 39** linafafanua zaidi juu ya hali ya upitiaji wa ripoti hizi.

**Jedwali Na. 39: Hali ya Upitiaji wa Ripoti za Ushirikishwaji wa Wazawa**

| Mwaka | Mipango Iliyoidhinishwa | Ripoti Zilizowasilishwa katika Tume ya Madini | Ripoti Zilizopitiwa na Tume ya Madini | Ripoti Zilizopitiwa (%) |
|---|---|---|---|---|
| 2020 | 87 | 82 | 82 | 100 |
| 2021 | 477 | 86 | 0 | 0 |
| 2022 | 437 | 46 | 0 | 0 |
| 2023 | 882 | 68 | 0 | 0 |
| 2024 | 151 | 56 | 30 | 54 |

***Chanzo:*** Mapitio ya Wakaguzi ya Ripoti za Ushirikishwaji wa Wazawa kuanzia Mwaka 2020 hadi 2024

699. **Jedwali Na. 39** linaonesha kuwa Tume ya Madini ilipitia ripoti zote zilizowasilishwa mnamo 2020, lakini ni asilimia 54 ya ripoti zilipitiwa ambazo

ziliwasilishwa mwaka 2024. Licha ya kuwasilishwa kwa ripoti hizi kati ya mwaka 2021 na 2023, Tume haikupitia ripoti yoyote katika miaka hii. Hali hii ilitokana na Tume kutotoa kipaumbele ili kuhakikisha inapitia ipasavyo taarifa hizo.

700. Mapitio machache ya ripoti za utekelezaji wa taratibu za uwezeshaji wa wazawa katika sekta ya madini uliathiri uwezo wa Tume ya Madini katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa kanuni za ushirikishwaji wa wazawa, kubaini changamoto za utekelezaji, na kuhakikisha utekelezwaji wa matakwa ya sheria.

701. Uhakiki mdogo wa taarifa za utekelezaji uliathiri uwezo wa Tume ya Madini kufuatilia kwa ufanisi ufuataji wa Kanuni za Ujumuishaji wa Rasilimali za Ndani, kubaini upungufu katika utekelezaji, na kutekeleza matakwa ya kisheria.

### 10.3.2 Maendeleo Yasiyojitosheleza katika Kuendeleza Uwezo wa Wazawa na Uongezaji Thamani ya Madini katika Sekta ya Madini

702. Nilibaini ujengaji uwezo wa wazawa katika sekta ya madini usiojitosheleza. Hii ilioneshwa na Tume ya Madini kutohakikisha urithishwaji wa teknolojia kutoka kwa wataalam na makapuni ya kigeni kwenda kwa wenyeji. Zaidi ya hayo, ukaguzi huu ulibaini kuwa Wizara ya Madini haukuweka msukumo wa kutosha katika suala la uongezaji thamani ya madini nchini, pamoja na usimamizi wa mipango ya urithishaji wa teknolojia ili kukuza uwezo wa wazawa. Upungufu huu umeelezewa kwa kina kama ifuatavyo:

#### (a) UKuzaji wa Uwezo wa Wazawa Usiojitosheleza Katika Sekta ya Madini

703. Mapitio yangu ya nyaraka zinazohusu ushirikishwaji wa wazawa kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/5 yalibaini ukuzaji wa uwezo wa wazawa haukufanywa vya ipasavyo, kinyume na Kifungu cha 104 cha Sheria ya Madini Sura ya 13 ambayo inawataka wamiliki wa leseni za madini kukuza uwezo wa wazawa katika mnyororo wa thamani wa sekta ya madini.

Hali hii ilidhihirishwa na mambo yafuatayo:

#### (i) Kukosekana kwa Urithishaji wa Teknolojia kwa Wazawa

704. Mapitio yangu ya Ripoti za Utendaji katika taratibu za ushirikishwaji wa wazawa kuanzia Mwaka ya Fedha ya 2020/21 hadi 2024/25 ilibainisha kuwa wamiliki wa leseni za madini walilenga zaidi kutoa mafunzo ya kawaida kwa wafanyakazi wazawa, badala ya kujikita katika urithishwaji teknolojia ili

kujenga uwezo wa wazawa katika kubuni na kutengeneza vifaa na teknolojia mbalimbali za migodini. Hali hii ilisababishwa na kutokuwapo kwa sera ya kitaifa ya urithishaji wa teknolojia katika sekta ya madini, ambayo ingetoa mwongozo wa utekelezaji wa mipango ya urithishwaji wa teknolojia. Hii ilikuwa kinyume na Kanuni ya 25 ya Kanuni za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini za mwaka 2018, na marekebisho yake ya mwaka 2022, ambazo zinahitaji Wizara ya Madini kuanzisha sera na uratibu wa kitaifa wa urithishaji wa teknolojia katika sekta ya madini.

705. Kutokuwapo kwa sera ya kitaifa kulikwamisha uandaaji wa mipango na miongozo ya kitaifa itakayowaelekeza wakandarasi wakuu, wakandarasi wadogo, wamiliki wa leseni na taasisi nyingine katika utekelezaji wa programu zinazolenga kukuza maendeleo ya kiteknolojia kwa wazawa nchini.

**(ii) Makubaliano ya Ubia Kati ya Makampuni ya Kigeni na ya Wazawa yasiyo na Tija**

706. Kupitia taarifa za Utendaji katika taratibu za ushirikishwaji wa wazawa, pamoja na mahojiano na maafisa kutoka Wizara ya Madini na Tume ya Madini, nilibaini kuwa kampuni za wazawa zinazoingia ubia na makampuni ya kigeni hazikuwa zikifanya kazi zinazofanana. Ubia huo ulilenga zaidi kukidhi mahitaji ya kiwango cha chini cha kumiliki hisa za kampuni ambacho ni asilimia 20 kwa wazawa, badala ya kuhakikisha ushiriki kwenye kazi zinazofanana ili kuleta fursa ya urithishwaji wa teknolojia na ujengaji ujuzi. Hali hii ilipunguza faida zilizokusudiwa ukiwemo urithishaji wa teknolojia kutoka kwa kampuni za kigeni kwenda kwa wazawa, kupunguza ukuaji wa uwezo wa wazawa, na hivyo kusababisha kuendelea kutegemea maarifa ya kigeni katika shughuli za uchimbaji wa madini.

**(b) Wizara ya Madini Kutohamasisha Ipasavyo juu ya Kuongeza Thamani ya Madini Nchini**

707. Mapitio yangu ya taarifa za uongezaji thamani pamoja na mahojiano na maafisa kutoka Wizara ya Madini vilibaini kuwa, Wizara haikutilia mkazo ipasavyo suala la uongezaji thamani ya madini nchini. Hali hii ilikuwa kinyume na matakwa ya Mwongozo wa Uongezaji Thamani ya Madini wa Mwaka 2020 unaoitaka Wizara kuhakikisha uongezaji thamani wa madini unafanyika ndani ya nchi kabla ya kusafirisha madini hayo nje ya nchi. **Jedwali Na. 40** linonesha hali halisi iliyobainika.

**Jedwali Na. 40: Utendaji katika Eeo la Uongezaji Thamani ya Madini Nchini Kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/21- 2024/25**

| Kundi la Madini | Njia ya Uongezaji Thamani wa Madini | Uongezaji Thamani Nchini (%) | Uongezaji Thamani Nje ya Nchi (%) |
|---|---|---|---|
| Madini ya Metali | Kuyeyusha na kusafisha | 53.8 | 46.2 |
| Madini ya Vito | Kuondoa sehemu mbovu za madini ghafi, ulainishaji wa sehemu ya juu, ung'arishaji wa madini | 38.7 | 61.3 |
| Madini ya Viwandani | Uchujaji, Uchomaji bila oksijeni, Usafishaji, Ufukizaji, Utenganishaji kwa njia ya umeme, utenganishaji kwa njia ya sumaku | 97.4 | 2.6 |
| Madini ya Ujenzi | Kupunguza ukubwa wa madini kwa kuyaponda na kuchekecha | 99.8 | 0.2 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Takwimu za Uzalishaji wa Madini wa Mwaka 2025

708. **Jedwali Na. 40** linaonesha kuwa utendaji katika uongezaji thamani wa madini ulikuwa juu kwa madini ya viwandani na madini ya ujenzi ambayo thamani yake iliongezwa ndani ya nchi kwa asilimia 97.4 na asilimia 99.8 mtawalia. Hii ilitokana na aina hii ya madini kutohitaji teknolojia na uwekezaji mkubwa katika uongezaji wake thamani. Kwa upande mwingine, uongezaji thamani wa madini ya metali na vito ulikuwa asilimia 53.8 na asilimia 38.7 mtawalia. Hali hii ilitokana na uratabu usiojitosheleza kwenye eneo hili.

709. Kutotilia mkazo suala hili kulichochea upotevu wa fursa za ajira, mapato, na ukuaji wa teknolojia ambavyo vingetokana na kutengenezwa kwa viwanda vya uongezaji thamani ya madini ndani ya nchi.

### (c) Wizara ya Madini Kutosimamia Ipasavyo Ukuaji wa Ujuzi na Mipango ya Urithishaji wa Teknolojia kwa Wazawa katika Sekta ya Madini

710. Nilipitia taarifa za Utekelezaji wa Ushikishwaji wa Wazawa kutoka katika makampuni ya madini kuanzia 2020 hadi 2024, na nikabaini kuwa Wizara ya Madini haikusimamia ipasavyo ukuaji wa ujuzi na mipango ya urithishaji wa teknolojia kwa wazawa katika sekta ya madini. Hii ilioneshwa na makampuni haya kutegemea mafunzo ya kawaida ya kazini, pamoja mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyuo kama mbinu pekee ya urithishaji wa teknolojia kwa wazawa.

711. Vilevile, uchambuzi wangu wa taarifa hizi ulionesha kuwa, katika miaka iliyokaguliwa mipango ya urithishaji wa teknolojia kwa wazawa haikusimamiwa ipasavyo kama inavyonekana katika **Jedwali Na. 41.**

**Jedwali Na. 41: Idadi ya Wajuzi wa Kigeni katika Migodi Iliyotembelewa Wakati wa Ukaguzi**

| Kampuni ya Madini | Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
| Mgodi wa Geita | 50 | 52 | 62 | 61 | 54 |
| Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Ruvuma | 0 | 0 | 6 | 9 | 27 |
| Kiwanda cha Simenti cha Dangote | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 |
| Mgodi wa Almasi wa Williamson | 2 | 5 | 5 | 5 | 7 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Utendaji katika Ushirikishwaji wa Wazawa Mwaka 2025

712. **Jedwali Na. 41** linaonesha ongezeko la wataalam wa kigeni katika nafasi za kitaalam migodini. Mgodi wa makaa ya mawe wa Ruvuma ulikuwa na wataalam wengi wa kigeni, ambapo idadi yao iliongezeka kwa zaidi ya asilimia 100 kutoka 0 mwaka 2020 mpaka 27 mwaka 2027. Kiwanda cha simenti cha Dangote kilikuwa na idadi sawa ya wataalam katika miaka yote minne. Mgodi wa Almasi wa Willaimson- Shinyanga ulikuwa na ongezeko la asilimia 7 ya wataalam wa kigeni kuanzia mwaka 2020 hadi 2024. Mgodi wa dhahabu wa Geita ulikuwa na wafanya kazi zaidi ya 50 kwa miaka yote kuanzia mwaka 2020 hadi 2024. Hali hii ilitokana na ukosefu wa ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara ili kujua namna makampuni ya madini yanavyotekeleza ukuaji wa ujuzi na mipango ya urithishaji wa teknolojia kwa wazawa.

713. Usimamizi usiojitosheleza wa ukuaji wa ujuzi na mipango ya urithishaji wa teknolojia kwa wazawa, uliongeza utegemezi kwa wataalam na makampuni ya kigeni, na hivyo kuwanyima wazawa fursa za kukuza uwezo wao na teknolojia katika sekta ya madini.

### 10.3.3 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Ushikishwaji wa Wazawa Usiojitosheleza

714. Mapitio yangu ya Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini kutoka Wizara ya Madini na Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi za Miaka ya Fedha 2020/21 hadi 2024/25, yalibaini kuwa Wizara na Baraza hazikufanya ipasavyo ufuatiliaji wa utekelezaji wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini. Maelezo ya kina juu ya suala hili yametolewa hapa chini;

**(a) Wizara ya Madini Kutofuatilia Ipasavyo Utendaji wa Tume ya Madini katika Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa kwenye Sekta ya Madini**

715. Nilipitia ripoti za mwaka za utendaji wa Wizara ya Madini kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25 na kubaini kuwa shughuli za ushirikishwaji wa wazawa hazikufuatiliwa ipasavyo. Hii ni kinyume na Kifungu cha 19(b) na (c) cha Sheria ya Madini Sura ya 123 kinachoitaka Wizara kufanya ufuatiliaji wa shughuli mbalimbali katika sekta ya madini, ikiwemo utendaji wa Tume ya Madini na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara.

716. Vilevile, ufuatiliaji usiojitosheleza ulidhihirishwa na ukosefu wa viashiria na vigezo vya kupima utendaji wa Tume ya Madini katika usimamizi wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa. Hali hii ilikuwa kinyume na aya ya 4.7.1 ya Mpango Mkakati wa Wizara ya Madini wa Miaka ya Fedha 2019/20-2023/24 inayosisitiza uandaaji wa mipango ya ufuatiliaji yenye viashiria na vigezo vya kutumia wakati wa kupima utendaji.

717. Kwa ujumla, ufuatiliaji wa utendaji wa Tume ya Madini usiojitosheleza, ulisababishwa na mambo yafuatayo:


(i) **Kutokuwapo kwa Mfumo wa Ufuatiliaji:** Mapitio yangu ya Mipango ya Utekelezaji ya Mwaka ya Wizara ya Madini na ripoti zake husika, pamoja na mahojiano na maafisa wanaohusika, yalibaini kutokuwapo kwa mfumo wa ufuatiliaji unaoainisha idadi, mawanda, mbinu, na viashiria vya utendaji kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini ufuataji wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini. Upungufu huu uliathiri uwezo wa Wizara kupima maendeleo katika kuongeza ushiriki wa watanzania kwenye ajira, ununuzi wa bidhaa na huduma, na uongezaji thamani wa madini.

**(ii)** **Kutokutolewa kwa Fedha ili Kuwezesha Ufuatiliaji na Tathmini:** Mapitio yangu ya Ripoti za Utendaji za Mwaka za Wizara ya Madini kwa miaka ya fedha 2020/21 hadi 2025/26 yalionesha kuwa wizara haikutoa fedha kutekeleza jukumu lake la ufuatiliaji na tathmini. Hali hii ilitokana na kutopewa kipaumbele kwa shughuli za ufuatiliaji na tathmini wakati wa utolewaji wa fedha. Kwa hiyo, Wizara ya Madini haikuweza kufuatilia ipasavyo utendaji wa Tume ya Madini katika kusimamia masuala ya ushirikishwaji wa wazawa.

### (b) Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi Halikusimamia Ipasavyo Masuala ya Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta Nyeti za Uchumi

718. Nilibaini kuwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lilifuatilia utekelezaji wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa kwa kukusanya taarifa kutoka sekta mbalimbali za uchumi. Hata hivyo, mapitio yangu ya ripoti za mwaka za ushirikishwaji wa wazawa Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25 zilizoandaliwa na Baraza zilionesha utoaji wa taarifa usioridhisha, kwani Baraza halikujumuisha taasisi zote katika sekta husika, kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 39**. Hali hii ni kinyume na matakwa ya aya ya 3.7 (1) ya Mwongozo wa Taifa wa Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta Mbalimbali za Uchumi wa mwaka 2019, ambao inalitaka Baraza kufuatilia utekelezaji wa masuala ya ushirikishwaji wa wazawa katika sekta zote za uchumi.

**Kielelezo Na. 39: Hali ya Utoaji Ripoti ya Ushirikishwaji wa Wazawa katika Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**




***Chanzo***: Uchambuzi wa Ripoti za Mwaka za Utekelezaji wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa kutoka Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi wa Miaka ya Fedha 2020/21 - 2024/25

719. **Kielelezo Na. 39** kinaonesha kuwa katika kipindi cha miaka miwili ya fedha, utoaji wa taarifa za utekelezaji wa masuala ya ushirikishwaji wa wazawa kutoka kwenye taasisi mbalimbali ulikuwa haujitoshelezi, ambapo taasisi nne tu kati ya 51 sawa na asilimia 8 zilifanikiwa kuandaa na kutoa taarifa kwa Miaka ya Fedha 2020/21 na 2021/22. Idadi ya taasisi iliongezeka kutoka nne hadi nane (sawa na asilimia 16) kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, na taasisi 12 (sawa na asilimia 24) kwa Mwaka wa Fedha 2023/24.

720. Ufuatiliaji usioridhisha uliofanywa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ulichangiwa na kutokuwapo kwa mfumo wa kisheria unaolipa nguvu Baraza kufuatilia utekelezaji wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta mbalimbali za uchumi. Kutokana na hali hiyo, taratibu za ushirikishwaji wa wazawa ulifanyika katika taasisi chache tu katika sekta mbalimbali, jambo lililochochea ufinyu wa fursa za kiuchumi kwa wazawa.

### (c) Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi Kutotoa Ipasavyo Ripoti kuhusu Utekelezaji wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa

721. Mapitio yangu ya Ripoti za Utendaji za Mwaka za Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kuanzia Miaka ya Fedha 2020/21 hadi 2024/25 yalibaini kuwa baadhi ya sekta za kiuchumi hazikujumuishwa katika ripoti za mwaka za utekelezaji wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa zilizoandaliwa na Baraza. Hali hii ilisababishwa na uwasilishaji usioridhisha wa ripoti hizi kutoka sekta mbalimbali, ikiwemo sekta ya madini. Utaratibu huu ulikuwa kinyume na Aya ya 4.2.1 Mwongozo wa Taifa wa Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta Mbalimbali za Uchumi wa mwaka 2019, unaolitaka Baraza kupokea ripoti kutoka taasisi mbalimbali mara mbili kwa mwaka. **Jedwali Na. 42** linaonesha maelezo ya kina.

**Jedwali Na. 42: Hali ya Utoaji wa Ripoti Juu ya Ushirikishwaji wa Wazawa kutoka katika Sekta Nyeti za Uchumi Kwenda Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi**

| Sekta ya Kiuchumi | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
|---|---|---|---|---|---|
| | Ripoti zilizopelekwa katika Baraza (%) | Ripoti zilizopelekwa katika Baraza (%) | Ripoti zilizopelekwa katika Baraza (%) | Ripoti zilizopelekwa katika Baraza (%) | Ripoti zilizopelekwa katika Baraza (%) |
| Sekta ya Uchimbaji na Nishati | 25 | 8 | 0 | 75 | 0 |
| Sekta ya Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano | 9.5 | 21 | 50 | 19 | 0 |
| Sekta ya viwanda na Biashara | 0 | 5 | 19 | 40 | 0 |
| Sekta ya Kilimo, Ufugaji na Uvuvi | 0 | 11 | 0 | 0 | 0 |
| Sekta ya Utalii | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Ripoti za Mwaka za Utekelezaji wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa kutoka Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi Miaka ya Fedha 2020/21 – 2024/25

722. **Jedwali Na. 42** linaonesha kuwa utoaji wa taarifa kuhusu utekelezaji wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika Baraza la Taifa la Uwezeshaji

Wananchi Kiuchumi, ulikuwa mdogo na ulipungua katika kipindi cha 2020/21 hadi 2024/25. Ingawa sekta za Uchimbaji na Nishati pamoja na Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zilionesha hali nzuri ya utoaji wa taarifa, utendaji wake ulibainika kubadilika-badilika kila mwaka. Wakati huo huo, utoaji wa taarifa kutoka sekta ya Viwanda na Biashara ilionesha kuimarika kabla ya kushuka hadi sifuri, ilhali utoaji wa taarifa kutoka sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na Utalii ziliendelea kutoa taarifa kwa kiwango cha chini kwa kipindi chote.

### 10.3.4 Uratibu Usiojitosheleza wa Utekelezaji wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa

723. Wizara ya Madini na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi zina jukumu kuu la kuratibu na kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile makampuni ya uchimbaji madini, jamii, taasisi za udhibiti, na taasisi za elimu. Juhudi za wadau hawa zinalenga kuhakikisha kuwa watanzania wanajumuishwa katika sekta ya madini kupitia ajira, kuwajengea uwezo, na ununuzi wa bidhaa na huduma zinazopatikana nchini.

724. Hata hivyo, nilibaini upungufu ufuatao:

**(a) Uratibu Usiojitosheleza Katika Utafiti na Uanzishwaji wa Kanzidata ya Bidhaa na Huduma Zinazopatikana Nchini**

725. Mapitio yangu ya nyaraka zinazohusiana na masuala ya ushirikishwaji wa wazawa zilizowasilishwa na Wizara ya Madini yalibaini kuwa Wizara haikuratibu utafiti wowote kuhusu masuala ya ushirikishwaji. Hali hii ni kinyume na Aya ya 3.1.3 (i) ya Majukumu ya Wizara katika Muundo wake wa mwaka, 2018, unaoitaka Wizara kuratibu utafiti juu ya uwezo wa ndani kutengeneza bidhaa na kutoa huduma zinazohitajika katika shughuli mbalimbali za madini na kutoa mapendekezo ya hatua zinazofaa za kuimarisha uwezo huo.

726. Vilevile, mapitio ya bajeti ya Wizara na mipango yake ya utekelezaji ya mwaka kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/25 yalionesha ukosefu wa rasilimali fedha zilizotengwa kwa ajili ya ufanyikaji wa utafiti katika eneo la ushirikishwaji wa wazawa kwenye sekta ya madini. Pia, hakukuwa na bajeti kwa ajili ya kutambua na kuandaa kanzidata ya huduma na wataalam waliopo nchini wenye uwezo wa kushiriki katika shughuli mbalimbali za madini. upungufu huu ulichangiwa na ukosefu wa mikakati ya Wizara, kama vile mipango ya kifedha, ambayo ingewezesha utafiti katika eneo la ushirikishwaji wa wazawa.

727. Kutokana na hali hiyo, uwezo wa wizara wa kupata taarifa za uhakika, kufuatilia maendeleo ya wazawa, na kutumia taarifa hizi katika maboresho ya sera ulikuwa mdogo, jambo lililoleta ugumu katika kupima athari za mipango ya ushirikishwaji wa wazawa na kubaini maeneo yanayohitaji maboresho.

**(b) Kamati za Kisekta za Ushirikishwaji wa Wazawa Kutofanya Vikao Ipasavyo**

728. Mapitio yangu ya taarifa za vikao kwa miaka ya fedha 2020/21 hadi 2024/25 yalibaini kuwa vikao havikufanyika kama ilivyotakiwa, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 43.** Hali hii ilikuwa kinyume na Aya ya 2.1.4 ya Mwongozo wa Taifa wa Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta Mbalimbali za Uchumi wa Mwaka 2019, inayozitaka Kamati za Kisekta za Ushirikishwaji wa Wazawa kufanya vikao viwili kila mwaka.

**Jedwali Na. 43: Hali ya Ufanyikaji wa Vikao vya Kamati ya Kisekta ya Ushirikishwaji wa Wazawa katika Baraza la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi**

| Mwaka wa Fedha | Vikao Vilivyohitajika | Vikao Vilivyofanyika | Utendaji (%) |
|---|---|---|---|
| 2020/21 | 2 | 0 | 0 |
| 2021/22 | 2 | 1 | 50 |
| 2022/23 | 2 | 1 | 50 |
| 2023/24 | 2 | 0 | 0 |
| *2024/25* | 2 | 0 | 0 |
| Jumla | 10 | 2 | 20 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa ya Vikao vya Baraza la Uwezeshaji wa Wanachi Kiuchumi katia Masuala ya Ushirikishwaji wa Wazawa Mwaka 2020/21-202425

729. **Jedwali Na. 43** linaonesha kuwa kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi 2024/5, vilitakiwa vikao kumi kwa ujumla, lakini vilifanyika vikao viwili tu, sawa na asilimia 20 ya utendaji. Ufanisi ulifikia kilele katika Mwaka wa Fedha 2021/22 na 2022/23, ukipata asilimia 50 kila mwaka, huku kukikosekana kwa mikutano iliyofanyika katika Mwaka wa Fedha 2020/21, 2023/24, na 2024/25. Hali hii ilisababishwa na kutokuwapo kwa sera kwa ajili ya sekta husika ambayo ingelipa nguvu Baraza katika kusimamia ufuataji wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa kwenye sekta mbalimbali.

730. Pia, nilibaini kuwa hali hii ya ufanyikaji wa vikao ilisababishwa na ukosefu wa kamati ya ushirikishwaji wa wazawa katika sekta mbalimbali. Nilibaini kuwa kamati ya namna hiyo ilikuwapo katika sekta ya madini pekee.



ISO 9001:2015 Certified

731. Kutokana na hali hiyo, uelewa wa masuala ya ushirikishwaji wa wazawa ulikuwa mdogo miongoni mwa wadau. Hali hii ilitokana na ukosefu wa mamlaka ya kisheria ya Baraza katika kusimamia masuala ya ushirikishwaji wa wazawa.

**(c) Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi Halikushiriki Ipasavyo Wakati wa Majadiliano kwenye Miradi ya Taifa ya Kimkakati**

732. Nilibaini kuwa ushiriki wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi katika Timu za Majadiliano za Serikali ili kuhakikisha masuala ya ushirikishwaji wa wazawa yanajumuishwa katika mikataba ya miradi ulikuwa mdogo. Hali hii ilikuwa kinyume na Aya ya 3.7(5) ya Mwongozo wa Taifa wa Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta Mbalimbali za Uchumi wa Mwaka 2019, inayolitaka Baraza kushiriki katika majadiliano wakati wa uandaaji wa mikataba mbalimbali ya miradi ya taifa ya kimkakati, ili kuhakikisha masuala ya ushirikishwaji wa wazawa yanajumuishwa kwenye mikataba hiyo.

733. Aidha, nilibaini kuwa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lilishiriki mara mbili tu kwenye majadiliano ya mikataba ya serikali kwenye miradi ya kimkakati, ambayo ni mradi wa gesi asilia na mradi wa bomba la mafuta. Ushiriki huu ulikuwa sawa na asilimia 12 pekee ya miradi yote 17 ya kimkakati nchini. Kutokana na hali hiyo, Baraza lilikosa fursa muhimu za kutetea na kuhakikisha upatikanaji wa fursa kwa ajili ya wazawa kwenye miradi ya kimkakati.

ISO 9001:2015 Certified

## 10.4 Athari za Changamoto Zilizobainishwa katika Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano

734. Usimamizi usiojitosheleza wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini unazuia mafanikio ya Mpango wa Tatu wa Taifa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Hii inatokana na ushiriki wa wazawa usiojitosheleza katika sekta ya madini. Hali hii pia inazuia ukuaji wa viwanda vya ndani kwani inapunguza fursa za ukuzaji wa ujuzi na urithishwaji wa teknolojia, na kusababisha kuendelea kutegemea maarifa na utaalam wa kigeni. Vilevile, hali hii inapunguza uongezaji wa thamani ya madini ndani ya nchi, inapunguza mapato, na kuzuia utengenezaji wa fursa za ajira, na hivyo kupunguza kasi ya ukuaji wa viwanda na ukuaji wa uchumi jumuishi.

735. Matokeo yake, faida za kijamii na kiuchumi zinazotarajiwa kutokana na matumizi ya rasilimali za madini kama vile kupunguza umaskini, maendeleo ya sekta binafsi, na matumizi endelevu ya maliasili hazikupatikana kikamilifu, na

hivyo kuzuia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu yanayohusiana na kazi bora, maendeleo ya sekta, na usimamizi bora wa rasilimali.

ISO 9001:2015 Certified

## SURA YA KUMI NA MOJA

## UTAFUTAJI NA USIMAMIZI WA RASILIMALIFEDHA

### 11.1 Utangulizi

736. Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya jumla ya ukaguzi yanayohusiana na Utafutaji na Usimamizi wa Rasilimali Fedha. Inaelezea pia eneo la ukaguzi, taasisi za serikali zilizohusishwa katika ukaguzi huu, uhusiano wa maeneo yaliyokaguliwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na athari zake katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu.

737. Kaguzi hizi za Ufanisi ni pamoja na:

(a) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya Kodi; na
(b) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji Shule za Umma.

#### 11.1.1 Usuli kuhusu Utafutaji na Usimamizi wa Rasilimali Fedha

738. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichukua hatua mbalimbali kuhusiana na Ukusanyaji na Usimamizi wa Rasilimali Fedha ili iweze kutoa huduma kwa wananchi. Moja ya vyanzo vya utafutaji rasilimali fedha ni kupitia Ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi.

739. Serikali ya Tanzania imefanya maboresho ya kuimarisha usimamizi wa mapato yasiyo ya kodi, ikiwa pamoja na kuanzisha Mfumo wa Malipo ya Kielektroniki wa Serikali ili kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji. Pamoja na jitihada hizi, bado kuna changamoto. Kuna ufanisi usioridhisha wa ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya kodi, kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25 ukusanyaji umepungua kutoka asilimia 84 hadi 74.3 kwa kipindi cha miaka mitatu.

740. Kadhalika, Tanzania ilianzisha ruzuku kwa ajili ya uendeshaji wa shule za umma mwaka 2002 na 2016 kwa shule za Msingi na Sekondari mtawalia, ili kukabiliana na uhaba wa fedha baada ya kufutwa kwa ada ya shule. Lengo likiwa kutoa Elimu bora kwa wote, kutoa vikwazo vya fedha, kuboresha ufikikaji na kuongeza idadi ya usajili wa wanafunzi.

### 11.1.2 Uhusiano wa Utafutaji na Usimamizi wa Rasilimali Fedha na Mpango wa Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano

741. Sehemu hii inaainisha uhusiano wa Utafutaji na Usimamizi wa Rasilimali Fedha na Mpango wa Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano.

742. Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi unaendana na Lengo 17, lenye nia ya kuimarisha njia ya utekelezaji na kuhuisha Ushirikiano wa Kimataifa kwa Maendeleo Endelevu.

743. Vivyohivyo, Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji Shule unaendana na lengo la 4, lenye nia ya kuhakikisha kuna elimu bora, jumuishi na yenye usawa na kuendeleza fursa za kujifunza kwa wote. Maeneo mahususi yanayohusiana yameelezwa kwenye **Jedwali Na. 44.**

**Jedwali Na. 44:Uhusiano Mahususi ya Utafutaji na Usimamizi wa Rasilimali Fedha na Mpango wa Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano**

| Jina la Ukaguzi | Lengo kwenye Mpango wa Maendeleo Endelevu | Shahaba Mahususi kwenye Mpango wa Maendeleo Endelevu | Eneo la Kipaumbele Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano |
|---|---|---|---|
| Usimamizi wa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji wa Shule | Lengo la 4. lenye nia ya kuhakikisha kuna elimu bora na jumuishi yenye usawa na kuendeleza fursa za kujifunza kwa wote | 4.1 Ifikapo 2030, kuhakikisha wasichana na wavulana wote wanapata elimu ya bure, kwa usawa na yenye ubora ambayo inaendana na uhalisia wa matokeo yanayotarajiwa | **5.5.1.** kuongeza matumizi kwenye elimu jumuishi yenye ujuzi, ugunduzi unaoendana na utafiti wa maendeleo |

ISO 9001:2015 Certified

| Jina la Ukaguzi | Lengo kwenye Mpango wa Maendeleo Endelevu | Shahaba Mahususi kwenye Mpango wa Maendeleo Endelevu | Eneo la Kipaumbele Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano |
|---|---|---|---|
| Usimamizi wa Mapato Yasiyo ya Kodi | Lengo 17. Lina lenga kuimarisha njia ya utekelezaji na kuhuisha Ushirikiano wa Kimataifa kwa Maendeleo Endelevu | 17.1: Kuinua jitihada za ukusanyaji wa rasilimali za ndani, ikiwa pamoja na kupitia msaada wa kimataifa kwa nchi zinazoendelea, ili kuboresha uwezo wa ndani katika ukusanyaji wa kodi na mapato mengine | 6.4.1. Kukuza uendelevu wa kifedha kwa kuendelea kudumisha hali thabiti za uchumi ili kuchangia ukuaji wa uchumi, kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa kupanua msingi wa kodi, kuongeza wigo wa kodi na kuboresha mfumo wa usimamizi wa kodi |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kwenye Mpango wa Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano wa Mwaka 2025

744. **Jedwali Na.** 44 linaonesha kuwa suala la mapato yasiyo ya kodi linahusiana na shabaha ya 17.1, ikiwa na lengo la kutafuta rasilimali fedha ili kuhakikisha utekelezaji na uendelevu wa malengo ya maendeleo endelevu.

745. Zaidi ya hayo, kuhusiana na Usimamizi wa Fedha za Ruzuku kwa Uendeshaji wa Shule za Umma unaendana na shabaha ya 4.1 inayolenga ifikapo 2030, kuhakikisha wasichana na wavulana wote wanapata Elimu ya bure na kwa usawa. Moja kati ya hatua zilizochuliwa na Fedha za Ruzuku zinawezesha kutolewa kwa Elimu bure na kwa usawa.

ISO 9001:2015 Certified

746. Vile vile, **Jedwali Na. 44** linaonesha kuwa mapato yasiyo ya kodi yanaendana na Shahaba ya 6.4.1 na 6.4.3, mtwalia ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, yenye lengo la utafutaji wa rasilimali fedha ili kuhakikisha utekelezaji wa mpango huo. Na kuhusiana na Usimamizi wa Fedha ya Ruzuku ya Uendeshaji Shule za Umma inahusiana na shabaha ya 6.4.1, inahamasisha matumizi kwa elimu jumuishi.

### 11.1.3 Mipango Mikakati na Jitihada za Serikali kuhusu Utafutaji na Usimamizi wa Rasilimali Fedha

747. Licha ya kuwa na Mpango wa Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, Wizara moja moja zimeandaa mipango mahususi ndani ya mipango ya kati. **Kielelezo Na. 40** Kinaonesha Mikakati ya Serikali kuhusu Ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi na usimamizi wa fedha za ruzuku za uendeshaji wa shule za umma.

**Kielelezo Na. 40: Mikakati ya Serikali kuhusu Usimamizi Ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi na Fedha za Ruzuku za Uendeshaji wa Shule za Umma**

**DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA, 2025**

- ✓ Inasisitiza usimamizi thabiti na wenye ufanisi wa uchumi
- ✓ Inahamasisha ongezeko la Mapato ya Ndani.
- ✓ Lenga kupunguza tegemezi kwa wahisani.
- ✓ Utulivu wa Kiuchumi unaooneshwa na uchumi wenye mfumuko wa bei wa chini na usawa wa msingi wa kiuchumi

**FYDP III 2021/22 - 2025/26**

- ✓ Utafutaji wa rasilimali fedha za ndani na nje kwa ajili ya kugharimia maendeleo.
- ✓ Kuimarisha ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya Kikodi Kutoka kwenye Vyanzo vinavyowezekana.
- ✓ Kuwa na sera imara na Ufanisi imara wa uchumi na kuifanya uwiano wa Deni la Umma na Pato la Taifa kuwa 28.2% ifikapo Juni 2025.
- ✓ Kuhamasisha usawa na upatikanaji wa Elimu bure kwa wote.

**MIKAKATI YA USIMAMIZI WA UKUSANYAJI WA MAPATO YASIYO YA KIKODI NA USIMAMIZI WA FEDHA ZA RUZUKU KWA UENDESHAJI WA SHULE ZA UMMA**

**MIPANGO MIKAKATI YA OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI, WIZARA YA FEDHA, WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI NA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO YA MWAKA (2021/22 - 2025/26)**

- Mpango wa Wizara ya Fedha ulijikita kuboresha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi ilikugharimia maendeleo ya taifa, kupanga malengo halisia ya ukusanyaji wa mapato, kuimarisha nidhamu ya fedha, na kupanua utumiaji wa mifumo ya TEHAMA ilikuboresha Ufanisi na kupunguza upotevu. Mapitio ya katikati ya muhula yanaangazia kuongeza mapato ya serikali na kupunguza mapungufu ya bajeti, huku mapato yasiyo ya kodi yakiangaliwa kama kipimo muhimu ukilinganisha na Pato la Taifa.
- Mpango wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi umeweka kipaumbele kwa usimamizi wa fedha, kupitia mipango imara, udhibiti, ufuatiliaji na tathmini, kwa lengo la kuboresha ukusanya wa Mapato kwa kujengea uweza mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye utayhmini wa Mapato ya ardhi, matumizi ya Tehama kwenye upimaji na utoaji wa hati, kuhusisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye kupimaji, na kuimarisha Taarifa za ardhi, sera na miundombinu.
- Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo inasisitiza upangaji mzuri, bajeti, na usimamizi wa rasilimali, unaounga mkono na utendaji thabiti wa taasisi. Mikakati muhimu inayohusiana na mapato inajumuisha kuimarisha upangaji na ufuatiliaji na tathmini, kuboresha mifumo ya usimamizi wa fedha na mapato na udhibiti wa ndani, kuendeleza utendaji wa taasisi, na kuboresha mifumo ya TEHAMA na usalama Taarifa. Halikadhalika Ofisi ya Waziri Mkuu-Tamisemi moja ya vipaumbele ni kusaidia kutolewa kwa elimu msingi bure.

**Mpango Mkakati wa Wakati wa Kati wa Wizara ya Ujenzi (2019/20 - 2023/24)**

Inalenga kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa kuongeza uwekezaji katika usambazaji wa maji, usimamizi wa maji taka, na ukuzaji wa rasilimali za maji, kuboresha urejeshaji wa gharama za huduma, kupunguza maji yasiyotoa mapato, kuimarisha ufuatiliaji na tathmini

**Mpango Mkakati wa Wakati wa Kati wa Tume ya Umwagiliaji(2023/24 - 2027/28)**

Inalenga kuongeza maeneo umwagiliaji, ilikuhakikisha ubora, ukusanyaji wa rasilimali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji, kutumia Mifumo ya TEHAMA kwenye ukusanyaji wa mapato, kushirikisha sekta binafsi, kuunga mkono wakulima wa umwagiliaji, na kukuza teknolojia na utofauti wa mazao.

*Chanzo:* Uchambuzi wa Wakaguzi kwenye Mikakati na Mipango iliyosimamia mapato yasiyo ya kodi na Fedha za Ruzuku za Uendeshaji Shule, 2025

748. Vilevile, nilibaini jitihada kubwa zilizochukuliwa na Serikali kwenye Ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi katika uanzishaji wa mifumo ya kielectroniki ili kuongeza uwazi na kupunguza upotevu wa mapato. Mifumo iliyoanzishwa ni:

(i) Mfumo wa Malipo ya Serikali: Ulianzishwa kwa lengo la kuwa mfumo mmoja wa kielectroniki wa Ukusanyi wa Mapato kwa Wizara, Idara na Mashirikia;
(ii) Mfumo wa TAUSI: Ulianzishwa mahususi kwa ajili ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Serikali za Mitaa; na
(iii) Utumiaji wa Mifumo ya TEHAMA: Wizara, Idara na Mashirika zinahimizwa kuhuisha Mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya usalama wa Taarifa na Usimamizi, Mfano Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

749. Vivyohivyo, kwa upande wa Usimamizi wa Fedha za Uendeshaji Shule, Mpango wa Sekta wa Maendeleo ya Elimu wa Mwaka 2021/22 hadi 2025/26 umeweka mkazo kwa kuimarisha utawala na usimamizi wa fedha za umma. Jitihada kuu iliyofanywa na Serikali ni utoaji wa Fedha za Undeshaji Shule kwa kila mwezi.

## 11.2 Lengo la Ukaguzi na Mawanda

### 11.2.1 Malengo ya Ukaguzi

750. Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini kama Wizara ya Fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu –Tamisemi zilikusanya na kusimamia rasilimali fedha ili kuhakikisha utekelezaji wa mpango uliopangwa.

ISO 9001:2015 Certified

751. Malengo Mahususi yalikuwa ni kuangalia kama:

(a) Wizara ya Fedha ilisimamia ipasavyo ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi ili kuhakikisha utafutaji wa kutosha wa Rasilimali Fedha za ndani;

(b) Ofisi wa Waziri Mkuu-Tamisemi ilisimamia ipasavyo Fedha za Ruzuku za uendeshaji shule kwa ajili ya gharama za uendeshaji na ununuzi wa vitabu, ili kuhamasisha upatikanaji wa Elimu kwa usawa.

### 11.2.2 Mawanda ya Ukaguzi

752. Kwenye Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mapato Yasiyo ya Kodi, mkaguliwa mkuu alikuwa ni Wizara ya Fedha. Ukaguzi ulihusisha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wizara ya Maji ambazo ni kati ya Taasisi za Serikali zenye mapato yasiyo ya kodi. Pia, ukaguzi ulimjumuisha Msajili wa Hazina, ambaye ana jukumu la kuhakikisha Ufanisi wa Mashirika ya

Umma. Halikadhalika Mashirika manne ambayo ni: Wakala wa Huduma za Misitu na Mamlaka ya Udhibiti ya Pembejeo Tanzania zilihusishwa, hizi ni taasisi zisizofanya biashara; Shirika la Nyumba la Taifa na Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania ambazo ni taasisi za kibiashara.

753. Zaidi ya Taasisi hizo, pia ilijumuisha mamlaka za serikali za mitaa nne ambazo ni: Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, Halmashauri ya Wilaya ya Momba, Halmashauri ya Jiji la Tanga, na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara. Pamoja na hayo pia Tawala za Mikoa za Songwe, Tanga, na Mtwara zilitembelewa kwa kuwa mamlaka za serikali za mitaa zinawasilisha taarifa za ukusanyaji ya Mapato kwa Tawala za Mikoa.

754. Ukaguzi ulijikita kwenye kutathmini mpangilio na muundo kwenye usimamizi wa mapato yasiyo ya kodi; kubaini vyanzo vipya vya mapato vinavyolingana na kanuni za ukusanyaji wa mapato; mifumo na michakato yenye ufanisi katika kuhakikisha makadirio halisi ya mapato yasiyo ya kodi; na mifumo na michakato ya ukusanyaji yenye ufanisi, Pamoja na ufuatiliaji na kuripoti kwa kiwango cha kutosha cha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi. Ukaguzi huo ulijikita kwa kipindi cha miaka minne (4) kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25.

755. Pia, ukaguzi wa usimamizi wa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji Shule za Umma, mkaguliwa mkuu alikuwa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI.

ISO 9001:2015 Certified

756. Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ilikuwa inahusika kwenye kutenga bajeti na kugawa ruzuku za kila shule kulingana na idadi ya wanafunzi waliosajiliwa. Pia, ilikuwa na jukumu la kusimamia na kudhibiti matumizi ya ruzuku hizo. Zaidi ya hayo, ukaguzi ulijumuisha Taasisi ya Elimu Tanzania. Hii ni Taasisi ya Serikali inayohusika na uzalishaji / ununuzi, na usambazaji wa vitabu vya masomo kwa shule za Umma.

757. Mahususi ukaguzi ulijikita kwenye uandaaji wa bajeti, utolewaji wa fedha na matumizi ya fedha za ruzuku za uendeshaji wa shule. Ukaguzi ulijikita kwa kipindi cha miaka mitatu (3) ya fedha ambao ni: 2022/23, 2023/24, na 2024/25.

## 11.3 Matokeo ya Jumla ya Ukaguzi kuhusu Ukusanyaji wa Mapato Yasiyo ya Kodi


### 11.3.1 Ukusanyaji na Mchango Usiotosheleza wa Mapato Yasiyo ya Kodi

758. Nilibaini kuwa mapato yasiyo ya kodi hayakukusanywa kwa ufanisi. Hii ilidhibitishwa kwa kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, na mchango mdogo wa mapato yasiyo ya kodi kwenye bajeti ya Taifa kama inavyoelezwa hapa chini.

**(a) Kutofikia kwa Malengo ya Ukusanyaji wa Mapato Yasiyo ya Kodi**

759. Nimebaini kuwa malengo yalilowekwa ya kukusanya mapato yasiyo ya Kodi hayakufikiwa kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25, kama ilivyoelezwa katika **Kielelezo Na. 41.**


**Kielelezo Na. 41: Uchambuzi wa Malengo na Kiwango Kilichokusanywa cha Mapato Yasiyo ya Kodi**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Taarifa Makadirio ya Mapato- Wizara ya Fedha (2021/22-2024/25) wa Mwaka 2025

760. **Kielelezo Na. 41** kinaonesha, mapato yasiyo ya kodi yaliongezeka kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2023/24, na baadae kupungua kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, kuna maboresho kwenye ukusanyaji. Mwelekeo wa ufanisi wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kwa kipindi cha miaka minne yameoneshwa kwenye **Kielelezo Na.42**.

**Kielelezo Na. 42: Uchambuzi wa Makadirio na Kiwango Kilichokusanywa cha Mapato Yasiyo ya Kodi**




*Chanzo:* **Uchambuzi wa Wakaguzi kwenye Taarifa ya Wizara ya Fedha kuhusu Mapato Yasiyo ya Kodi Yaliyokusanywa Mwaka** 2025

761. **Kielelezo Na. 42** kinaonesha kuwa mapato ya yasiyo ya Kodi kwa Miaka ya Fedha 2022/23 na 2023/24, yalifikia asilimia 79 na 74, mtawalia. Mapato yasiyo ya kodi hayakufikia lengo lililowekwa kutokana na ufanisi usioridhisha wa Mashirika ya Umma. Hii ilitokana na kuanzishwa kwa ruzuku za mbolea kwenye Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania na kutofuatilia uwasilishaji wa gawio kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania.

ISO 9001:2015 Certified


762. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Fedha haikufuatilia vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi vilivyotoa kiasi kikubwa na kidogo kutokana na ukosefu wa taarifa za kina kuhusu vyanzo hivyo, kwani Wizara ya Fedha haikuwa na Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mapato Yasiyo ya Kodi. Hii ilisababisha ukusanyaji wa taarifa za mwenendo wa utendaji kwa kila chanzo kushindikana na kutotambua vyanzo vya mapato vinavyoshindwa/kusalia bila kufanya kazi.

763. Ukusanyaji usiotosheleza wa mapato yasiyo ya kodi unasababisha serikali kushindwa kufadhili miradi ya umma na kuongeza utegemezi wake wa mikopo na kwa wadau wa maendeleo.

**(b) Mchango Usiotosheleza wa Mapato Yasiyo ya Kodi kwenye Bajeti ya Taifa**

764. Nilibaini kuwa mchango wa mapato yasiyo ya kodi kwenye Bajeti ya Taifa ni kwa asilimia 6 hadi 6.9 kuanzia Mwaka 2021/22 hadi 2024/25 kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 43.**


**Kielelezo Na. 43: Uchambuzi wa Bajeti Kulingana na Vyanzo vya Mapato**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti wa Mwaka 2025

765. **Kielelezo Na. 43** kinaonesha kuwa mchango wa mapato yasiyo ya kodi yanachangia kiwango cha chini kwenye Bajeti ya Taifa, kiwango kidogo zaidi kilikuwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Uchambuzi zaidi wa mchango wa mapato yasiyo ya kodi kwa asilimia umeonesha kwenye **Kielelezo Na. 44.**

**Kielelezo Na. 44: Asilimia ya Mchango wa Mapato Yasiyo ya Kodi kwenye Bajeti ya Taifa**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kwenye Taarifa za Wizara ya Fedha za Utekelezaji wa Bajeti, 2025

766. **Kielelezo Na. 44** kinaonesha mchango wa mapato yasiyo ya kodi ni asilimia 6 na 6.9 ikionesha nchi inategemea zaidi kwenye Mapato ya Kodi.

767. Zaidi ya hayo, ukaguzi ulichambua, mchango wa mapato yasiyo ya kodi kwenye bajeti za taasisi zilizochaguliwa kwenye ukaguzi, kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 45.**

**Jedwali Na. 45: Uchambuzi wa Taarifa kwa Asilimia Upungufu wa Mchango wa Mapato Yasiyo ya Kodi kwenye Bajeti**

| Taasisi | | Tofauti ya Asilimia ya Mchango wa Bajeti (Makadirio dhidi ya Uhalisia) | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Wizara, Idara na Wakala za Serikali | Tume ya Taifa ya Umwagiliaji | 585.8 | 561.4 | 51.0 | 2.9 |
| | Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 139.7 | 152.5 | 244.8 | 107.7 |
| | Wizara ya Habari Sanaa Utamaduni na Michenzo | 0.5 | 0.0 | 0.9 | 0.5 |
| | Wizara ya Maji | 0.1 | 0.1 | -0.2 | 0.3 |
| Taasisi za Umma Zisizofanya Fanya Biashara (15%) | Wakala Huduma za Misitu | -0.29 | -0.60 | -0.90 | -2.23 |
| | Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania | 2.36 | -0.25 | 1.17 | 0.00 |
| Taasisi za Umma zinazofanya Umma (Gawio) | Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania | -0.02 | -0.03 | 0.96 | -0.33 |
| | Shirika la Taifa la Nyumba | 0.25 | 0.00 | 0.00 | -0.74 |
| Mamlaka za Serikali za Mtaa | Halmashauri ya Momba | 0.3 | -2.0 | -4.8 | -1.3 |
| | Halmashauri ya Musoma | 0.8 | 0.4 | -0.4 | -0.7 |
| | Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara | 4.7 | 5.5 | 2.5 | -5.3 |
| | Halmashauri ya Jiji la Tanga | -0.2 | 0.5 | 0.4 | 5.4 |

ISO 9001:2015 Certified

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu asilimia ya Mchango wa Mapato Yasiyo ya Kodi kwenye Bajeti wa Mwaka 2025

768. **Jedwali Na. 45** linaonesha kuwa kwa Wizara, Idara na Wakala, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi zilichangia kiwango kidogo tofauti na ilivyokadiliwa kwenye bajeti, kwa taasisi zilizo chaguliwa kwa miaka yote iliyokaguliwa, ikifuatiwa na Mamlaka ya Uthibiti wa Mbolea kwa Mashirika ya Umma. Hata hivyo, asilimia kwa kiwango cha upungufu kilikuwa chini ya 5.5.

769. Hii ilitokana na kutotumia vyanzo mbadala vya Mapato, Ufanisi usiotosheleza wa ukusanyaji wa mapato, na kutofikia kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato.

### 11.3.2 Upungufu wa Muundo na Uwezo wa Taasisi kwenye Usimamizi wa Mapato Yasiyo ya Kodi

770. Nilibaini upungufu wa muundo na uwezo wa taasisi kwenye usimamizi wa mapato yasiyo ya kodi kama inavyoelezwa hapa chini.

#### (a) Uwezo Usiotosheleza wa Muundo wa Majukumu kwenye Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato Yasiyo ya Kodi


771. Nilibaini kuwa wafanyakazi watatu kati ya ishirini na wawili (22) kwenye Kitengo cha Sera za Fedha walikuwa wanashughulikia usimamizi wa mapato yasiyo ya kodi kwa wizara, idara na wakala 74 na mashirika ya umma 70 yaliyopo chini ya Msajili wa Hazina. Uhaba wa wafanyakazi ulichangiwa na kutotolewa kwa majukumu na wajibu ipasavyo jambo ambalo linasababisha ukosefu wa ufuatiliaji unaofaa.

772. Kukosekana kwa wafanyakazi wa kutosha wa kusimamia mapato yasiyo ya kodi kulitokana na muundo wa kitengo ambao unaathiri ubainishaji wa majukumu yanayohusiana na mapato yasiyo ya kodi, kama ilivyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 45**.

773. Kukosekana kwa majukumu yaliyoainishwa yanazuia kuainisha upungufu wa wafanyakazi na kusababisha nafasi za wafanyakazi kutokuwapo kwenye orodha ya wafanyakazi wa Wizara ya Fedha wanaohitajika, kinyume na kifungu cha 5 cha Sheria ya Fedha za Umma [Sura.348 Toleo la. 2020], kinachoitaka Wizara Fedha kuhakikisha ufanisi wa mifuko, muundo na uwezo wa kusimamia ukusanyaji wa mapato.

ISO 9001:2015 Certified

**Kielelezo Na. 45: Uchambuzi wa Upungufu na Athari Zake**




***Chanzo*:** Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Wajibu na Majukumu ya Wizara ya Fedha wa Mwaka 2025

774. **Kielelezo Na. 45** kinaonesha kuwa majukumu ya usimamizi wa mapato yasiyo ya Kodi hayajaainishwa kwenye Wizara ya Fedha. Nilibaini kuwa, majukumu 5 kati ya 10 yaliyoainishwa kwenye muundo wa Wizara ya Fedha yanaendana na kodi, yanayobaki yanaendana na kodi na yasiyo ya kodi. Hakuna jukumu lililoelezwa kwa ajili ya usimamizi wa mapato yasiyo ya kodi.

775. Kwa nyongeza, sheria zilizopo, hasa Sheria ya Fedha za Umma na Kanuni zake, zimetoa tu masharti ya jumla bila mwongozo wa kina wa kiutendaji unaohusiana na mapato yasiyo ya kodi.

776. Upungufu huu kwa pamoja ulikwamisha uwezo wa Serikali wa kuratibu, kufuatilia, na kupanua ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kwa ufanisi.

777. Zaidi ya hayo, nilibaini kutokuwapo kwa Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa zisizo za Kodi, ambao ungeboresha ufuatiliaji wa vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi kwenye ngazi ya Wizara. Wizara ya Fedha haikuwa na hifadhi ya taarifa kamili iliyojumuishwa ya vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi. Taarifa zipo kwenye mifumo mbalimbali isiyounganishwa, ikiwemo Mfumo wa pamoja wa Usimamizi wa Bajeti uliokuwapo, Mfumo wa PlanRep na Mfumo wa Taarifa wa Msajili wa Hazina bila kuiwezesha Wizara kupata Taarifa zote za mifumo hiyo.

778. Pengo hili lilitokana na usimamizi duni wa mapato yasiyo ya kodi, ukiacha Wizara ya Fedha bila Taarifa ya vyanzo hivyo. Matokeo yake, upangaji, ukusanyaji, ufuatiliaji, na uwajibikaji wa mapato yasiyo ya kodi katika Taasisi za Serikali hazikufanyika ipasavyo.

### (b) Ukosefu wa Mfumo wa Uratibu kati ya Taasisi

779. Nilibaini kuwa Wizara ya Fedha ilichukua hatua ya kuziagiza Wizara, Idara na Wakala (Kupitia barua ya 14 July 2023 yenye Kumb. CAB.481/558/01) ya kuteua Maafisa watakao ratibu masuala ya mapato yasiyo ya kodi. Hata hivyo, haikuainisha muundo wa uratibu utakavyokuwa mahususi kuhusiana na vikao vya mara kwa mara, na jinsi ya kubadilishana Taarifa na Wizara ya Fedha.

ISO 9001:2015 Certified

780. Kwa undani, upungufu huo unaoneshwa kwenye **Jedwali Na. 46**. Ukosefu wa namna ya uratibu ni kinyume na Sehemu 5.2.5 ya Mpango wa Tatu wa Miaka Mitano ya Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2021/22-2025/26, unaitaka Serikali kupanua vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi na taratibu za malipo.

**Jedwali Na. 46: Uchambuzi wa Njia za Uratibu kwenye Usimamizi wa Mapato Yasiyo ya Kodi**

| Shughuli iliyochambukiwa | Wizara | Msajili wa Hazina | Mamlaka ya Serikali za Mitaa |
|---|---|---|---|
| Utoaji wa Taarifa Mara kwa Mara | v | v | x |
| Vyanzo vya Mapato | x | x | x |
| Kwenda Kuona eeneo | v | x | x |
| Mikutano ya Wahusika Muhimu | x | v | x |
| Mikutano ya Jumla | v | v | x |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Uratibu kati ya Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu-Tamisemi, na Msajiri wa Hazina

**Ufunguo:**
V - Ilijumuishwa
X – Haijajumuishwa

**Jedwali Na. 46** linaonesha kuwa, kulikuwa na upungufu uliobainishwa katika uratibu wa usimamizi wa mapato yasiyo ya kodi, licha ya kuwa na Afisa anayeshughulikia uratibu kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina, na kwa wizara husika kuwasilisha taarifa za kila mwezi; mchakato huo haukuwapo kimaandishi. Zaidi ya hayo, taarifa hizi hazikuainisha kwa kina vyanzo vya mapato na hakukuwa na muda ulioainishwa kwa ajili ya mikutano na maafisa wanaohusika na uratibu pamoja na wadau wengine kuhusu usimamizi wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi.

Pia, nilibaini kwamba ukosefu wa mfumo maalumu wa uratibu kutoka Wizara ya Fedha hadi Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Mamlaka za Serikali za Mitaa ulisababisha kushindwa kwa ufanisi katika kushirikiana kwa taarifa.

781. Nilibaini kwamba ukosefu wa uratibu wa kutosha ulitokana na ukosefu wa muundo rasmi wa uratibu na kila taasisi kusimamia ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kivyake.

**(c) Mikakati Isiyojitosheleza Iliyojikita kwenye mapato yasiyo ya kodi**

782. Nilibaini kuwa, Wizara ya Fedha ilikuwa na mikatati isiyojitosheleza iliyojikita kwenye ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2024/25. Ingawa Mkakati wa kati wa Ukusanyaji wa Mapato ulizinduliwa 2025, nilibaini kuwa mkakati huo umeweka mkazo kwenye sekta ya madini (mirabaha na tozo ya ukaguzi), Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI (kodi ya pango la ardhi); sekta ya utalii (tozo ya utalii), na ada kutoka mashirika ya umma (gawio na michango). Mpango huu wa kati wa ukusanyaji wa mapato unajumuisha pia mapato ya huduma, ushuru wa mazao, ada za mali, ada za mabango na leseni ya biashara.

783. Kadhalika, nilibaini kuwa mpango wa kati ulijumuisha vyanzo vichache vya mapato yasiyo ya Kodi na ulikuwa na mikakati michache ya ukusanyaji wa mapato yasiyo ya Kodi.

784. Hii inatokana na kutojumuisha ipasavyo kwa vyanzo vyote vya mapato na mikakati isiyotosheleza ya ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi. Hali hii inaisababishia Wizara ya Fedha kutumia vyanzo vyote vya Mapato vilivyopo.

### 11.3.3 Ubainishaji Hafifu wa Vyanzo vya Mapato Yasiyo ya Kodi

785. Wakati wa Ukaguzi nilibaini kuwa vyanzo vya mapato yasiyo ya Kodi havikuongezeka na vilipungua kwa Wizara, Idara na Wakala, ambazo ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Ardhi, Nyumba na



ISO 9001:2015 Certified

Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maji, na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Pia, nilibaini kuwa ni Shirika la Umma moja kati ya manne yaliyochanguliwa ambayo ni Wakala wa Misitu Tanzania, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania na Shirila la Taifa la Nyumba yalikuwa na vyanzo vipya. Kwa kuongeza Halmashauri 3 kati ya 4, zilizochaguliwa ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Momba, Musoma, Manispaa ya Mtwara, na Jiji la Tanga, zilifanya ubainishaji wa Vyanzo vipya vya Mapato Yasiyo ya Kodi. Upungufu kwenye ubainishaji wa Vyanzo vipya umetokana na:

**(a) Kutokuwapo kwa Utaratibu Rasmi Uliowekwa kwa ajili ya Utambuzi wa Vyanzo Vipya vya Mapato**

786. Nilibaini kuwa Wizara, Idara na Wakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma yaliyochaguliwa, kwa kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/22 to 2024/25 hazikuweka utaratibu rasmi wa Utambuzi wa vyanzo vya Mapato. Pamoja na kuwa muongozo wa Mipango na bajeti Sehemu ya 2.3.2 wa 2024/25 inaelekeza kuwa na mikakati ya kupanua wigo wa vyanzo vipya vya Mapato vinavyoendana na msingi wa ukusanyaji wa mapato.

787. Hata hivyo, ni Shirika moja tu ambalo ni Wakala la Misitu Tanzania kati ya Mashirika manne linatumia njia ya kufanya utafiti kubaini vyanzo vipya vya mapato na kubadili viwango vya kutoza, ingawa utaratibu huu haujawekwa kimaandishi.

ISO 9001:2015 Certified

788. Hii imetokana na kukosekana kwa utaratibu rasmi zilizoainishwa na Wizara ya Fedha juu ya utambuzi wa vyanzo vipya vya mapato. Kadhalika, kulikuwa na ukosefu wa njia za Wizara ya Fedha kufuatilia ili kuhakikisha Wizara, Idara na Wakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma zina utaratibu rasmi wa kubainisha vyanzo vipya vya Mapato.

**(b) Upungufu wa Kanzidata Jumuishi ya Vyanzo vya Mapato Yasiyo ya Kodi**

789. Nilibaini kukosekana kwa Kanzidata ya hifadhi ya taarifa ya vyanzo vya Mapato visivyo vya kodi katika Wizara ya Fedha. Taarifa zipo kwenye mifumo tofauti ikiwa pamoja na mfumo wa pamoja wa Usimamizi wa bajeti, mfumo wa PlanRep, na Mfumo wa Taarifa wa Msajili wa Hazina. Wizara ya Fedha haina ufikiaji kamili wa taarifa za mifumo hiyo.

790. Wizara ya Fedha kupitia mfumo wa pamoja wa Usimamizi wa Bajeti inaweka Taarifa za Vyanzo halisi vya mapato kutoka Wizara na kwenye Idara zenye Fungu. Hivyo, haina Taarifa halisi ya vyanzo vya Mapato kutoka kwenye Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambazo zinatunza Taarifa

za vyanzo vya Mapato kwa Mfumo wa PlanRep, ambapo Wizara ya Fedha haina uwezo wa kuona Taarifa zilizopo kwenye mfumo huo.

791. Hii imetokana na na kutounganishwa kwa mifumo hiyo, inayoweka taarifa za vyanzo vya Mapato, na ufuatiliaji usiotosheleza unaofanywa na Wizara ya Fedha hasa kutokana na kutoweka wazi majukumu na uwajibikaji kwenye usimamizi wa mapato yasiyo ya Kodi.

792. Hali hii ilisababisha, Wizara ya Fedha kushindwa kuona vyanzo vyote vya mapato visivyo vya Kodi, na kuhakikisha vyanzo vyote vinajulikana na vinafuatiliwa ili kubaini vyanzo visivyo tumika na vile vinavyokusanya kidogo.

793. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa Wizara ya Fedha haikuweka kipaumbele kwa vyanzo vya kipaumbele kwa sababu ya kukosekana kwa Kanzidata ya taarifa ya jumla ya vyanzo vyote. Wizara inatunza tu taarifa zinazohusu mapendekezo ya wadau kuhusu viwango vya kutoza kwa Mapato ya kodi na yasiyo ya kodi.

### (c) Kokoseka kwa Utafiti wa Kubaini Vyanzo Vipya vya Mapato Visivyo ya Kodi

Nilibaini kuwa kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/2 hadi 2024/25, Wizara haikufanya Utafiti wa kuweza kubaini vyanzo vipya vya mapato visivyo vya Kodi. Kutokana na hali hiyo, mapato yasiyo ya kodi yaliendelea kutegemea vyanzo vilevile vya mapato vya jadi. **Jedwali Na. 47** limebainisha vipengele vya kina vinavyoweza kutoa fursa ambavyo vilipaswa kufafanuliwa katika utafiti kwa ajili ya kubaini vyanzo vipya vya mapato.

**Jedwali Na. 47: Vipengele Vinavyopaswa Kuelezwa katika Utafiti kwa ajili ya Vyanzo Vinavyowezekana vya Mapato Yasiyo ya Kodi**

| Eneo | Kuangaliwa kwa Kina |
|---|---|
| Kuendana na lengo la Sera | Kusaidia Malengo ya Serikali |
| Uhimilivu wa Chanzo cha Mapato | Kuwa na Mapato ya Uhakika |
| Uendelevu | Uwajibikaji wa kwa Mazingira na Jamii |
| Usawa | Mchango wa Haki na Upatikanaji |
| Ufanisi | Njia sahihi za ukusanyaji na gharama ndogo ya usimamizi |
| Unyumbulifu | Uwezo wa kuendana na mabadiliko |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Mbinu Bora kwa ajili ya Utafiti kuhusu Vyanzo Vinavyowezekana vya Mapato wa Mwaka 2025

794. **Jedwali Na. 47** linaonesha taarifa muhimu kwa kubainisha vyanzo vya mapato vilikosekana kutokana na kutofanyika kwa tafiti. Pengo lililoonekana lilitokana na kukosekana na kutowapo kwa jukumu la kufanya tafiti za vyanzo vya Mapato kwenye Wizara, Idara na Wakala, Mashirika ya Umma na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na kusimamia mapato yasiyo ya kodi.

795. Kutoweza kutafuta vyanzo vipya vya mapato yasiyo ya kodi kumezuia kupanuka na ukuaji wa mapato ya ndani, na kusababisha utegemezi wa vyanzo vya mapato vilivyokuwapo.

### (d) Kuwapo kwa Vyanzo vya Mapato Ambavyo Havijaibuliwa

796. Nilibaini Wizara ya Fedha haijaweza kuibua vyanzo vyote vya Mapato vilivyopo. Hii ni kwa sababu Wizara inategemea kwenye vyanzo vilivyopo kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Bajeti wa Pamoja ambao una taarifa ya vyanzo vilivyowekwa na Wizara, Idara na Wakala pekee, na hakuna njia ya kujua vyanzo vyote vilivyopo kwa Wizara, Idara na wakala, Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa. **Jedwali Na. 48** linaonesha kuwapo kwa Vyanzo vya Mapato ambavyo havijaibuliwa.

**Jedwali Na. 48: Baadhi ya Vyanzo vya Mapato ambavyo Havikuibuliwa**

| Taasisi | Vyanzo vya Mapato ambavyo Havikuibuliwa |
|---|---|
| Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | Kuuza Taarifa za Ardhi (Taarifa za Kijiografia, Ramani za Kidigitali) |
| | Tozo na Adhabu ya Kuchelewesha Kulipa |
| Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo | Haki za Kibiashara za Kutumia Jina la Uwanja |
| Wizara ya Maji | Kibali cha Kumwaga Maji Machafu |
| Tume ya Taifa ya Umwagiliaji | Mafunzo ya Umwagiliaji |
| | Tozo na Adhabu kwa Kuchelewa Kulipa |
| Wakala wa Misitu Tanzania | Fursa ya Biashara ya Kaboni inayotokana na Hifadhi ya Misitu |
| Mamlaka ya Uddhibiti wa Mbolea | Ada ya Usajili |
| | Ada ya Leseni |
| Shirika la Taifa la Nyumba | Tozo na Adhabu kwa Kuchelewa Kulipa |
| | Haki ya kuendeleza kwenda juu |
| | Kukodisha Juu ya Paa la Nyumba kuweka vifaa vya Kuvuna Umeme wa Jua |
| Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania | Tozo ya usafirishaji wa gesi |
| | Fursa ya Biashara ya Kaboni inayotokana na kupunguza hewa chafu |
| Halmashuri ya Wilaya ya Momba | Tozo za kumbi za Muziki/Mchezo, Tozo za kuegesha Magari |
| | Kodi za Nyumba, Ada ya Ukaguzi wa Nyuma (Kuku), Ada za Magulio |
| Halmashuri ya Wilaya Musoma | Tozo za kumbi za Muziki/Mchezo, adhabu, ada za mbolea, Tozo ya Kupangisha Nyumba, Leseni kwa Tiba Asilia,Kibali kwa Tiba Asilia, Usajili wa Vikundi, pango la kukodisha maduka |
| Halmashuri ya Manispaa ya Mtwara | Mchanga, Udongo, Tofali, Kokoto, Ukodishaji wa usafiri, Ada ya Ukaguzi wa Nyuma (Kuku), Bahati |

| Taasisi | Vyanzo vya Mapato ambavyo Havikuibuliwa |
|---|---|
| | Nasibu, Tozo ya Kukodisha Maduka, uazaji wa vitabu na Ada ya Magulio |
| Halmashuri ya Jiji la Tanga | Ada ya Leseni ya Hoteli, matangazo, Tofali, Adhabu, Ada za Mbolea, Ada ya Ukaguzi wa Nyama |
| | Bahati Nasibu, Usajili wa Vikundi, uuzaji wa vitabu, uduvi na Ada ya Magulio |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu vyanzo ambavyo havijaibuliwa kwa Taasisi zilizotembelewa,2025

797. **Jedwali Na. 48** linaonesha kuwapo kwa vyanzo ambavyo havijaibuliwa. Vilevile, nilibaini kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizotembelewa, hakuna Halmashauri ambayo imebaini au kukusanya kutoka kwenye chanzo ambacho halmashauri nyingine inatumia kukusanya Mapato.

798. Hii inatokana na uratibu usiotosheleza kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na kutobadilishana taarifa namna ya kupanua mapato yasiyo ya kodi.

### 11.3.4 Upungufu wa Namna ya Kukadiria Kiwango Halisia cha Kukusanya Mapato Yasiyo ya Kodi

799. Nilibaini kuwa njia zilizokuwa zinatumia kukadiria Mapato ya kukusanya hazijitoshelezi kama inavyoelezwa hapa chini.

**(a) Kutokuwapo kwa Utaratibu Rasmi wa Kukadirio ya Mapato Yasiyo ya Kodi**

ISO 9001:2015 Certified

800. Nilibaini kuwa Taasisi za Serikali hazikuwa na utaratibu rasmi wa kukadiria kiwango cha mapato yasiyo ya kodi ya kukusanywa. Taasisi zilikuwa zinatumia taarifa zilizopita kuweza kukadiria Mapato yatakayokusanywa. Hii ilisababisha kutofanyika kwa baadhi ya hatua muhimu kwenye kutengeneza makadirio ya uhalisia.

**(b) Kukosekana kwa Makadirio yenye Uhalisia kwa Taasisi za Serikali**

801. Nilibaini kuwa Wizara, Idara na Wakala, na Mashirika ya Umma, makadirio hayakuwa na uhalisia, kiwango kilichokadiriwa kilibadilika wakati vyanzo vilikuwa vimebaki vilevile au vimepungua. Pia, kwa baadhi ya matukio makadirio ya Mapato yalikuwa yanapanda ghafla, wakati vyanzo vimepungua, wakati mwingine makadirio yanabaki kuwa juu, ilihali makusanyo halisi ya Mapato mara zote yanakuwa chini.

802. Hii ni kinyume na Kanuni ya 39(3) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 (kama zilivyorekebishwa 2022), inaelekeza makadirio ya Mapato yawe ya uhalisia kwa kuzingatia Taarifa za uhakika. **Jedwali Na. 49** linaonesha

mwelekeo wa vyanzo, makadirio na mapato yaliyokusanywa na Wizara, Idara na Wakala.

**Jedwali Na. 49: Mwelekeo wa Vyanzo, makadirio na Mapato Yaliyokusanywa na Wizara, Idara na Wakala (Sh. bilioni)**

| Wizara, Idara na Wakala | 2021/22 | | | 2022/23 | | | 2023/24 | | | 2024/25 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Chanzo** | **Makadirio** | **Makusanyo** | **Chanzo** | **Makadirio** | **Makusanyo** | **Chanzo** | **Makadirio** | **Makusanyo** | **Chanzo** | **Makadirio** | **Makusanyo** |
| NIRC | 11 | 30 | 0.7 | 9 | 126 | 0.9 | 9 | 10 | 2.1 | 8 | 3.6 | 1.5 |
| MICAS | 9 | 1 | 0.8 | 4 | 0.9 | 0.9 | 4 | 1.0 | 0.7 | 4 | 1.0 | 0.9 |
| MLHHS | 11 | 221 | 131 | 11 | 250 | 155 | 11 | 300 | 139 | 11 | 250 | 157 |
| MoW | 3 | 1 | 1 | 3 | 1 | 1.2 | 3 | 1.2 | 1.3 | 3 | 1.4 | 1.2 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Makadirio ya Mapato Mwaka 2021/2-2024/25

803. **Jedwali Na. 49 l**inaonesha kuwa makadirio kwa Wizara, Idara na Wakala hayakuendana na vyanzo vya Mapato vilivyopo na Ufanisi wa ukusanyaji. Badala yake, Makadirio yalikuwa yanabadilika, kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo mara zote makadirio yalikuwa chini ya kinachokusanywa.

ISO 9001:2015 Certified

804. Nilibaini hali hiyo kwa Mashirika ya Umma kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 50,** kuwa makadirio hayakuzingatia idadi ya vyanzo vya mapato vilivyopo au kiwango kilichopendekezwa, ilikuwa inazingatia taarifa na ufanisi uliopita.

**Jedwali Na. 50: Makadirio kwa Mashirika ya Umma Yaliyochaguliwa (Kiwango Sh. bilioni)**

| Mwaka wa Fedha | Wakala wa Misitu Tanzania | | Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzaia | | Shirika la Taifa la Nyumba | | Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Makadirio ya Mapato Yasiyo ya Kodi | Asilimia (Ongezeko / Pungufu) | Makadirio ya Mapato Yasiyo ya Kodi | Asilimia (Ongezeko / Pungufu) | Makadirio ya Mapato Yasiyo ya Kodi | Asilimia (Ongezeko / Pungufu) | Makadirio ya Mapato Yasiyo ya Kodi | Asilimia (Ongezeko / Pungufu) |
| 2021/22 | 21,824 | - | 8,190 | - | 1,500 | - | 2,500 | - |
| 2022/23 | 20,000 | -8 | 14,658 | 79 | 1,000 | -33 | 2,000 | -20 |
| 2023/24 | 24,268 | 21 | 2,334 | -84 | 1,200 | 20 | 20,000 | 900 |
| 2024/25 | 26,150 | 8 | 24,268 | 940 | 1,200 | 0 | 20,000 | 0 |

***Chanzo***: Uchambuzi wa Wakaguzi Mapato Yasiyo ya Kodi wa Mwaka 2025

805. **Jedwali Na. 50** linaonesha kuwa Mashirika ya umma hayakuzingatia muongozo wa Msajili wa hazina wa kuongeza Makadirio ya Mapato kwa asilimia 10 kila mwaka. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, Makadirio ya Wakala wa Misitu Tanzania yalipungua kwa kiwango kidogo ukilingasha na mashirika mengine, wakati kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, Makadirio ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania yalipungua kidogo.

806. Hali hii ilitokana na kukosekana kwa utaratibu rasmi wa namna ya kufanya ukadiriaji wa Mapato ya kukusanya na kutumia taarifa zilizopita. Hii inafanya serikali kupata changamoto ya kuwa na makadirio ya juu au ya chini ya mapato yasiyo ya kodi, inaathiri uaminifu wa Bajeti na Utekelezaji wake. Hii inazuia ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali, mtiririko wa utabiri wa Mapato, na kuongeza utegemezi wa fedha kutoka kwenye vyanzo vya nje.

### (c) Kutofanyika Mapitio ya Viwango vya Kutoza Ukilinganisha na Bei ya Soko na Gharama za Huduma za Umma Ipasavyo

807. Nilibaini kuwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania alifanya mapitio ya viwango vya kutoza mara kwa mara kwa Mwaka 2023/24 na 2024/25. Pia, Shirika la Taifa la Nyumba nalo lilifanya mapitio 2023/24. Mapitio hayakufanyika kwa Wizara, Idara na Wakala kwa kipindi cha kuanzia 2021/22 na 2024/25. Tozo hazikubadilika kwa miaka kadhaa ingawa kuna mabadiliko ya bei za soko na gharama za utoaji wa huduma kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 51,** Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imekuwa na gharama zilezile za uwanja kwa kipindi chote cha kuanzia Mwaka 2021/22-2024/25, hata

pia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji tozo zake hazijabadilika. Vivyohivyo, kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi gharama za upimaji na umiliki hazikubadilika ingawa kulikuwa na kuongezeka kwa gharama za upimaji, uthamini na utawala.

**Jedwali Na. 51: Hali ya Mapitio ya Gharama kwa Mashirika ya Umma**

| Shirika la Umma | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
|---|---|---|---|---|
| Shirika la Taifa la Nyumba | x | x | v | X |
| Shirika la Maendeleo yaMafuta Tanzania | x | x | x | X |
| Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania | x | x | x | X |
| Wakala wa Huduma ya Misitu Tanzania | x | x | v | V |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Hali ya Mapitio ya gharama za Tozo wa Mwaka 2025

**Ufunguo**
V-Mashirika yaliyofanya mapitio
X-Mashirika ambayo hayajafanya mapitio

808. **Jedwali Na. 51** linaonesha kutofanyika kwa mapitio kwa viwango vya ada na tozo, hii ilitokana na kukosekana kwa muongozo wa kisheria unaowataka kufanya mapitio ya ada na tozo baada ya muda fulani. Kutokufanyika kwa mapitio mara kwa mara kunasababisha huduma kutozwa kidogo na kukusanya mapato kidogo kutoka kwa Mapato yasiyo ya kodi.

809. Hii inapunguza uwezo wa serikali kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vya ndani na kuongeza wigo wa kutafuta fedha kutoka vyanzo vya nje, hali inayosababisha kuongezeka kwa madeni.

### 11.3.5 Taratibu na Mifumo ya Ukusanyaji Kutokuwa na Ufanisi wa Kutosheleza

810. Nilibaini upungufu kwenye mifumo na taratibu za ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, kukosekana kwa taratibu sanifu za kiuendeshaji kwenye ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi na matumizi yasiyotosheleza ya mifumo ya TEHAMA. Hii ni kinyume na Kanuni 57 ya Kanuni ya Fedha ya Umma ya 2001 (kaa ilivyorekebishwa 2022) kama ilivyoelezwa hapa chini:



ISO 9001:2015 Certified

### (a) Kukosekana kwa Taratibu Sanifu za Kiuendeshaji kwenye Ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya Kodi

811. Nilibaini kukosekana kwa taratibu sanifu za kiuendeshaji kwenye ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya kodi kwenye Taasisi nilizozikagua, na kila taasisi inakusanya inavyoona inafaa. Hii imefanya kujilimbikiza kwa madeni kwenye Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, kwani wakulima hawakuweza kulipa madeni yao kutokana na taratibu kutofautiana. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inatofauti ya mfumo wa malipo kwa mikoa tofauti. Kwa sasa kuna ulingaifu kwa mikoa ya Mwanza, Tanga, Dodoma, Arusha na Mbeya, ila kwa Dar es Salaam bado inatumia mfumo tofauti.

### (b) Matumizi Yasiyotosheleza ya Mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya Ukusanyaji wa Mapato Yasiyo ya Kodi kwa Ufanisi

812. Nilibaini ufanisi usiojitosheleza kwenye mifumo wa ukusanyaji na ukosefu wa upatikanaji wa intaneti katika baadhi ya maeneo, hasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Momba na Halmashauri ya Wilaya ya Musoma. Hali hii inakwamisha utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa Tanzania wa 2024–2034.

813. Pia, nilibaini ufanisi usiojitosheleza wa mfumo wa kutoa ankra na taarifa, hali hii niliikuta Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambapo Mteja inampasa kutembelea kwenye Ofisi za Wizara ili kupata ankra kwa ajili ya kufanya malipo. Hii inazuia ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya kodi.

814. Kadhalika, nilibaini kuwa Mamlaka za Serikali za Halmashauri ya Wilaya ya Momba, Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara, Halmashauri ya Wilaya ya Musoma na Halmashauri ya Jiji la Tanga, zilikuwa na mashine za kukusanyia Mapato zisizotosheleza, kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 52.**

**Jedwali Na. 52: Hali ya Mashine za Kukusanya Mapato kwenye Halmashauri Zilizotembelewa**

| Jina la Halmashauri | Mashine Zinahitajika | Mashine Zilizopo | Mashine Zinazotumika | Mashine Zilizoharibika | Mashine Zilizopungua |
|---|---|---|---|---|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Momba | 72 | 56 | 45 | 11 | 27 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Musoma | 63 | 87 | 43 | 44 | 20 |

| Jina la Halmashauri | Mashine Zinahitajika | Mashine Zilizopo | Mashine Zinazotumika | Mashine Zilizoharibika | Mashine Zilizopungua |
|---|---|---|---|---|---|
| Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara | 90 | 72 | 37 | 15 | 53 |
| Halmashauri ya Jiji la Tanga | 200 | 134 | 86 | 48 | 114 |

*Chanzo:* **Uchambuzi wa Wakaguzi** vyanzo vya Mapato wa Mwaka 2025

815. **Jedwali Na. 52** linaonesha kuwapo kwa uhaba wa mashine za kukusanyia mapato. Halmashauri ya Momba ilikuwa na upungufu wa mashine 27, Musoma mashine 20, Mtwara 53, Tanga inaonesha kuwa na upungufu mkubwa wa mashine 114. Hii inaathiri ukusanyaji wa Mapato kinyume na kifungu 17A (1) cha Sheria za Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya 2019.

### 11.3.6 Ufuatiliaji na Utoaji Taarifa Hafifu kuhusu Ukusanyaji wa Mapato Yasiyo ya Kodi

816. Nilibaini kuwa Wizara ya Fedha haikuhakikisha ipasavyo juu ya ufuatiliaji na utoaji taarifa kuhusu ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya kodi kama ifuatavyo:

ISO 9001:2015 Certified

#### (a) Kukosekana kwa Mipango na Utaratibu Rasmi wa Ufuatiliaji na Utoaji wa Taarifa juu wa Ufanisi wa Ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya Kodi

817. Nilibaini kuwa Wizara haikuwa na utaratibu rasmi na mipango ya ufuatiliaji wa ufanisi wa ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya kodi. Hii ni kinyume na Sehemu ya 4.6.1(vii) wa muongozo wa mpango na Budget 2024/25.

818. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa Wizara ya Fedha haijatoa kiolezo sanifu kinachotoa muongozo wa kupima ufanisi wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, Hali hii ilisababisha kila Wizara, Idara na Wakala kutuma taarifa Wizara ya Fedha kwa muundo tofauti tofauti. Pamoja na kuwa Wizara, Idara na Wakala zilikuwa zinawasilisha makisio ya fedha ya kila mwezi, hakuna Ushahidi kuwa taarifa zilikusanywa kwa pamoja. Kwa hivyo, ufuatiliaji ulikuwa unafanyika kwa tukio na kwa kuangalia mawasiliano bila kuzingatia mpango wa upimaji wa ufanisi.

### (b) Kukosekana kwa Mfumo wa Taarifa wa Kuweza Kufuatilia Ufanisi wa Ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya Kodi

819. Nilibaini kuwa, Wizara ya Fedha haikuwa na mfumo wa taarifa wa kuweza kufuatilia ufanisi wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kwa Wizara, Idara na Wakala.

820. Pia, Wizara ya Fedha haikuunganishiwa mfumo wa Msajili wa Hazina, na wa Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ingawa Sehemu ya 4.6.1 (ix) ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa 2024/25, unataka kuimarisha kwa tathmini na ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mpango ili kuendana na malengo ya Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

821. Hata hivyo, hakuna mfumo wowote unaotoa taarifa za ufuatiliaji na tathmini na ufuatiliaji haufanywi kwa mfumo wa TEHAMA na Taarifa za kila mwezi zinawasilishwa kwa kupitia barua pepe au nakala ngumu kwa maelekezo ya barua kutoka Wizara ya Fedha.

### (c) Kukosekana kwa Viashiria Vya Kupima Utendaji wa Kufuatilia Ufanisi wa Ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya Kodi

822. Nilibaini kuwa Wizara ya Fedha, na Taasisi za Serikali (Wizara, Idara na Wakala) zilizokaguliwa hazikuwa na viashiria vya kupima utendaji kwa ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi. Wizara, Idara na Wakala zilikuwa zinatuma taarifa za Mapato ambazo zimejikita kwenye kutoa takwimu za jumla na ambazo sio za kina, bila kutathmini ufanisi na viashiria vilivyowekwa. Hali hiyo inaizuia Wizara ya Fedha kutofanya Uchambuzi wa kina juu ya taarifa zilizowasilishwa.

### (d) Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Wizara ya Fedha Hazikufuatilia Ukusanyaji wa Mapato kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa

823. Nilibaini kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Wizara ya Fedha hazikufuatilia ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi. Kilichofanyika ni utoaji wa mafunzo namna ya kutumia Mfumo wa TAUSI kwenye ukusanyaji wa mapato na kuuhuisha. Hii ni kinyume na Sehemu ya 5.1.3 wa Mwongozo wa Serikali wa Tathmini na Ufuatiliaji.

Ufuatiliaji usiotosheleza na utoaji taarifa unaizuia Serikali kubaini, na kuongeza vyanzo vya Mapato yasiyo Kodi na kukosa Mapato ya Ndani na kusababisha kuongezeka kwa utegemezi kwenye vyanzo vya nje.

## 11.4 Matokeo Jumla ya Ukaguzi wa Usimamizi wa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji wa Shule za Umma

824. Wakati wa Ukaguzi nilibaini kuwa fedha za ruzuku za uendeshaji wa shule kwa ajili ya kugharimia uendeshaji na ununuzi wa vitabu zilipangwa kidogo ukilinganisha na idadi ya wanafunzi, na hizo hazikutolewa zote na kwa ufasaha na baadhi zilizotolewa hazikutumika kwa lengo lililokusudiwa, kama ilivyoelezewa hapa chini.

### 11.4.1 Fedha za Ruzuku za Uendeshaji wa Shule za Umma Hazikutengwa kwa Utoshelevu

825. Nilibaini kuwa Fedha za Ruzuku za Uendeshaii wa Shule kwa ajili ya kugharimia uendeshaji wa shule na kwa ajili ya ununuzi wa vitabu hazikutengwa kwa utoshelevu kama inavyoelezwa hapa chini.

### (a) Fedha za Rukuzu za Ununuzi wa Vitabu Hazikutengwa kwa Utoshelevu

826. Nilibaini kuwa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji Shule zilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa vitabu zilikuwa hazitoshelezi ukilinganisha na idadi ya wanafunzi kama ilivyoelekeza kwenye aya ya tatu ya Muongozo wa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI wa Utaratibu wa Kutumia Fedha za Ruzuku za Undeshaji wa Shule za Umma za Msingi na Secondary, 2015. Upungufu wa Fedha zilizotengwa ulikuwa kati ya asilimia 46 na 74 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 53**.

**Jedwali Na.53: Kiwango cha Fedha za Rukuzu za Ununuzi wa Vitabu Kilichotakiwa na Kilichotengwa**

| Mwaka wa Fedha | Kilichitakiwa kwa Kuzingatia Idadi ya Wanafunzi (Sh. milioni) | Kiwango Kilichotengwa (Sh Milioni) | Kiwabgo Kilichopungua (Sh Milioni) | Asilimia ya Upungufu (%) |
|---|---|---|---|---|
| 2022/23 | 81,717 | 44,000 | 37,717 | 46 |
| 2023/24 | 88,955 | 34,400 | 54,555 | 61 |
| 2024/25 | 93,678 | 24,309 | 69,369 | 74 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Sensa ya Shule, Bajeti ya Maendeleo ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI (kwa Mwaka 2022/23, 2023/24 na 2024/25) wa Mwaka 2025

827. **Jedwali Na. 53** linaonesha kuwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, fedha iliyotengwa ni Sh. bilioni 44 kati ya Sh. bilioni 81, hii ilichangia upungufu kwa asilimia 46, upungufu huo uliongeza kwa asilimia 61 kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 na asilimia 74 kwa Mwaka 2024/25.

828. Hali hii ilisababishwa na ukomo wa bajeti uliowekwa na Wizara ya Fedha kwa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI juu ya Bajeti ya Ruzuku bila kuzingatia idadi ya wanafunzi.

829. Hali hii ilichangia upungufu wa vitabu. Kwa mfano, kwa shule za msingi, uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi wa 1:1 haikufikia uwinao kwa Mwaka 2022/23,2023/24 na 2024/25. Hii inahatarisha kutofikia lengo la kuwa na kitabu kimoja kwa mwanafunzi kwa somo iliyowekwa kwenye Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu kwa 2025/26 hadi 2029/30.

### (b) Utengaji wa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji wa Shule usio na Uwiano kwa Shule za Msingi na Sekondari

830. Nilibaini kuwa utengaji wa Fedha za Ruzuku kwa ajili ya uendeshaji wa shule za msingi zilikuwa zinatengwa zaidi ya zinazopaswa kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, 2023/24, na 2024/25; na kwa Shule za Sekondari zilitengwa chini ya kiwango kilichopaswa kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 na 2023/24, isipokuwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 54.**

**Jedwali Na. 54: Fedha za Ruzuku ajili ya gharama za Shuleni zilizopaswa Kutengwa na zilizotengwa**

| Mwaka wa Fedha | Aina ya Shule | Bajeti Zilizotengwa (Sh) | Bajeti Iliyotakiwa (Sh) | Juu/(Chini)Bajeti (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| 2022/23 | Msingi | 73,964,982,000 | 65,235,048,000 | 8,729,934,000 |
| | Sekondari | 32,407,575,000 | 35,294,850,000 | (2,887,275,000) |
| 2023/24 | Msingi | 76,255,740,000 | 64,946,244,000 | 11,309,496,000 |
| | Sekondari | 35,387,575,000 | 38,466,937,500 | (3,079,362,500) |
| 2024/25 | Msingi | 76,596,924,000 | 64,439,850,000 | 12,157,074,000 |
| | Sekondari | 42,614,112,500 | 41,427,475,000 | 1,186,637,500 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Sensa za Shule za Mwaka na Ukomo wa Bajeti (2022/23, 2023/24 na 2024/25) wa Mwaka 2025

831. **Jedwali Na. 54** linaonesha bajeti za uendeshaji wa shule zilizotengwa kwenye Ruzuku za uendeshaji Shule za Msingi kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, 2023/24, na 2024/25 zilizidi kwa Sh. bilioni 8.7, Sh. bilioni 11.3, na Sh. bilioni 12.2 mtawalia. Tofauti na shule za Sekondari ambazo zilitengewa fedha chini ya kiwango kilichopaswa kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 na 2023/24 kwa Sh. bilioni 2.9 na Sh. bilioni 3.1. Hata hivyo, kwa Mwaka wa fedha 2024/25, zilitengewa Sh. bilioni 1.19 juu ya kiwango kinachotakiwa.

832. Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, inaonesha kuwa wakati wa maoteo ya Bajeti ilitumia maoteo ya wanafunzi ambao sio walio kwenye sensa ya Mwaka

ya Shule, kwa sababu sensa inahitimishwa tarehe 31 Machi kila mwaka, ikiashiria kuwa taarifa za darasa la kwanza, kidato cha kwanza na kidato cha tano hazikujilikana.

833. Hali hii ilisababisha shule za msingi kutengewa fedha nyingi na shule za sekondari kutengewa fedha kidogo zaidi ya iliyotakiwa ukilinganisha na idadi ya wanafunzi waliosajili.

### (c) Kiwango kidogo na kisicho sawa cha fedha za uendeshaji zinazopelekwa shuleni kila mwezi

834. Wakati wa Ukaguzi nilibaini kuwa, kwa wastani kiwango cha chini kilichopokelewa kwa shule za kilikuwa Sh. 1,365.15 na Sh. 16,815 kwa shule za msingi na sekondari mtawalia, na kiwango cha juu kilikuwa Sh. 3,564,190 na Sh. 4,228,923 kwa shule za msingi na sekondari Mtawalia. Kwa nyongeza, nilibaini kuwa, kwa wastani asilimia 15 ya shule za sekondari na asilimia 26 ya shule za msingi zilipokea fedha za ruzuku kwa Mwezi, kiwango ambacho ni kidogo kuliko posho za madaraka ya Sh. 250,000 na Sh. 200,000 kwa Wakuu wa shule. **Jedwali Na. 55** inaonesha taarifa za fedha za chini na juu zilizopokelekwa shuleni, pamoja na taarifa za shule zilizopokelekewa ni kidogo kuliko posho za madaraka wa Wakuu wa Shule

**Jedwali Na. 55: Mwenendo wa Fedha za Ruzuku za Uendshaji Zinazopelekwa Shule za Msingi**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Shule | Kiwango cha Fedha Kilichopelekwa (TZS) | | Shule za Msingi ziliopelekewa Fedha kidogo kuliko posho za madaraka wa Wakuu wa Shule | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kiwango cha Chini | Kiwango cha Juu | Idadi | Asilimia (%) |
| 2022/23 | 17,202 | 3,072.00 | 3,746,793 | 4,263 | 25 |
| 2023/24 | 17,823 | 501.69 | 3,582,502 | 4,821 | 27 |
| 2024/25 | 18,044 | 521.76 | 3,363,275 | 4,970 | 28 |
| **Wastani** | **17,690** | **1,365.15** | **3,564,190** | **4,685** | **26** |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakuguzi kwa Fedha Zilizoombwa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kwa Wizara ya Fedha (kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi 2024/25) wa Mwaka 2025

835. **Jedwali Na. 55 l**inaonesha utofauti wa fedha zinazopokelewa kwa mwezi kwa shule za msingi kwa ajili ya kugharimia uendeshaji ni Sh. 3,072, Sh. 501, na Sh. 521 kwa miaka ya fedha 2022/23, 2023/24, na 2024/25, mtawalia, wakati shule zingine zikipokea hadi Sh. 3,746,793 kwa kipindi hicho.

Hali hii pia ilijitokeza kwa shule za sekondari kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 56**.

**Jedwali Na. 56: Mwenendo wa Fedha za Ruzuku za Uendshaji Zinazopelekwa kwa Shule za Sekondari**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Shule | Kiwango cha Fedha Kilichopelekwa (Sh.) | | Shule za Sekondari ziliopelekewa Fedha kidogo kuliko posho za madaraka wa Wakuu wa Shule | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kiwango cha Chini | Kiwango cha Juu | Idadi | Asilimia (%) |
| 2022/23 | 4,263 | 21,118 | 3,895,981 | 621 | 15 |
| 2023/24 | 4,821 | 14,248 | 4,227,935 | 840 | 17 |
| 2024/225 | 4,970 | 5,078 | 4,562,853 | 628 | 13 |
| Average | 4,685 | 16,815 | 4,228,923 | 696 | 15 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakuguzi kwa Fedha Zilizoombwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa Wizara ya Fedha (kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi 2024/25) wa Mwaka 2025

836. **Jedwali Na. 56 l**inaonesha utofauti wa fedha zilizopokelewa kwa mwezi kwa shule za sekondari kwa ajili ya gharama za uendeshaji ni Sh. 21,118, Sh. 5.078, na Sh. 14,248 kwa miaka ya fedha 2022/23, 2023/24, na 2024/25, mtawalia, wa kati shule zingine zikipokea hadi Sh. 4,562,853 kwa kipindi hicho.

837. Kutolewa kwa Kiwango kidogo na kisichosawa kwa mwezi kinatokana na njia iliyotumika kukokotoa fedha za ruzuku za uendeshaji shule kuzingatia idadi ya wanafunzi bila kuangalia gharama zingine ambazo hazizingatii idadi ya wanafunzi.

838. Hali hii inaathiri shule ndogo zenye idadi ndogo ya wanafunzi. Mara nyingi shule zenye wanafunzi wachache ni zile zilizopo mbali na mjini. Shule hizo zinalazimika kusubiri fedha ziwe nyingi ndipo zikachukuliwe ili kuepuka gharama za usafiri ambazo ni kubwa kuliko fedha anazo kwenda kuchukua.

### 11.4.2 Utoaji wa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji Shule Isivyotosheleza na Isivyosahihi

839. Nilibaini kuwa sio fedha zote zilizotengwa zilizotolewa, na zilizotolewa hazikukokotolewa kwa usahihi kwa kuzingatia kiwango na idadi ya wanafunzi kama inavyoelezwa hapa chini.

### (a) Fedha za Ruzuku Zilizotengwa kwa ajili ya Ununuzi wa Vitabu Zilitolewa Kiwango Kidogo

840. Nilibaini kuwa kiwango kilichotengwa kwa ajili ya ununuzi wa vitabu kwa Miaka ya Fedha 2022/23 hadi 2024/25 ilikuwa Sh. bilioni 59.3 (Sawa na Asilimia 58) ya Fedha zilizotengwa za Sh. bilioni 102.7. Kwa undani juu ya fedha zilizopangiwa zinaonesha kwenye **Jedwali Na. 57.**



NAOT ISO 9001:2015 Certified


**Jedwali Na. 57: Fedha zilizotenga na zilizotolewa kwa ajili ya Ununuzi wa Vitabu**

| Mwaka wa Fedha | Kiwango Sh. bilioni | | | Asilimia ya Fedha Zilzotolewa (%) |
|---|---|---|---|---|
| | Kiwango Kilichotengwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI | Fedha Zilizotolewa na Wizara ya Fedha | Upungufu | |
| 2022/23 | 44 | 14.8 | 29.2 | 34 |
| 2023/24 | 34.4 | 17.2 | 17.2 | 50 |
| 2024/25 | 24.3 | 27.3 | -3 | 112 |
| **Jumla** | 102.7 | 59.3 | 43.4 | 58 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakuguzi kwa Fedha Zilizotengwa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na Zilizotolewa kwa ajili ya Ununuzi wa Viatabu (kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi 2024/25) wa Mwaka 2025

841. **Jedwali Na. 57** inaonesha kuwa, kiwango cha Sh. bilioni 43.4 sawa na asilimia 42 ya fedha zilizotengwa kiasi cha Sh. bilioni 102.7, kwa ajili ya ununuzi wa vitabu hazikutolewa. Hali hii iliathiri ununuzi wa vitabu kwa wakati kwa ajili ya shule za umma. Hata hivyo, utoaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitabu umeimarika, hii inaonesha kuna uelekeo chanya kwenye utolewaji wa fedha kama inavyoneshwa kwenye **Kielelezo Na. 46.**

**Kielelezo Na. 46: Kuongezeka kwa Mtiririko wa Utolewaji wa Fedha kwa ajili ya Ununuzi wa Vitabu**




***Chanzo:*** Uchambuzi wa wakuguzi kwa Fedha zilizotengwa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na zilizotolewa kwa ajili ya Ununuzi wa Viatabu (kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi 2024/25) wa Mwaka 2025

842. **Kielelzo Na. 46** kinaonesha kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 na 2023/24, asilimia 34 na 50 ya fedha zilizotengwa zilitolewa, mtawalia. Lakini kwa Mwaka, 2024/25, zilitolewa kwa asilimia 112. Hii inaonesha fedha zilizotolewa zimezidi zilizopangwa, ongezeko lilitokana na malipo kwa deni la vitabu kwa Mwaka 2023/24.

### (b) Fedha Zilizotolewa za Ruzuku za Uendeshaji Shule ni Zaidi ya Kiwango Kilichopaswa Kutolewa

843. Nilibaini kuwa Fedha zilizotolewa za ruzuku za uendeshaji kwa ajili ya kugharimia uendeshaji wa shuleni kwa kuzingatia Idadi ya Wanafunzi kwa mujibu wa sensa za shule za kila mwaka zimezidi kiwango kilichotakiwa. Kwa ujumla, kwa kipindi cha kuanzia Mwaka 2022/23 hadi 204/25 kiwango kilichozidishwa ni Sh. millioni 14,475 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 58.**

**Jedwali Na. 58: Utofauti kati ya Fedha Zilizopaswa Kutolewa na Zilizotolewa**

| Mwaka wa Fedha | Fedha Zilizotolewa (Sh. Milioni) | Fedha Zilizotakiwa Kutolewa (Sh Milioni) | Tofauti (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|
| 2022/23 | 107,088 | 105,505 | 1,583 |
| 2023/24 | 114,549 | 109,744 | 4,806 |
| 2024/25 | 119,991 | 111,905 | 8,086 |
| **Jumla** | **341,628** | **327,154** | **14,475** |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa wakuguzi kwa Fedha zilizoombwa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kwa Wizara ya Fedha (kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi 2024/25), 2025

844. **Jedwali Na. 58** linaonesha mtiririko wa kutoa fedha nyingi zaidi ukilinganisha na idadi ya wanafunzi inaongezeka kila Mwaka kuanza 2022/23 hadi 2024/25, kiwango kilichozidi kinaongezeka kutoka Sh. millioni 1,583 kwa Mwaka 2022/23 hadi Sh. millioni 8,086 kwa 2024/25.

### (c) Ukokotoaji wa Kiwango cha Fedha za Ruzuku za Uendeshaji Shule Haukufanyika kwa Usahihi

845. Nilibaini kuwa Kiwango kilichotumika kukokotoa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji wa Shule, zilizoenda shuleni moja kwa moja haukufanyika kwa usahihi. Kwa mfano, kwa shule za Msingi kiwango kilichotumika kwa mwanafunzi kwa mwezi ilikuwa kati ya Sh. 501.01 hadi Sh. 528.18, badala ya Sh 500 kwa mwanafunzi kwa mwezi kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 59**. Kwa Shule ya Sekondari, ilikuwa kati ya Sh.1,054.39 na Sh 1,176.42 badala ya Sh. 1,041.667 kwa mwanafunzi kwa mwezi kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 60**.

**Jedwali Na.59: Kiwango kilichotumika na kilichopaswa kutumika kwa Shule za Msingi**

| Mwaka wa Fedha | Kiwango kwa mwanafunzi kwa mwezi | | | Kiwango cha Fedha Kilichoongezeka |
|---|---|---|---|---|
| | Kiwango Kilichopaswa | Kiwango kilichotumika | Tofauti | |
| 2022/23 | 500 | 501.01 - 518.06 | 1.01 - 18.60 | 690,041,538 |
| 2023/24 | 500 | 501.69 - 518.18 | 1.69 - 18.18 | 1,999,320,000 |
| 2024/25 | 500 | 521.76 - 528.18 | 21.76 - 28.18 | 3,486,471,500 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa wakuguzi kwa Fedha zilizoombwa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kwa Wizara ya Fedha (kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi 2024/25), 2025

846. **Jedwali Na. 59** linaonesha kuwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, kiwango kwa mwanafunzi kwa mwezi kiliongezeka kwa kati ya Sh. 1.01 hadi Sh.18.6. Kiwango hicho kiliendelea kuongezeka hadi Sh. 21.76 na baadae Sh.28.18 kwa Mwaka 2024/25. Hii inasababisha kutolewa kwa fedha zaidi ya zinazohitajika kwa Sh.690,041,538 Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi Sh.3,486,471,500 kwa mwaka 2024/25. Hali hii ilitokea pia kwa shule za sekondari kama inavyooneshwa kwenye, **Jedwali Na. 60.**

**Jedwali Na. 60: Kiwango kilichotumia na kilichopaswa kutumika kwa Shule za Sekondari**

| Mwaka wa Fedha | Kiwango kwa Mwanafunzi kwa wezi | | | Athari ya Kiwango Kilichoongezeka |
|---|---|---|---|---|
| | Kiwango Kilichopaswa | Wigo wa Kiwango Kilichoombwa | Utofauti wa Kiwango Kilichoombwa na Kilichotakiwa | |
| 2022/23 | 1,041.67 | 1,054.39 - 1,129.68 | 12.73 - 88.01 | 893,274,260 |
| 2023/24 | 1,041.67 | 1,095.32 - 1,141.76 | 53.65 - 100.10 | 2,806,400,181 |
| 2024/5 | 1,041.67 | 1,159.85 - 1,176.42 | 676.42 - 659.85 | 4,599,361,713 |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakuguzi kwa Fedha Zilizoombwa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kwa Wizara ya Fedha (kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi 2024/25) wa Mwaka 2025

847. **Jedwali Na. 60** linaonesha kuwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/23, kiwango kilichotolewa kwa mwanafunzi kwa mwezi kiliongezeka kwa kati ya Sh. 12.73 hadi Sh. 88.01, ikaongeza tena hadi Sh. 676.42, na ikafikia sh 659.85 kwa mwanafunzi kwa mwezi kwa Mwaka 2024/25. Hii ilisababisha kutolewa kwa fedha zaidi ya zilizohitajika kwa Sh. 893,274,260 Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi Sh. 4,599,361,713 kwa Mwaka 2024/25.

848. Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ilibainisha kuwa Ruzuku ya uendeshaji shule, ni moja ya sehemu ya progarmu ya Elimu bure kwa fedha kwanza zilitengwa kwa sehemu zingine, zinazobaki zote zilielekezwa kwenye Ruzuku za uendeshaji shule bila kujali kiwango cha kupelekwa kwa mwanafunzi kwa

mwezi. Hali hii ilisababisha kutolewa kwa fedha zaidi ya zinazopaswa kutolewa kwa kiwango cha Sh. Bilioni 14.47.

### 11.4.3 Fedha za Ruzuku Hazikutumika Ipasavyo

849. Nilibaini kuwa fedha zilitolewa kwa ajili wa ununuzi wa vitabu kwa kiwango fulani hazikutumika ipasavyo kama inavyoelezwa hapa chini.

**(a) Ununuzi wa Vitabu kwa ajili ya Wanafunzi ambao sio Walengwa**

850. Nilibaini kuwa kwa kutumia Fedha za Ruzuku za Uendeshaji Shule, jumla ya vitabu 760,549 vya mtaala wa Shule Maalamu za Kingereza vyenye thamani ya Sh.1,410,893,336, vilinunuliwa kwa ajili ya Shule za Mtaala wa Kingereza kuanzia Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi 2024/25 inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 61**. Hii ni kinyume na sehemu 3.10 of Waraka No. 6 wa 2015 wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknologia unaozuia Fedha za Ruzuku za Uendeshaji Shule kutumika kwa Shule za umma zinazoendesha kama shule binafsi. Ilibainika kuwa Taasisi ya Elimu Tanzania haikujua juu ya huo waraka na ilieleza kuwa vitabu hivyo pia vilijumuishwa kwenye mahitaji ya vitabu yaliyowasilishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI.

**Jedwali Na. 61: Mtiririko wa Ununuzi wa Vitabu kwa Shule za Mtaala wa Kingereza**

| Mwaka wa Fedha | Namba ya Vitabu | Jumla ya Gharama (Sh) |
|---|---|---|
| 2022/23 | 24,662 | 130,203,580 |
| 2023/24 | 352,222 | 471,236,615 |
| 2024/25 | 383,665 | 809,453,141 |
| **Jumla** | **760,549** | **1,410,893,336** |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa wa Wakaguzi kwenye Mikataba ya Ununuzi wa Vitabu 2022/23 hadi 2024/25 wa Mwaka 2025

851. **Jedwali Na. 61** linaonesha idadi ya vitabu vilivyonunuliwa vya Mtaala wa Kingereza ilikuwa inaongezeka Mwaka hadi mwaka.

852. Hii ilisababishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI. Kwa sababu baadhi ya vitabu vya Mtaala wa Kingereza vilikuwa kwenye orodha ya mahitaji yaliyowasilishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na vingine havikuwapo kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 62**.

**Jedwali Na. 62: Mtiririko wa Vitabu vya Mtaala wa Kingereza Vilivyoagizwa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Vitabu Vilivyoagizwa | Jumla ya Gharama (Sh) |
|---|---|---|
| 2023/24 | 297,105 | 382,810,960 |
| 2024/25 | 85,236 | 284,168,716 |
| **Jumla** | **382,341** | **666,979,676** |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi Taarifa ya Vitabu vilivyoagizwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2023/4 na 2024/25 wa Mwaka 2025

853. **Jedwali Na. 62** linaonesha Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI iliagiza vitabu 382,341 vya mtaala wa Kingereza kwa Mwaka 2023/24 na 2024/25. Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ilieleza kuwa vitabu hivyo vilinunuliwa ili kupunguza tatizo la ukosefu wa vitabu kwa shule za mtaala wa Kingereza.

854. Kutumia fedha za Ruzuku kwa kununua vitabu kwa wanafunzi ambao si walenga kulizuia kufikia uwiano wa kitabu na mwanafunzi kwa somo wa 1: 1 ili kufikia lengo la Elimu bure na bora kwa wote.

**(b) Utofauti Idadi na Thamani Vitabu Vilivyoagizwa na Vilivyopelekwa**

855. Nilibaini utofauti wa Idadi na Thamani ya Vitabu vilivyoagizwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na vile vilivyosambazwa kama inavyoelezwa kwenye **Jedwali Na.63.**

ISO 9001:2015 Certified

**Jedwali Na. 63: Utofauti wa Idadi na Thamani Vitabu Vilivyoagizwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Vilivyosambazwa na Taasisi ya Elimu Tanzania**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Vitabu vilivyoagizwa | Thamani ya Viatbu vilivyoagigzwa (Sh) | Idadi ya Vitabu Vilivyonunu | Thamani ya Vitabu vilivyonunuliwa (Sh.) | Utofauti wa Vitabu |
|---|---|---|---|---|---|
| 2023/2024 | 9,981,903 | 17,207,678,613 | 3,546,529 | 9,211,568,225 | 6,435,374 |
| 2024/2025 | 12,468,514 | 24,309,498,000 | 13,161,905 | 24,007,056,934 | (693,391) |
| **Jumla** | **22,450,417** | **41,517,176,613** | **16,708,434** | **33,218,625,159** | **7,128,765** |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Idadi na Thamani ya Vitabu Vilivyoagizwa na Vilivyonunuliwa (kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi 2024/25) Mwaka 2025

856. **Jedwali Na. 63** linaonesha utofauti wa idadi ya vitabu ulikuwa mkubwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 kwa Mwaka wa Fedha 2024/25.

857. Taasisi ya Elimu Tanzania, iliainisha kuwa, kwa Mwaka 2024/25, vitabu vilinunuliwa vingi zaidi ya vilivyohitajika kwa sababu kwa Mwaka 20223/24 walikuabaliana kusambaza vitabu 9,981,903 vyenye thamani iliyokadiriwa kuwa

Sh.17,200,000,000. Hata hivyo, fedha hazikwenda kwa wakati ikachangia ununuzi wa viatabu 3,546,529 vyenye thamani ya Sh.9,211,568,225. Hata hivyo, Uchambuzi wa Wakaguzi ulibaini kuwa, vitabu 2,011,421 vyenye thamani ya Sh. 5,468,433,162, vilivyosambazwa haviendani na vile vilivyoagizwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI. Hali hiyo, ilitokea pia kwa Mwaka 2024/25, ambapo kati ya vitabu 13,161,905 vilivyoagizwa ni vitabu 9,977,388 viliendana na maoni ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI. Vitabu 3,184,517 vyenye thamani ya Sh.6,339,176,382 havikuwa vile vilivyoagizwa.

858. Hii ilitokana na utathmini na ufuatiliaji usiotosheleza ili kujua kama vitabu vilivyosambazwa vinaendani na mahitaji yaliyoainishwa.

## 11.5 Athari ya Changamoto Zilizobainishwa katika Kufikia Malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Mendeleo Endelevu

859. Shabaha 4.1 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu inalengo la kuhakikisha Wasichana na Wavulana wote kupata Elimu bure, bora na kwa wote ifikapo 2030. Fedha za Ruzuku za Uendeshaji Shule za Umma ina mchango kwenye kutimiza lengo hili. Kwa ngazi ya shule ya Msingi, ufanisi umefikia asilimia 80 kwa wastani, na kwa sekondari ufanisi umeongezeka hadi kufikia asilimia 92 kwa 2024. Kwa Kidato cha tano na sita, ufanisi uliongezeka pamoja na kuongezeka kwa Idadi ya Wanafunzi.

ISO 9001:2015 Certified

860. Aidha, kuanzia mwaka 2022 hadi 2024, kumekuwa na maendeleo makubwa ya ujumuishaji hasa kuhusu Jinsia na wanafunzi wenye mahitaji maalamu. Viashiria vya usawa wa kijinsia vinaonesha kwamba usajili wa wanawake katika ngazi ya msingi na sekondari, umezidi kidogo ule wa wanaume. Katika mwaka 2022 na 2023, usajili wa wanaume ulikuwa asilimia 51 na 52. Mwelekeo ulibadilika kidogo mwaka 2024 ambapo wanaume walichukua nafasi ya juu kwa kufikia asilimia 53, ingawa tofauti ya kijinsia kwa ujumla ilikuwa ndogo katika miaka yote mitatu.

## SURA YA KUMI NA MBILI

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 12.1 Utangulizi

861. Sura hii inatoa hitimisho linalotokana na mapitio na uchambuzi wa matokeo ya ukaguzi kutoka katika ripoti 18 za ukaguzi wa ufanisi zilizofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika mwaka wa 2025. Pia, inatoa mapendekezo mahususi kwa taasisi zilizokaguliwa.

### 12.2 Hitimisho la Jumla

862. Ukaguzi unatambua juhudi za taasisi zilizokaguliwa katika kuboresha utendaji wao ili kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, ambayo yanalenga mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Maboresho yameonekana katika utoaji wa huduma za afya; utoaji wa huduma za malezi kwa wazee na huduma za kisheria kwa wananchi; usimamizi wa uhifadhi wa nafaka za kimkakati; usimamizi wa usalama mahali pa kazi na utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi; udhibiti wa huduma za maji; usimamizi wa mfumo wa usafirishaji; utunzaji wa mazingira; usimamizi wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini na utafutaji na usimamizi wa rasilimali fedha.

ISO 9001:2015 Certified

863. Pamoja na juhudi hizi, bado kuna changamoto kubwa zinazokwamisha ufikiwaji wa malengo yaliyokusudiwa. Udhaifu uliobainika unahitaji hatua za haraka ili kuoanisha juhudi za serikali na Malengo ya Maendeleo Endelevu, na Mpango wa wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano ili kuhakikisha maendeleo endelevu ya kiuchumi na ya binadamu.

#### 12.2.1 Hitimisho Mahususi

**(i) Utoaji wa Huduma za Afya**

864. Licha ya jitihada kubwa zilizochukuliwa kuhakikisha utoaji wa huduma za afya nchini, ninahitimisha kuwa Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na Bohari ya Dawa, hazikuhakikisha wala kusimamia ipasavyo utoaji wa huduma za afya. Kwa ujumla, nilibaini upungufu katika utoaji wa huduma za afya ya mfumo wa fahamu kwa watoto, hali iliyotokana na uchunguzi usioridhisha wa watoto wenye matatizo ya mfumo wa fahamu katika ngazi ya chini ya utoaji wa huduma za afya, jambo lililokwamisha

utoaji wa matibabu na huduma za urekebu kwa wakati. Aidha, ninahitimisha kuwa Wizara ya Afya na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI hazikuhakikisha ipasavyo utoaji wa huduma za afya ya uzazi, hali iliyosababisha vifo vingi vya akina mama wakati wa kujifungua na kuathiri ufikiwaji wa shabaha ya 3.1 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Mwisho, nilibaini kuwa Bohari ya Dawa, Wizara ya Afya na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI hazikuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa dawa muhimu katika vituo vya afya vya umma, hali iliyodhoofisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

**(ii) Utoaji wa Huduma za Malezi kwa Wazee na Huduma za Kisheria kwa Wananchi**

865. Kupitia kaguzi za ufanisi nilizofanya, nimebaini kuwa, mifumo ya Tanzania ya kusaidia makundi yenye uhitaji ni dhaifu na haifanyi kazi ipasavyo na hivyo kushindwa kutimiza upatikanaji wa haki na ubora wa maisha ya wazee wasiojiweza. Huduma za msaada wa kisheria zimetolewa kwa kiwango kisicho na usawa, ambapo takribani asilimia 30 ya watoa huduma wamejikita katika Kanda ya Mashariki na mijini, huku maeneo ya vijijini yakibaki bila huduma za kutosha. Utambuzi wa wazee wasiojiweza unategemea takwimu zisizo sahihi na mbinu zisizo thabiti. Hali hii imesababisha asilimia 99.92 ya watu wenye uhitaji kukosa huduma za kijamii za serikali. Nyumba za wazee zinakabiliwa na miundombinu iliyochakaa na upungufu wa wafanyakazi kwa asilimia 67, huku wakazi wake mara nyingi wakikosa bima ya afya, chakula chenye lishe, au vifaa saidizi.

ISO 9001:2015 Certified

866. Changamoto hizi zinachangiwa na ukosefu wa ufuatiliaji na uratibu. Nyumba za wazee hazijapokea usimamizi wa kusaidia kwa kipindi cha miaka minne, na viashiria vya utendaji havipo. Kwa ujumla, upungufu huu unaweka hatarini utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu.

**(iii) Usimamizi wa Uhifadhi wa Nafaka za Kimkakati**

867. Ukaguzi unahitimisha kuwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula na Wizara ya Kilimo hawajasimamia kwa tija na kwa ufanisi hifadhi ya nafaka za kimkakati ili kuhakikisha upatikanaji wa chakula na kuwa na bei himilivu. Hii ni kwa sababu ya usimamizi usiyojitosheleza wa mchakato wa ununuzi ili kuhifadhi akiba ya kutosha ya nafaka za kimkakati, kwa kuwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ameweza kufikia asilimia 58 tu ya lengo lililowekwa la uhifadhi wa chakula. Pia, imebainika usimamizi usiojitosheleza wa miundombinu ya kuhifadhi nafaka kiasi cha kusababisha kuwa na miundombinu yenye uwezo wa

kuhifadhi asilimia 57 tu ya lengo. Kadhalika, imebainika uhakika usiojitosheleza wa ubora wa nafaka zilizohifadhiwa, na ukarabati usiojitosheleza wa ghala unaofanywa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kiasi cha kusababisha kutotumika kwa eneo lenye uwezo wa kuhifadhi nafaka la tani 57,000.

868. Pia, kuna uratibu usio jitosheleza kati ya wadau na Wizara ya Kilimo katika kusimamia uhifadhi wa nafaka za kimkakati ambapo Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula na Wizara ya Kilimo wote walikuwa na idara zilizopewa jukumu la kutambua masoko ya ndani na ya kimataifa ya nafaka.

**(iv) Usimamizi wa Usalama Mahali pa Kazi na Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi**

869. Ukaguzi unatambua juhudi za Serikali kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi katika kusimamia usalama mahali pa kazi na huduma za fidia kwa wafanyakazi nchi nzima. Hata hivyo, licha ya juhudi hizo, usimamizi wa ukaguzi wa afya na usalama mahali pa kazi na utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi bado hauna ufanisi nchini. Upungufu unaochangia hali hii ni pamoja na: kuongezeka kwa kiwango cha vifo mahali pa kazi, ukaguzi usioridhisha wa maeneo ya kazi yaliyosajiliwa, kuchelewa kwa ukaguzi wa maeneo ya kazi, na kukosekana kwa usimamizi wa usalama wa afya mahali pa kazi. Aidha, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi haukuwa na ufanisi katika kulipa madai ya fidia ya wafanyakazi na ilicheleweshsha ushughulikiwaji wake. Aidha, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi hausajili kwa ufanisi waajiri wanaostahili, haukusanyi kwa ufanisi michango kutoka kwa waajiri, wala hausimamii kwa ufanisi uzingatiaji wa sheria miongoni mwa waajiri waliosajiliwa kama inavyotakiwa na Kanuni za Fidia kwa Wafanyakazi za mwaka 2016.

**(v) Udhibiti Mamlaka za Maji**

870. Ukaguzi unahitimisha kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji haijadhibiti ipasavyo mamlaka za maji. Licha ya juhudi za udhibiti zinazofanywa na Mamlaka hii, si mamlaka zote za maji zinasambaza maji ambayo yanakidhi viwango vya ubora vinavyohitajika kwa jamii. Zaidi ya hayo, baadhi ya mamlaka za maji zilizosajiliwa hazina miundombinu ya kutibu majitaka ambapo hadi Mwaka wa Fedha 2023/2024, asilimia 28 ya mamlaka za maji 82 ndio zilikuwa na miundombinu ya kutibu majitaka.

871. Pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kuidhinisha tozo za maji, bado kulikuwa na changamoto kadhaa ikiwemo baadhi

ya mamlaka za maji kutumia tozo zilizoisha muda wake, pamoja na upungufu katika kuweka viwango vya tozo na kuzifuatilia. Kwa kuongezea, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ilifanya shughuli za ufuatiliaji wa ubora wa maji bila kupima viwango vyote vya ubora wa maji kama vilivyoainishwa katika Mpango wa Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji wa mamlaka za Maji. Matokeo yake, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ilikosa uhakika kama maji yaliyotolewa kwa jamii yalikidhi viwango vinavyohitajika kwa vigezo ambavyo havikupimwa.

**(i) Usimamizi wa Mfumo wa Usafirishaji**

872. Ninahitimisha kuwa Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi, na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI hazijasimamia ipasavyo mfumo wa usafiri kutokana na kuwapo kwa upungufu katika upangaji na uwekaji vipaumbele vya maboresho ya miundombinu ya barabara, kutowapo kwa matengenezo kinga ya mizani za barabarani, na kutowapo kwa upangaji na udhibiti unaojitosheleza wa huduma za usafiri mijini. Upungufu huu ulipunguza ufanisi katika uboreshaji wa hali ya barabara, udhibiti usiojitosheleza wa uzito wa magari barabarani, na kupunguza ufikiwaji na ufanisi wa huduma za usafiri wa mijini.

**(ii) Utunzaji wa Mazingira**

873. Ukaguzi huu unahitimisha kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira na wizara za sekta hazijasimamia ipasavyo uhifadhi wa mazingira na utekelezaji wa miradi ya nishati safi kwa mujibu wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mpango wa Maendeleo Endelevu. Hali hii inaoneshwa na Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira kutotekeleza ipasavyo hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kuongeza ustahimilivu wa nchi dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi. Pia, Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI hazikusimamia kikamilifu shughuli za urejeshaji miti. Hii ni kwa sababu, shughuli za urejeshaji miti zinakabiliwa na changamoto kama upungufu wa miche, utunzaji wa miti usijitosheleza baada ya kuipanda, kiwango kidogo cha usimamizi jumuishi wa misitu, kutowapo kwa mipango ya usimamizi, upangaji mdogo wa rasilimali na serikali za mitaa katika kusimamia misitu, na uratibu mdogo miongoni mwa wadau.

874. Licha ya uwekezaji wa serikali katika nishati jadidifu, ikiwa pamoja na miundombinu ya kiwango kikubwa kama vile Mradi wa Kufua Umeme wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere wenye uwezo wa Megawati 2,115, Wizara ya Nishati na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji hazijasimamia miradi hii

kwa ufanisi ili kuhakikisha kuwapo kwa mchanganyiko wa nishati uliolingana ambao ungesaidia usalama na uendelevu wa nishati. Hii ni kwa sababu bado kuna changamoto katika kuhakikisha kunakuwa na mchango wa kutosha wa miradi ya nishati jadidifu kwenye mchanganyiko wa nishati kama ilivyopangwa.

**(iii) Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini**

875. Ukaguzi wangu unahitimisha kuwa Wizara ya Madini, Tume ya Madini na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi hazijasimamia ipasavyo utekelezaji wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya madini. Ushiriki wa Watanzania katika mnyororo wa thamani wa madini umeendelea kuwa mdogo huku idadi ya wataalamu wa kigeni katika nafasi za uongozi na kiufundi ikiendelea kuwa juu na mishahara yao ikiwa mikubwa zaidi kuliko ya wazawa. Aidha, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020 hadi 2024, thamani ya ununuzi wa bidhaa na huduma zilizopatikana ndani ya nchi ilikuwa asilimia 33 pekee ikilinganishwa na asilimia 67 ya thamani ya ununuzi wa bidhaa na huduma zilizotoka nje ya nchi. Vilevile, ukuaji wa ujuzi na urithishaji wa teknolojia kwa Watanzania haukuwa ya kuridhisha kwani ni asilimia 30 tu ya wafanyakazi waliopata mafunzo katika kampuni za madini zilizofanyiwa tathmini mwaka 2024.

**(iv) Utafutaji na Usimamizi wa Rasilimali Fedha**

ISO 9001:2015 Certified

876. Nina hitimisha kuwa Wizara ya Fedha, haijasimamia ipasavyo ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi hatimaye kuchagiza upatikanaji mdogo wa mapato yasiyo ya kodi nchini. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI haijasimamia kwa ufanisi utengaji wa fedha za ruzuku za uendeshaji wa shule ili kugharimia gharama za uendeshaji shule na ununuzi wa vitabu, na hivyo kuathiri utoaji wa elimu na kwa usawa.

## 12.3 Mapendekezo

877. Sehemu hii inawasilisha mapendekezo ya ukaguzi kulingana na uchambuzi wa changamoto zilizoelezwa katika sura ya tatu hadi ya kumi na moja. Ili kushughulikia changamoto zilizojitokeza katika utoaji wa huduma za afya; utoaji wa huduma za malezi kwa wazee na huduma za kisheria kwa wananchi; usimamizi wa uhifadhi wa nafaka za kimkakati; usimamizi wa usalama mahali pa kazi na utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi; udhibiti wa huduma za maji; usimamizi wa mfumo wa usafirishaji; utunzaji wa mazingira; usimamizi wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa katika sekta ya

madini; na utafutaji na usimamizi wa rasilimali fedha, ninapendekeza yafuatayo:

(a) Wizara ya Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI pamoja na Bohari ya Dawa zinahimizwa kuhakikisha utoaji wa kutosha wa huduma za afya ya uzazi na huduma za afya ya mfumo wa fahamu, pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa dawa muhimu katika vituo vya afya vya umma;

(b) Wizara ya Katiba na Sheria inapaswa kuandaa na kupitisha rasmi Sera ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria pamoja na Rejesta ya Kitaifa ya Kidijitali ili kuondoa pengo la kimkakati lililopo katika utoaji wa huduma za msaada wa sheria;

(c) Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu zinapaswa kuoanisha mchakato wa utambuzi wa wazee wasio na uwezo na kuipa kipaumbele kwa kina mipango ya ukarabati wa miundombinu kwenye makazi ya wazee 13 yanayomilikwa na serikali;

(d) Wizara ya Kilimo na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula wanatakiwa kuimarisha uratibu wa kimkakati wa ununuzi, uhifadhi na mifumo ya usimamizi wa gharama ili kuimarisha ununuzi wa nafaka na udhibiti wa ubora. Pia, wanatakiwa kuhakikisha ufanyaji wa tathmini ya hali ya ghala na kuwa na ratiba za matengenezo. Vilevile, wanapaswa kuhakikisha ufuatiliaji thabiti wa nafaka zilizohifadhiwa ili kuhakikisha kiwango kinachotakiwa cha kuanzia mwaka muda wote kinafikiwa kwa kuzingatia ubora na wingi wa nafaka, na kuimarisha uwazi, ufanisi, na uendelevu katika usimamizi wa hifadhi ya nafaka;

(e) Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi anahimizwa kuimarisha michakato ya usajili wa maeneo ya kazi ili kuhakikisha usajili unafanyika kwa wakati, na kutekeleza ukaguzi wa afya na usalama mahali pa kazi kwa kutumia mfumo wa vigezo vya vihatarishi ili kuhakikisha ukaguzi huo unakuwa na tija katika kupunguza ajali na vifo vitokanavyo na kazi;

(f) Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi unahimizwa kuimarisha ugatuzi wa shughuli zake katika Ofisi za Kanda kwa kuweka malengo ya utendaji yaliyo wazi, pamoja na mfumo wa ufuatiliaji, na kuandaa mipango ya uhamasishaji inayopimika itakayojumuisha makundi yote lengwa, ikiwemo waajiri na wafanyakazi wa sekta binafsi na serikali;

(g) Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji inatakiwa kuimarisha mfumo wake wa udhibiti kwa kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa masharti ya leseni, ufuatiliaji wa ubora wa maji na uandaajia wa tozo za maji, kwa kuanzisha utaratibu mzuri wa kurekebisha hesabu kulingana na utekelezaji wa tozo iliyoisha wakati wa uandaaji wa tozo na hivyo kuboresha ubora wa huduma, uendeshaji wa miundombinu, kutunza mazingira, na ufanisi wa udhibiti kwa jumla;

(h) Wizara ya Uchukuzi na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI zinahimizwa kuboresha huduma za usafiri wa umma kwa kuhakikisha kuwa upangaji na utekelezaji wa mfumo wa usafiri mjini unazingatia uunganishaji wa miundombinu ya aina tofauti za usafiri, ushirikishaji wa makundi yote yenye mahitaji maalumu, na kuunganisha mifumo ya taarifa za usafiri mijini ili kuwezesha ufuatiliaji na udhibiti wa huduma za usafiri kwa ufanisi;

(i) Wizara ya Ujenzi inahimizwa kuboresha miundombinu ya barabara kwa kuweka kipaumbele katika miradi ya barabara ili kuhakikisha kuwa miradi yenye matokeo makubwa inapewa kipaumbele. Pia, kipaumbele kitolewe kwa matengenezo ya miundombinu ya barabara katika ugawaji wa rasilimali ili kuboresha hali ya jumla ya mitandao ya barabara, ikiwa pamoja na miundombinu ya mizani;

ISO 9001:2015 Certified

(j) Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira na wizara za sekta zinahimizwa kuimarisha usimamizi wa uhifadhi wa mazingira kwa kuhakikisha upatikanaji wa fedha, uratibu kati ya wadau unaojitosheleza, mifumo imara ya ufuatiliaji na tathmini, na kuimarisha uwezo wa kiufundi katika usimamizi wa masuala haya kwenye ngazi zote, hasa serikali za Mitaa;

(k) Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI zinapaswa kuimarisha usimamizi wa shughuli za urejeshaji misitu kwa kuhakikisha upangaji na utekelezaji wa mipango ya upandaji miti kwa ufanisi, kuimarisha uratibu kati ya wadau, pamoja na kuweka mifumo imara ya ufuatiliaji na tathmini ili kusaidia urejeshaji endelevu wa misitu;

(l) Wizara ya Nishati, kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, inahimizwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mitambo ya kufua umeme na miundombinu ya usafirishaji ya usafirishaji umeme

iliyoko katika hatua mbalimbali za ujenzi, ili kuhakikisha kuwa ujenzi huo unazingatia viwango vya ubora vinavyokubalika na tarehe za kuanza kazi kibiashara zilizokubaliwa;

(m) Wizara ya Madini, Tume ya Madini, na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi zinahimizwa kuimarisha usimamizi wa taratibu za ushirikishwaji wa wazawa kwa kuendeleza viwanda vya ndani, kuboresha sera za urithishaji wa teknolojia, kuimarisha usimamizi na ukaguzi, pamoja na kuanzisha mfumo wa kisheria wa kitaifa utakaohakikisha ufanyikaji na ufuatiliaji madhubuti wa masuala haya katika sekta zote;

(n) Wizara ya Fedha inashauriwa kuweka taratibu za kutambua vyanzo vipya vya mapato; kuanzisha mifumo na michakato madhubuti ili kuhakikisha makadirio halisi ya mapato yasiyo ya kodi, na si tu kwa kutumia taarifa zilizopita bali msingi wa taarifa wa vyanzo hivyo; na kuhakikisha taratibu za ukusanyaji zilizosanifiwa zinatumika katika Taasisi Zote ili kuhakikisha usawa na uwazi, pamoja na kuimarisha udhibiti wa ndani,na ufuatiliaji wa mifumo ya utendaji;

(o) Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI inatakiwa kuhakikisha kuwa, ukokotoaji wa fedha za ruzuku unazingatia viwango vinavyofaa na kwa kutumia takwimu rasmi za idadi ya wanafunzi. Pia, ishirikiane na Wizara ya Fedha kuhakikisha kuwa iwapo fedha zilizopelekwa shuleni hazijapokelewa zipelekwa tena kwa wakati na matumizi ya fedha ya ruzuku yajikite kwenye malengo yaliyokusudiwa.

# Viambatisho

ISO 9001:2015 Certified

## Kiambatisho Na. 1: Kaguzi za Ufanisi Zilizofanyika Zikihusianisha na Maudhui ya Malengo ya Maendeleo Endelevu Pamoja na Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano

| Jina la Ukaguzi | Malengo ya Maendeleo Endelevu | Shabaha | Eneo la Kipaumbele katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano |
|---|---|---|---|
| Utoaji wa Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu na Neva kwa Watoto | Lengo la 3: Afya Bora na Ustawi | 3.8 - Huduma za afya kwa wote, ikijumuisha upatikanaji wa huduma bora za afya, upatikanaji wa dawa muhimu zilizo bora kwa gharama nafuu, na upatikanaji wa chanjo kwa wote. | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, 5.5: Maendeleo ya Watu. |
| Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya ya Umma | Lengo la 3: Afya Bora na Ustawi | 3.8 - Huduma za afya kwa wote, ikijumuisha upatikanaji wa huduma bora za afya, upatikanaji wa dawa muhimu zilizo bora kwa gharama nafuu, na upatikanaji wa chanjo kwa wote. | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, 5.5: Maendeleo ya Watu. |
| Utoaji wa Huduma za Afya ya Uzazi | Lengo la 3: Afya Bora na Ustawi | 3.1 - Kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi kwa uwiano wa vifo 70 kwa vizazi hai 100,000 ifikapo mwaka 2030. | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, 5.5: Maendeleo ya Watu. |
| Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria kwa Wananchi Wasiojiweza | Lengo la 1: Tokomeza Umaskini | 1.3: Utekelezaji wa mifumo ya hifadhi ya jamii ili kuongeza ufikiwaji wa watu maskini na wanaoishi mazingira hatarishi. | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, 5.5: Maendeleo ya Watu |
| | Lengo la 5: Usawa wa Jinsia | 5.2: Kukomesha aina zote za unyanyasaji wa wanawake na wasichana katika maeneo ya umma na binafsi. | |
| | Lengo la 10: Kupunguza Matabaka | 10.3: Kutoa fursa sawa na kupunguza tofauti za matokeo kwa | |

| Jina la Ukaguzi | Malengo ya Maendeleo Endelevu | Shabaha | Eneo la Kipaumbele katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano |
|---|---|---|---|
| | | kuondoa sheria na desturi za kibaguzi. | |
| | Lengo la 16: Amani, Haki na Taasisi Imara | 16.3: Kuweka mkazo wa utawala wa sheria kwa ngazi za taifa na kimataifa na kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wote, hasa kwa makundi yaliyo kwenye mazingira hatarishi na yaliyotengwa. | |
| Utoaji wa Chakula, Makazi na Huduma za Malezi kwa Wazee | Lengo la 1: Tokomeza Umaskini | 1.3: Utekelezaji wa mifumo ya hifadhi ya jamii ili kuongeza ufikiwaji wa watu maskini na wanaoishi mazingira hatarishi. | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, 5.5: Maendeleo ya Watu |
| | Lengo la 3: Afya Bora na Ustawi | 3.8 - Huduma za afya kwa wote, ikijumuisha upatikanaji wa huduma bora za afya, upatikanaji wa dawa muhimu zilizo bora kwa gharama nafuu, na upatikanaji wa chanjo kwa wote. | |
| Usimamizi wa hifadhi ya nafaka za kimkakati | Lengo la 2: Tokomeza Njaa | 2.1: Kutokomeza njaa, kuwa na uhakika wa chakula na kuboresha lishe.<br><br>2.2: Kuhamasisha kilimo endelevu | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano,5.3: Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma |
| Usimamizi wa ukaguzi wa usalama na afya mahali pa kazi | Lengo la 8: Kazi ya Staha na Ukuaji wa Uchumi | 8.8: Kuweka mkazo kwenye ukuaji wa uchumi ulio jumuishi na endelevu, ajira na kazi zenye staha kwa wote. | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano,5.5: Maendeleo ya Watu |
| | Lengo la 3: Afya Bora na Ustawi | 3.9: Maisha yenye afya na kuhamasisha afya bora kwa wote. | |

ISO 9001:2015 Certified

| Jina la Ukaguzi | Malengo ya Maendeleo Endelevu | Shabaha | Eneo la Kipaumbele katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano |
|---|---|---|---|
| | | Ensure healthy lives and promote well-being for all at all ages. | |
| Ufanisi kuhusu utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi | Lengo la 8: Kazi ya Staha na Ukuaji wa Uchumi | 8.8: Kuweka mkazo kwenye ukuaji wa uchumi ulio jumuishi na endelevu, ajira na kazi zenye staha kwa wote. | |
| | Lengo la 1: Tokomeza Umaskini | 1.3: Utekelezaji wa mifumo ya hifadhi ya jamii ili kuongeza ufikiwaji wa watu maskini na wanaoishi mazingira hatarishi. | |
| Udhibiti wa Huduma za Maji | Lengo la 6: Maji Safi na Usafi wa Mazingira | 6.1: Usimamizi endelevu wa maji na usafi wa mazingira kwa kuhakikisha upatikanaji wa maji safi ya kunywa kwa gharama nafuu kwa wote.<br><br>6.2: Kuwapo kwa mazingira safi na salama kwa wote na kutokomeza uchafuzi wa mazingira kwa kujisaidia hadharani.<br><br>6.3: Kuboresha usafisaji wa majitaka na kupunguza uchafuzi wa mazingira. | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano: 5.5 Maendeleo ya Watu |
| Usimamizi wa Mchakato wa Upangaji wa Uboreshaji wa | Lengo la 11: Miji Endelevu na Jamii | 11.2: Kufanya miji na makazi ya watu kuwa jumuishi, salama, himilivu na endelevu . | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano: 5.2 |

ISO 9001:2015 Certified

| Jina la Ukaguzi | Malengo ya Maendeleo Endelevu | Shabaha | Eneo la Kipaumbele katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano |
|---|---|---|---|
| Miundombinu ya Barabara | Lengo la 9: Viwanda, Ubunifu, na Miundombinu | 9.1: Kujenga miundombinu imara, kuhamasisha ukuaji wa viwanda endelevu, na kuchochea ubunifu. | Uchumi Shindani na Shirikishi |
| Usimamizi wa Uendeshaji wa Mizani | Lengo la 9: Viwanda, Ubunifu, na Miundombinu | 9.1: Kujenga miundombinu imara, kuhamasisha ukuaji wa viwanda endelevu, na kuchochea ubunifu. | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano: 5.2 Uchumi Shindani na Shirikishi |
| Usimamizi wa Huduma za Usafiri Mjini katika Majiji Makubwa | Lengo la 11: Miji Endelevu na Jamii | 11.2: Kufanya miji na makazi ya watu kuwa jumuishi, salama, himilivu na endelevu . | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano: 5.2 Uchumi Shindani na Shirikishi |
| Utekelezaji wa Miradi ya Nishati Jadidifu | SDG 7: | 7.2: Upatikanaji rahisi, wenye uhakika na endelevu wa nishati bora. | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano: 5.2 Uchumi Shindani na Shirikishi |
| Ukaguzi wa Ufanisi katika Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi nchini Tanzania | Lengo la 2: Tokomeza Njaa | 2.3 Kuweka mkazo katika kuongeza mazao ya kilimo na kuongeza kipato cha wazalishaji wadogo wa mazao ya kilimo kufikia mwaka 2030. | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano,5.3: Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma |
| | Lengo la 6: Maji Safi na Usafi wa Mazingira | 6.1: Usimamizi endelevu wa maji na usafi wa mazingira kwa kuhakikisha upatikanaji wa maji safi ya kunywa kwa gharama nafuu kwa wote. | |

ISO 9001:2015 Certified

| Jina la Ukaguzi | Malengo ya Maendeleo Endelevu | Shabaha | Eneo la Kipaumbele katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano |
|---|---|---|---|
| | Lengo la 13: Tabianchi Chukua Hatua | 13.1 Kuweka mkazo katika kuimarisha ustahimilivu na uwezo wa kukabiliana na Athari za mabadiliko ya tabianchi ifikapo mwaka 2030. | |
| Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Shughuli za Urejeshaji Misitu | Lengo la 15: Maisha juu ya Ardhi | 15.1: Inasisitiza kuhakikisha uhifadhi, urejeshaji,na matumizi endelevu ya mifumo ya ekolojia na maji ifikapo mwaka 2030. | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano,5.3: Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma |
| Ukaguzi wa ufanisi katika Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini | Lengo la 8: Kazi ya Staha na Ukuaji wa Uchumi | 8.5: kufanikisha kuwapo kwa ajira bora za kudumu na kazi zenye staha kwa wote. | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, 5.3: Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma |
| | Lengo la 9: Viwanda, Ubunifu, na Miundombinu | 9.3: Kuwawezesha wafanyabiashara wadogo kuongeza thamani ya bidhaa zao. | |
| | | 9.5: Kuhamasisha utafiti, uwezo wa tekinolojia na ubunifu. | |
| | Lengo la 12: Kuwajibika, Matumizi na Uzalishaji | Target 12.6: Kuhimiza makampuni kufuata mbinu endelevu za kiutendaji na utoaji wa taarifa. | |
| Ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya Kodi | Lengo la 17: Ushirikiano wa Malengo | 17.1: Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano: 5.2 Uchumi Shindani na Shirikishi |
| Usimamizi wa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji wa Shule za Umma | Lengo la 4: Elimu bora | 4.1: Kuhakikisha wasichana na wavulana wote wanapata elimu bora ya msingi na | Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano: 5.5 |

| Jina la Ukaguzi | Malengo ya Maendeleo Endelevu | Shabaha | Eneo la Kipaumbele katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano |
|---|---|---|---|
| | | sekondari bure na kwa usawa ifikapo mwaka 2030. | Maendeleo ya Watu |

***Chanzo:*** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi wa Mwaka 2025

ISO 9001:2015 Certified




**Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**
**4 Barabara ya Mahakama**
**S.L.P 950,**
**Tambukareli, 41104 Dodoma, Tanzania**
**Simu: +255 (026) 2161200**
**Barua Pepe: ocag@nao.go.tz**

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT
ISO 9001:2015 Certified